

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 22 Julai, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 258

**Barabara Zilizo Chini ya Halmashauri ya Misungwi**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara zilizo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ni mbaya sana na wakati wa masika hazipitiki: mfano Misungwi – Nguge – Mondo – Mwaniko; Kabale – Ng’obo – Mwamboku – Ikungumhulu na Isenengeja – Mahando: Je, barabara hizo zikoje kila moja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, hali ya barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi za Misungwi – Nguge – Mondo – Mwaniko (kilomita 21), Kabale – Ng’obo – Ikungumhulu (kilometa 9) na Isanengeja – Mahando (kilometa 7) si ya kuridhisha na barabara hizi zinapitika kwa shida hasa wakati wa mvua. Kwa ujumla, barabara hizi zinahitaji kufanyiwa ukarabati ili ziweze kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanya matengenezo katika barabara hizo ziweze kupitika wakati wote kwa kupitia Mfuko wa Barabara, Serikali imefanya mambo yafuatayo:-

Kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009, Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi shilingi milioni 60 kwa ajili ya matengenezo ya Barabara za Misungwi – Nguge – Mondo –Mwaniko, yenye urefu wa kilometa tano. Mkandarasi kwa ajili ya kufanya kazi hii amekwishapatikana na mchakato wa kusaini mkataba unaendelea na kazi itaanza mara moja. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha 2009/2010, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, imepanga kutumia kiasi cha shilingi milioni 65 kwa ajili ya matengenezo ya Barabara ya Misungwi – Mondo yenye urefu wa kilometa tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ilipanga kuifanyia matengenezo sehemu korofi (*Sport Improvement*), Barabara ya Kabale – Ng’obo – Ikungumhulu, yenye urefu wa kilomita tatu kwa gharama ya shilingi milioni 17.7. Mkandarasi amekwishapatikana na ameanza kufanya kazi hiyo. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi imetenga kiasi cha shilingi milioni 21 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi katika barabara hiyo yenye urefu wa kilomita nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Isenengaja – Mahando itafanyiwa matengenezo kupitia Programu ya Kuboresha Sekta ya Kilimo (*District Agricultural Sector Improvement Programme (DASIP)*), kwa gharama ya shilingi milioni 20 kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha barabara zake katika Halmashauri kulingana na hali ya uchumi itakavyoruhusu.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijauliza maswali mawili, nimwombe afikishe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri ambayo aliifanya alipotutembelea na kutuahidi shilingi milioni 60 na zimetetelezwa. Pia afikishe lawama kwa watendaji ambao wamekuwa wazito sana katika utekelezaji wa kutoa fedha hizo, tumezipata tarehe 3 Julai, 2009 ni ucheleweshaji wa hali ya juu. Kwa hiyo, lawama ziwafikie hawa ambao walizichelewesha.

(a) Kwa kuwa shilingi milioni 60 ukijumlisha shilingi milioni 65 itakuwa ni fedha nyingi sana; je, Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya Mkutano huu unaweza kupata nafasi ya kutembelea eneo hilo na baadaye ukajionea mwenyewe jinsi pesa itakavyotumika?

(b) Kwa kuwa Barabara ya kutoka Kabale kwenda N’gobo – Ikungumhulu ni mbaya sana; mwaka jana wewe mwenyewe wakati unanijibu uliahidi kwamba, kulikuwa na shilingi milioni 55 lakini badala yake zimetumika shilingi milioni 17; je, hizo nyingine ambazo uliniahidi hapa zimekwenda wapi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii, kupokea pongezi zako kwa ajili ya Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na lawama. Ninadhani na wewe utatusaidia kwa sababu unatoka kule.

Ninataka nimthibitishie Mheshimiwa Shibiliti kwamba, nimezungumza na watendaji hawa na Mheshimiwa Mbunge kama anavyozungumza jana nimekwenda kwa mara ya tatu, nikachukua barua na kumwambia hizo shilingi milioni 60 tumeingiza katika akaunti ipi. Hela zilikuwa zimeingizwa katika Mfuko wa Barabara na tumezungumza nao nikawaambia zililetwa hapa kwa ajili ya kutengeneza barabara. Ninapozungumza hapa, nina hakika kwamba wananisikia, wamelaumiwa na Mbunge wao kwamba hawafanyi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kumpongeza sana Mbunge kwa namna anavyofuatilia. Amenikaba vizuri na ndiyo kazi ya Mbunge kuikaba Serikali mpaka tukaweza kufika hapa. Sasa kuna hizi hela zinazozungumzwa hapa, ambazo ninaweza nikajibu zote kwa pamoja. Ni kweli kwamba, tunaendelea kufuatilia hizi hela kipengele kwa kipengele.

**NAIBU SPIKA:** Kuibana Serikali siyo kuikaba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Kuibana, unajua Kiswahili hiki kinachanganyika na Kichaga humo humo unisamehe. Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa, hela hizi tumeshazipeleka na hizo shilingi milioni 65 nazo zimekwenda.

Sasa anazungumza kuhusu hizi shilingi milioni 55 ambazo zimetumika shilingi milioni 15. Nataka nikuthibitishie kwamba, nitaendelea kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge, kuhakikisha kwamba, hizi hela zote zimekwenda kama zilivyokuwa zimepangwa. Naomba yeye atoe ushirikiano kwetu, tutasaidiana na tutazifuatilia hela hizi ambazo anaziulizia.

Kuhusu suala la kuja kule, tunachofanya kama Serikali ni kuweka mfumo ambao unafanya kazi badala ya kungoja mpaka Waziri aje pale. Namwomba atusaidie, lakini mimi naahidi kwamba, nikipata nafasi nitaomba ruhusa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, niende kule nikaangalie vizuri nijithibitishie. (*Makofi*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mfumo wa mgawanyo wa hizi fedha na ukilinganisha mtawanyiko wa barabara ambazo ziko kwenye vijiji, barabara nyingi za Halmashauri ni nyingi zaidi kuliko za *trunk road*; lakini mfumo wa kugawa fedha ni mdogo zaidi kwenye Halmashauri ambayo haina mapato ya kutosha: Je, Serikali haiwezi kurekebisha mgawanyo huu ukawa nusu kwa nusu kwa Halmashauri na nusu nyingine ikaenda kwenye *TANROAD* ili barabara zote za Halmashauri ziweze kuboreshwa na kupitika kwa muda wote wa mwaka mzima? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu, hili ni swali la kisera.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Seleli, Mbunge wa Nzega kama ifuatavyo:-

Nashukuru sana unakumbusha hapa kwamba, hili ni suala la Kisera, ambalo siwezi kulifanyia maamuzi hapa. Ninataka nikubaliane na Mheshimiwa Lucas Seleli kwamba, barabara zilizopo katika Halmashauri, zimeonekana ni nyingi ukilinganisha na kiasi cha fedha ambacho kinapangwa kule. Fedha zinazokwenda kule ni zile za *Road Fund*. Kimoja ambacho tumefanya hapa ni kwamba, sasa hivi tumeamua kwamba, hela hazitakuwa zinapitia tena TAMISEMI, zitakuwa zinakwenda moja kwa moja katika Halmashauri zinazohusika. Tumelipokea hili na tutaliangalia, kwa sababu ni suala la kisera siyo suala ambalo naweza nikaliamua hapa, lakini tumelipokea na tutazingatia ushauri huo. (*Makofi*)

Na. 259

### **Michango ya Wananchi Katika Miradi**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Je, Serikali iko tayari kuweka kiwango cha asilimia 15 badala ya asilimia 20 kwa mchango wa wananchi na kuangalia upya bajeti yake katika Miradi ya Ujenzi ya *TASAF*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), unajengwa katika dhana ya ushiriki wa jamii katika kupanga mipango yao ya maendeleo. Miradi ya *TASAF* hutekelezwa kwa ubia kati ya Serikali Kuu, Halmashauri za Wilaya na Miji, Wananchi wa Jamii husika, pamoja na Wafadhili mbalimbali ikiwemo Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapatio ya kati ya maendeleo ya utekelezaji wa *TASAF* awamu ya pili kuanzia Novemba, 2007 hadi Machi 2008, yameonesha suala la uwezo wa wananchi kuchangia katika miradi mbalimbali ya maendeleo ni miongoni mwa changamoto kubwa katika utekelezaji wa Mradi wa *TASAF*. Changamoto nyingine ni pamoja na kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi na mafuta, hivyo kusababisha viwango vilivyokadiriwa kutoweza kukamilisha miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliona hilo, Serikali pamoja na Wafadhili, wamekubaliana kupunguza kiwango cha michango ya jamii kutoka asilimia 20 hadi asilimia 15 kwa miradi yote ya ujenzi. Aidha, viwango vya michango ya Wafadhili katika

miradi ya ujenzi vimependekezwa kuongezwa hadi kufikia dola za Kimarekani 45,000 kutoka dola 30,000 zilizokuwa zikitolewa kama kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosubiriwa sasa ni kukamilisha kwa taratibu za mkataba wa makubaliano ili viwango hivi vipya vianze kutumika. Hivyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira kwani suala hili Serikali imeliona na imelishughulikia. (*Makofi*)

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwa kinachosubiriwa sasa ni taratibu tu na mimi navuta subira kusubiri hizo taratibu:-

(a) Je, ni lini utaratibu huo utakamilika?

(b) Kwa kuwa baadhi ya miradi ya kijamii hasa ile ya walemavu na ya UKIMWI wakati mwingine inapomaliza mradi wenyewe inakuwa si endelevu; je, tatizo wananchi wanakosa elimu au ubunifu wa ile miradi yenyewe?

**NAIBU SPIKA:** Subira ni pamoja tarehe usubiri tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lini kama nilivyomwambia, namwomba avute subira, haya ni mambo ya majadiliano, lakini wameonesha utayari kinachosubiriwa ni kusaini mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya watu ambao wako katika hali duni ya maisha, uendelevu wa miradi hiyo ndiyo kitu ambacho tunakiweka mbele. Kwa hiyo, hawa wanaoanzisha hiyo miradi ya maskini, watu wenye UKIMWI mara nyingi huwa tunawawezesha wale jamaa zao ambao wanawahudumia ili waendelee kufanya shughuli hizo. Kwa hiyo, tunawategemea wale ambao wamepata mafunzo ya kufanya shughuli mbalimbali za kuweza kuleta uwezo wa kujikimu katika jamii, waendelee kuwahudumia jamii ile maskini. Ahsante.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa imedhihirika wazi kwamba Miradi ya *TASAF* imeleta mafanikio mazuri; je, Serikali haioni kwamba kuna sababu za msingi kabisa kuongeza Miradi kupitia *TASAF* ambayo ufanisi wake na viwango vyake umethibitika kuwa ni mzuri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nashukuru kwa kuona miradi hii inafanikiwa vizuri. Pia ningependa kumfahamisha kwamba, mpaka sasa *TASAF* ni mradi tu; kwa hiyo, kinachofanywa ni kukifanya kiwe chombo kisheria ambacho kitaweza kupata ruzuku na kupata misaada kutoka mashirika mengine duniani. Kwa sasa mfadhili mkubwa ni World Bank na hivyo tunaamini itakapokuwa taasisi au itakapokuwa wakala au chombo ambacho kimeundwa kisheria, itakuwa na nguvu zaidi ya kuweza kupata misaada mingi zaidi kutoka nchi nyingine na hivyo kuwa na uwezo wa kutekeleza miradi mikubwa zaidi na mingi.

**Utengenezaji wa Barabara kwa Fedha za STABEX**

**MHE. WILSON M. MASILINGI (K.n.y. MHE. MOHAMED RAJAB SOUD)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wakulima na Wananchi wa Muleba kwa ujumla tumenufaika na fedha za *STABEX* kwa kutengenezewa Barabara ya Kanyambo – Rubya – Ibuga na Daraja la Kamwana:-

- (a) Je, ni fedha kiasi gani zilitumika kufanya kazi hiyo?
- (b) Je, kama fedha za *STABEX* hazikutosha kwa nini Serikali haikuongeza fedha ili kipande cha barabara kuanzia Kanyambogo hadi Kashasha kitengenezwe vizuri pia?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za ukarabati wa Barabara ya Kanyambogo – Rubya – Ibuga pamoja na daraja la Kamwana ambao ulikamilika mwezi Machi 2007 chini ya Mpango wa *STABEX*, uliharimu jumla ya shilingi milioni 137.1.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zilizokarabatiwa chini ya Mpango huu, zote ni za Halmashauri ya Wilaya na zilichaguliwa kwa kufuata vigezo vilivyokubaliwa kwa kushirikisha Wilaya husika. Fedha zote za kugarimia Mradi huu kwa asilimia 100 ni za Jumuiya ya Ulaya (*EU*), chini ya mpango wa *STABEX*, ambapo Wakala wa Barabara walipewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa kazi hizo tu. Kwa kuwa Barabara ya Kanyambogo hadi Kashasha ni ya Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, ni jukumu la Halmashauri ya Muleba kupanga na kupata fedha za kufanyia matengenezo barabara hiyo, pamoja na kipande kilichobaki ili kufanya ipitike msimu wote wa mwaka.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii *STABEX System* haipo tena na Serikali bado haijalijulisha Bunge; je, Serikali inaweza kulijulisha Bunge hivi sasa kwamba *STABEX* haipo na utaratibu wake sasa umebadilika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, huu utaratibu wa *STABEX* ulikuwa unatumika wakati ule ambapo uuzaji wa kahawa kupitia masoko ya Jumuiya ya Ulaya na kipindi kile ambapo utaratibu huo ulikuwa unatumika kwa kuuza mazao kupitia Vyama vya Ushirika ili fedha za *STABEX* zikija zilikuwa zinawarudia wakulima kwa kufuatana na rekodi zilizokuwa kwenye kumbukumbu za Vyama vya Ushirika. Baada ya Mfumo wa Soko Huria kuingia, Mfumo wa *STABEX* ukaonekana kwamba, sasa kumfikishia mkulima moja kwa moja ukawa na ugumu na

ndiyo maana hizo fedha za mwisho zilipokuja, ikaamuliwa ziende kutumika katika maeneo ya wakulima wa kahawa kwa kuhudumia barabara ambazo zinapita katika maeneo ya wakulima wa kahawa. Hizo ndiyo zilikuwa fedha za mwisho na kwa sababu utaratibu huo ulikuwa unawalenga wakulima wa kahawa waliokuwa wanauza mazao yao kupitia kwenye Masoko ya Jumuiya ya Ulaya, ndiyo maana sasa hivi Mpango huo hautumiki tena. (*Makofi*)

**MHE. FUYA J. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hizi fedha za STABEX hazitakuwepo tena na sisi tunaolima Kahawa tulikuwa tunafaidi kutokana na hizi fedha; na kwa kuwa barabara zilizotengenezwa zilitengenezwa katika viwango vizuri sana; je, Mheshimiwa Waziri sasa atakubaliana na mimi kwamba Serikali izichukue hizi barabara na kuzipandisha daraja kuwa za Mkoa ili ziweze kuendelea kutunzwa vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba, fedha za STABEX zilitumika kwa ajili ya matengeneza ya barabara pale tu ilipokuwa imekosekana kumbukumbu za kuwapata mkulima mmoja kuweza kupata malipo yaliyokuwa yanastahili kwao. Suala la kwamba, sasa hivi barabara zile ambazo zilikuwa zinahudumiwa na STABEX zipandishwe daraja ili ziweze kuhudumiwa na TANROAD, niseme tu kwamba, wiki tatu zilizopita, tulitoa maelezo hapa ya vigezo vilivyotumika katika upandishaji wa madaraja barabara na zoezi hilo litakuwa linaendelea.

Kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira, katika barabara ambazo zilikuwa zinahudumiwa na STABEX ambazo sasa hivi ziko chini ya Halmashauri ya Wilaya, ziendee kuhudumiwa na Halmashauri ya Wilaya wakati vigezo vya upandishaji barabara vitakapokuwa vinapitiwa mara kwa mara, pengine nyingine zinaweza zikakidhi vigezo hivyo.

Na. 261

### **Usafiri wa Ndege - Iringa**

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojibu Swali Na. 208 ilisema kuwa, huduma za usafiri wa ndege haziwezi kupelekwa Iringa kwa kuwa hakuna biashara; lakini pamoja na ukweli huo Wananchi wa Iringa hawawezi kushabikia biashara ambayo haipo na nina uhakika kwamba mara ikijulikana na kutangazwa kuwepo kwa usafiri huo, wafanyabiashara na watu wengi toka sehemu mbalimbali za Mkoa wa Iringa wataanza kuitumia huduma hiyo:-

Je, kwa nini Iringa isiunganishwe na njia nyingine za anga kama vile Mbeya, Sumbawanga, Songea na Miji mingine ya Kusini kwa lengo la kuimarisha biashara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Nduli kilichopo Mkoani Iringa ni moja kati ya viwanja bora hapa nchini. Miundombinu ya Kiwanja ikiwemo barabara ya kutua na kurukia ndege ni imara, iliyojengwa kwa lami na hivyo kukifanya kiwanja kutumika wakati wote wa mwaka. Aidha, Serikali kupitia mamlaka ya viwanja vya ndege, imekuwa inakifanyia matengenezo madogo madogo kwa kutoa fedha kila mwaka ili kiweze kutumika kwa kiwango cha kuridhisha kama inavyotakiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*ICAO*).

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ya Kiwanja cha Ndege cha Nduli ni ukosefu wa abiria na mizigo ya kutosha ili kuyavutia makampuni yanayofanya usafiri wa anga hapa nchini yaweze kutoa huduma kwenye kiwanja hicho.

**NAIBU SPIKA:** Msaidie Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri kakae.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Nenda kakae Mheshimiwa Naibu Waziri. Msaidieni atoke nje kabisa. Wasaidizi mko wapi mumsaidie?

*Hapa Naibu Waziri wa Miundombinu (Mhe. Hezekiah N. Chibulunje) alishindwa kujibu swali kutokana na kuugua ghafla na kutolewa nje ya Ukumbi*

**NAIBU SPIKA:** Naomba ujibu upya swali namba 261.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie kulijibu swali hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Nduli kilichopo Mkoani Iringa ni moja kati ya viwanja bora hapa nchini. Miundombinu ya Kiwanja ikiwemo barabara ya kutua na kurukia ndege (*runway*) ni imara, iliyojengwa kwa lami na hivyo kukifanya kiwanja kutumika wakati wote wa mwaka. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, imekuwa ikiifanyia matengenezo madogo madogo kwa kutoa fedha kila mwaka ili kiweze kutumika kwa kiwango cha kuridhisha kama inavyotakiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*ICAO*).

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ya Kiwanja cha Ndege cha Nduli ni ukosefu wa abiria na mizigo ya kutosha ili kuyavutia makampuni yanayofanya usafiri wa anga hapa nchini, yaweze kutoa huduma kwenye kiwanja hicho.

Aidha, kiwanja hakina kituo cha mafuta na hivyo kuyalazimisha makampuni ya ndege kujaza mafuta kwenye ndege zao ili ndege ziweze kwenda Iringa na kurudi na



hivyo kupunguza uwezo wa kubeba abiria au mizigo na kwa namna hiyo kuongeza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge la kuunganisha njia ya Iringa na miji mingine kama vile Mbeya, Sumbawanga na Songea, kwa lengo la kupata abiria na mizigo ya kutosha. Wizara na Serikali kwa ujumla, itaendelea kuyashawishi makampuni ya ndege kuangalia uwezekano wa kuunganisha njia ya Iringa na miji mingine kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa majibu ya Wizara. Nichukue nafasi hii kumpa pole ndugu yangu Mheshimiwa Chibulunje na kumwomba Mwenyezi Mungu, amsaidie apone mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali la nyongeza kwani imekuwaje? Hama *microphone* husikiki.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba ni jukumu la Serikali kuweka mazingira sahihi kuvutia biashara; kama ndivyo kwa nini basi Serikali isijenge kituo cha mafuta ambacho Waziri amesema ni muhimu kabla hatujaendelea? Naomba majibu.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Galinoma kama ifuatavyo:-

Serikali inadhamiria na ina mpango maalum wa kuhakikisha kwamba, inafanya maboresho katika Viwanja vya Ndege ili kuweza kurahisisha na kuwezesha usafiri wa anga uwe imara kwa nchi nzima. Kwa hivi sasa Serikali inashughulikia Kiwanja cha Ndege cha Iringa. Vilevile inavishughulikia kuvijengea miundombinu viwanja saba nchini, ambavyo vitaikuza hadhi ya kuwezesha kupitisha ndege kubwa zaidi na miundombinu yake ya kurukia na kutua iwe bora, ikiwemo pia miundombinu ya Kiwanja cha Ndege cha Iringa.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Chrisant Mzindakaya, badala yake swali hilo ataliuliza Mheshimiwa Killimbah.

Na. 262

### **Kutengeneza Chumvi Kutokana na Maji ya Bahari**

**MHE JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. DKT. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inafahamu kuwa maji yote ya Bahari ya Hindi yana chumvi ambayo inaweza kutengeneza chumvi ya kula na kutengeneza madawa ya kemikali:-

Je, kuna mipango gani mikubwa ya kutengeneza chumvi kutokana na maji hayo ili kuliwezesha Taifa kuongeza mapato?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, naomba kutua maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maji ya bahari yana chumvi ambayo inaweza kutengeneza chumvi ya kula na pia kwa matumizi ya viwandani kwa kukausha maji hayo. Hapa nchini chumvi inayotakana na maji ya bahari, huzalishwa katika maeneo kadhaa kwenye fukwe za Bahari ya Hindi za nchi yetu. Maeneo yanayozalisha chumvi itokanayo na maji ya bahari ni pamoja na Kunduchi katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mikindani Mkoani Mtwara, Saadani na Changwahela huko Bagamoyo katika Mkoa wa Pwani, Ukanda wa Pwani wa Mkoa wa Lindi na Mtwara, Buyunikuu/Uzinia - Pangani na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Serikali wa kupanua shughuli za utengenezaji chumvi kutokana na maji ya bahari, umeendelea kutekelezwa kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuamsha ari ya kuongeza juhudi za uzalishaji chumvi kwa kutumia maji ya bahari. Juhudi hizo zimewezesha kampuni tano kupewa leseni kubwa za uzalishaji wa chumvi.

Kampuni hizo ni Seasalt Limited yenye leseni mbili katika maeneo ya Saadani na Changwahewa Bagamoyo; Kibo Match Corporation Limited iliyo na leseni moja huko Muheza; Kayvee Holdings Limited ambayo ina leseni moja huko Buyunikuu/Uzimia Pangani; Thorn Tree Minerals Limited yenye leseni mbili huko Ras Nunge na Kitame Bagamoyo; na Timbers Limited iliyo na leseni moja huko Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya mpango wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo, hatua mbalimbali za kuwahamasisha wachimbaji wadogo zimekuwa zikiendelea kufanyika, ambapo hadi sasa zaidi ya leseni ndogo 269 za uzalishaji chumvi zimekwishatolewa kwa wavunaji chumvi wakiwemo Jeshi la Magereza, ambalo linazalisha chumvi katika kitongoji cha Machole Mkoani Lindi, Vyama vya Ushirika na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pamoja na kukaribisha wawekezaji kutoka nje kuwekeza kwenye uzalishaji wa chumvi, pia imeendelea kuwahimiza wazalishaji chumvi wadogo kujiunga pamoja na kuanzisha ushirika wa kutengeneza chumvi ili wajijengee mazingira mazuri ya kukopesheka na pia waweze kupewa mafunzo na misaada mbalimbali kwa urahisi. Aidha, Serikali imekuwa ikizihamasisha Taasisi mbalimbali zikiwemo Jeshi la Magereza, kuanzisha au kupanua shughuli zao za uzalishaji chumvi.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kutokana na majibu yake ameeleza dhahiri kwamba yapo maeneo mengi yanayoweza yakazalisha chumvi, lakini inaelekea ni suala la uratibu: Kutokana na maeneo hayo kuwa mengi na kwa sababu chumvi inaweza kuleta pato kwa Taifa letu; je, Wizara yake pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara wako tayari sasa kutengeneza mkakati wa kupata kiwanda kimoja kikubwa hapa nchini ambacho kinaweza kikatibu maeneo yote na tukatengeneza chumvi na baadae chumvi hiyo tukaitumia kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Bonde la Wembere Kijiji cha Nkonkilangi huko Jimboni kwangu Wirama Magharibi kuna eneo wananchi wanatengeneza chumvi na magadi yanapatikana. Ninachotaka kujua, Waziri anayo tarifa hiyo na kama anayo wana mkakati gani kutengeneza eneo hilo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara yangu na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuweka mkakati wa kujenga kiwanda kimoja, ufafanuzi wake ni kama tunavyofahamu, sera yetu ni shirikishi hasa kuhusu sekta binafsi. Suala ambalo sisi tunajenga mazingira mazuri ya Kitaasisi na Kisheria, lakini wachezaji wakubwa katika shughuli zote za kiuchumi ni sekta binafsi, pamoja na kwamba kuna nyakati Serikali inaweza kuingia.

Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, sisi tumeshajiandaa; mikakati ipo na mazingira mazuri yapo ya kuishirikisha sekta binafsi, pamoja na Taasisi nyingine kadiri zitakavyoona inafaa kuingia katika shughuli hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taarifa ya kuwepo chumvi na magadi kwenye Bonde la Wembere, Wizara yangu inafahamu hilo, lakini kama nilivyosema, Serikali kiseria ilishajiondoa kufanya shughuli moja kwa moja za uzalishaji hasa katika shughuli za kibiashara. Niendeleo kumhamasisha Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine, pamoja na Watanzania wenzetu kwamba, hii nayo ni mojawapo ya fursa ambazo wawekezaji watakaopenda kuwekeza katika maeneo haya, wanakaribishwa na sisi Serikali tuko tayari kuratibu kuwezesha uhalali wa shughuli hizo ambazo wangependa kuzifanya.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri; ni kweli kabisa kwamba chumvi inayovunwa Tanga, Bagamoyo, Dar es Salaam, Lindi na Mikindani inasaidiwa na Serikali lakini kasi ya kusaidia uvunaji wa chumvi hii ni ndogo sana kwa sababu...

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Serikali iendelee kusaidia kwa sababu sisi wa mikoa hii ambayo tunalima chumvi, haitusaidii wakati mwingine tunanunua chumvi kutoka Mombasa kwa sababu chumvi tunayovuna haina ubora.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa unahutubia, swali lako ni nini? Usituhutubie.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali itasaidia viwanda kwa ajili ya utengenezaji wa chumvi hii? Tunaomba msaada wenu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mikidadi kama ifuatavyo:-

Serikali ipo tayari kuendelea kusaidia wawekezaji wetu katika sekta hii ndogo ya chumvi, kwa kadiri ambavyo tutaletewa maombi ya kuweza kusaidia.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante tunaendelea na swali lingine, Mheshimiwa Said Amour Arfi atauliza swali hilo.

Na. 263

### **Hitaji la Umeme Sumbawanga**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza: -

Kwa kuwa umeme wa uhakika bado ni tatizo kubwa linalokwamisha maendeleo Mkoani Rukwa:-

(a) Je, ni lini Mji wa Sumbawanga, Namanyere na Mpanda itaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa?

(b) Je, ni hatua gani za haraka za dharura na muda mrefu zimechukuliwa kuondoa kero ya umeme kukatika, kupanda na kushuka mara kwa mara katika Mji wa Sumbawanga?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la umeme katika Mkoa wa Rukwa linachangiwa na kiwango cha umeme kisichotosheleza (*Low Voltage*) kutoka Zambia. Mipango iliyobuniwa ya kufunga *capacitor Bank* kuboresha upatikanaji wa umeme kutoka

Zambia, umeonekana kutokuwa na tija kwa kuwa hata huko Kaskazini mwa nchi hiyo umeme hautoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoeleza hapa Bungeni tarehe 10 Aprili, 2008 wakati tukijibu swali la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Kalambo kuwa, kuunganishwa kwa Mkoa wa Rukwa katika Gridi ya Taifa, kumejumuishwa katika Mradi wa Umeme ujulikanao kama *North West Grid*. Mradi huo utaunganisha kwenye Gridi ya Taifa Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa.

Kwa sasa Serikali inatafuta wafadhili wa kuweza kuufadhili mradi huo. Mkoa wa Rukwa ukiunganishwa na Gridi ya Taifa, Miji ya Sumbawanga, Namanyere na Mpanda, itaunganishwa pia.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tulieleza hapa Bungeni tarehe 16 Julai, 2009 kuwa, Serikali inatambua kuwa Mji wa Sumbawanga kwa sasa unategemea umeme kutoka Zambia ambao sio wa uhakika na kiwango cha ubora wake si cha kuridhisha. Hatua za muda mfup au za dharura ni kununua majenereta manne yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 1.25 kila moja ili Mji wa Sumbawanga uwe na uhakika wa kupata umeme. Maombi ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa majenereta hayo manne pamoja na mengine manane kwa ajili ya Wilaya za Ngorongoro, Kasulu na Kibondo, yamejumuishwa katika bajeti ya mwaka 2009/2010, ambayo tutaiwasilisha keshokutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za muda mrefu ni kuunganisha Mkoa wa Rukwa kwenye Gridi ya Taifa kama nilivyoeleza hapo awali. Jitihada nyingine zinazofanywa na Serikali ni pamoja na ziara ya Mheshimiwa Naibu Waziri wangu wa Nishati na Madini ya tarehe 6 Aprili, 2009 nilipomtuma kwenda Zambia, kukutanana na Waziri wa Nishati wa Nchi hiyo ili kujadili upatikanaji wa umeme Sumbawanga. Matokeo ya ziara hiyo ni kwamba, Serikali ya Zambia imekubali kuwekeza kwenye mitambo ya umeme ya Chasimba ili kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme wa kituo hicho, kwa kuunganisha na Kituo cha Umeme cha Mbala kinachosafirisha umeme kwenda Sumbawanga.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunahitaji utulivu ndani, maana kila mtu anaendelea na mazungumzo. Nendeni mkazungumze nje kama mnataka. Siyo kila mtu anaongea! Mheshimiwa Arfi swali la nyongeza.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswala mawili ya nyongeza. Awali ya yote, kwa niaba ya Wananchi wa Mji wa Mpanda, napenda kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zako za kuondoa tatizo la umeme katika Mji wa Mpanda. Nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yako Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Rukwa unatarajiwa kuungwa katika Gridi ya Taifa kutokea *North West* ifikapo mwaka 2020 kama Mpango Kabambe wa TANESCO unavyoelekeza. Ni busara ipi ya kawaida iliyotumika ya kuchukua umeme umbali wa kilomita 1000 kutoka Sumbawanga mkaacha kuchukua kutoka Mbeya kilomita 340? Ni busara gani ambayo mmeitumia kutoa umeme Geita kuuleta Sumbawanga badala ya Mbeya kuupeleka Sumbawanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, swala pili; kwa kuwa Mkoa wa Rukwa ulikuwa umejiandaa katika uwekezaji mkubwa na kufanya kongamano la wawekezaji pale Sumbawanga; ni matarajio ya Mkoa tuweze kuingia katika viwanda, lakini hatuwezi kuingia katika viwanda bila kuwa na umeme wa uhakika; je sasa Serikali itakuwa tayari kuangalia vianzo vya umeme vinavyopatikana katika Mkoa wa Rukwa na hususan mpango wa umeme kutokana na upepo katika eneo la Usevya kwa ajili ya Mji wa Mpanda itakuwa tayari kufanya utafiti huo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa niaba ya Serekali, naomba kumshukuru Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Jimbo lake na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla, kwa kuonesha *appreciation*, kwa kuonesha kuridhika kwao na juhudi zinazofanywa na Serikali kuhusu kuimarisha huduma ya umeme katika Mkoa wa Rukwa. Kuhusu busara iliyotumika, hili ni suala la kitaalamu, lakini niseme tu kwamba, Mheshimiwa Mbunge amesema Mpango Kabambe wa kuimarisha huduma ya umeme. Nchi inaonesha kwamba, mikoa hii itaunganishwa kwenye mwaka 2020. Tulisema wakati wa semina tarehe 12, tulipokuwa tunaiendesha kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, Mpango Kabambe ule si msahafu ambao haubadiliki. Tulisema changamoto kubwa tuliyonayo kama Taifa ni upatikanaji wa rasilimali fedha, ambayo itatuwezesha kuwekeza katika miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za Serikali zinaendelea kufanywa kuhakikisha kwamba, mipango mingi iliyooneshwa katika Mpango Kabambe ule inatekelezwa kabla kuliko inavyooneshwa. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Watanzania kwa ujumla kwamba, juhudi zinaendelea na tunaamini kwamba, pengine mwaka 2020 ni mbali sana, kuweza kuunganisha Mikoa hiyo. Kwa nini ilionekana kwamba upembuzi yakinifu uliofanywa umeme uunganishwe kutoka Wilaya ya Geita kupitia Mikoa na maeneo ambayo yapo upande wa Kaskazini Magharibi badala ya kutokea Mbeya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni suala la kitaalamu na hilo tumejiridhisha baada ya kufanya na kuzingatia mambo mengi, yakiwemo maeneo ambayo umeme huo utapitia, lakini pia na kuangalia *focus* ya muda mrefu kwa nchi kwamba, tukishawekeza kwa kupitia ile kwa sababu itajengwa *transmission line* yenye nguvu kubwa zaidi, nadhani kwamba, hii njia itatunufaisha kuliko ambavyo tungetumia njia ambayo inatokea Mbeya, ambayo inahitaji kuboreshwa kwa sasa. Serikali ipo tayari kuendelea kushughulikia vyanzo vingine kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amependekeza na

zoezi limeshaanza kupitia Wakala wa Nishata Vijijini na Wizara ya Nishati na Madini, Wataalamu wetu wapo wanaendelea kuratibu kupitia maeneo mbalimbali nchini.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Mkiwa.

**Na 264**

**Jeshi la Polisi Kuwa Karibu na Wananchi**

**MHE. MKIWA A. KIMWAGA (K.n.y. MHE. SAVELINA S. MWIJAGE)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wana mategemeo makubwa kwa Serikali yao pamoja na Jeshi la Polisi kwa kuwalinda pamoja na mali zao:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni vizuri Vituo vya Polisi vikawa karibu na wananchi ili kupunguza usumbufu kwa wananchi?

(b) Je, kwa nini traffic wa barabarani wasiwe na vituo maalumu ikiwezekana wajengewe vibanda?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata huduma muhimu karibu na maeneo yao wanayoishi, ikiwemo huduma ya Jeshi la Polisi. Hata hivyo, kutokana na uwezo mdogo wa kiuchumi, bajeti inayotengewa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, haiwezeshi Serikali kutimiza azma yake hiyo ya kusogeza huduma ya Polisi mpaka kwenye ngazi ya Kata na karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uwezo mdogo wa kiuchumi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), inaendelea kuona uwezekano wa kujenga Kituo cha Polisi katika kila Kata hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya jibu hili, kutokana na ukubwa wa nchi yetu, sio rahisi kuwa na vituo vidogo vya kudumu kwa askari wa usalama barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wa Usalama Barabarani kila mmoja ana kituo chake cha kazi (*Duty Station*). Askari hawa huwepo barabarani kufanya doria na operesheni ili kuzuia kutendeka kwa makosa sambamba na kuongoza magari na kuchukua hatua pale ambapo kuna uvunjifu wa Sheria.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ujambazi wa kushtukiza unatokea mara kwa mara hapa nchi kwetu; je, Serikali iko tayari sasa kuboresha Jeshi la Doria ili kuwapa vifaa vipya vya kisasa ili kukabiliana na ujambazi huo?

Swali la pili; kwa kuwa Waziri amesema bajeti inayotengwa haitoshi kutimiza azma hiyo; je, Serikali sasa iko tayari kuboresha vituo vilivyopo na kuwapeleka mafunzo Askari Polisi wale 7000 ili waje kusaidia kwenye vituo hivi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoieleza katika hotuba yangu ya bajeti, Serikali imejipanga kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya Jeshi la Polisi na tutaendelea kufanya hivyo katika miaka inayokuja kadiri ya uwezo wa Serikali. Katika kuendeleza ujenzi wa vituo, kama nilivyoieleza katika bajeti yangu ya mwaka huu, miradi ambayo tunaendelea nayo kwa mwaka huu ambayo tulianza mwaka jana ni kuendelea kujenga Kituo cha Mpanda, Ludewa, Newala, Bukombe na Meatu. Kwa mwaka 2009/2010, tutaendelea kujenga Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mkoa ya Mara, Manyara Ofisi ya Wakuu wa Polisi Wilaya za Bahi, Bagamoyo na Njombe na Ofisi za Wilaya za Kipolisi za Mbagala na Rorya. Nia ya Serikali ni kwamba, hawa Askari 7000 ambao wataajiriwa, watasambazwa katika vituo mbalimbali hapa nchini.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri, nilitaka kumuuliza swali dogo tu la nyongeza. Moja ya kazi ya Polisi ni kusaidia biashara ili iweze kufanyika vizuri, lakini ukiangalia magari yanayotoka Dar es Salaam kwenye Bandari yetu yakiwa yanakwenda labda Tunduma ama mpakani mwa Burundi na Rwanda, unakuta *traffic* wako *almost* unaweza ukasimamishwa zaidi ya mara 40, hivi hatuwezi kuona kwamba hawa *traffic* nao wanachelewesha biashara?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swali la kaka yangu Mheshimiwa Peter Serukamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, kuna vituo vingi ambavyo vinasimamisha magari katika barabara zetu hasa hizi barabara kutoka Bandarini katika mipaka ya nchi mbalimbali. Tayari tumekwishaelekezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kufanya kazi kwa pamoja na *customs* na taasisi nyingine ambazo zinaweka *road blocks* sehemu mbalimbali kuhakikisha kwamba, tunasimamisha haya magari kwa pamoja.

Kitu ambacho ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Serukamba ni kwamba, ofisi yangu itajitahidi kuhakikisha kwamba, Jeshi la Polisi halitakuwa kati ya vikwazo vya kufanya biashara isifanyike hapa nchini. Tutashirikiana na wenzetu ili kuhakikisha kwamba, wale ambao wanapitisha mizigo yao kihalali, wanapitishwa bila matatizo, lakini tutaendelea kuwa na polisi barabarani ili kuhakikisha kwamba, magendo, suala la usafirishaji wa binadamu na biashara nyingine ambazo sio halali, zinazuiliwa kutokana na kazi ya Jeshi ya Polisi inavyotakiwa kufanywa.



**Kupatikana kwa Madawa Bandia Aina ya Metakelfin**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza: -

Kwa kuwa usalama wa afya ya mlaji ni muhimu sana na kwamba hivi karibuni Serikali kupitia Taasisi ya Chakula na Madawa iliripoti kupatikana kwa dawa bandia (*fake*) aina ya metakelfin inayotibu malaria:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni kwa nini dawa hizo zilifika kwa watumiaji huku kukiwa na uangalizi mkubwa wa *entry points* zote?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha hali hiyo haijitokezi tena?

(b) Je, wale wananchi waliotumia dawa hizo na kuathirika watapatiwa fidia?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mamlaka ya Chakula na Dawa, imeweka mkakati wa uangalizi wa kutosha kwenye mipaka yetu (*Entry Points*) ili kudhibiti uingiaji wa dawa na vifaa tiba visivyo na kiwango. Hata hivyo, kutokana na ukweli kwamba, nchi yetu imezungukwa na nchi jirani nane na mipaka mingi iliyo rasmi na isiyo rasmi (njia za panya), baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu hutumia mwanya huo kuingiza nchini dawa bandia.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa inayofanywa na Serikali kulinda maeneo ya mipakani, naomba nitumie fursa hii, kupitia Bunge Tukufu, kutoa rai kwa mwananchi yeyote mwenye taarifa kuhusu wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara haramu ya dawa bandia, kutoa taarifa hiyo kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa au Polisi ili hatua zinazostahili ziweze kuchukuliwa kwa wahusika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa, dawa bandia haziingii katika nchi yetu. Baadhi ya mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

Ukaguzi katika mipaka inayoingiza bidhaa nchini umeimarishwa. Tumeanzisha Kikosi Kazi baina ya Mamlaka ya Chakula na Dawa na Jeshi la Polisi; mojawapo ya majukumu ya kikosi hiki ni kufanya operesheni za mara kwa mara kubaini dawa bandia katika soko.

Tumeweka maabara zinazohamishika katika mipaka ya kuingiza dawa nchini, ambapo dawa zilizoombewa vibali vya kuingizwa nchini, hupimwa pale pale mpakani kabla ya kuingizwa kwenye soko ndani ya nchi.

Serikali inaendelea kufungua Ofisi za Mamlaka ya Chakula na Dawa za Kanda ili kuimarisha udhibiti wa bidhaa hizi nchini. Jitihada zinaendelea kuongeza ofisi hizi za kanda katika maeneo zaidi ya nchi yetu.

Elimu inatolewa kwa umma kupitia vyombo vya habari kwa kuwaelimisha kuhusu namna ya kutambua dawa inayohisiwa kuwa bandia na pia namna ya kutoa taarifa katika vyombo husika zitakazosaidia kuondolewa kwa dawa hizo katika soko na pia kuchukua hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, serikali haina taarifa ya mwananchi yeyote aliyedhurika na *metakelfin* bandia zilizokamatwa nchini hivi karibuni. Hata hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inasimamia Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya Mwaka 2003, ambapo yeyote atakayebainika kuingiza bidhaa za dawa, chakula na vipodozi visivyokidhi viwango atawajibishwa kisheria ikiwa ni pamoja na kulipa fidia kwa walioathirika na dawa husika, kwa kuzingatia sheria nyingine za nchi. Aidha, *TFDA* haihusiki katika kutoa fidia kwa walioathirika.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu hayo, nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa athari za madawa na vipoozi bandia ni kubwa sana na pengine hupelekea ulemavu wa maisha, vifo na hata kupata magonjwa kama vile *cancer*; na kwa kuwa sababu kubwa ya uingizaji holela ya madawa haya kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni pamoja na ukosefu wa watumishi katika mamlaka husika; je, Serikali inasemaje kuhusu hilo; inaweza ikaongoza utumishi katika mamlaka hiyo?

(b) Hivi karibuni magazeti mengi yametoa matangazo ya madawa mbalimbali kwa mfano yanayoongeza ukubwa wa matiti, makalio na kupunguza tumbo na tulipopita katika Banda la Maonesho la Wizara ya Afya, Wataalamu walisema kwamba madawa hayo yana athari kubwa hasa *cancer*. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu hilo na anatoa tamko gani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba, *TFDA* wana upungufu mkubwa wa wataalamu ili kuweza kukabiliana na athari za dawa ambazo ni feki au bandia, lakini *TFDA* au Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inayo mpango wa kuongeza wataalamu ili kuhakikisha kwamba, hawa watu wanapatikana katika maeneo niliyoyataja katika jibu langu la msingi ili kuweza kuona kama wanakidhi haja ya kufanya ukaguzi wa papo kwa papo, lakini vile vile katika yale maeneo ambayo ni njia za panya au ni mipaka ambayo inaweza ikaingilia kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, dawa zile ambazo zinaingia na zinauzwa katika masoko ambayo TFDA au Serikali inakataa kwamba zina athari kubwa, zile dawa za kuongeza makalio na matiti, tamko ambalo tunalitoa ni kwamba, TFDA kama chombo cha Serikali na kwa sababu yenyewe huwa ina mpango wa kuwa inafanya ukaguzi wa mara kwa mara; kawaida huwa zikipatikana zile dawa huwa zinashikwa na wale watu wanachukuliwa hatua.

Napenda nichukue nafasi hii, kupitia Bunge lako Tukufu, niwakumbushe wananchi, tumekuwa tukisema hapa Bungeni kwamba, dawa zozote mbali ya hizi ambazo zinaongeza makalio na matiti, dawa zozote zile ambazo zinatakiwa mtu atumie; ni lazima aweze kupata ushauri kutoka kwa wataalamu. Kwa hiyo, naomba wananchi watusikilize kote waliko, marufuku kutumia hizi dawa kwa sababu zitaweletea madhara makubwa na itakuwa na matatizo sana kwa afya zao.

**NAIBU SPIKA:** Niliruhusu swali hili kwa sababu linahusu hali halisi. Mheshimiwa Simbachawene, swali lingine la nyongeza.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa usalama wa rajamu hasa kwa kutumia madawa umekua sasa hivi, maduka ya dawa ni sawa sawa na maduka ya *hardware* kwamba hushangai kumkuta aliyeanzisha duka la dawa mtoto wake na mke wake wako pale na hivyo kujiuzia kiholela tu kama wanauza cement, sukari na bati. Serikali inalifahamu suala hili na je, itaweka utaratibu gani wa kudhibiti hali hii ya kuuza ovyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara yetu ya Afya na Ustawi wa Jamii, ilipokuwa inafanya ukaguzi wa hapa na pale, iliona kwamba kweli kuna upungufu katika dawa hizi za kuuziwa maduka ya dawa.

Sasa hivi Serikali ina mpango umenza wa kuweka maduka ambayo yanaitwa maduka ya dawa muhimu, ambayo kwa kifupi tunasema ADO. Maduka haya utakuta kuna mtu ambaye analimiliki lile duka lakini muuzaji anaweza akawa ni mtoto au mtu wake, lakini huyu mtu atakuwa amepata mafunzo. Kwa hiyo, kama anazungumzia maduka haya ya ADO, nataka niwahakikishie kabisa wale watakaokuwa wanauza dawa katika maduka ya ADO ni wale ambao wamepata mafunzo kabisa. Kwa hiyo, watakuwa na utaalamu. Ppia nichukue nafasi hii, kwa wale ambao wanauza tu kiholela kama anavyosema *hardware*; hili ni kosa, kwa hiyo, tunawaagiza wale wakaguzi wa Wilaya na Mikoa wahakikishe wanapitia katika maduka hayo na kuona wale ambao wanauza bila kibali wanaacha mara moja.

Na 266

### **Tanzania Kujitegemea Kiuchumi**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa mtikisiko wa kifedha Duniani (*World Financial Crisis*) uliotokea hivi karibuni ulisababisha kuyumba kwa uchumi wa nchi za nje na wahisani tunaotegemea kusaidia bajeti yetu:-

Je, Tanzania inaandaa mazingira gani ya kujitegemea ili kuinusuru nchi kuyumba kiuchumi katika kipindi hiki kigumu?

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Jimbo la Chamaban, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa kipekee, Serikali imeandaa mazingira ambayo yatasaidia nchi yetu katika kujitegemea pamoja na kuinusuru isiyumbe kiuchumi katika kipindi hiki cha mtikisiko wa fedha na kiuchumi duniani. Yaliyoandaliwa ni mambo yafutayo:-

(i) Kuongeza eneo la kilimo, matumizi ya mbegu bora, mbolea, zana bora za kilimo na kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji;

(ii) Kupunguza gharama katika Sekta ya Utalii kwa lengo kwa kuwavutia watalii zaidi, ikiwa ni pamoja na watalii wa ndani;

(iii) Kuwasilisha Sheria ya Madini ili iweze kuweka mazingira ya kusaidia mapato ya Serikali;

(iv) Kuifanyia marekebisho Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa lengo la kupunguza upotevu;

(v) Kuendelea kulinda uwekezaji katika Sekta ya Miundombinu kwa lengo la kukuza ukuaji wa uchumi;

(vi) Kuboresha mifuko ya dhamana ili kuwezesha wajasiliamali wadogo na wa kati kuweza kuendelea na biashara zao;

(vii) Kuipa nguvu Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato;

(viii) Kuimarisha ufanisi wa kiutendaji katika Bandari ya Dar es Salaam;

(ix) Kuongeza mashirikiano na nchi rafiki za mashariki katika nyanja za kiuchumi, kibiashara na upatikanaji wa mikopo nafuu; na

(x) Kuongeza kazi kwa kuwahamasisha wawekezaji ndani na nje kuwekeza katika viwanda na hasa viwanda vya kusindika matunda.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa hivi karibuni Shirika la Fedha la Dunia (*IMF*) limeionya Tanzania juu ya ongezeko la urari wa malipo, yaani *balance of payment*, kutokana na mtikisiko wa uchumi Duniani; na jambo hili kwa mtazamo wao litapunguza kwa kiasi kikubwa uwezo wa Serikali wa kutekeleza Sera zake za Kifedha, yaani *fiscal and monetary policies* ili kufikia lengo la kujitegemea. Je, Serikali ina mpango gani wa kujinasua na hali hii?

Swali la pili, kwa kuwa Wanawake wa Tanzania ni wadau wakubwa wa maendeleo na wao pia wameathirika na mtikisiko huu wa uchumi duniani. Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuwasaidia Wanawake wa Tanzania katika jambo hili? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kama nilivyoeleza kwamba, tukitekeleza mambo niliyoyasema, Serikali itakuwa na uwezo mzuri wa kuweza kupata mapato na kupunguza hilo pengo katika *balance of payment*. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge, afuatilie vizuri na utekelezaji wake tutafikia hayo malengo.

La pili, Wanawake wa Tanzania ni kama Watanzania wengine, wana nafasi katika kila eneo ambalo nimelizungumzia. Wao vile vile ni wajasiriamali, watafaidika na hiyo mikopo ambayo Mifuko ipo ya kuweza kuwawezesha wanawake. Kwa hiyo, kwa mtazamo huo, namwomba vile vile Mheshimiwa Mbunge afuatilie katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali pia umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, leo tunayo orodha ya wageni ni kubwa na kama kawaida inachukua sana muda. Kwa kiwango kikubwa, tutakuwa tunakwenda kwa makundi kwa sababu inachukua muda sana. Wageni waliopo leo hii, kwanza kabisa ni wageni wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Philip Marmo, wao ni Walimu Wakuu wa Shule zilizofanya vizuri katika mitihani ya kumaliza Elimu ya Msingi Wilayani Mbulu, Manyara. Shule tatu za kwanza za Sekondari na 10 za kwanza za Msingi mwaka 2008.

Shule hizo ni hizi: Kuna walimu wakuu wa shule tatu za kwanza, ambao ni Mwalimu Wimina Diagno, Shule ya Sekondari ya Bagieshi. Mwalimu Mkuu yuko wapi? Inawezekana amekosa nafasi. Kuna Mwalimu Doho wa Shule ya Sekondari ya Magange, hapo kazi leo kujibu maswali. (*Kicheko*)

Kuna Mwalimu James Dahaye wa Shule ya Sekondari ya Dokta Olseni, sijui wako wapi kama wamekosa nafasi basi nadhani watahudhuria. Kuna walimu wakuu wamefuatana na walimu watatu kila shule ambao ni walimu wakuu wa shule nne za kwanza za msingi. Yuko wa Shule ya Msingi ya Aicho, Mwalimu Isack Ona. Kuna

Shule ya Msingi Mewadani, Mwalimu Daudi Safari. Kuna Shule ya Msingi Halka, Mwalimu Maliki Nyerere. Kuna Shule ya Msingi Bisigeta, Mwalimu Helena Masei. Nadhani kama wamekosa nafasi wataweza kupata nafasi baadaye.

Wageni wengine ni walimu wakuu wa shule sita zinazofuatia kwa ubora Wilayani, wakiongozana na Mkuu wa Kituo Binafsi cha Elimu, Waratibu wa Elimu wa Kata zao, Viongozi wa Elimu Wilaya na Viongozi Wakuu wa Wilaya akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Mbulu na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo. Mkuu wa Wilaya ya Mbulu yuko wapi na Mkurugenzi wake? Nafikiri watapata nafasi baadaye.

Tunao wageni wa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, ambao ni mke wake Pamela David Mathayo. Ahsante karibu. Kuna Rina Cleopatra David Mathayo, mtoto wake, ooh! Bado mdogo mdogo. Ahsante. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Haroub S. Masoud, ambao ni Bwana Said Omar (Mzaa Chema); sijui ndiyo nini tena? Yuko wapi Said Mzaa Chema? Aah! Yuko Mzee pale. Bwana Mwandamizi Zubeir, Katibu wa ZTFF Wilaya ya Kati; yule pale. Kuna Bwana Ali Yussuf, Katibu Mwenezi CCM, Mkoa wa Kusini. Kuna Bi. Fatuma Omar na Mwana Kheri Ali na Bi. Amour Mohamed, hawa wameongozana na Mzee Mzaa Chema bila shaka. (*Makofi*)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto. Yupo Katibu wa CCM Wilaya ya Kiteto, yupo Katibu Mwenezi CCM Wilaya, yuko Katibu Wazazi, Katibu wa Mbunge Mwenezi Kata ya Kibaya na Dereva wa CCM Wilaya. Naomba wote hawa wasimame walipo, kama wamekosa nafasi basi baadaye.

Tuna wageni wa Mheshimiwa James Musalika kutoka Kampuni ya Madawa ya Tiba Mbadala, *Daina Pharmacy International*, yenye Makao Makuu yake Dar es Salaam na Tawi Mjini Mwanza, Dodoma, wanaonesha maonesho katika Viwanja vya Bunge, ambao wanaongozwa na Bwana Allan Bomani, hawa wako wapi? Wote wasimame huko walipo. Basi Wabunge nadhani mtakwenda kuona madawa hayo.

Halafu tunao wageni 65 wa Mheshimiwa Monica Mbega, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Manispaa ya Iringa. Pia Wenyeviti, Makatibu Wenezi na Makatibu wa Fedha na Uchumi wa Kata katika Manispaa ya Iringa wanaongozwa na Bwana Abeid Kiponza. Karibuni Wanyalukolo jisikieni mko nyumbani. (*Kicheko/Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi wa Ludewa, wanatoka Tarafa ya Mwambao mwa Ziwa Nyasa, Wilaya ya Ludewa. Wanaongozwa na Mwenyekiti Lotalisi Finguru, Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Kilondo. Wasimame wageni wa Mheshimiwa Profesa kokote walipo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Kapteni John Komba, ambaye ni Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Lituhi, Ndugu Paul Maundi. Ndugu Paul Maundi yuko wapi? Nadhani Lituhi hawajambo? Mimi kule nilikuwa na rafiki zangu wengi.

Kuna wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, ambao ni wachezaji 10 wa mchezo wa *Pool Table* wa Mkoa wa Dodoma, watakaowakilisha Mkoa wa Dodoma katika mashindano ya Taifa ya *Safari Lager Pool Table Taifa* huko Mbeya mwezi wa nane; wanaongozwa na Mwenyekiti huyo Fred Mushi. Naomba na timu yake yote wasimame. Ahsante sana. Nawatakia kheri huko mnakokwenda, mkafanye mambo yenu vizuri. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Balazi Dkt. Getrude Mongella, ambao ni Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Kagunguli na Mwenyekiti Serikali ya Kijiji cha Butulu, Butiama. Naomba wasimame hapo walipo. Mzee Mongella mwenyewe bahati mbaya ameomba asiwepo. Mzee Stephen Mongella yupo? Yupo Dodoma hayupo humu ndani.

Tuna wanafunzi 40 na walimu wao kutoka Shule ya Sekondari Nkuhungu Dodoma. Walimu na wanafunzi wapo wapi? Simameni mlipo. Ahsante, nafikiri wengine wamekosa nafasi wataingia mchana humu ndani. Wanafunzi 50 na walimu wao kutoka Shule ya Sekondari Kikuyu Dodoma. Walipo wasimame na kama hawapo, wako kule nyuma na wengine watapata nafasi baadaye.

Wanafunzi 43 kutoka Bahi Shule ya Msingi, Mwitikira B wako wapi? Ahaa! Simameni; wengine wako huku na wengine wako kule. Tuna wanafunzi 30 kutoka Shule ya Msingi Mnadani, nafikiri Dodoma, kama wamekosa nafasi wataingia baadaye. Wanafunzi 30 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), naomba wasimame kama wapo, kama hawapo watakuja baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, nina wageni wa Mheshimiwa Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ambao ni Bwana Abubakar Gati, Katibu wa CCM wa Wilaya, yuko wapi sijui? Yupo Ndugu Iramba, Katibu Mwenezi, yupo George Katangasa, Katibu wa Mbunge, wako Madiwani watano wa Viti Maalum sijui wako wapi? Wako Makatibu Kata 11 wa CCM wa huko kwao. Wako Makada saba wa CCM; wasimame walipo. Kwa hiyo, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo ya kazi. Wageni wote mnakaribishwa kama mnavyoona Ukumbi wetu hautoshi, lakini tutajitahidi kufanya utaratibu ili wengine hasa watoto washiriki kidogo na wenzao waingie. Wote wanakaribishwa na ninyi nyote mnakaribishwa, hata kama hatukuwataja kwa majina.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Abdisalaam Khatib, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 5 asubuhi, kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika Chumba Na. 219 saa tano. Naona Ndugu Abdisalaam kuna matangazo mawili? *Okay!* Hili la jana.

Halafu nilitangaza jana Kamati ya Uongozi ya Bunge, kwa maana Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge, kutakuwa na Kikao leo saa saba mchana kwenye Chumba cha Mikutano cha Spika. Ofisi pia inatangaza kwamba, katika Viwanja vya Maonesho vya Bunge kuna maonesho yafuatayo:-

Machapisho ya Chuo Kikuu cha Mzumbe, Machapisho ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Machapisho ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, halafu kompyuta za kisasa, wote mnaalikwa kutembelea maeneo hayo na mkafanye kile kinachofaa wakati huu.

Waheshimiwa Wabunge, tunao muda mchache leo, tuna wachangiaji ningetamani wawe wengi zaidi lakini muda hautoshi. Kwa hiyo, kwanza, leo tutaendelea, tutajitahidi mpaka jioni kadiri inavyowezekana. Katibu kwa Shughuli za leo.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Atakayeanza kuchangia leo ni Mheshimiwa Charles Keenja, atafuatia Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Dkt. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa Alhaj Dkt. Juma Ngasongwa. Mheshimiwa Charles Keenja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja hii muhimu na nianze kwa kusema tangu mwanzo kwamba, naiunga mkono kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwanza, kwa kazi nzuri anayofanya na kwa hotuba iliyoandaliwa vizuri sana. Nampongeza pia Naibu wake, Katibu Mkuu aliyebobea katika masuala ya Ushirika na Naibu aliyebobea katika masuala ya kilimo, kwa kazi nzuri wanazoendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Wizara ambayo ina wataalam waliobobea kielimu, waliobobea kiuzoefu na kwa kujituma na ukiangalia mambo yao utaona yameandaliwa kitaalamu. Tatizo linalonitia wasiwasi ni kwamba, wengi wa wataalam hawa wamekaribia kustaafu, baadhi wameshastafu na wengine wameondoka kwenye shughuli za kilimo kwa sababu mbalimbali. Wizara inapaswa kuchukua hatua za haraka sana, kuhakikisha kwamba, inaandaa utaratibu wa kujaza mapengo yanayobaki katika Wizara kutokana na kustaafu kwa watumishi hao. *(Makofi)*

Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, ilipata nafasi ya kutembelea baadhi ya Vituo vya Utafiti na tulikuta matatizo matatu. La kwanza ni hili la kustaafu kwa watumishi na kwa hiyo, kuacha mapengo makubwa ambayo hayajajazwa. La pili, ni mishahara



midogo ambayo inawakatisha tamaa na wengine kulazimika kuhama nchi kwenda kufanya kazi kwenye maeneo yenye maslahi mazuri zaidi. Tatu ni mazingira ambayo yamechoka sana na kule ambako yameshafanyiwa matengenezo kukosekana kwa vifaa muhimu vya kufanyia kazi. Hili linahusu sekta yote ya Kilimo na nafikiri Mawaziri wanaohusika, wangechukua hatua kuhakikisha kwamba, mazingira haya yanarekebishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ni Kituo cha Utaalam. Pale ndipo tunapotarajia tukute wataalamu wenye elimu ya juu kabisa, tukute wataalamu wenye ujuzi na uzoefu na inachukua muda kuandaa wataalamu hawa. Inahitaji kufanya kila linalowezekana, kuhakikisha kila wanapoandaliwa wanabaki ama sivyo Taifa litakuwa linapoteza rasilimali muhimu sana. Nawapongeza sana Watumishi wa Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana wakulima wa nchi hii, ambao ndio wanaozalisha asilimia zaidi ya 90 ya chakula tunachokula. Hata vyakula tunavyoagiza kutoka nje, tungeweza kuvizalisha huku nchini kama tungeweka mipango mizuri ya kuvizalisha. Wakulima wetu wadogo wanaotumia jembe la mkono, wanaotumia nguvu nyingi sana kulima na utaalam mdogo sana, wanalilisha Taifa hili, wanahakikisha kwamba wanatoa mchango mkubwa wa asilimia 26 katika Pato la Taifa, asilimia 26 ya pesa za kigeni na malighafi tunazotumia katika viwanda vyetu. Nawapongeza wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tufike mahali tumsaidie mkulima huyu. Kwa sababu hawa wakulima ambao ni asilimia 70 ya Watanzania, ndiyo walio masakini kuliko Watanzania wengine wote. Wanafanya kazi kubwa, wanazalisha sana, wanatulisha, wanatupatia pesa za kigeni na kuusimamia uchumi huu, lakini hali zao ni duni sana. Kwa hiyo, ni lazima Serikali na Taifa kwa ujumla, tuchukue hatua za kuhakikisha kwamba, wakulima hawa hali zao zinainuka, wanakuwa na hali bora zaidi kuliko walizo nazo. *(Makofi)*

Wengi sana wanajiita wakulima lakini ni wachache sana ambao wako tayari kwenda kushiriki katika kilimo hiki. Tumewaachia wanawake, tumewaachia Wazee, ndiyo wakulima wetu wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuchukue hatua tuhakikishe tunawasaidia na hatua ya kwanza ni kuhakikisha kwamba, wana ardhi ya kutosha. Hofu yetu kubwa tunapozungumza juu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kwamba, watakuja watu hapa wakachukua ardhi, wakafanya watakavyofanya wakatuacha sisi barabarani, lakini hatuhakikishi kwamba kila mkulima ana ardhi ya kutosha kwa mahitaji yake. Hekta tuseme tano ambazo ni sawa sawa na eka 12 ili kuhakikisha kwamba, anaweza sasa akazalisha kibiashara na siyo kujikimu tu na hili ni muhimu sana, tuhakikishe mapema iwezekanavyo kwamba linafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida walichukua hatua za kuhakikisha kwamba, wanapima mashamba ya watu wao na wakagundua kwamba kuna wananchi

walikuwa na ardhi kidogo na wengine hawana kabisa. Sasa ni lazima tuchukue hatua kama hawa wananchi ni wakulima basi wawe na ardhi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wapate mafunzo ya kilimo bora, sidhani kama ni cha kisasa. Kilimo bora, tuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Vyuo vya Kilimo, vya Mifugo, tuna Shule za Msingi kila Kijiji, hatuna sababu ya kutokuwapa wakulima hawa mafunzo ya moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, tuhakikishe wanapata mahitaji yao na wanayapata kwa wakati. Tumekuwa na tatizo kubwa sana la mbolea, lakini tukihakikisha kwamba, mkulima anapata mbolea yake kwa wakati, anapata mbegu bora za kutosha na kwa wakati, hali yake ya uzalishaji itainuka na umaskini wake utakuwa umepungua kwa kiasi kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengine ambayo hatupaswi kufanya. Kuna siku moja nilikwenda dukani nikakuta kuku kutoka Brazil wanauzwa Tanzania na huyo mtu anayeuzwa anapata faida. Ni jambo la ajabu sana. Ukienda katika maduka yote haya yanayouza, wanayaita *groceries*, utakuta mpaka mboga za majani zinaagizwa kutoka nje ya nchi. Lazima tulinde soko la ndani kwa ajili ya wakulima wetu kama tunavyolinda viwanda vyetu, ndivyo tunavyopaswa kulinda soko la ndani kwa ajili ya faida ya wakulima wetu na uchumi wetu. Hatuwezi kuendelea kuagiza kila kitu kutoka nje na kuvijaza katika mashelfu yetu halafu tukauziana hapa, tukasema kwamba, sasa uchumi wetu unakua; utakuwa vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia katika eneo hili ni suala la kuhakikisha kwamba, wakulima wana vivutio vya kuwafanya wapende kulima, vya kuwafanya Wabunge hawa wachukue mashamba walime. Kuwafanya wafanyabiashara wachukue mashamba walime. Kama kuna vivutio vinavyohitajika, basi vipatikane ili kuwafanya watu hawa waweze kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na kaulimbiu nyingi. Hatujawahi kuwa na upungufu wa kaulimbiu hata siku moja. Zote zinasifu kilimo, zinaeleza umuhimu wa kilimo katika uchumi wetu. Tulipokuwa na Siasa ni Kilimo tulichukua hatua za Viongozi wote kuimba kilimo na kilimo chetu nina hakika, kiliendelea vizuri. Baada ya hapo, tukaendelea kuita Kilimo ni Uti wa Mgogo, sijui kilimo cha kufanya nini. Hakuna mtu aliyetoka tena kwenda kuhimiza kilimo. Tuliishia kuimba na sasa tuko kwenye kaulimbiu mpya inayoitwa Kilimo Kwanza. Nashauri kwamba, tufanye makusudi kabisa ya kuandaa Programu za Kutekeleza hicho (Kilimo Kwanza); ili kuhakikisha kwamba, kilimo sasa kinachukua nafasi hiyo ya kwanza katika uchumi wetu, kinakua, kinazalisha kwa wingi, tunauza nje na tunapata ziada ya kuwekeza katika Sekta nyingine za Uchumi. Ndiyo iwe kweli kwanza. Katika nchi zote duniani, kilimo kilikua kwanza ndiyo kikawezesha Sekta nyingine kukua. Tanzania kilimo chetu kimedumaa. Tuliambiwa hapa kwamba, tunatarajia kahawa itazalishwa tani 50,000 kwa mwaka huu. Ukirudi nyuma miaka 30 utakuta ni hizo hizo tani 50,000, hazijawahi kuongezeka. Ukienda kwenye chai ni tani hizo hizo 10,000 haziongezeki. Mkonge kidogo naona kama unataka kuinuka, kutokana na wakulima wadogo kushiriki.

Ukiangalia kilimo chetu kimedumaa hakikui. Kwa hiyo ni lazima turudi sasa tuhakikishe kwamba, tunaandaa Programu ya kukiwezesha kilimo hiki kukua kumwezesha mkulima mdogo azalishe kwa wingi sana. Kuwezesha wawekezaji wakubwa waingie katika kilimo ili kilimo kiweze kukua. Mambo tunayofanya, yanaelekea kupingana na malengo yetu. Tulikuwa na viwanda vya mbolea. Hakuna hata kimoja kinachofanya kazi isipokuwa hiki cha Minjingu; cha Tanga kilishakufa siku nyingi hata kilikozikwa hatujui. (*Makofi*)

Tulikuwa na viwanda vya kuzalisha zana za kilimo, pale UFI kwenye Jimbo langu la Ubungo na Mbeya. Vile viwanda vilishafungwa siku nyingi. Tunaagiza hata kisu cha kukata nyama kutoka Uchina, hatuna tunachozalisha humu ndani lakini tunasema Kilimo Kwanza. Kilimo Kwanza bila kuweka misingi ya kuki-*support* hakitakuwepo. Tutakuwa tunapiga maneno tu hapa. Kwa hiyo, lazima turudi tufufue viwanda vya kuzalisha zana za kilimo. Rais wa Awamu ya Tatu, alitembelea South Korea; wa South Korea wakakubali kuja kujenga matrekta madogo madogo haya ya *power tiller*, hapa nchini na wakaleta timu kuja kuangalia uwezekano wa kufanya hivyo. Wakaondoka hatukufuatilia. Sasa ni wakati wa kufuatilia South Korea waje kutujengea kiwanda cha *power tillers* zizalishwe hapa hapa halafu ndiyo tuzisambaze. (*Makofi*)

Hili lengo aliloagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu la *power tillers* 50 kwa kila Wilaya, zingetoka kwenye viwanda vyetu wenyewe. Pamoja na viwanda hivi vya kutengeneza *power tiller* na majembe na kadhalika. Nirudie kusema kwamba, jembe la mkono ndilo limetufikisha hapa tulipo na tutaendelea kulihitaji. Sioni kama itafika siku kila mtu atalima kwa *power tiller* au trekta; hatuwezi. Singida wamejitahidi sana, asilimia kubwa sana wanalima kwa plau na ukienda vile vile Bariadi unakuta karibu asilimia 100 wanalima kwa matrekta na plau. Nawapongeza sana, lakini bado jembe la mkono litashirikiana na hivi vyombo vingine kulima.

Tuongeze juhudi kuhakikisha kwamba, tunaendelea kufanikiwa. Tujenge viwanda vya mbolea humu humu nchini, kwa sababu tuna malighafi ya kutengenezea mbolea. Tuna gesi na tunaambiwa kwamba, pale Mkuranga imekuwa gesi nyingine nyingi kabisa, acha ile tuliyoikuta katika maeneo mengine mawili. Tutumie rasilimali zetu tuzalishe mbolea kwa wingi, kuhakikisha inapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu kwa mkulima wetu ili kilimo hiki kiweze kukua. Sijui ni nini kinachotucheleweshwa, maana tunapeana taarifa tu kwamba, kuna watu wanataka kuja kuwekeza. Safari yao imekuwa ndefu mno, ifupishwe waje mapema wakajenge viwanda hivi ili vituwezeshe kutekeleza majukumu haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze sana Serikali kwa hatua ambayo inachukua ya kuhakikisha kwamba, wakulima wanapata mbolea kwa ruzuku ili kupunguza bei. Baadhi ya mbolea zimepanda kiasi kwamba, mkulima sasa hawezi tena kuzimudu. *DAP* naambiwa ni shilingi zaidi ya laki moja. Huyu mkulima atakayeweza kununua mfuko mmoja wa kilo 50 wa *DAP* kwa shilingi laki moja na kwa heka ngapi sasa. Ni matatizo kabisa. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali, tunaipongeza kwa kuongeza hii ruzuku. Utaratibu wa vocha, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, ambaye

amezunguka nchi nzima akiutangaza utaratibu huu. Bado una upungufu na huo upungufu uondolewe ili uweze kwenda vizuri zaidi. Baadhi ya wakulima wanaopata hizi vocha wanaziua, wanapata pesa kidogo wanakwenda kilabuni wanakunywa pombe. Kilimo hakiwezi kukua kwa kunywa pombe. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mianya inayovuruga huu utaratibu mzuri irekebishwe ili tufike mahali tuhakikishe kwamba, mkulima huyu anapata mahitaji yake ya pembejeo, anazitumia vizuri, anaongeza uzalishaji na anainua ubora wa maisha yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni hili la kuagiza mashine kutoka nje ili tupunguze kutumia nguvu za mwanadamu kulima na wanadamu tunapotumia nguvu zetu, tunatumia nguvu za wanawake na nguvu za wazee kama mimi. Naipongeza sana Serikali, lakini sasa tuhakikishe kwamba, tunaanzisha vituo kwa ajili ya matrekta haya, siyo lazima viwe vya Serikali, vinaweza kuwa ni vituo vya watu binafsi waliokopa wakaweka matrekta haya kwa wingi, wakaweka na mbegu, kukawa na utaalumu katika Kituo hicho. Kwa hiyo, mkulima anayehitaji utaalum anakwenda mahali pamoja, anapata kila anachohitaji ili kurahisisha kilimo chake. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana na tukajifunze kule Sumbawanga ambako tayari wameshapiga hatua kubwa sana ya maksai ili kuangalia wanaendeshaje utaratibu wao kule na huko kwingine. Tuige tuweze kuendesha utaratibu kama huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo chetu kinaweza kikakua kama tukichukua hatua sahihi, kama tukipunguza maneno tukaongeza vitendo. Kama tukisimamia wote kilimo hiki, kila Kiongozi ikawa kazi yake ya kwanza ni kusimamia kilimo, kitakua. Hata wananchi wanaokaa mijini, ungewauliza ungeweza kuwapa mashamba wangetoka wakalime. Lazima tuandae mipango ya kuwawezesha wakulima.

Kwa hayo machache, naunga mkono hoja na nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya ajiandae na Mheshimiwa Paul Kimiti.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Wasira, kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuendeleza kilimo. Naomba nimpongeze pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, wakiwemo Wataalam wa Ugani walioko katika Vijiji wanaofanya kazi na niwapongeze wakulima wetu na hasa wanawake wanaolima chakula kuhakikisha Tanzania hii inapata chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri aliyofanya ya kuhakikisha kwamba, mikoa ile mitano iliyochaguliwa ya

kuboresha kilimo inabadilishana uzoefu. Mikoa hii ikiwemo Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Kigoma na kuweza kuhakikisha kwamba, wataalamu wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge pia wanashirikishwa kikamilifu. Nampongeza sana kwa kazi hiyo ambayo ameifanya na kazi nyingine ambazo anaendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niipongeze serikali kwa kuwa na wazo ambalo tumelizungumzia la kuwa na Mfuko au kuwa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Nililizungumza hili katika hotuba yangu niliyochangia Wizara hii katika mwaka 2007 na ninashukuru kwamba, Wizara inalifanyia kazi lakini linachukua muda mrefu mno, mazao haya hayatiliwi umuhimu na ninaendelea kuisisitiza; ninaomba iletwe kabla ya mwaka huu kwisha kwa sababu tunalima mazao mengi. Kilimo cha choroko kiko wapi? Ukienda nchi za wenzetu hata ukienda hotelini wanapika chakula kinachotokana na choroko. Choroko zetu ziko wapi? Kunde zetu ziko wapi? Njugu zetu ziko wapi? Ni nani anayeyazungumzia mazao haya ambayo yanaonekana kusahaulika? Tuna mazao mengi ambayo yangeweza kutuondolea umaskini, lakini hayatiliwi umuhimu kwa sababu hakuna chombo ambacho kinayazungumzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafikiri kama tutakuwa tumesisitiza hili na kuhakikisha kwamba, tunakuwa na hii Bodi, ifanye kazi ihakikishe kwamba mazao haya yanatiliwa umuhimu. Hivi sisi wanapokuja wageni, nikiangalia naona vyakula vingi vinavyopikwa hotelini ni vyakula vile visivyokuwa vya asili. Utamaduni wa Mtanzania unatakiwa uhimizwe, tupike vyakula ambavyo ni vya asili yetu. Ninashukuru Bunge hili kwamba, tunaweza pia kula viazi na mihogo, hivyo ndio vyakula vya asili tunavyohitaji kuvipata. Ninaomba na sisi Mkoa wa Iringa, tuwe na soko la mazao pale Makambako kama ilivyo Kibaigwa. Iwe ni *centre* ya mazao ambapo tunaweza kuuza mazao yetu kama ilivyo Kibaigwa, Mkoani Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie tena suala la pembejeo. Pembejeo ni muhimu sana kwa kilimo na Mkoa kama wa Iringa, ambao unazalisha kwa wingi, ulitakiwa upate pembejeo hizi zaidi ya mikoa mingine kwa sababu ya mazao tunayozalisha, kwa mfano, tunazalisha mahindi, ndio hayo hayo yanayotumika kwa chakula na pia yanatumika kwa biashara. Zao la viazi mviringo, halijapewa umuhimu wa kuhakikisha kwamba, tunapewa pembejeo hizi. Ningependa kuiomba Serikali na nina uhakika Mheshimiwa Waziri ni msikivu sana na ataweza kuhakikisha kwamba, pembejeo hizi zinaongezwa. Ninapongeza mfumo wa vocha na pia pembejeo hizi zitolewe mapema. Kwa mfano, Wilaya ya Makete, sasa ni karibu wanaandaa kilimo, mbolea inapotolewa tayari walishapanda, inakuwa haina maana. Mbolea au pembejeo za kilimo zierendane na msimu wa maeneo yanayohusika ili kuhakikisha kwamba, zinatumiwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie suala la utalamu wa kilimo. Ninajua kabisa kwamba, utalamu ni muhimu sana, wataalamu wanasomeshwa vyuoni lakini ninaomba hili pia lichukuliwe kama ni dharura kama tunavyochukua masuala mengine kuboresha maslahi yao.

Wataalamu wanaosoma kilimo wengi hawakubali kwenda kuwa wataalamu vijijini, kwa sababu mazingira ni magumu, hawana nyumba, hawana vitendea kazi, matokeo yake wanabadilisha fani wanakwenda kwenye fani nyingine. Kama tunataka hawa wataalamu waweze kufanya kazi vizuri wawahudumie wakulima, tuwajengee mazingira bora; Kilimo Kwanza kitakuja kwa kuboresha wataalamu. Wataalamu wapende kwenda vijijini, hawatapenda kwenda vijijini kama huduma muhimu hazipo; hana nyumba atakwenda kuishi wapi? Hana hata chombo cha usafiri na tukizingatia kwamba kazi yake ni ya kutembelea mashamba, atakwendaje wakati wa mvua? Kwa hiyo ni muhimu sana tuboreshe. Wengine wamepewa pikipiki, lakini mafuta wanaweka wao wenyewe; hivi ni kweli jamani? Mshahara mdogo huu anaopata ndio atumie pia na kuweka mafuta kwenye pikipiki? Mheshimiwa Waziri, hebu tufikirie hayo kwanza na hatutaboresha kilimo kama hatutafikiria masilahi ya watumishi wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upatikanaji wa pembejeo nimeshalizungumzia, lakini ninapenda pia hizi pembejeo ziweze kuwafikia wakulima wakiwemo wanawake. Kuna Mfuko wa Pembejeo, napenda nikuombe Mheshimiwa Waziri, huo Mfuko utoe mikopo kwa SACCOS za wanawake ili waweze kufikiwa wanawake wengi zaidi. SACCOS za wanawake kama SACCOS ya Wanawake wa Iringa Mjini, SACCOS ya Wanawake wa Iringa Vijiji, SACCOS ya Wanawake Kilolo, SACCOS ya Wanawake Makambako, SACCOS ya Wanawake Ulembwe, SACCOS ya Wanawake Makoga na SACCOS nyingine za Wanawake nchini ili tuhakikishe kwamba, na wao wanaondokana na jembe la mkono. Tunaomba tupewe pembejeo za kilimo na nina uhakika kwamba, Mkoa wa Iringa utakuwa wa kwanza kwa Mfuko wa Pembejeo kwenda kuangalia hizi SACCOS za Wanawake na kuwapa pembejeo za kilimo ikiwemo na matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kwa vijana. Vijana ni wengi na kama wenzangu walivyokwishachangia, mzigo wa kilimo wameachiwa wanawake na wazee. Vijana wengi hawawezi kuingia kwenye kilimo mpaka tuweke utaratibu mzuri. Ninakumbuka zamani kulikuwa na shule za kilimo, hivi zimekwenda wapi hizi shule? Wanafunzi walikuwa wanafundishwa tokea wanapokwenda sekondari, wanasema anakwenda kwenye shule ya kilimo, zikiwemo shule nyingine kama Ruvu, nazijua zilikuwa nyingi; hivi huu utaratibu umekwenda wapi? Nilikuwa ninaomba huo utaratibu ufufuliwe, stadi za maisha ambazo vijana wanafundishwa ziwe pamoja na stadi za maisha za kujikita katika kilimo na kilimo ambacho ni bora; walime kwa utalaamu. Ningependa kushauri kwamba, wanafunzi wanaofikia kumaliza darasa la saba, kabla hawajamaliza waelimishwe na wafundishwe kuhusu kilimo na pia wapewe nyenzo; sio kupewa mafunzo tu, hivi wataanzia wapi; mitaji iko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vikundi vya vijana viundwe, lakini wafundishwe kukipenda kilimo toka wakiwa shule ya msingi ili wanapomaliza kama wataendelea basi wawe wanapenda kilimo. Kilimo kinachukiwa na watu wengi hasa vijana, kwa sababu wanaona kilimo cha wazazi wao kila siku ni kilekile cha mkono. Kwa hiyo, hakuna mtu atakayependa kuingia kwenye fani ya kilimo na ukizingatia kwamba wote, karibu robo tatu, tumezaliwa na wakulima, lakini kwa sababu kile kilimo hakina tija, watu hawapendi kuingia kwenye kilimo mpaka tutakapoboresha masilahi ya kilimo na kuhakikisha kwamba, watoto wetu wanapenda kilimo. Kwa maana hiyo ni kwamba,

akitoka pale, akipewa mafunzo, apewe na nyenzo za kufanyia kazi. Vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa, wafundishwe kutokana na mazingira wanayotoka.

Kama anatoka Mkoa wa Iringa, afundishwe mazao yale yanayopatikana kwenye ule Mkoa na kuoneshwa ni mahali gani anapoweza kupata mtaji wa kuanza kufanya biashara na hasa kujikita kwenye kilimo na kuhakikisha kwamba, anapata soko la kuweza kuuza mazao yake kwa sababu saa nyingine analima lakini mahali pa kuuza mazao hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakika wa chakula majumbani; mwaka jana nilipochangia Wizara hii, niliomba nikasema tuwaangalie wazee huko vijijini; hawa wazee wanalea watoto yatima na wenye mazingira magumu. Wana mzigo wa kulea, lakini pia wana mzigo wa kutafuta chakula. Hivi Serikali jamani haiwezi kufanya mpango wale wote wenye shida wakapembua ni familia ngapi za wazee hazina chakula na kuhakikisha kwamba wanapewa chakula? Wana mzigo wa kulea, hawapewi chochote na bado wana mzigo wa kutafuta chakula. Matokeo yake hawa watoto wanasoma mara mbili au mara tatu kwa wiki, siku nyingine wanahangaika kutafuta chakula. Mheshimiwa Waziri, ukimaliza Bunge nakuomba tuongozane nikakuoneshe watoto wanavyopata shida; chakula hawana halafu hatuwaangalii, hebu tuboreshe tuhakikishe kwamba, kunakuwa na chakula mashuleni. Wilaya kama ya Makete, Wilaya kama ya Ludewa, Wilaya ya Njombe na Wilaya ya Iringa Vijijini, tumeshaona tatizo hili limeshajitokeza. Matatizo ni makubwa, tuhakikishe kwamba watoto wanapewa chakula; kwa nini chakula hakitolewi mashuleni? Kwa nini mikoa michahce tu imechaguliwa kutoa chakula mashuleni, watoto wanahangaika?

Mimi ninaomba hili lilitiwe umuhimu, wazee wapewe chakula, mikoa iangalie ni familia ngapi zinazoongozwa na wazee, zinaongozwa na watoto. Wakuu wa kaya, wapewe chakula cha kutosha kwa mwaka mzima na pia ili kupunguza tatizo, kiwepo chakula mashuleni kwenye mikoa au wilaya zenye matatizo na tukizingatia kwamba, Mkoa wa Iringa una tatizo kubwa la maambukizi makubwa ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha chai ni muhimu sana na tunawapongeza wakulima, wakiwemo wakulima wa Jimbo lako, kwa juhudi kubwa wanazofanya za kuhakikisha kwamba, kilimo cha chai kinaboreshwa na wakulima wote wa Mkoa wa Iringa. Kilimo hiki kitaboreshwa tu kwa kuhakikisha pembejeo zinapatikana na wataalamu wa kutosha. Hivi tutaongezaje mazao kama pembejeo za uhakika hazipo? Hivi tutakuwaje na mazao ya kuzalisha kwa wingi kama nilivyosema wataalamu hawapo? Mikoa hii iangaliwe; na maeneo yote haya ambayo yanahimiza kilimo cha kahawa au kilimo cha chai na kuhakikisha kwamba, wanapata soko na mahali pa kuuzia chai yao ikiwemo kujenga viwanda karibu na eneo la kiwanda chao au eneo la mazao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kilimo ambacho kinalimwa kwenye maeneo ya miji. Kwa mfano, tumekuta maeneo mengine wakulima wanalima, kwa mfano, Mijini au Manispaa, wanapolima hawakuambiwa halafu baadaye mazao yao yanakuja kung'olewa na hii inaleta kero kubwa sana kwa wananchi. Tuangalie yale

maeneo hata kama ni Manispaa, yaliyokaa pembezoni ambako hakujawahi kufikiwa, yaani sio katikati ya mji, waruhusiwe kulima kwa sababu wengine ni wazee, hawana uwezo wa kwenda kulima nje ya mji. Kwa hiyo, wale wanaolima pembezoni, waruhusiwe walime mazao yao ili waweze kuvuna; isipokuwa katikati ya mji. Hili limekuwa ni kero kubwa kwa watu hasa mazao yao yanapokatwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha zao la mihogo kwa nchi za wenzetu ni zao kubwa na linaleta pesa nyingi za kigeni. Sisi tuna maeneo ambayo yanavumilia ukame na zao hili linavumilia ukame. Kwa nini zao hili halihimizwi likalimwa katika sehemu nyingi na likaweza kuwakomboa wakulima ili wapate fedha? Tunaangalia mazao mengine na haya ndio niliyosema mazao ya asili, nafikiri Bodi hiyo itakapokuwa imeundwa ndio itakayotatua matatizo yote haya, ikiwemo kilimo cha zao la mihogo, ambalo ni zao kubwa, ambalo nchi za wenzetu wamefaidika nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. DKT. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mawazo yangu kuhusu hoja iliyowasilishwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Kwanza, ningependa kumpongeza yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalamu wa Wizara, kwa hotuba nzuri waliyoileta. Pia ninataka niseme kuwa mimi binafsi, ninamfahamu Mheshimiwa Stephen Wasira, kazi hii aliyopewa hata yeye mwenyewe anaipenda na nina hakika ndio maana anafanya vizuri na tunamtakia kila la heri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, ningependa kusema mambo yafuatayo: La kwanza, katika kitabu hiki ambacho Waziri ametoa, kurasa za 46 na 47, kuna jedwali linaloonesha takwimu za mazao ya mbegu za kutengeneza mafuta ya kula. Kwa leo nitapenda tuwe tunajiuliza, hivi kwa mfano kama tukitaka kujitosheleza kwa mafuta ya chakula kutokana na kulima mbegu ni nani mwenye jukumu la kufanya hiyo kazi maana inawezekana hatuna mwenyewe, ndio maana kila siku tuna takwimu? Tujiulize hivi mwenyewe hasa ni nani kwa sababu kilio na mwenyewe kama kilio hakina mwenyewe watu wengine wataliaje? Ninataka tujiulize na Waziri mwenyewe atakaposimama kujibu, ninataka tusaaidiane tuulizane ni nani mwenye jukumu kwa sababu kilimo chetu tumeachia wakulima wadogo tu, wanahangaika wenyewe wakipenda? Kwa hiyo ni lazima Serikali yetu, Mikoja na Wizara, tukubaliane kuwa na mpango unaofanana ili kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi natoa ushauri kwamba, tujiwekee miaka mitano ijayo, Tanzania ijitosheleze kwa mbegu za mafuta na kujitosheleza kwa mafuta ya kula na kuuza ziada nje ya nchi. Mimi nakusudia Bunge lijalo kuleta hoja kuhusu suala la mafuta, kwa sababu hata kule Wizara ya Fedha, niliuliza mtakapokuwa mnaleta Sheria ya kuondoa 10% ya ushuru wa kodi ya mafuta mtaandika nini maana duniani; Malaysia na Indonesia, hakuna *crude oil*? Hivi hasa mnapoweka kwenye vitabu mnaotoa wapi hiyo *crude oil* na ninyi hamuilimi wanaolima hawana *crude oil*?



Pili, hoja yangu itahusu kuwepo mipango ya wenye viwanda wanaosindika mafuta, waingie mikataba ya kulima mbegu za mafuta na mikoa. Mkoa wa Pwani, Morogoro na Kigoma na Rukwa, kwa pamoja ukiichanganya eneo la kulima mbegu za mafuta ya mawese ni kubwa kuliko Malaysia tunakoagiza mafuta. Pili, wenzetu wa Zambia, wamechagua kampuni inaitwa ZAMBEF, wamewapa eneo wameanza kulima na wana mpango wa kulima hekta 25,000 za michikichi. Uganda vivyo hivyo. Sasa hawa watu wetu wanaong'ang'ania kuendelea kuagiza mafuta wanaita *crude oil*, tutafanya hivi mpaka lini; kwa nini hatujitegemei? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, alisema kwamba, Kenya wanasema ninyi Tanzania, mna eneo kubwa la kuweza kulima mbegu za mafuta na mkatuuzia; mbona hatulimi? Mimi najua Serikali haiwezi kulima, lakini ni lazima tuwe na mpango wa kujitosheleza katika mbegu za mafuta ya kula. Kwa hiyo, ninajiandaa nitakuja na takwimu na nitasema ni fedha ngapi ambazo Serikali itaingiza kwa hao tuliowasamehe mafuta ambazo wangetumia kuwekeza kwenye kilimo cha mafuta, ndivyo inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka tunaimba kusindika mazao tunayolima, pamba kwa mfano. Wakoloni waliondoka wakatuachia pamba na sisi sote tunaendelea kulima pamba, bei ya pamba imeshuka imebidi Serikali ilipe fidia. Leo hii kuna viwanda Dar es Salaam, vinavyotengeneza nguo, wanaagiza *grey sheeting* kutoka nje kisha wanaweka rangi na kutengeneza kanga. Sisi tunaendelea kuuza pamba nje, kwa nini hatusemi kwamba kuanzia sasa mpaka mwaka fulani viwanda vyetu vijengwe vya kutoa nyuzi? Suala hili ni kuamua, kama hatuamui haitawezekana.

Wanaokuja kujenga viwanda watajenga wanavyotaka wao, vinavyowapa faida haraka. Sasa hivi watu wenye viwanda ambao mnaweza kusema wanasindika mazao yetu ni Morogoro hapa, kumejengwa kiwanda kizuri wanasindika *juice* kutokana na mananasi. Nao wameingia mikataba na wakulima na wanawafundisha namna ya kununua mananasi, wengine kufuata mfano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili iliyopita, nilikuja hapa na matunda, *juice* za bandia na *juice* za *chemicals* nilikuja nazo humu. Leo nchi yetu watu wetu wanakunywa *juice* bandia wanaweka rangi tu; kwa nini tunaruhusu mambo haya? Mambo haya hayatakiwi; lazima tuyazuwue kwa kuwa na mpango wa kutengeneza *juice* ya matunda, sio kwa kusema. Tunasema kutoka sasa mpaka mwaka fulani, nchi ijitosheleze kwa jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri wanamsaidia Rais, Rais anatembea sana Tanzania anaijua; Waziri Mkuu; na Mawaziri wanajitahidi, lakini baadhi ya Makatibu Wakuu wa Serikali wanaijua Uingereza kuliko Rukwa na ndio wanaiendesha Serikali hawa; na ndio wanaowashauri Mawaziri! Sasa itawezekanaje kama hawatembelei Mikoa? Haya ninayoyaeleza ni kweli, haifai Watendaji Wakuu kuijua nchi yao kwa kuisoma kwenye ramani. Kwa hiyo, mipango itakuwa ya kusoma kwenye ramani nchi itakwendaje? Mawaziri wenyewe wakienda mikoani, wanakwenda peke yao na Makatibu wao, wanawaacha Makatibu Wakuu Wizarani, wakirudi ndio wanamwambia mshauri

wake. Kwa nini hamuwaambii mwende nao mikoani? Tusaidieni kuwashirikisha kwenda mikoani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuseme ukweli; kazi ya kulisha watu sio ya mkulima ni ya Serikali. Mwaka huu Rukwa tutakuwa na ziada. Serikali kama wameweka kununua tani 22,000, wakishazinunua nyingine wawaachie wakulima wauze wanakotaka; kwa nini wanazuiwa? Mahindi ya Rukwa hayawezi kuja Dar es Salaam, kulisafirisha gunia kutoka Mbozi na Rukwa haiwezekani, gunia moja ni shilingi 10,000 utnauzi kwa shilingi ngapi? Ninachosema hapa, turuhusu biashara halali, tuzuwie za magendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokwenda Kigoma, Wabunge wa Kigoma ni mashahidi; Rais alinituma akasema kaondoe magendo, nikakaa miezi mitatu nikarudi; nikasema Mheshimiwa Rais, magendo ya Kigoma yana umri mkubwa kuliko mimi, nipe muda. Nikahalalisha biashara na tulifanya biashara kubwa kweli. Tulilingizilia Taifa *USD 17 Million* kwa mwaka. Sasa ninachosema, Serikali ituruhusu tuuze mahindi kokote, lakini halali, hizo fedha za kigeni ndio zitumike kuagiza mahindi kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sumbawanga kuna Mtanzania amejenga kiwanda cha kusindika unga wa mahindi, amepata soko Zaire wamemkatalia kuuza unga. Waziri Mkuu, alipokea malalamiko hayo, mimi ninashauri mwenye kiwanda aruhusiwe kuuza unga na mahindi nje ya nchi. Kiwanda chake hakiwezi kushindana na viwanda vikubwa vya Dar es Salaam, ambavyo pia vinauzi mahindi nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mbolea, ninaishauri Serikali katika suala la Minjingu tusingumbe, tuendeleo ku-*campaign* itumike. Tutambue maeneo ambako inafaa itumike, kule ambako haifai tusingumbe. *TFC* miaka mitano iliyopita, walipata shida ya kuuza Minjingu, kwa mwaka mmoja walikuwa wanauza tani 100 tu.

Mwaka jana wameuza tani 5,000, kwa hiyo, imeanza kukubalika. Sisi tuna tatizo, kwa mfano, kama huu utaratibu uliowekwa sasa na Serikali wa kusema *DAP* na ile nyingine, vyote viwe sawa, baadaye tutauwa mbolea ya Minjingu na ndio mbaya kwa sababu vitu vyetu wenyewe hatuvisaidii. Tuendeleze elimu kwa mkulima, mambo mapya ni elimu, bidhaa zote duniani ni elimu na ndio maana watu wanafanya matangazo. Watu wanaotuzia simu na vocha mpaka leo wanaendelea kutangaza. Kila jambo ni matangazo, ni elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya maelezo haya, naomba niseme tena kwamba, nitajiandaa Bunge lijalo nilete hoja ya namna ya kujitegemea. Nchi ni kujitegemea. Ninakwenda kufanya hesabu nijue *juice* za rangi ni ngapi na za *chemicals* ni ngapi. Ninakwenda pia kufanya hesabu ya fedha zinazotumika kununua maua ya bandia kutoka nje; hatuwezi kuruhusu mambo haya, maua yamejaa chungu nzima, Bwana Mrema, mkulima wa maua. Unawezaje kuweka maua ya bandia nyumbani kwako ukaacha maua halali tulinyo Tanzania? Ninakwenda kufanya hesabu ni fedha ngapi zimetumika kuleta maua ya bandia kutoka Uchina ili tuje tuzungumze vizuri Taifa lijijandalie mikakati ya kujitegemea. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Hayo maua unamletea nani hizo hesabu? Utamletea nani hesabu hizo, maana hujaomba ruhusa kwamba unataka kuleta. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa namwita Mheshimiwa Paul Kimiti, atafuatiwa na Mheshimiwa Janguo.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie suala zima la kilimo katika maisha ya binadamu. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Kilimo, ambao wengi kwa bahati nzuri ninawafahamu, wachapa kazi. Tuna imani waliyotuletea tutajaribu kuyazingatia ili tuone tunayatekeleza namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nitumie nafasi ya awali kwa niaba ya Watu wote wa Mkoa wa Rukwa; kwanza, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa mambo yafuatayo: Kwanza kwa kutuhakikishia sisi Wana-Rukwa ya kwamba, kuanzia mwishoni mwa mwaka huu, barabara zetu za Mkoa wa Rukwa – Tunduma – Sumbawanga, Sumbawanga – Mpanda, zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Mimi nasema ninamshukuru sana, kwa sababu ndio ukombozi wa Wana-Rukwa katika uzalishaji wa chakula. Pia nimashukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla, kwa kutuongezea fedha kwa ajili ya pembejeo, hasa fedha za ruzuku zimeongezeka karibu maradufu. Mimi nasema, tunashukuru kwa hilo na pia kuongeza fedha za *ASDP* ambayo ndio ukombozi mkubwa sana wa mkulima mahali popote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani ya pekee ambayo ninataka niiongezee kidogo na Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya ameizungumzia ni jitihada za serikali katika kuondoa mahindi pale Sumbawanga, ambayo yalikuwa yamelundikana mpaka kujaa nje. Sisi tunaishukuru Serikali kwa sababu inatupa nafasi ya kuweza kuleta mazao mengine katika msimu huu unaokuja. Pili ni ajira kwa vijana wetu, pale mjini vijana wanapata ajira nzuri sana. Tatu ni uhakika kwamba, sasa tutapata nafasi ya kuanza kununua kutoka vijijini kuleta mjini. Ninasema ninashukuru sana kwa hilo kwa sababu ni mwanzo mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimwombe Mheshimiwa Waziri, mambo kadhaa ambayo ameyaeleza. Ninataka niwakumbushe Mheshimiwa Wabunge, mpango wa pili wa maendeleo ya miaka mitano kama mnakumbuka, ilikuwa ni 1969 – 1974 na mpango huo ulikazania zaidi suala zima la kilimo. Nyote kama ni mashahidi mnakumbuka, tulikuwa na wimbo ambao ulikuwa unaimbwa na Mzee Makongoro; “*Kuleni chakula bora cha kuujenga mwili na kujenga nyumba safi pa kulala pawe bora.*” Dira ilikuwepo; ni dira ambayo kila mmoja alikuwa anaiimba; tulikuwa na dira ambayo ndio ilifanya sasa kilimo kipambe moto na ndio kilichozaa Agizo la Iringa la 1972; ni mtiririko huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sijui Wizara ya Kilimo tuna nini? Sijui kuna mzimu gani pale? Mipango inakuja mizuri sana, lakini inakuwa haikai kwa muda mrefu.

Baya zaidi hata Mawaziri wake hawakai sana. Nitawapeni mfano; tangu Mzee Bryceson, Waziri wetu wa kwanza mwaka 1963, ambaye ndiyo alikaa muda mrefu, waliofuata wote hakuna aliyekaa zaidi ya miaka mitatu, isipokuwa Mheshimiwa Keenja. Mheshimiwa Keenja alikaa miaka mitano. Mheshimiwa Mzee Malecela alikaa miaka sita. Wengine wote 21, tuko 10 humu ndani ya Bunge, pamoja na mimi mwenyewe, miaka miwili, mitatu; kuna nuksi gani ndani ya Wizara ya Kilimo? Lazima kuwe na *continuity*. (Makofi)

La pili ni hili tatizo la kuigawa Wizara ya Kilimo na Mifugo, mimi bado naona ni kasoro kubwa. Kilimo na Mifugo kila wakati imekuwa ni kitu kimoja; walijenga umoja, ushirikiano na ndiyo maana hata vurugu hizi hazikuwepo. Sasa wamekuwa wawili, kila mmoja ni mbabe upande wake; Mifugo mbabe upande wake, Kilimo mbabe, ndiyo maana tunagombana kila siku. Wakulima na Wafugaji, nakumbuka wakati mmoja niliwahi kusema mkulima huyu huyu ndiyo anayefuga na ndiyo analima. Wasukuma ndiyo wakulima. Hivi ugomvi uko wapi? Sasa yako mambo tunaweza kuyazungumza tukajua uzuri na ubaya na Wizara hii ya Mifungo imekuwa ikipelekwa kwenye Maji, sasa iko na samaki! Sasa ni vizuri likaangaliwa katika misingi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimshauri Waziri; wenzangu wamezungumza na mengi Waziri uliyoyaandika kwenye hotuba ni ya utekelezaji. Katika Wilaya zetu, tunatakiwa kuyasimamia ili haya yaliyoandikwa yaweze kufikiwa. (Makofi)

Sasa ili uweze kufanikiwa, nataka nishauri yafuatayo: Kwanza ni suala zima la kuangalia wataalamu wetu. Wataalamu tunao wengi, mimi niliwahi hata kufikiria kwamba, hivi kwa nini Mabwana Shamba hawapati nafasi ya kutosha kwenda kwenye kazi za mafunzo ambayo ni *practical*? Vijana wetu siku hizi wanatoka shuleni kwenye vyuo moja kwa moja wanakuwa mabwana shamba. Bwana Shamba lazima upate nafasi ya kwenda kujifunza kilimo *practically* kwa wakulima wenyewe. Mtindo wa zamani ulikuwa huwezi kupata cheo cha Ubwana Shamba bila kukaa kijijini na wakulima angalau hata miezi sita. Leo Bwana Shamba anatoka darasani moja kwa moja; *it is wrong*. Bwana Shamba ajifunze pamoja na wakulima, akae nao, hilo ni muhimu lazima tulizingatie. Pia ili tuweze kuwatambua popote, tuanze kufikiria kuwapa *uniform* hawa watu tuwatambue. Nalisema hilo makusudi mazima itatusaidia. Kuna Mabwana Shamba wanajificha, huwezi kuwatambua hata ukiwapita unawakuta vilabuni huwezi kujua kama wamejificha. Bwana Shamba unaweza kumtambua kwa kumlazimisha awe na sare ili na wazee wawatambue; ni vizuri tukaliangalia hili litatusaidia. (Makofi)

Baya zaidi, nadhani tuiombe Serikali itusaidie mipango yetu ya maendeleo zaidi inategemea fedha za nje. Nalisema hilo kwa sababu nimeona. Mwaka jana kama Mheshimiwa Waziri unakumbuka, katika taarifa yako ya mwisho wakati wa kuomba fedha uliomba fedha kwa ajili ya maendeleo na ukaomba karibu shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya fedha za maendeleo kutoka hapa nchini, lakini shilingi bilioni 17 uliziomba kutoka nje. Mwaka huu tumerudia kosa lile lile, umeomba shilingi bilioni 2.5 kutoka ndani lakini shilingi bilioni 90 kutoka nje. Maana yake wakiondoka wafadhili ndiyo mwisho wetu, tunaendelea kutegemea wafadhili hatutafika mahali popote, kama ni Kilimo Kwanza nguvu zetu zote zitumie fedha zetu wenyewe tuanzie hapo ili tuwe na

uhakika ya kwamba, tukianzisha *projects* zitaendelea na hazitakwama mahali popote. Mimi naomba hilo liangaliwe. (*Makofi*)

Vilevile suala la upatikanaji wa pembejeo, wenzangu wamelizungumza na wote ninaungana nao, lakini jambo ambalo tumekuwa tukilisahau ni suala zima la kutumia utaalamu wetu na wataalamu waliopo hasa Tengeru, Chuo cha *Horticulture*, ambacho kinashughulikia mambo ya matunda, mboga za majani ili angalau sasa *horticulture* nayo ianze kupewa msukumo unaostahili. Leo tunasema tuna *commission* ambayo imewekwa kisheria; hivi kweli Tume hii ya Horticulture inafanya nini?

Nami ninachoogopa hata kiwanja cha ndege ambacho tunakianzisha kule Songwe, kitakaa hakina kazi kama hatuwezi kuzalisha mazao yatakayofanya ndege zinapokuja zitoke na mazao, mboga za majani, maua na ndizi. Sehemu nyingine wanapeleka ndizi mpaka Ulaya na zinapatikana sana Nyanda za Juu Kusini, hali yake ya hewa ni nzuri tunaweza kuzalisha mazao ya kila namna, lazima tujiandae ili Kiwanja cha Songwe kikianza kisiwe cha kubeba watu. Ndege haina faida kama inabeba watu pekee. Hata treni, ukiona treni inabeba watu faida yake ni kidogo. Treni zinatengenezwa ili zibebe mizigo na binadamu. Ninaomba hilo liangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, ningeomba viwanda vitusaidie. Mheshimiwa Waziri, yote unayofanya kwa nia nzuri usipopata msaada kutoka kwenye viwanda au kutoka Wizara mbalimbali, utakwama kutekeleza Agizo la Serikali la Kilimo Kwanza. Sasa ni suala la Wizara mtambuka na suala hilo linakuja kila Wizara, nayo ilete mapendekezo yake namna ya kuweza kuimarisha hii azma ya Serikali kuhakikisha tunafanikiwa katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana vyuo vyetu kuanzia vya VETA, navyo vianze kufikiria mipango yao ya mafunzo ilingane na azma hii ya Kilimo Kwanza. Vijana wasijifunze mambo ya ufundi tu, lakini wajufunze na suala la kilimo, iwe ni kilimo cha kufa na kupona, katika mitaala yao kuwe na kilimo, lakini kilimo cha vitendo waende mpaka vijijini. Nimeshukuru ya kwamba, vijana safari hii watakwenda kusimamia mambo ya pembejeo. Mimi nasema nakupa pongezi Mheshimiwa Waziri, kwa sababu vijana ambao wako katika vyuo vyetu, zaidi ya 1000 wakisambaa nchi nzima, kwanza, watajifunza zaidi nini kinafanyika vijijini. Pia watatuletea hamasa na uhuni unaofanywa na baadhi ya mawakala wetu wa pembejeo utapungua sana. Mimi nina imani kabisa huo mwanzo utatusaidia. (*Makofi*)

Vyuo Vikuu kama Morogoro, naomba tuangalie *syllabus* zao. Tungependa wataalamu waliosomea kilimo na kubobea katika kilimo, wajiingize katika suala zima la kilimo. Wameanza pale Morogoro; kuna vikundi vya vijana ambao ni wataalamu, wameanzisha taasisi za kujitegemea kwa mambo ya kilimo, wengine mambo ya *food processing*; mimi nasema ni mwanzo mzuri. Wataalam hao wote lazima wajifunze utaalamu wa namna ya kuendesha biashara. Ujasiriamali ndiyo unatakiwa wajifunze katika vyuo ili wakitoka wakulima wetu wanaozidi kuchoka, wataanza kuingia katika shughuli za kilimo na tusidanganyike hii idadi ya watu wanasema 80% ya watu wote wa Tanzania wako vijijini si kweli, wanaolima sasa wamepungua.

Wataalamu wanasema imefikia kwenye asilimia 70 labda 69 ndiyo wamebaki vijijini, wengine wote wanakuja mijini. Sasa tusipoingiza wataalamu wakatusaidia ili kueneza kilimo cha wataalamu, tutakwama hatutafika mahali popote. Ninadhani tusiachie wazee wakaendelea kulima. Vijana tuingie na utaalumu na sayansi na teknolojia. Kinachotakiwa, yote haya yaliyoandikwa, lazima yasimamiwe na sisi wenyewe katika maeneo yetu, tusitegeme Wizara itasaidie. Katika maeneo yetu, tuangalie kila hela inayoletwa, inafanya kazi iliyokusudiwa na wala isihamishwe kwa gharama yoyote; mara kujenga shule, mara zahanati, tutafanya makosa tutakuwa tumevunja azma hiyo ambayo imekuja nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba sana mawakala wa pembejeo ambao sio waaminifu, tutapambana nao kwa sababu wanawaibia wakulima na anayemwibia mkulima maskini atakufa maskini na si tabia nzuri kuwaibia wakulima. Mawakala wawe waaminifu na wagonjwa lazima tuhakikishe tunawaweka pembeni. Mimi nina imani kabisa hayo yatafanikiwa, nilikuwa nimemwomba Mheshimiwa Keenja, akumbuke kuna kampuni moja ya *ERTH FOOD* ambayo ilikuwa inasambaza pembejeo. Pembejeo hizo ni za mbolea ambazo si za kemikali. Tungemwomba Waziri, wale wanaohusika kama inawezekana tuwaombe waanzishe viwanda hapa nchini. Viwanda hivyo wangeweza kuanzisha kwa sababu vinatumia malighafi za hapa hapa, vinatumia makapi na hata wakati mwingine majani ya karanga, baada ya kuvuna karanga zako ndiyo unatumia hayo kwa ajili ya mbolea tena ni mbolea nzuri sana katika mpango wa kilimo hai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ninawatakia wataalamu kila la heri katika kazi zao. (*Makofi*)

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele yako ili nami nichangie hoja hii ya kilimo. Pili, napenda kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Tatu, ningependa kuwapongeza sana Mheshimiwa Wasira na Makamu wake, Mheshimiwa David Mathayo na Wasaidizi wao wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa hotuba yenye matumaini iliyowasilishwa kwa ufasaha sana; hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni uhai, kilimo ni uchumi, kilimo ni biashara, kilimo ni maendeleo, kwa hiyo, niipongeze Serikali yetu kwa kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Vilevile napenda kuwapongeza Viongozi wa Nchi za Afrika, kwa kuhakikisha kwamba, kila wanapokutana wanaliweka mbele suala la kilimo. Walipokutana kule Maputo mwaka 2003, waliazimia lengo la kila nchi katika bajeti zao kutenga asilimia isiyopungua kumi kwa ajili ya kilimo na kuanzisha Mpango wa *Comprehensive Africa Agriculture Development Program (CAADAP)*. Walipokutana mwaka huu kule Sirte Libya, ambako Mheshimiwa Waziri ulikuwepo, kaulimbiu ya Mkutano wao ilikuwa ni Kilimo kwa Maendeleo na Kujihami kwa Njaa au kwa lugha ya kigeni, *Agriculture for Development and Food Security*. Kwa maana hiyo basi, sisi hapa Tanzania ni vizuri tukahakikisha kwamba, sekta hii inapewa uzito unaostahili tukizingatia msukosuko wa uchumi, fedha, upungufu wa chakula na kupanda kwa bei za chakula duniani; hapana

budi Watanzania tihakikishe kwamba, kilimo tunakifanya kwanza kikweli kweli, sio kwa maneno kama walivyosema wenzangu walionitangulia. Pamoja na jitihada za Wizara kukweka mikakati mbalimbali ambayo imeelezwa kwenye hotuba hii, kama Taifa, bado naona kama hatujakipa kilimo ule uzito unaostahili.

Tuchukue kwa mfano bajeti ya mwaka jana, kilimo ukichanganya na mifugo na uvuvi, katika bajeti nzima ya mwaka 2008/2009, kilitengewa shilingi 155,204,000,000 tu. Mwaka huu kimeongezewa kidogo, kwenye bajeti hii kilimo kimetengewa shilingi 173,123,000,000, hili ni ongezeko la asilimia 45. Tunaweza kuipongeza Serikali kwa kuona kwamba, angalau wameongeza. Ukichukua viwango hivi ukalinganisha na bajeti nzima, kilimo mwaka jana kilitengewa kama hesabu zangu sio potofu, kilitengewa asilimia 2.5 na mwaka huu kimeshuka asilimia 2.2; tunakwenda wapi? (*Makofi*)

Viwango hivi mbali ya kuwa chini ya lengo la tamko la Maputo nililolisema, haviridhishi na hali inaonekana inapungua. Hili sio kosa la Wizara, lakini nasema kama Taifa, bado hatujakipa kilimo nguvu inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa sekta binafsi, katika hali ya kwamba, Serikali yenyewe haiwezi kumudu mahitaji yote ya sekta hii. Sekta binafsi kuna maeneo ambayo haiwezi ikajiingiza kirahisi, kwa sababu inategemea zaidi kupata faida. Kwa hiyo, katika maeneo kwa mfano ya mafunzo ya maafisa ugani, ruzuku kwenye pembejeo, uzalishaji wa mbegu nzuri, huduma za utafiti, usimamizi wa usambazaji wa pembejeo, usimamiaji wa mashamba darasa vijijini, haya ni mambo yanayohitaji kusimamiwa na kugharimiwa na Serikali. Usipoiongeza bajeti ya sekta hii, mambo haya tutakuwa tunacheza nayo. Kweli katika hotuba hii, Mheshimiwa Waziri umetamka kwamba, kuna mashamba darasa 1995 ambayo yanagusa wakulima 51,623 kwa nchi nzima yenye watu milioni 40, hili ni sawa na tone la maji katika bahari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa natambua kati ya haya niliyoeleza Serikali inayashughulikia, lakini nasema kwamba, Wizara ingeweza kufanya zaidi kama bajeti ingeangaliwa kwa hali ya juu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye kilimo cha umwagiliaji, katika hali ya sasa ambapo dunia imekubwa na mabadiliko ya hali ya hewa, iko haja ya kuelekea zaidi katika kilimo cha umwagiliaji. Hivi sasa dunia inatafakari kupata Azimio jipya badala ya Kyoto, kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa (*Global Warming*) na njaa ambayo imezagaa sehemu nyingi. Tunafarijika kuwa, Wizara katika hotuba hii inajali mazingira na matumizi bora ya ardhi. Sanjari na haya, ningetegemea katika mpango huu, kungekuwa na mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji ambacho sikioni, ukiondoa yaliyoelezwa katika ibara ya 118 hadi 121 na ibara 135 hadi 136. Mimi nadhani kuna haja ya kuihamasisha Serikali, ikaangalia zaidi katika suala la umwagiliaji ambalo ni chini ya asilimia mbili ya mahitaji ya nchi hii.

Hapa ningependa kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya za Kisarawe, Kibaha na Morogoro Vijijini, nimshauri Mheshimiwa Waziri, ametaja kwamba kuna skimu 40 za umwagiliaji. Ninasema kwamba, katika hizo skimu 40 usisahau Bonde la Mto Ruvu, hasa baada ya utekelezaji wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda, ambalo Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, alikuwa amelisemea eneo hili. Wananchi kule wanalima mazao ya mpunga, kunde, maboga, ufuta na mazao mengine, kama wataunganishwa katika skimu hizi, naamini kwamba, uwezo wao wa kuzalisha utakuwa mkubwa na mchango wangu katika masuala ya chakula utakuwa mkubwa pia.

Nihamie kwenye Zao la Korosho, niwazungumzie wakulima wa korosho. Katika hotuba hii, Zao la Korosho limetajwa kwenye sehemu mbalimbali zikiwemo ibara za 27, 66 na 133. Katika kipindi cha 2007/2008 hadi 2008/2009, uzalishaji wa korosho kama ilivyosemwa katika hotuba kwamba umeshuka, umeshuka kwa asilimia 20.22. Hili kwa sisi wa Ukanda wa Pwani ni pigo kubwa sana, kwani baada ya minazi kufa hasa kukumbwa na maradhi, zao lililobaki la biashara ni korosho na kama korosho inashuka, maana yake ni kwamba, umaskini katika Ukanda wa Pwani kuanzia Tanga mpaka Mtwara, utakuwa umezagaa.

Kwa hiyo basi, pamoja na sababu mbalimbali ambazo zimeelezwa katika hotuba hii, naona kwamba sababu kubwa ni upungufu, ukosefu na ucheleweshaji wa pembejeo. Sitaki kusema sana juu ya hili, kwa sababu wenzangu wengi wamezungumzia pembejeo. Kwa korosho ni jambo muhimu sana. Kwa hiyo ni vizuri Serikali imelitambua hili. Ninakupongeza Waziri kwa kujaribu kuondoa ukiritimba wa wale mawakala wa pembejeo na kuongeza idadi ya aina za pembejeo ya korosho. Hii nadhani itasaidia zao hili liweze kwenda mbele. Kwa hiyo ni muhimu mwaka huu, madawa yaagizwe mapema na yawafikie wakulima mapema ili Zao la Korosho liweze kupata nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya maamuzi mawili katika Sekta hii ya Kilimo, ambayo binafsi sikubaliani nayo. La kwanza ni la kusitisha ukusanyaji wa mapato wa Bodi za Mazao kwa matumizi yao wenyewe, badala yake, Serikali inawapa ruzuku. Ninadhani hili linadumisha ile ari ya Bodi za Mazao kujitahidi kuzalisha zaidi, kukusanya zaidi na kupata faida ili waweze kumudu gharama zao na kupata ziada. Kwa upande mwingine, Serikali imejibebesha mzigo, sasa Bodi hizi zote zitakuwa zinaweka misulusulu kama ilivyokuwa mashirika ya umma zamani pale Hazina kungojea ruzuku. Mimi nafikiri uamuzi huu Serikali iufikirie upya ili kuona angalau kunakuwa na motisha ya Bodi hizi kuweza kujitutumua zaidi katika kuongeza mapato.

Pili, uamuzi unaohusu Bodi ya Korosho peke yake, nayo ni kwamba, hii ndiyo Bodi pekee ambayo inatozwa ushuru wa mauzo ya nje kwa korosho ambazo hazikubangukiwa. Nia ilikuwa nzuri, kuhamasisha ubanguaji hapa nchini, lakini uwezo wa viwanda tulivyonavyo mpaka sasa hivi bado haujafika mbali. Kwa hiyo, inaelekea kwamba, kodi hii itaendelea kuwepo kwa muda mrefu sana. Baya zaidi, ushuru huo unagawanywa katika mafungu: asilimia 5.5 inakwenda kwenye wilaya zinazozalisha korosho, asilimia moja inapelekwa kule Naliandele kwa ajili ya utafiti wa Zao la Korosho na asilimia 3.5 inakwenda Hazina. Hapa ndipo kwenye ugomvi wangu. Hivi kwa nini hii



asilimia 3.5 isirejeshwe kwa wakulima ili waweze kuongeza uzalishaji? Tunaweza kufanya hivyo kwa njia mbili: kwa kuongeza ruzuku ya pembejeo au kuongeza bei ya korosho kwa mkulima ili mkulima aweze kupata motisha ya kuweza kuzalisha zaidi.

Serikali ifikirie upya, kwa sababu ninaamini kwamba, hili linadhoofisha uzalishaji wa korosho katika maeneo haya. Bahati nzuri Waziri Mkuu yupo, nakuomba Mheshimiwa Waziri uzungumze na Waziri wa Fedha, mlipeleke suala hili kwenye Baraza la Mawaziri ili asilimia 3.5 ihamie kwa wakulima, iweze kuwapa motisha zaidi kwa kulizalisha zao hili. (*Makofi*)

Sina haja ya kuzungumza zaidi juu ya manufaa ya pembejeo na ruzuku, kwa sababu haya yameelezwa vizuri sana katika Hotuba yako Mheshimiwa Waziri, kwenye ibara ya 47. Kwa hiyo, ninaamini kwamba; ni jambo ambalo linaeleweka Serikalini. Nikupongeze tu Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wako kwamba, baada ya kugundua upungufu ulioorodheshwa katika ibara ya 49, mmeamua kuazimia kufanya marekebisha yaliyoorodheshwa katika sehemu ya pili ya ibara hii. Nawatakieni kila la heri na muweze kuyatekeleza hayo ambayo mmeamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ninaunga mkono hoja (*Makofi*)

**MHE. ALHAJI DKT. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya na kuweza kushiriki katika mjadala huu mkubwa wa rafiki yangu, Mheshimiwa Steven Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Pili, naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii. Kama walivyofanya wenzangu, ninaomba niwashukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wao, kwanza, kwa maandalizi na kuwasilisha vizuri hotuba yao ya bajeti, lakini pili kwa kazi nzuri wanayoifanya pale Wizarani. Mimi ni Bwana Shamba wa siku nyingi, niliingia kilimo kwa mara ya kwanza mwaka 1962 Novemba, kama *Assistant Field Officer*, nikapatapata mafunzo kidogo na baadaye nikaenda nje kusoma kama Bwana Shamba, nikarudi nikafanya kazi sehemu mbalimbali katika nchi yetu, pamoja na kusimamia utafiti wa *sisal* pale Mlingano.

Kwa hiyo ni Bwana Shamba, ninawajua wenzangu hawa kwamba, wana kazi nzito na ninawatakia kila la heri katika kazi yao hii nzito ambayo wanaifanya. Naomba pia niwapongeze wapiga kura wangu wa Ulanga Magharibi na kuwashukuru sana kwamba, wamekuwa wakiniunga mkono, tunashirikiana nao bega kwa bega katika kujiletea maendeleo katika jimbo letu. Katika kata 12 tuna shule za sekondari 11 na katika suala la kilimo hili tunapiga hatua, sisi ndiyo tunaotoa mpunga mwingi katika Mkoa wa Morogoro na kuleta Morogoro mpaka Dar es Salaam. Mpunga wetu ni maarufu unaitwa tule na bwana na ukiupata lazima mama ahakikishe anakula na mzee (baba). (*Kicheko*)

Kwa hiyo, kazi hii nzuri tumeifanya katika miaka mitano, sita hivi. Suala la bei nitalizungumza baadaye, ni muhimu sana nilisemee kidogo hapa. Waziri amesema vizuri hapa, akimnukuu Dkt. Norman Baulaw, ambaye amemwita Baba wa Mapinduzi ya Kijani (*Green Revolution*). Kweli yule baba ni Mmarekan, lakini kafanya kazi kubwa sana katika kufanya Mapinduzi ya kusaidia Mapinduzi ya Kijani kule Asia. Amesema vizuri sana kwamba, pembejeo muhimu na ya kwanza ni utashi wa kisiasa. Mara nyingi siku nyingine huwa ninashangaa wenzangu wakizungumza hapa wanasema wanapuuza uamuzi wa kisiasa, kumbe uamuzi wa kisiasa ndiyo unaojenga mambo. (*Makofi*)

Sasa wewe mwanasiasa ukidharau uamuzi wa kisiasa, mimi ninakushangaa sana. La pili, kuna pembejeo na kadhalika, lakini pembejeo ya pili muhimu kwa mkulima ni bei ya mazao yake, Waingereza wanaita *producer price*. *Producer price* ikiwa nzuri, ndiyo bei ya moja kwa moja, ndiyo pesa yake mkulima, inaingia mfukoni mwake hakuna namna nyingine ya mkulima kupata pesa ni kwa bei tu. Kwa hiyo, nakupa mfano; Jimbo la Ulanga Magharibi lilikuwa moja ya katika Mkoa wa Morogoro wanaolima pamba bora, lakini bei ilikuwa kero mno mpaka sasa hatulimi tena. Leo tunajinadi pale jinari ya kwanza imejengwa mwaka 1943, ilijengwa Malinyi nyumbani kwangu, wengi wenu hamkuwepo hapa, mimi nikiwa na miaka miwili ilijengwa pale. Hiyo ndiyo ya pili kujengwa; ya kwanza ilijengwa Morogoro Mjini, ikafuata hii ndiyo ikaenda ya Kilosa, halafu ya Kiberege, Malinyi na Mwaya. Hatulimi pamba kwa sababu ya bei tu. Hivi sasa tumejikita katika mpunga, tunalima vizuri mpunga na tuna hali nzuri.

Vilevile tunalima mahindi vizuri. Suala la bei lazima tuliwekee mkazo na mimi ninaungana na ndugu yangu hapa Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya, kaka yangu kwamba, hapana ku-*intervene* kwa kutumia *administrative fiat*, kutumia amri halali mnaziita za Serikali kusema hapa weka kizuizi ama watu wasipeleke mahindi nje. Mnawaangusha wakulima kwa sababu hapo ndipo wanapopata bei nzuri. (*Makofi*)

Bei ya mpunga Malinyi, mwaka mmoja uliopita ilikuwa shilingi 25,000, mwaka huu imefikia shilingi 60,000. Mimi ninalima mpunga na nina magunia pale wala sisemi, lakini nina mpunga wangu pale siuuzi nangoja mpaka mwezi Desemba au Januari hivi bei itakapofika shilingi laki moja. (*Makofi*)

Hivi vipingamizi vinanikera kweli kweli. Huwa nagombana na wenzangu wale wanaoweka viziuzi wanasema, ooh bwana, kuna njaa! Wapi? Kama kuna njaa, Serikali inunue chakula, ipeleke kwenye maeneo yenye njaa. Usinifanye mimi mkulima nim-*subsidise* mwananchi mwenzangu, kwa nini? Kwa nini mimi nim-*subsidise* mwananchi mwenzangu tena mwananchi mwenzangu huyu, ni mzembe, halimi, ndiyo! Halimi! Sasa mimi kwa nini unanifanya nipate adhabu ya kum- *subsidise* huyu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uchumi wa soko, *principle of intervention of the Government, is at the market place*, ndiyo uchumi wa soko! Unakwenda ku-*intervene* kwenye soko na asikudanye mtu kwamba uchumi hau-*intervene* kwenye soko, hakuna! Wamarekani wamefanya mfano mzuri sana safari hii wame-*intervene* kwenye soko sana. Waulize Mabepari wenyewe! Sasa ninyi msifanye ujamaa, mnachanganya ujamaa kidogo na uchumi wa soko, hapana! Tumeamua uchumi wa soko achana na uchumi wa ujamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona mdogo wangu pale, Mheshimiwa Aggrey Mwanri ananicheka, anasema mzee leo anafoka kidogo, hizo ndizo *principle* za kiuchumi, *intervene at the market* pale. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najua pia kwamba *the market is not fairly, it does not distribute wealth equally*, hii ni kweli, soko haligawi mali au raslimali kwa usawa, ni kweli kabisa, ndiyo! Lakini twende sokoni pale pale, ndiyo tukaelewane pale, kama unataka kugawana mali vizuri basi tumia soko, usitumie Kanuni hizi za kiutawala ambazo zinaonea watu wengine na ndiyo zinadumaza kilimo katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utashi wa kilimo tulikuwa nao mzuri kwa mfano Siasa ni Kilimo lakini tulikosea mambo mawili, mimi ni *planner*, kwanza hatukuweka *resource* kwani kilimo ni *resources* lazima uwe na kilimo cha umwagiliaji, ni lazima kumwagilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu Dkt. Borlaug, alichokifanya pale ni mbegu, dawa za kuua wadudu...

**NAIBU SPIKA:** Ni Dokta nani?

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Dkt. Borlaug, yule aliyemtaja Mheshimiwa Waziri Ukurasa wa tatu katika hotuba yake, ni Dkt. Norman Borlaug, ni Mmarekani yule.

Lakini pia ni kwamba kulikuwa na pesa za kufanya *irrigation, true wealth in India* kwani India ilikuwa ni nchi ya njaa lakini imeondokana na njaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Pale Thailand ukipita kama unakwenda Bancok kwa ndege, utaona mashamba mengi ya mpunga ya *irrigation*. Bila *irrigation* hamuwezi kupata *self reliance*, haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie FAMOGATA maana ni agizo la Rais, nalo hili ni la muhimu. Kwanza, namshukuru Waziri Mkuu kaondoa ubishi huu wa chakula kingi kwa nchi yetu maana *focus* ile ya Mikoa sita mimi naunga mkono mia kwa mia, ile *focus* ni sawasawa. Tukitaka tuwe na chakula cha kujitosheleza na ziada ya kuuza nje lazima tukazanie Mikoa sita ile kwa chakula na lazima pia tukazanie kilimo cha umwagiliaji, hawa watu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, wana kitu kizuri sana wanakiita *Quick Win*. Dhana ya *Quick Win* maana yake ni kupanga ni kuchagua, msifanye Sera ya Jongoo, unajua jongoo ana sera! Mama Jongoo aliambiwa na mtoto wake kwamba, mama, miguu mingi namna hii, mguu gani au miguu ipi nianze nayo kutembea? Mama akasema tembea mwanangu tembea. Mtoto akauliza tena mguu upi nianze kutembea nao? Mama akasema mwanangu tembea tu. Sasa hiyo sera haifai kwa sisi. Mwananchi ni lazima umpange kwa sababu kupanga ni kuchagua na unapanga kwa sababu gani? Ni kwa sababu huna rasilimali za kutosha kwa hiyo lazima useme Mikoa sita hii mimi nitaiwekea nguvu ili iwe ghala ya Taifa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais kaenda mbali zaidi, akasema Mkoa wa Morogoro unaweza kuwa ghala ya Taifa kwa kutumia FAMOGATA, sasa Waziri

pale ametaja katika sentensi mbili au tatu katika ukurasa wa 46 na 96 na wa 34 nadhani basi. Lakini mimi nasema kama tunataka kupanga ni kuchagua basi tutilie mkazo Mkoa wa Morogoro kwa sababu Mkoa wa Morogoro una mito 142 inayotiririka mwaka mzima. Ina eneo siyo chini ya ekari 125,000 za kumwagilia hivi sasa tunamwagilia ekari 8000 tu, kama ilivyo Kitaifa tuna eneo kubwa lakini tunamwagilia 3%, hatuwezi kuondokana na njaa, ni lazima tufanye kazi ya kumwagilia na msiopepe gharama kwani kupanga ni kuchagua tufanye kazi ya kusaidia kilimo cha umwagiliaji ndiyo tutafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zana ni muhimu vilevile pale Morogoro kuna ubia katiya *DEMACO*, *FBE Bank* na wakulima kwa kupitia *SACCOS* zao. Mimi katika Jimbo langu nimepata matrekta saba mwaka huu kwa kutumia utaratibu huo wa kushirikiana. Sasa naomba Serikali muwasaidie hawa watuy wa Benki na mshirikiane nao muone ni namna gani wanaweza wakaongeza ugawaji wa matrekta na utaratibu wao wa kukopesha ni mzuri zaidi kuliko benki nyingi katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la zana ni muhimu na hatuwezi kuendelea na jembe la mkono, kwanza haya matrekta madogo kwa Mkoa wa Morogoro ni sehemu chache tu yatatumika kwa sababu hayana nguvu sana lakini matrekta makubwa ndiyo yenye uwezo kwa sababu udongo ule ni *heavy soil*, kwa hiyo, ni lazima yapatikane matrekta makubwa. Lakini pia ni lazima tuendelee mbele tupate *harvester*, *planter*, *seeders* na *wider* yaani zana zote za kilimo zitasaidia kuongeza uzalishaji wa kilimo katika nchi vinginevyo hatuwezi kupiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa fursa hii. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba tu nitoe taarifa kwamba, kadi yangu haionekani hapa, kwa hiyo, ninatumia kadi ya Mheshimiwa Aziza, ili niweze kupata mawasiliano kwa kuongea ndani ya ukumbi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya pekee kabisa, nianze kwa kuwashukuru Wataalamu wa Kilimo katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Songea. Katika kile kidogo kinachopatikana, watu wale wametoa ushirikiano mkubwa sana kuhakikisha kwamba maendeleo ya kilimo yanapatikana ndani ya Jimbo la Peramiho na Halmashauri ya Wilaya ya Peramiho. Kwa kweli, lazima niseme ninawashukuru kwa niaba ya wakulima wote wa Jimbo la Peramiho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niishukuru Serikali kwa ujumla na pia nimshukuru Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri wake, wameonyesha mfano dhahiri kabisa wa kusimamia maendeleo haya ya kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais amesimama imara kuhakikisha mtikisiko wa kiuchumi hautuathiri maendeleo ya nchi yetu na hasa kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu mambo mawili kabla sijaingia kwenye hoja ambazo nimekuja nazo. Kwanza kabisa, wenzangu wengi wamesema lakini hotuba ya Mheshimiwa Waziri pia imezungumza, Mheshimiwa Waziri Mkuu naye ninapongeza sana alisimamia agenda ya Mikoa sita kuwa ni sekta kiongozi katika uzalishaji wa mazao ya chakula, hilo ni suala la msingi na ni maamuzi ya busara kabisa katika nchi yetu. Lakini mimi niseme kwamba wale wanaozalisha chakula kwa mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambao ndiyo wanaongoza kwa kuzalisha mahindi katika Mkoa wa Ruvuma, hawana zao lingine la biashara kwa kuwa Serikali na nchi imewapa jukumu la kuzalisha chakula kwa ajili ya nchi ya Tanzania na tunajua kwamba kwa kuzalisha chakula na kutokuzingatia zao lingine la biashara, wananchi wale wanategemea hata mapato ya Halmashauri yapatikane kutokana na zao lile wanalolizalisha yaani zao la chakula ambalo ni Mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunapata matatizo kidogo siku za nyuma, mahindi yote yanayozalishwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Songea yananunuliwa moja kwa moja na Kitengo cha Hifadhi ya Chakula ya Taifa. Kwa maana hiyo, Serikali hailipi *cess* kwenye Halmashauri yetu kwa sababu chakula kile kinatoka kwenye mkono wa kushoto kuingiza kwenye mkono wa kulia lakini mtu ni yule yule mmoja. Hivyo, Halmashauri ilikuwa inakosa mapato lakini nasema naishukuru Serikali iliamua kuanza kuzingatia kulipa ruzuku kwenye Halmashauri yetu kufidia mapengo ya bajeti ya Halmashauri ambayo yanapotea kwa kuuza mahindi kwa ajili ya hifadhi ya chakula na siyo kwa wafanyabiashara wengine ili kuokoa tatizo la njaa kwenye nchi yetu. Naishukuru sana Serikali na naipongeza. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie tu ruzuku hiyo iongezeke kwa sababu maendeleo yamekuwa yakiongezeka na ruzuku tuliyokuwa tunapewa ni kidogo, ninaomba sasa iongezeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niishukuru Serikali imetoa pia ruzuku kwa ajili ya mazao mengine ya biashara kama vile Pamba, Korosho, Kahawa na kadhalika. Mpaka sasa pesa zile zimeshafikishwa kwa wanunuzi wa mazao hayo kama ya Pamba kule Maswa na maeneo mengine. Lakini wanunuzi wale waliopewa pesa na Serikali hawajaanza kulipa ruzuku kwenye Halmashauri zetu, ninaomba nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, kama Serikali imeshawapa ruzuku na wao waone umuhimu wa kutoa ruzuku kwenye Halmashauri yetu kwa maana ya *cess* ili Halmashauri zetu zisipate shida na zisiweze kufa. Tunahitaji ujenzi wa shule, ukarabati wa madarasa na kadhalika, Halmashauri zinategemea ruzuku hiyo, kwa hiyo, ninaomba tushirikiane pamoja tusiiangushe nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza. Kwa kweli mimi nawapongeza sana kwani ni hoja nzuri na ni hoja ya msingi. Nilikuwa namsoma Mr. Ban Kin Moon, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, katika *report* yake aliyoitoa tarehe 06 Juni, 2009 yaani mwaka huu, amesema kwamba suala la maendeleo katika dunia yetu, limekwenda vizuri kwenye malengo ya kimilenia katika sekta za huduma ya jamii kwa mfano elimu, afya, kupambana na maradhi na kadhalika tunakwenda vizuri. Lakini hofu ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, imejitokeza wazi baada ya mtikisiko mkubwa sana wa kiuchumi. Katika *report* yake pia amesema anaziomba nchi zote za G8 na G20, zione uwezekano

wa kuongeza fedha kuziokoa nchi maskini zinazoendelea zifanye kila linalowezekana kupambana na umaskini lakini kwa kupunguza tatizo la chakula katika nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Pakistan, inasemekana toka mwaka 2007 asilimia 20% ya wananchi kule watakuwa na njaa na ukiangalia bei ya ngano katika nchi ile ilipanda kwa 66%. Ethiopia 45% watakuwa na njaa, bei ya mahindi ilipanda kwa 100%. Nataka kusema nini? ninachotaka kusema ni kwamba mfanyabiashara yeyote anatumia mwanya wa biashara unaopatikana mbele ya uso wake ili aweze kujinufaisha. Mimi nadhani ni nafasi yetu sasa Tanzania kuchukua mwanya huo wa biashara na tukazalisha ziada na ziada hiyo ingeweza kutusaidia sana Watanzania tukaweza kuondokana na umaskini na tukapiga hatua kabisa kwenye maendeleo ya nchi yetu. Kama hali ndiyo hii, nchi za G20 zimekubali kuchangia karibu USD bilioni 20 kwa miaka mitatu kuhakikisha chakula kinatoshelezwa katika dunia sisi sasa ndiyo tunge-*take advantage* ya kuhakikisha hizo bilioni 20 zinaletwa ndani ya nchi ya Tanzania, ndiyo tungehakikisha kwamba pesa hiyo sasa sisi ndiyo tunai-*grab*, tunajua kwamba tutashikilia huo sasa ndiyo muhimili mwingine wa kutuletea maendeleo. Ndiyo maana nasema agenda ya kuongeza uzalishaji wa chakula, kwa kweli tukisimama nayo imara, ni agenda ambayo itatupeleka mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anatuambia mahitaji ya chakula katika nchi yetu ilikuwa kwenye nafaka ni lazima tuwe na tani 6,575,508 lakini zilizopo ni tani 5,265,305 na tuna upungufu wa tani karibu 1,313,139. Sasa upungufu huu hautufanyi uzalishaji wetu wa ndani na hasa wa mazao ya chakula na hasa kwa kuzingatia kwamba soko la chakula ndiyo linalopanda juu, mazao ya biashara tumeshindwa kujitayarishia mkakati wa kuwa na viwanda endelevu na kuwa na namna ya kuyafanya mazao haya yaweze kutengenezwa na kusindikwa ndani ya nchi tukayauza yakiwa ghafi na kuongeza pato letu. Hebu tusimame, huku kwenye chakula tunaweza kujisaidia, tunaweza kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama uzalishaji wetu mpaka sasa tukianza na kilimo kama uti wa mgongo wa taifa, kilimo kama sekta kiongozi, kilimo kama mapinduzi ya kijani na sasa Kilimo Kwanza lakini bado kwenye nafaka tuna tofauti ya tani karibu 1,313,139, ninafikiri hapa bado tuna hatua nyingine ndefu ya kwenda mbele. Ni lazima tujiulize nini kifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya tathmini ya namna gani? Nampongeza sana Mheshimiwa Paul P. Kimiti, alisema hapa na mimi ninanukuu tena, Ukiangalia kwenye *development budget* pesa yetu ya ndani ni kweli kabisa ni shilingi 2.5 bilioni, pesa ya nje kwa mwaka huu ni shilingi bilioni 90, kwenye taarifa ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Mr. Ban Kin Moon, amesema kama kweli *commitment* ya nchi hizo zilizoendelea, hao Ma-G8 na G20 ya kusaidia wananchi katika nchi zinazoendelea ni ku-*donate* hizo fedha lakini amesema wazi kwamba kuna *delay* kubwa sana ya fedha hizi kutolewa kwenye hizo nchi kwani wanaji *commit* lakini fedha hawatoi, wakati mwingine zinachelewa. Sasa mimi najiuliza kama shilingi bilioni 90 hizi zika-*delay* hicho Kilimo Kwanza kinakuwaje? Kitakuwa kilimo kesho!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninaomba pia nijue bajeti ya mwaka huu, inatuambia kwamba kwa mfano Mkoa wa Arusha kwenye *Subvote* 4486, ya maendeleo ya kilimo kwenye Wilaya, imetengewa shilingi bilioni 3.3, mwaka jana zilitengwa shilingi bilioni 2.6, hapa Dodoma mwaka jana walitengewa shilingi bilioni 2.7 na mwaka huu shilingi bilioni 2.3. Hawa Iringa jirani zangu walitengewa shilingi bilioni 3.9 na mwaka huu shilingi bilioni 4.3 lakini mimi na Ruvuma yangu pamoja na Jimbo langu la Peramiho jumla yetu tulitengewa shilingi bilioni 4.1 na mwaka huu shilingi bilioni 4.3. Mimi ninapenda Mheshimiwa Waziri atuambie zile za mwaka jana zote zilifika? Kama zilifika, katika kila Wilaya tumepiga hatua gani? Maana hizi zote ni fedha za nje, tuna matarajio hizi nazo zitafika na zitatupeleka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Edward Lowassa, wakati ule alipokuwa Waziri Mkuu, alituita tujenge mkakati wa kuhakikisha kilimo katika kila zao kinapiga hatua kwa namna fulani. Tumeshafanya *review* na kuona yale malengo yamefikia hatua ipi? Mimi sijaona kama tumeita tena mkutano mwingine wa kujipima ili kuona kama yale tuliyojiwekea sasa tumefika hatua gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko haja ya kuamua kabisa kwa dhati kwamba Kilimo Kwanza kiwe ni Kilimo Kwanza. Tufanye nini? Bado mbegu bora haziwafikii wakulima kwa muda unaotakiwa. Sasa ili sekta ya kilimo na hasa uzalishaji wa chakula iwe endelevu, ni kuhakikisha idadi ya mimea inayozalishwa shambani ni mimea inayohitajika na kwa ubora unaotakiwa. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtoto wa mkulima alikuja kule kwangu, aliona na akapata moyo na kwa kweli nakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu agenda ya mbegu bora ndiyo suala pekee la kutuondoa hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuendelea kuhakikisha udongo unaotumika katika kilimo unazingatia hali halisi ya mazingira na hali ya ubora kwa kutumia pembejeo na hasa mbolea zilizobora na kwa wakati unaotakiwa na kwa namna inayotakiwa ya kiutalaamu. Hilo ni suala lingine ambalo tunatakiwa kuhakikisha na wananchi wa Jimbo la Peramiho wamenikumbusha sana hilo niliombe na Serikali ilifikirie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia inatakiwa tufanye utafiti wa kupambana na wadudu na magonjwa yanayoweza kuharibu mazao yetu na kuturudisha nyuma kwenye kilimo. Tumepiga sana kelele kuhusu suala la utafiti, hilo nalo lizingatiwe, lakini masuala ya masoko ya uhakika na zana za kuwawezesha wakulima kulima kilimo cha kitaalamu, hiyo ni agenda nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zimejipangia bajeti, zitasaidia kuweka matrekta kwenye vikundi, tunao Mfuko wa Pembejeo hali ya fedha ya mfuko huo ingeongezeka ndiyo ingesaidia sana kuhakikisha wakulima wale mmoja mmoja, wanapata matrekta kwa kiasi kinachotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pembejeo *trend* yake ikoje? Matrekta 99,827 hapo ukijumlisha matrekta makubwa, *power tiller* na yaliyokarabatiwa. Katika *population* ya watu milioni takribani 41, matrekta ndiyo haya yanayotumika na yaliyopelekwa na Mfuko wa Pembejeo, bado tuko nyuma sana kwa hiyo tupeane nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kusema kwamba Benki ya Wakulima, ni kitu cha msingi lakini vilevile niungane na wenzangu kusema kwamba Vyama vya Akiba na mikopo ndiyo kimbilio la wakulima wadogo wadogo katika kujitafutia mahitaji yao. Lakini tuisahau kuboresha viwanda ili mazao yetu yatakapouzwa nje yaweze kusindikwa kuwa ghafi na yasiuzwe bila kusindikwa ili kuyaongezea *value* kwa ajili ya kukuza uchumi katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya yakifanyika, yatatusaidia sana kwani wakulima wako tayari, motisha yao ni kuona mipango hii mizuri inayozungumzwa inawafikia na iwe ni mipango shirikishi. Kwa mfano, tukisema Kilimo Kwanza basi iwe Kilimo Kwanza katika sekta zote, tulikuwa na elimu ya kujitegemea kwenye shule zetu zote za kilimo, hii Kilimo Kwanza imehusishaje shule zetu za kilimo na wao wafundishe Kilimo Kwanza kama ilivyokukwa zamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Vyu vya Maendeleo ya Jamii, namshukuru Mheshimiwa Margaret Sitta kwenye bajeti yake mwaka huu ametenga shilingi milioni nne kwa ajili ya kupeleka matrekta madogo kwenye Vyu vya Maendeleo ya Jamii. Nilitegemea hata Wizara ya Sayansi na Teknolojia na yenyewe ingezungumza Kilimo Kwanza kwa mtindo wake. Kwa hiyo, unaona kwamba wote tunazungumza lugha moja na mtu wa mwisho anayefaidika ni mkulima. Ama kwa mfano, ili wananchi wetu wa vijijini, waweze kufikia masoko kwa haraka barabara za kuwafikia zikoje? Kwa hiyo, unaona kila Wizara na kila sekta ingekuwa na *component* hapa na kutuonyesha katika Kilimo Kwanza wao wanasema nini, ingetusaidia sana na ninadhani tungetoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema Mheshimiwa Stephen M. Wasira, tunakujua ni mchapakazi, Mheshimiwa Mathayo David Mathayo, tunajua ni mchapakazi, hebu simameni imara tusaidieni. Ninaomba tu-*take advantage* hii ya tatizo la njaa ulimwenguni kuinua uchumi na kuwaondolea Watanzania umaskini waliokuwa nao, tutaondoka na utaona kwamba maisha ya Watanzania yataboreka zaidi. Bado tunahangaika sana na umaskini wa kipato. Tumesema 70% ya wananchi wa Tanzania ni wakulima, hawa wakiwezesha, kwa kweli umaskini utakuwa umeondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuipongeza Serikali kwa mkakati huu na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na kwa kweli niwape hongera ya kazi maana huo ndiyo msembo ambao Mheshimiwa Lowassa alitufundisha zama zile, hongera kwa kazi, kwa kweli kwa Wizara, Waziri, Naibu Waziri na timu yake yote na ninapenda kwa namna ya pekee niwape hongera nyingi za kazi za kilimo, wapiga kura wangu wa Jimbo la Kasulu Mashariki na wapiga kura wote wa Mkoa wa Kigoma, kwa sababu sisi kwetu, kilimo ni maisha yetu na Kilimo ni wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninapenda kwa muda mchache huu, hii dhana ya Kilimo Kwanza, naona kama inapotoshwa hivi. Kilimo Kwanza kusema kweli chimbuko lake ni Azimio la TANU la mwaka 1972 kule Iringa ndiyo iliibua hii hoja



kwamba siasa ya TANU ni kilimo na kwa tafsiri pana mwaka 1972 walisema kwamba Siasa ni Kilimo. Sasa huu mkanganyiko kwamba Kilimo Kwanza ni dhana ya wafanyabiashara, sijui walikaa kwenye kikao cha TNBC, si kweli ni kupotosha na kuchanganya maneno tu haya. Kilimo Kwanza, ni siasa ya TANU na ni siasa ya CCM tangu mwaka 1972.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mbunge mmoja alikaa kwenye *television* majuzi akaanza kueleza Kilimo Kwanza kana kwamba imeibuliwa mwaka 2009, si kweli Mheshimiwa Stephen M. Wasira wewe unajua, Kilimo Kwanza ni *Policy* ya TANU tangu mwaka 1972. Nilitaka kuweka mambo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzunguzia Kituo cha Kilimo cha Bugaga. Mheshimiwa Stephen M. Wasira, tena wewe ni Waziri wa siku nyingi, kule Kigoma tulikuwa na Chuo cha Kilimo cha Mbondo, Wizara ikakifunga eti wananchi wa Kigoma hawahitaji Chuo cha Kilimo, tukashangaa. Sasa kilichobaki pale ni kituo cha Kilimo cha Bugaga. Mheshimiwa Waziri Kituo cha Kilimo cha Bugaga unakiita bustani, kile ni kituo, kina majengo, raslimali watu, miundombinu yake lakini kwenye hotuba hujasema unafanya nini na Kituo cha Kilimo cha Bugaga. Niseme kwamba ni *oversight* na hata katika orodha ya vituo ulivyoviweka, umesema eti kituo cha Bugaga na vingine umeweka Wilaya zao lakini Kituo cha Bugaga ukasema kiko Kigoma, hapana hicho kituo kiko Kasulu na ni kituo cha mwaka 1974 na hiyo ni tafsiri kwamba Mheshimiwa Waziri hata hujui kituo chenyewe hicho kiko wapi. Kwa kweli itabidi aje Kasulu, naam! Itabidi Mheshimiwa Waziri baadaye sina shida ya kushika mshahara wako lazima nijue *status* ya Kituo cha Kilimo cha Bugaga ambacho ni cha Kitaifa na ambacho sisi kama Halmashauri hatukihudumii kwa dhana kwamba ni Kituo cha Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa, hiki ndio kituo pekee katika kanda yetu ile ambacho kinafanya utafiti wa *horticulture* yaani mboga na matunda. Nyumba zake zinaanguka, gari lake liko kwenye mawe na *it seems* hata Waziri hajui kiko wapi kituo hiki. *In fact*, ukiacha Tengeru, kituo kingine cha *horticulture*, ni Bugaga lakini ni ajabu kwamba kwenye hotuba yake Mheshimiwa Stephen Wasira, naona hujakigusia na ninashawishika kuamini kwamba watu wa Wizarani, kituo hiki mmeamua kukitelekeza kwa sababu hata kwenye kurasa ambazo zimetaja orodha ya vituo, kituo hiki hakijatajwa na kwa makosa umesema eti ni bustani, nani kakuambia ni bustani? Hili ni eneo lenye ekari 200 yaani ni eneo kubwa sana na zimetengwa mahususi kwa ajili ya utafiti na kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije haraka haraka kwenye Mikoa sita inayozalisha chakula. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipoteuliwa, alikuja na agenda hii ya kilimo na Mikoa hii sita ikateuliwa kuwa mahususi kwa kuzalisha chakula. Lakini Mheshimiwa Waziri kwenye mkakati wake bado hajalieleza Bunge hili tunatokaje hapa tulipo na tunajitoshelezaje kwa chakula hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia takwimu zimetajwa katika ukurasa wa 12 na 13, lakini hazioneshi wazi mazao hayo yatalimwa wapi, kwa kiasi gani, tutazalisha

namna gani, kwa kutumia nyenzo gani na nani atafanya nini. Hayo yote Mheshimiwa Waziri wa Kilimo hayakubainishwa katika hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukurasa wa 12 na 13 ni takwimu umezipachika tu, tani milioni mbili (2,000,000), zinatoka wapi? Kama ni mahindi Ruvuma, mwaka huu wanazalisha mahindi kiasi gani? Kigoma kiasi gani? Tabora kiasi gani? Hakuna! Ni mambo ya jumla jumla tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri aweze kutueleza vizuri. Lazima waje na mkakati hapa ambao utatutoa hapa tulipo vinginevyo itakuwa ni hadithi za miaka yote, Kilimo *is a very serious issue* jamani, lazima tuwe na mkakati mahususi kwamba, tunatoka hatua hii kwenda hatua hii na nyenzo ni hizi. Hii itatusaidia zaidi kuliko kwenda na mambo ya jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika Mkoa hii sita ambayo ni pamoja na Mkoa wa Kigoma, ni suala la mbolea. Hili limezungumzwa sana, lakini kuna suala la mbegu na madawa. Sisi katika Mkoa wa Kigoma, tumekuwa na utamaduni kupitia Wizara ya Kilimo, mbolea na mbegu zinafika zikiwa zimechelewa. Tunaomba sana waratibu wa Wizara yake, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, mbolea ikifika ikiwa imechelewa inakua haifanyi kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mbegu, Mheshimiwa Jenista amelizungumza vizuri, maana ili wakulima wetu watoke hapa tulipo ni lazima tuanze pale tulipo na msingi wa kutoka pale tulipo ni mbolea na mbegu bora. Ili huyu mkulima anayelima kwenye kishamba chake cha jembe la mkono aongeze uzalishaji pale alipo, hiyo ndiyo jinsi ya kutoka pale tulipo, pengine baadaye ndiyo inakuja zana pana ya kuwa na vitendea kazi kama matrekta na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mradi wa *DADPs*, ukurasa wa 26. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo katika ukurasa wa 26 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, mwenyewe amekiri kwamba, ubora wa mradi wa *DADPs* ni asilimia arobaini na nane (48%). Mimi nilidhani wenzetu wa Wizara wangukuja wakatusaidia mpaka sasa huu ni mwaka wa tatu wa kutekeleza *DADPs*, kama mpaka sasa ubora wa mpango huu ni chini ya asilimia hamsini (50%) basi kuna tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipendekeze mambo yafuatayo ili kuboresha programu hii ya *DADPs* ambayo kwa kweli ndiyo kichoteo cha pesa za kilimo katika Halmashauri zetu. Kwanza, ni kupeleka wataalamu Wilayani. Halmashauri nyingi Mheshimiwa Waziri wa Kilimo hazina wataalamu, wataalamu wamejirundika kwenye maofisi huko juu, wataalamu watoke maofisini waende kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kupeleka vitendea kazi katika ngazi za Wilaya, na la tatu ni kuwekeza katika miundombinu, iwe katika umwagiliaji, ni mambo ambayo ni muhimu sana ili kuweza kuboresha mpango huu wa *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije mpango wa *DASIP*. Mwaka jana nilizungumzia kwa kweli kutoridhishwa na jinsi *DASIP* inavyoratibu mambo yake katika Mikoa ile minne ambayo inahusika na mradi wa *DADPs*. Sisi Kigoma, Kasulu, Kibondo, ni kati ya Wilaya ambazo ziko katika mpango huu wa *DASIP*. Mwenyewe Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 27 wa hotuba yake, amekubaliana na maneno yangu ya mwaka jana kwamba, bado kuna matatizo ya usimamizi wa fedha, kutoshirikisha walengwa katika kuibua miradi na ujenzi duni wa miundombinu na zaidi ya hayo, mwaka jana nilishauri Makao Makuu ya *DASIP* kwa Kanda yetu ya Magharibi, ni Mwanza lakini mtu anayeratibu miradi iliyoko Kasulu na Kibondo, anatoka Mwanza, anasafiri kilomita mia nane (800) kuja kuratibu ujenzi wa soko Kasulu, nikashauri kwamba, kwa nini kupitia programu ya *DASIP* msihamishe baadhi ya maofisa wa *DASIP* walioko Mwanza wakaja Kigoma ili huduma zile ziweze kuwa karibu? Mwaka jana nilikueleza Mheshimiwa Waziri na nikapata fursa ya kuzungumza na wataalamu wa *DASIP*, wakaniambia mnajiandaa lakini sasa ni mwaka mzima bado mnajiandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Bugaga, nimezungumza na hii narudia tena Mheshimiwa Waziri, *with a serious note*, lazima nipate maelezo ya Bugaga kama sipati maelezo ya Bugaga itabidi mshahara wako mchana huu tuugawane.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za ugani ni muhimu sana, ukurasa wa 38 wa hotuba hii wameeleza vizuri sana na mimi naomba msisitizo uelekezwe katika kuanzisha vituo vya rasilimali za kilimo na mifugo vya Kata. Narudia tena, Vituo vya Raslimali za Kilimo na Mifugo katika ngazi ya Kata, tuwekeze katika maeneo hayo ili tuondoke hapo tulipo katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwa haraka haraka utafiti uliofanywa na Chuo cha Mlingano kwa Wilaya za Kasulu, Kibondo na Kigoma vijijini. Tunaomba sana kama inawezekana Mheshimiwa Waziri, tafiti zilizofanywa za kuchora ramani katika Mkoa wa Kigoma juu ya sehemu zinazoweza kulima kahawa kwa Kibondo, Kasulu na Kigoma Vijijini, tunaomba ramani hiyo tuipe kabla ya Bunge kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu ukurasa wa 75 na 79 wa kitabu hiki. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba shilingi bilioni 2.5 zimetengwa kwa ajili ya uratibu kwa ajili ya sekretarieti za Mikoa na shilingi bilioni 21.9 kwa ajili ta uratibu katika ngazi ya Taifa. Naomba sana hizo fedha kwa kweli zihuishwe ili zifanye kazi iliyokusudiwa. Ukiangalia kazi zilizotajwa ukurasa wa 79 shilingi bilioni 21.9 ni uratibu tu, ukurasa wa 79 mpaka 81 ni uratibu tu. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, unawezaje kutenga shilingi bilioni 21.9 kwa uratibu? Kuimarisha timu za taifa, kujenga uwezo wa sekretarieti za Mikoa, kuangalia uwezekano wa kuwa na waratibu wa programu, kuboresha mwongozo, kuimarisha mfumo, kuratibu bodi, kuwezesha, aah jamani shilingi bilioni 21.9 katika umasikini huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, anasa hii inatoka wapi? *Twenty One billion* kwa ajili ya uratibu wa Kitaifa? Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, wewe ni Waziri wa siku nyingi,

tafadhali sana rudi uketi na wenzako, hizi fedha wekeni kwenye uwekezaji wa kilimo, acheni haya mambo ya uratibu jamani, naomba sana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 81 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ni masuala ya *DASIP*. Mambo ambayo yameanishwa ukurasa wa 81 kwenye mradi wa *DASIP*, Mheshimiwa Waziri sio uwekezaji katika kilimo! Kuendelea kujenga uwezo, mafunzo mbalimbali, kuwezesha Halmashauri, kufanya *review*, kuimarisha *SACCOS*, jamani huu ni uwekezaji katika kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee maneno aliyoyazungumza Mheshimiwa Dkt. Ngasongwa, hatuwezi kutoka hapa tulipo kama hatuwekezi katika Kilimo. Lazima tu-*invest* katika Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, niombe zile Wizara zilizotajwa kwamba ni Wizara za Kilimo; Mifugo, Kilimo chenyewe, Maji na Umwagiliaji, TAMISEMI, nina mpango wa kuja na hoja binafsi katika Bunge lijalo, tuletewe programu mahususi ya hizi sekta zinazohusika na kilimo juu ya namna ya kuondoka hapa tulipo. Nina mpango wa kuja na hoja binafsi wakati muda utakapofika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Waziri ni mwenzangu, naunga mkono hoja lakini ninapenda kupata maelezo ya Bugaga *Seed Farm*. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kuhusu suala hili la Kilimo Kwanza. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Wasira pamoja na Naibu Waziri, pamoja na Wataalmu wote wa Kilimo, kwa jinsi ambavyo wametuletea hotuba ya bajeti inayohusu Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme Serikali imefanya uamuzi wa busara sana kuleta katika bajeti hii, suala la Kilimo Kwanza, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kalambo na wananchi wa Mkoa wa Rukwa, sisi tunaipongeza Serikali na tunapongeza Wizara hii na kuiomba isimamie kwa karibu na fedha nyingi ziende kutekeleza mahitaji ya wananchi ili Kilimo Kwanza kiweze kuleta manufaa. Kwa sababu bila hivyo, tutaendelea na mchezo tu wa kutoa matamko ambayo hayaleti manufaa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, katika Mkoa wa Rukwa, suala la Kilimo Kwanza limekuwepo tangu siku hizo kwa sababu mkulima wa Rukwa hasukumwi kwenda kufanya kazi, mkulima wa Rukwa anahitaji mbolea, anahitaji wataalamu, anahitaji pembejeo na mbegu, kisha anakwenda kulima wala hakuna mtu anayemsukuma. Hivyo, suala hili la Kilimo Kwanza kwake siyo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza ninukuu ukurasa wa 57, *paragraph* ya 93 ambayo Mheshimiwa Waziri ameandika kuhusu hifadhi ya udongo na matumizi bora ya ardhi. Ameandika hivi:-

*“Wizara imekamilisha utayarishaji wa rasimu ya awali ya Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Matumizi bora ya Ardhi na Kilimo (National Agricultural Land Use Planning and Management Master Plan)”. Mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aliyoyaeleza hapa, ni maeneo mazuri kwa kilimo kwa nchi nzima, sawa kabisa nakubaliana naye lakini nimuulize swali, hivi anapotoa suala la matumizi bora ya ardhi anajua kwamba Wizara inayohusu Mifugo nayo imetoa sera yake ya kuendelea kutumia maeneo mazuri ya kilimo kwa ajili ya kufugia wanyama na kuhakikisha wanyama wanaongezeka mpaka waweze kumaliza ardhi iliyo nzuri kwa kilimo? Analijua hili? Wamefanya mawasiliano gani kuhakikisha kwamba, maeneo yatakayotumika kwa ajili ya kilimo, ni tofauti na maeneo yatakayotumika kwa ajili ya ufugaji? Hakuna mawasiliano yoyote! Nchi hii itaendelea kuteketea na itamalizika na tutaendelea kutazamana, njaa itaendelea kutukumba kama nchi ya Tanzania na tutaendelea kuomba chakula kutoka nje kwa sababu hatuna mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba, maeneo ya ufugaji ni haya na maeneo mazuri kwa Kilimo ni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, anayozungumza Mheshimiwa Waziri hapa kwamba, ni maeneo mazuri kwa ajili ya kilimo ndiyo hayo hayo maeneo ambayo sasa yanatumika na wafugaji na kwa sababu yana malisho mazuri, mifugo inaongezeka bila idadi na mfugaji anaendelea kufurahi. Naomba Wizara hizi mbili zikae pamoja waone jinsi ya kuondokana na jambo hili, la sivyo nchi hii haina mpango uliothabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, naomba nizungumzie kuhusu pembejeo. Nchi ya Tanzania, sehemu kubwa ya Mikoa yetu usipokuwa na mbolea na pembejeo nyingine, huwezi ukapata mazao yaliyo mazuri. Hivyo tunaomba tuisitize kuhusu suala la mbolea kama walivyosisitiza wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mbolea ya ruzuku tunaomba, mbolea hii iwe inanunuliwa mapema na ikiwezekana inunuliwe wakati bei ya mafuta imeshuka kwa sababu sehemu kubwa ya mbolea hii ni mazao ya mafuta ya petroli. Wakinunua mapema, bei ya mbolea inakuwa chini, siyo kama tulivyonunua mara ya mwisho mwaka jana, tumenunua wakati bei ya mafuta ilikuwa juu na gharama ya mbolea hii ikawa kubwa kiasi ambacho wakulima wengi walishindwa kununua. Tunaomba Serikali ilizingatie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mbolea hiyo ifike mapema kwa mkulima ili aweze kuipata wakati huu anapovuna na anapouza mazao ili awe na uwezo wa kununua ile mbolea. Lakini tukichelewa, tukaita wakati ameshamaliza kuuza mazao yake, hawezi kuinunua mbolea ile ndio maana na vocha mnazogawa zinazwa kwa wale mawakala wanaosambaza mbolea. Hivyo, tunakuomba Mheshimiwa Waziri, kwa uangalifu mkubwa sana mbolea ifike kila mahali mlipopanga mapema ili wananchi waweze kuinunua kabla hatujafikia kwenye msimu wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mbolea ya Minjingu, Wabunge wengi wamesimama hapa wanalalamikia mbolea ya Minjingu, sasa pale wanapolalamikia

kwamba mbolea haifai, hakuna sababu ya kubishana, ni Wizara na Serikali kukubali kwamba kama mbolea hii inaonekana haifai mahali pale, basi hatupeleki mbolea aina hii, tutapeleka mbolea ambayo wakulima wamezoea kuitumia, basi imekwisha na wakulima watapata mbolea wanayoihitaji. Lakini tukilazimisha, tunaendelea kuleta mkorogano kati ya Serikali na wananchi ambao wanailalamikia mbolea hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zana za kilimo, zana za kilimo zote ni muhimu sana, zana hizi zipatikane mapema. Lakini kinachoshangaza, viwanda vyetu vya zana za kilimo vyote vimekufa. UFI imekufa, Zana za Kilimo Mbeya, haipo tena na viwanda vingine vilivyokuwepo vilivyoanzishwa wakati ule hakuna. Je, Wizara hii haijawahi kupata hata mwekezaji mmoja katika zana za kilimo? Kwa kweli, inashangaza! Tuendeleo kupata plau, haya majembe ya kukokotwa na ng'ombe kutoka Zimbabwe, kutoka India, kutoka China wakati tunaweza tukatengeneza zana hizi hapa hapa!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa, tunatumia majembe ya kukokotwa na ng'ombe kwa kiasi cha asilimia 80, lakini majembe yote yanatoka nje. Hivi kweli Serikali na Wizara hii ya Kilimo bado tunaendelea kutaka kupoteza fedha za kigeni kwenda kununua zana hizi kutoka nje badala ya kutengeneza humu ndani? Mimi nadhani Wizara ijipange vizuri, itupe majibu, ina mpango gani kuhusu Kilimo Kwanza na uzalishaji wa zana za kilimo humu ndani. Hatuwezi tukaendelea kununua hata jembe la mkono lile tunalotumia kwa ajili ya kupalilia, tunakwenda kununua India, tunakwenda kununua China wakati tuna uwezo wa kutengeneza! Tulikuwa tunatengeneza hapa nchini, kwa kweli ni jambo la kushangaza na kusikitisha sana. Tunaomba sana Waziri atakapokuwa anajibu, atueleze mipango yake thabiti kwa sababu kuboresha Kilimo Kwanza katika nchi hii ni pamoja na kutengeneza zana ambazo ni rahisi kutengeneza, tusiendeleo kuagiza kutoka nje kwa tunatumia fedha zetu za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mbegu, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atumie juhudi yake yote, Taasisi kama Magereza na JKT wazalishe mbegu za kutosha zitakazosaidia kushusha bei ya mbegu kwa mkulima. Haingii akilini tunaendeleo kuagiza mbegu kutoka Kenya na wale wanatembea nchi nzima, wanafika hata Mkoa wa Rukwa wanakuja kuuza mbegu wakati Serikali ipo na tunazo Taasisi ambazo zingeweza kuzalisha mbegu na zikaweza kuuzwa kwa bei ya chini. Mimi nasema, hili haliwezekani, hatuwezi kuendeleo kutumia fedha zetu za kigeni kwenda kununua mbegu kutoka nchi jirani. Ni lazima na sisi tuzalishe za kutosha na za bei nafuu kuliko kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa za kuua wadudu hivyo hivyo, wakulima wengi wanateseka kwa sababu mazao yao yanaharibiwa na wadudu yakiwa shambani na yakiwekwa ghalani nayo yanashambuliwa. Vipo vyuo vingi sana ambavyo vimeishafanya utafiti na dawa ile iliyofanyiwa utafiti inaweza kuzalishwa. Naomba Wizara hii isimamie dawa zizalishwe za kutosha ili tuweze kulinda mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masoko, suala hili kwa Mkoa wa Rukwa kwa kweli ni mwiba. Naomba nilieleze kama alivyoeleza Mheshimiwa Mzindakaya na Mheshimiwa Kimiti. Mimi Jimbo langu la Kalambo, liko kilomita 76 kutoka Mbala –

Zambia na Bandari ya Kasanga inapatikana katika Jimbo langu la Kalambo. Kwenda Zambia ni kilomita 76, mimi nimeishafika Mbala kuuza mahindi yangu, lakini kuyapeleka Dar es Salaam ni kilomita 1,500. Bei ya mazao Dar es Salaam kwa mahindi yanayotoka Sumbawanga kwa sababu ya barabara na mambo mbalimbali ni ya chini sana. Naomba sana fikirieni jinsi ya kuturuhusu tuuze mazao yetu ya ziada katika nchi jirani. Tutauza, Burundi wanayafuata wenyewe, Congo wanayafuata wenyewe, sisi tutauza halali ili tuhakikishe kwamba tunapata bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SGR* wakishanunua mahindi yote wanayohitaji, sasa na ile alibaki tutafanya nini, tuendeleo kuweka kwa sababu Serikali inasema tuna njaa wakati wananchi wanahitaji kwa ajili ya kukimu mahitaji yao? Hili haliwezekani, tutafutieni bei nzuri ya mahindi na bei ya alizeti kwa sababu ndiyo mazao ya kilimo ambayo yanastawi vizuri katika Mkoa wetu wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umwagiliaji, umwagiliaji uko kwenye Wizara ya Maji na Umwagiliaji, lakini ni suala ambalo linawahusu Wizara ya Kilimo. Tunaomba sana, tunaomba sana mtusaidie jinsi ya kuweza kuboresha umwagiliaji mdogo mdogo na umwagiliaji wa kiwango kikubwa ili tuweze kuongeza mapato kwa ajili ya wakulima wetu. Mimi ninayo miradi miwili pale Katuka na Singiwe, Wizara ya Kilimo ndiyo itakayosimamia mambo haya yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechoka kuzungumza kuhusu Maafisa Ugani. Kama watu hawawezi kufanya kazi, tunaomba Wizara hii ihakikishe kwamba inawastaafisha au itupatie Maafisa Ugani wanaoweza kushirikiana na wakulima ili mazao yaweze kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ardhi katika Jimbo la Kalambo, ni ardhi ambayo ukipeleka matrekta haya wanasema *Power Tillers*, hayawezi kulima vizuri. Tunaomba matrekta makubwa ndiyo yaweze kupatikana katika Jimbo la Kalambo kwa sababu ndiyo yanayoweza kulima vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala moja nililozungumzia mwaka jana ambalo mpaka leo wala sijapatiwa majibu, nilizungumza katika bajeti, kuna ugunduzi ambao umefanywa na wakulima wa kawaida, Mkoa wa Rukwa au katika Jimbo langu la Kalambo wanalima mara mbili, wakati wa kiangazi wanalima kitu wanaita Fuga Unyevu, ni kilimo ambacho kinatumia *Osmosis*. Nilizungumza hili mwaka jana, hakuna mtu aliyenijibu wala aliyechukua hatua za kuweza kuelewa kitaalam maana yake nini. Tunapata mazao karibu mara mbili, ni kama vile tunapata mvua mara mbili, kwa nini hatujaweza kufuatilia?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuzuia wizi wa vocha. Wakulima wengi wameuza vocha zile kwa mawakala kwa sababu mbolea ilichelewa kufika, bei ikawa juu, wakashindwa kununua. Sasa vocha wamepewa, wakaona kwa nini wakae nazo, wakaziua. Tunaomba safari hii mbolea ije mapema, wakati wakiwa na mazao, wameuza wamepata fedha, waweze kuhakikisha kwamba wananunua mbolea. *Ma-DC*

pamoja na Maafisa Kilimo, wasimamie kwa karibu na wale wanaonunua vocha bila kupeleka mbolea wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu kwa wakulima, mimi nadhani kazi hii bado hatujaifanya kiasi cha kutosha. Tuwapatie wakulima elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Stakabadhi ya Mazao Ghalani pamoja na SACCOS, hizi SACCOS ni lazima ziimarishwe ili kuwasaidia wakulima wadogo wadogo wasiokuwa na mtaji mkubwa. Stakabadhi ya Mazao nayo pia iimarishwe katika vijiji vyetu kama Matai, Mwimbi, Ulumi, Msanzi, Mwazye, Sopa, Mkowe na maeneo mengine katika Mkoa wa Rukwa ambao wanaweza kustakabadhi mazao na wanaweza kupata bei nzuri hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, usindikaji wa mazao katika Mkoa wa Rukwa hauwezekani kama hatupati umeme. Sasa Kilimo, Nishati na Madini lazima viende pamoja ili tuwende kupata umeme tusindike mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huyu anayesindika mahindi akapata unga, Dar es Salaam kuna viwanda vingi vinavyouza unga, yule wa Sumbawanga hawezi kuja kuuza Dar es Salaam, kwa nini msimruhusu akauza Zambia, akauza Congo, Burundi na sehemu nyinge, kwani kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, lakini naomba mtupatie soko ili na wananchi wetu waweze kupata faida. Ahsante! (*Makofi*)

**MHE. OMARI S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kabla sijaanza kuchangia, nitumie nafasi hii, kutoa rambirambi na pole kwa wananchi wa Babati Mjini, ambao jana walipata msiba wa Mzee Mohe ambaye alikuwa Mwenyekiti wa CCM wa Tawi la Maisaka B, ni eneo la nyumbani kwangu. Kwa hiyo, nataka nitumie nafasi hii kuwapa pole na rambirambi zangu. Kwa kweli Mzee huyo alikuwa Mzee mwenye hekima, busara na Mzee anayeheshimika sana kwenye eneo lote. Basi kwa kuwa ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu, nitumie nafasi hii kusema nimwombe Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, hii dhana ya Kilimo Kwanza, nataka niseme kwanza, sijui sasa mtizamo wetu utakuwaje kwenye MKUKUTA kwa sababu mantiki ya hii ni kukusanya rasilimali zote au nyingi iwezekanavyo tuzipeleke kwenye kilimo. Lakini, vile vile tunao Mpango wa MKUKUTA ambao vile vile unahitaji kuhakikisha kwamba sekta zingine zote zinashirikishwa. Sasa ni lazima tuwe waangalifu hapa, tuone nafasi sasa ya Kilimo Kwanza iko wapi kwenye Mpango wa MKUKUTA. Nilitaka kwanza niseme hivyo.



Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, niseme tu kwamba Kilimo Kwanza maana yake kuwekeza kwenye kilimo na maana yake kama walivyosema wenzangu lazima kuwe na Benki ya Kilimo, nakubaliana kabisa, kwa sababu Benki zingine kwa kweli haziwasaiddii wakulima, kwa hiyo kuna haja ya kuwa na Benki ya Kilimo. Vile vile kuna haja ya kuhakikisha kwamba ardhi ya wakulima inapimwa ili waweze kupata mikopo, upatikanaji wa pembejeo na vile vile hifadhi ya chakula, lakini kubwa zaidi ni namna ya kusimamia kilimo chenyewe. Sasa, mazungumzo yangu au hoja yangu itajikita katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza na Hifadhi ya Taifa ya Chakula (*SGR*). Nimesoma tangazo kwenye gazeti la Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo na Chakula, wametangaza bei za mazao na naomba ninukuu kama nilivyosoma, wametoa mazao mawili tu, amesema hivi:-

*“Kwenye vituo vikuu, mahindi kilo 100 shilingi 30,000/= (Kwa maana ya gunia, kilo moja ni shilingi 300/=) na mtama gunia la kilo 100 shilingi 26,000/=. Kwenye vituo vidogo, mahindi itakuwa shilingi 25,000/= kwa gunia la kilo 100 na mtama shilingi 22,000/=”.*

Hii ametoa ndugu yangu Katibu Mkuu, Mohamed Muya ambaye namfahamu vizuri. Sasa mimi nawauliza, hizi bei ziko wapi? Mbaya zaidi wamesema baada ya bajeti hii kupita ndiyo vituo hivi vya *SGR* vitafunguliwa, na isipopita? Lakini hata hivyo, hii bei ya shilingi 30,000/= iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, jana hapa tumeendelea kusikiliza bei, Mheshimiwa Lubeleje wa Dodoma hapa alisema bei hapa sokoni hapa, sasa hivi mjini ni shilingi 48,000/= kwa gunia la mahindi la kilo 100. Sasa hii bei ya shilingi 30,000/= ya Wizara hii inatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza leo kwenye vyombo vya habari, kule Longido bei ya gunia ni shilingi 70,000/=:, ninyi hii ya kwenu ya shilingi 30,000/= inatoka wapi? Mko nyuma sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka nitoe tahadhari kwa Wizara hii. Mkitaka tufanikiwe katika Kilimo Kwanza, tuwachie wananchi watafute bei nzuri na ninyi kama Serikali kama mnataka kununua mazao, ingieni kwenye ushindani huo, bei ni ya soko, tusiwakandamize hawa wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimefanya hesabu ya ekari moja, gharama ya eka moja tu ya kilimo, ukianza kutoka kusafisha na kulima ni mara mbili katika maeneo mengi, ununue mbegu, mbolea, uje upalilie, uvune, uhifadhi, usafirisha, unapata jumla ya gharama ya shilingi 365,000/= kwa eka moja, tena nimeacha na vitu vingine. Mkulima huyu anatazamiwa kuvuna gunia 10 au 15. Akiyuna 10, akiuza kwa bei hii ya shilingi 30,000/= maana yake anapata 300,000/=:, akipata 15 ambayo kidogo ni afadhali, atapata shilingi 450,000/=: Kwa hiyo, kwa gunia 10 atakazouza kwa bei hiyo ya Serikali atapata hasara ya karibu 65,000/=:, hajafanya kitu chochote. Akipata gunia 15 na akauza kwa bei

hiyo ya shilingi 30,000/= ya Serikali atapata faida 85,000/= tu kwenye eka, anapeleka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima twende kwenye hali halisi, nini kinachotokea kule. Nina wasi wasi bei hizi wanazipanga mezani! Kwa hiyo, nilitaka niseme kuhusu tahadhari ya bei kwamba ni vizuri kuwachia wakulima wapate bei kulingana na soko na tusiwazuie kuuza. Tunapowazuia, tunazuia na uwezo wao wa kurudi tena shambani, ndio kinachotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye zao ambalo katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri sijaliona lakini zao hili linalimwa zaidi kule Babati, nalo ni mbaazi na najua Mheshimiwa Waziri akienda kule kwao anapita Babati na kipindi hiki cha kiangazi akifika anaona kijani kitupu, ni kwa sababu ya mbaazi. Mbaazi ni zao ambalo linahitajika sana kwenye nchi za Asia, India, Pakistani na nchi zingine, wananunua sana mbaazi kutoka kwetu Babati. Sasa zao hili halionekani, linafanyiwafanyiwa utafiti lakini sioni kama Serikali inatilia mkazo zao hili la mbaazi na naambiwa linatumika sana kutengeneza biskuti na vitu vingine, kwa hiyo, ni zao muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao hili wanapokuja kununua watu ambao wanasafirisha, maana wako wafanyabiashara ambao wanatoka huko na wanakuwa na wakala huku gunia linafika shilingi 60,000/= wakati mwingine hata shilingi 80,000/= haya ndiyo mazao ya kutiliwa mkazo kwa sababu yanasaidia kupunguza gharama za mkulima. Kwa hiyo, nashauri Wizara hii iangalie zao hili na itafute soko kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko soko la wazi kabisa la mbaazi na kama nilivyosema sisi ni wakulima wa mbaazi sana na katika maeneo mengine, mbaazi inatumika vile vile kama mboga. Nimeambiwa unaweza ukatengeneza pilau nzuri sana kupitia mbaazi, ni mboga wakati bado zikiwa mbichi. Kwa hiyo, Wizara iende zaidi ya mazao hayo ya mtama na mahindi haya mengine vile vile yanasaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisogee kwenye jambo lingine, tunaposema Kilimo Kwanza, tunatakiwa vile vile tuangalie kodi zinazotowwa kwenye vifaa vya kilimo. Nakumbuka kwenye bajeti tumesamehe kodi za trekta, lakini vipuri na vifaa vyake hatujavisamehe, hizi *power tillers* ambazo tunasema, sawa tunawapelekea wananchi kupitia miradi ya *DADPs* na kadhalika na wananchi wanaonunua matrekta na kadhalika, watapata matatizo makubwa sana na hizi *power tillers* katika muda mfupi itakuwa matatizo kwa sababu spea zake zinatozwa *VAT*. Ukinunua sahani ya jembe linatozwa *VAT*, spana *VAT*, nati *VAT*, jembe lenyewe ukilinunua lingine *VAT* inatozwa, hatuisaidii Kilimo Kwanza na huku ndiko kwenye matatizo makubwa kwa sababu vitu hivi ndivyo vitakuwa vinanunuliwa mara kwa mara. Sahani zitakwisha baada ya muda mfupi, lazima tutakwenda kununua na kuna *VAT* kule tukitaka tuondoe *VAT* huko badala ya kusamehe trekta lenyewe, trekta lenyewe halina maana sana kama hamna jembe. Kwa hiyo *VAT*, ni vizuri iondolewe huku kwenye zana hizi au spea za vifaa vya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kuna kodi ile ya leseni (*Motor Vehicle License*) ambayo tulikuwa tunatoza kwenye trekta mwaka ilikuwa ni shilingi 150,000/=

tumeiondoa, tumefanya vizuri kuiondoa kwa hiyo trekta sasa hivi hazina hiyo kodi ya leseni. Lakini sasa hivi wakulima wanapata taabu na wengine wananipigia simu kutoka kwenye maeneo ya Galapo kule, Magugu na wapi kwamba trela zile zinazosomba mazao zinatozwa hiyo leseni, sasa tunafanya kipi? Umesamehe trekta umeacha trela, trela inalipiwa vile vile Bima zile zilizosajiliwa zikibeba tu mazao kwa sababu hatujaisamehe basi na yenyewe inatozwa. Sasa hiki ni kikwazo kikubwa sana tena bahati mbaya sana ndugu zangu hawa wanaokusanya vitu hivi wanakwenda wakati ambapo wakulima ndio wanasomba mazao, wanazuia mambo mengi sana. Kwa hiyo, nilitaka eneo hili nalo liangaliwe vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nadhani niende kwenye lile suala la ruzuku hasa ya vocha. Kwenye ukurasa wa 32 Mheshimiwa Waziri amejaribu kueleza changamoto ambazo ziko pale lakini vile vile kwenye kitabu chake, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba ninukuu, kwa mfano kwenye hotuba yake amesema:-

*“Wakulima 737,000 walipata hizo vocha na sasa tunatazamia kwamba wakulima milioni moja na nusu waingie kwenye shughuli hiyo”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tujiulize matokeo yake kweli ni nini, tunajua? Kweli kuna mafanikio, kuna mapinduzi ya kilimo yaliyofanyika kwa kuwapa watu hawa hizi vocha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, kwenye ule ukurasa, Mheshimiwa Waziri amesainisha upungufu, amesema vocha kuchelewa kuwafikia wakulima kwa wakati na hili limesemwa na amesema katika mkakati sasa ataleta mapema, tunamshukuru. Lakini kwenye *bulletin* ya mwisho ukurasa wa 33, katika kutaka kukabiliana na upungufu huo, amesema kuanzia msimu ujao, mkulima atatakiwa kuchangia malipo ya tofauti ya bei ya pembejeo kabla hawajapewa vocha ili kuzuia wakulima kutumia vocha kinyume na makusudio. Sasa nataka niulize tu kwamba hivi wakulima ambao hao tunawataka walipie tofauti ya bei ni hawa hawa ambao wamepata ukame? Kweli inawezekana, hivi tunamjua huyu ambaye tunataka tumbadilishe ili tupate mapinduzi ya kilimo, ni huyu huyu ambaye ana uwezo mdogo kabisa ambaye tunaona alipe kabisa tofauti kabla! Ni huyu huyu ambaye tunampa bei ndogo ya shilingi 300/= kwa kilo au kwa gunia shilingi 30,000/= Kwa kweli nadhani hapa hatutawatendea wakulima haki kama hii ndiyo dhana ya kwenda kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunaona tatizo gani kama mkulima tukafanya kile kipande chake cha eka moja kwa sababu zile vocha zinatolewa kwa eka moja ikawa ndiyo dhamana, tukamkopesha na wakati wa mavuno ndio tukachukua sasa zile fedha! Tunaona tatizo gani, kwamba shamba lake la eka moja iwe tu dhamana pale? Vinginevyo kwa utaratibu huu, bado vocha hizi zitakwenda kwa watu wenye uwezo, hawa wananchi wa kawaida, wakulima hawa wadogo wadogo, watakwenda tu kwa watu wenye uwezo na zitakwenda huko na mimi tathmini yangu kama wengine wanavyosema nilitazamia Wizara ingeandika zaidi haya mambo yaliyotokea katika maeneo yetu hata kama ni moja, lakini nimesikia na kule Rukwa akisema Mheshimiwa pale kwamba kulikuwa na wizi, kwa kweli tatizo la vocha matatizo yaliyojitokeza, tathmini yangu kwenye eneo langu

inasema hivi vocha hizi zilikwenda kwenye mikono ya watu ambao hawakuwa hata na mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, sasa namwita Mheshimiwa Jacob Shibiliti na atamalizia Mheshimiwa Michael Laizer.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, nawafahamu vizuri sana, shughuli wanaiweza, ni mahali pao, tuwape kila ushirikiano ili waweze kufika huko walikopania kutupeleka. Kwa hali hiyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilizungumzia mambo mbalimbali. Kwa masikitiko makubwa sana, nianze na hilo ambalo linanipa shida sana katika Jimbo langu la Misungwi na limekuwa ni kero kubwa kwa watumishi wetu hao, ni tatizo la maji katika Chuo cha Ukiruguru. Nimezungumza kwa muda mrefu sana lakini utekelezaji wake haupo kabisa. Anayehusika ni Wizara hii na mwingine ni Wizara ya Fedha, mpaka leo wananchi wa maeneo hayo, watumishi wanateseka hawana maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishawahi kuuliza swali hapa Bungeni kwamba wanafuata maji Mwanza kwa roli mara ngapi, mara mbili, lakini hakuna utekelezaji. Wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Maji kule Ihelele, tuliongea na Mheshimiwa Waziri, yeye mwenyewe ndio akaniuliza Mheshimiwa Shibiliti, vipi suala lako la Ukiruguru. Sikuwa na jibu wakati ule, nikafuatilia, maana yeye alinihakikishia kwamba Jeshi limeanza kujenga, kitu ambacho hakipo kabisa. Ninapenda nipate majibu kwa leo ili watumishi hao na wananchi wa maeneo ya Mwalogwabagole, Buganda pamoja na Nyangorongo, waweze kuona watafaidikaje na mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao wataalam mbalimbali ambao wako Wizarani sasa hivi wamefanya kazi katika eneo hilo na tatizo hilo wameliacha likiwepo hapo. Ninaye Ndugu Kapande, ni Mkurugenzi wa Mafunzo, kile Chuo cha Mafunzo safari hii kinategemea kuwa na wanafunzi wasiopungua 260. Mwaka jana walikuwa na wanafunzi 180, watapata wapi huduma ya maji katika hali hiyo? Hawa ndio tunawahitaji, Maafisa Ugani ambao watakwenda vijijini, wanasoma kwenye mazingira magumu namna hiyo? Towni jibu ili wananchi wa maeneo hayo na watumishi wangu wa Ukiruguru, waweze kupata jibu la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie Mfuko wa Pembejeo. Nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 90, sikuamini katika macho yangu kwamba umepanga kununua matrekta makubwa 115, haya yalikuwa yanatosha kwa Mkoa wa Mwanza tu, lakini umepanga kwa nchi nzima. Jamani hivi tuna nia kweli na mfuko huu unawapa kazi ya kukopesha matrekta 115 kwa nchi nzima, Wilaya yangu yenyewe

kwanza haijafaidika kabisa na mfuko huu na Mkurugenzi nimwombe kabisa ajiandae, nitakuja na watu watano tu, hizi mia zingine utagawanya kwa nchi nzima ili angalau trekta tano zipatikane kwenye Wilaya ya Misungwi na hawa wananchi tayari wako na yapo maombi zaidi na wana kila sifa ya kuweza kununua matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu, mwaka jana tulitenga shilingi bilioni tatu baadaye kutokana na zile fedha za *EPA* shilingi bilioni tatu tukaongeza. Makusanyo ya madeni mengine wakapata shilingi bilioni 2.7 kwa maana nyingine mwaka jana wametumia shilingi bilioni 8.7, lakini mwaka huu katika bajeti hii umewapa shilingi bilioni 5.8, wameshuka. Kwa maana nyingine Mheshimiwa Waziri, jaribu kujipanga kama inawezekana uwaongeze warudi katika ile *level* ya mwanzo wapewe hata shilingi bilioni 10 hivi, ili hao wenye mfuko huo waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzia mambo ya ushirika na biashara za mazao. Kwa ruhusa yako, kabla sijaeleza haya matatizo yanayofuata, nisome majibu ambayo Mheshimiwa Waziri kama atayazingatia basi tutakuwa tumeondokana na matatizo hayo. Ukurasa wa 76 katika hotuba ya Waziri ameeleza hivi:-

*“Ni kutokana na ukweli huo, dhana ya Kilimo Kwanza inasisitiza umuhimu wa kuanzisha Benki ya Kilimo hapa nchini. Uanzishaji wa Benki hiyo umepewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2009/2010”, mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naendelea na matatizo. Nikiri kwanza Serikali imekuwa sikivu, Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa tunaongea hapa, wanayaelewa sana mambo yetu. Kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais alipoona tatizo la wafanyabiashara kwamba mwaka jana walipata hasara kwenye zao la pamba akatamka kwamba watasaidiwa katika vyombo vya fedha na baadaye waweze kufanya biashara ya kununua mazao yao. Cha ajabu hilo jibu nililolisoma kwa maana ya Benki zetu, zile Benki za *CRDB*, *NMB* na kadhalika sio mali yetu, kwa hiyo, matamko ya Serikali hayazingatiwi huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushahidi mpaka leo hii Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Shinyanga (*SHIRECU*), nao walikuwa kwenye mkumbo huo, walipata hasara, wangesaidiwa ili wapate fedha za kufanyia biashara kwa msimu huu, mpaka ninapozungumza hapa, hawajanunua hata kilo moja ya pamba, wamenyimwa mkopo na hivyo vyombo vya fedha, kwa maana nyingine sauti ya Serikali haijasikilizwa huko. Niombe sana Mheshimiwa Waziri, afuatilie suala hili vinginevyo hawa watu wa *SHIRECU* waahirishe kufanya kazi ya pamba mwaka huu, ni karibu mwezi mzima hawajafanya biashara sasa hivi. *Target* yao ilikuwa kilo milioni 15, wakinunua chini ya kilo hizo milioni 15 watapata hasara, wasaidieni ili waweze kufanya biashara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekee kwenye Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Mwanza. Bahati nzuri mwaka huu, wameanza vizuri wali-*target* kununua kilo milioni 55, lakini baadaye wakapunguza ikaja kwenye kilo milioni 15. Wao wamepata

mkopo na wameingia mkataba wa *CRDB* wa shilingi bilioni tatu, wamekwenda kuchukua hizo fedha wakapewa shilingi bilioni moja ya kuanzia. Wamesambaza kwenye Vyama vya Msingi, kwa mwikio wa wananchi pamba wamepeleka nyingi kuliko hiyo shilingi bilioni moja iliyosambazwa kwenye Vyama vya Msingi. Masharti ya Benki yakaanza kuingilia pale. Kwanza msombe hiyo pamba halafu ndio tuwaongeze zingine kutokana na ule mkopo wa shilingi bilioni tatu. Wamechukua shilingi bilioni moja tu, shilingi bilioni mbili bado ziko Benki na wamezuiwa mpaka wasombe pamba yote ya shilingi bilioni moja iliyoko kijijini wakati tayari wananchi walikuwa wameshazidi hii shilingi bilioni moja iliyosambazwa kwenye Vyama vya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ni kwenye Chama cha Msingi cha Butobela, kulikuwa na zaidi ya kilo 54,000, kati ya kilo 20,000 zilikuwa hazijalipiwa, umma ulikwenda pale kuzuia pamba hii isisombwe kwanza mpaka hizo kilo 20,000 zilipwe. Wakazuia pamba, kwa hiyo, usombaji wa pamba kutoka kwenye Vyama vya Msingi umeshindikana, ni matatizo makubwa sana, jibu ni Benki ya Wakulima. Hivi vyombo vingine wakati wa kukopa ni wazuri kweli, baada tu ya kusaini mkataba, wanaanza matatizo makubwa. Wahasibu kwenye Vyama vya Msingi sasa hivi hawapo kabisa kwa kuhofia kupigwa. Watu wanahitaji wagawane pamba yao na hiyo pamba imechanganyika na iko pamba iliyolipiwa na nyingine haijalipiwa ni vigumu sana kupambanua hayo maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri ingilia kati. Kwa bahati mbaya sana katika kijiji cha Bujula kuna kilo 17,000 zimechomwa moto kutokana na ugomvi ugomvi huo. Tayari Polisi wa Geita wameshakamata hawa wahusika na utaratibu unaendelea wa kuangalia pamba ambayo haijahiribika zaidi. Hayo ni matatizo ambayo yanatokana na *CRDB* kutotoa fedha wakati mkataba wamesaini shilingi bilioni tatu. Meneja Mkuu ni kutoka Serikalini, Mhasibu Mkuu ni kutoka Serikalini, kwa nini wasiaminiwe hawa watu wazuri? Juzi juzi wamechagua viongozi wengine ni wazuri sana, lakini wameshindwa kuaminika. Nikuombe Mheshimiwa Waziri lifuatilie suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Bodi za Mazao Mchanganyiko. Tuna tatizo kubwa sana la mazao mchanganyiko. Sisi Mkoa wa Mwanza na Shinyanga, tuna zao kubwa sana la dengi, lakini halina Bodi na wananchi wanajuzia tu hawajui utaratibu wowote unaoendelea. Tujitahidi sana tupate chombo hicho ili angalau wakulima wa dengi nao waweze kunufaika na zao lao hilo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu, maandalizi ya msimu yanaanza sasa, Bodi ya Pamba kwanza ianze kutangaza ile tofauti ya bei kutoka shilingi 360/= kwenda shilingi 440/= ile shilingi 80/= wambe kwa kutumia vyombo vya habari, wapeleke taarifa kwenye vyombo, watangaze mara kwa mara hiyo shilingi 80/= itapatikanaji ili watu wasipunjwe. Lakini pia ugawaji wa madawa sasa ungelipeleka kwenye Vyama vya Msingi au eneo lolote linalohusika kutokana na mauzo haya ya pamba yanayoendelea watu waweze kujiwekea akiba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, ninaona kabisa niishie hapo na kuomba Serikali ifuatilie kwa kina sana ili angalau wakulima hawa waweze kunufaika na zao la pamba. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninapenda nimwite Mheshimiwa Michael Laizer achange kwa sababu tunazo dakika 10 nisingependa kuzipoteza hivi hivi. Lakini kwa kutumia kanuni ya 28(2), inaniwezesha kuongeza muda, nitakaoongeza, ni wa dakika tano.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nakushukuru kwa kuniongezea dakika hizi tano ili niweze kusema machache kuhusu Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kusema kwamba katika Jimbo langu nadhani ni Jimbo mojawapo ambalo lina njaa kubwa sana. Leo nimesikia kwenye magazeti wakisema kwamba Jimbo la Longido liko hatarini watu kufa njaa. Lakini naishukuru Serikali sana kwa sababu walituingalia kwa jicho la huruma na wametupa tani 3,600 naishukuru sana Serikali. Nilipokwenda Jimboni, kuona hali ni mbaya, nikamtumia meseji, kwa kweli walishirikiana na Waziri Marmo akaja Jimboni akaona hali kwamba sio nzuri. Lakini bado tunaomba fedha za kusambaza chakula, hazikupelekwa fedha za kutosha, kwa hiyo, chakula hicho bado hakijagawanywa kutokana na uhaba wa fedha za kusambaza katika maeneo ili wananchi wapate chakula. Bado naiomba Serikali watupe hizo fedha ili wananchi waweze kupata chakula wasife njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kusema machache kuhusu kilimo. Labda wenzangu watafikiri kwamba Longido ni Jimbo la wafugaji tu, lakini sivyo, Longido kuna Kata za wakulima. Ukienda huko West Kilimanjaro, ni wakulima wazuri wa ngano, maharagwe, mahindi, kwa hiyo, wanalima mazao ya biashara. Tunapakana na ndugu yangu Mwanri pale, anajua kabisa kwamba katika Kata zetu zilizoko West Kilimanjaro, ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachoshangaa ugawaji wa pembejeo unaelekezwa kwenye baadhi ya maeneo lakini sijawahi kuona pembejeo zikielekezwa huko West Kilimanjaro. Sijui ni wakulima wa mashamba makubwa kiasi gani ndio wanastahili wapewe pembejeo!

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa kidogo kwa sababu kuna jambo ambalo Serikali hawajalitia maanani kuhusu mkopo. Mkopo unaozungumzia ni mkopo wa watu wenye uwezo, ni mkopo wa matajiri, sijui mkulima mdogo mdogo katika maeneo yangu atapataje mkopo huu, kwa sababu mashamba yenye hati kwanza hawana. Ukimwambia alipie sehemu ya vocha hana fedha, anategemea mpaka apate mazao, kwa nini yale mazao ya shamba lake yasiwekwe rehani, kwa sababu anategemea kwamba baadaye atapata mavuno?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado hatujamuangalia mkulima mdogo. Mkulima mdogo hata kama hauzi lakini awe anajitosheleza kwa chakula, bado ameisaidia Serikali hii kwa sababu Serikali haitafuti tena chakula cha kuwapelekea wananchi. Kila mtu akijitosheleza sio mpaka uwe na chakula cha ziada cha kuuza nje au za kufanya biashara, inasaidia Serikali. Naomba Mheshimiwa Waziri au Serikali iangalie jambo hilo ili wakulima wadogo wafaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakulima wadogo ambao hawawezi wakachukua matrekta, uwezo wake ni kupata jembe la kukokotwa na wanyama, lakini hata hilo jembe hawezi kununua, nao wangepewa mkopo ili wapate haya majembe ya kukokotwa na mifugo kwa mkopo. Huo ndio uwezo wake. Hata ukinunua matrekta hatuwezi tukanunua kila mtu awe na trekta lake kutokana na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni soko. Jimbo langu tunapakana na Kenya. Soko kubwa katika maeneo ya mipakani, bahati mbaya sisi hatuna soko lililoko upande wa Tanzania, masoko yote yako mpakani upande wa Kenya. Kwa hiyo, huwezi ukataka kuuza chakula ukapeleka sehemu nyingine mpaka Arusha unaona ni mbali. Halafu baya zaidi upande wa Kenya ndio kuna bei. Sasa kwanza, ni gharama kupeleka mazao masoko yaliyoko huko kwetu Tanzania, ya huku Kenya ndiyo yako karibu, lakini unaambiwa usiuze huko Kenya, inatupa shida kidogo kwa sababu kule Rombo tunakopakana na soko, wanauza Kenya. Kata yangu ya Olomog wanauza nao huko huko kwa sababu ndiko kuna soko ambalo lina fedha na liko karibu. Kama ukimwambia mwananchi tumia soko lililoko mahali fulani basi ulete wafanyabiashara waje kununua mazao katika maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia, ni madhara yaliyoletwa na ukame huu. Katika maeneo ya Jimbo langu, kuna wazazi ambao wameshindwa kuwasomesha watoto, watoto wako nyumbani wanakwenda shuleni wanarudishwa kwa ajili ya ada na unashindwa la kumwambia huyo mzazi kwa sababu hana uwezo na hana kitu cha kuuza, ukame umeleta madhara makubwa. Naomba Serikali itafute namna ya kuwasaidia hao watoto kwa sababu wanafunzi wengi sana wako nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi mzazi mmoja ananipigia simu ananiambia sasa ni afadhali ukatishie Bunge uje kutafuta namna ya kuwapeleka hawa watoto shuleni kwa sababu watoto hawapo shuleni wako nyumbani kwa sababu ya kukosa ada. Sasa mimi sina fedha za kuweza kuwalipia ada watoto wote ambao wazazi wao wameshindwa kuwasomesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia, ni watalaam Maafisa Ugani. Katika Kata zetu, Kata zetu ni Kata kubwa halafu vijiji viko mbalimbali. Kata moja ya Kitumbeni, kijiji kiko kilomita 60, kingine kilomita 53, kingine kilomita 45 ndivyo ilivyo katika Kata zetu. Sasa Afisa Ugani atatembeleaje mashamba yote ya wakulima kutoa elimu, haiwezekani? Mbaya zaidi, unakuta kuna Kata ambazo hawana Maafisa Ugani, sasa hii elimu sijui itatolewaje?



Mheshimiwa Naibu Spika, ebu tuangalie na kilimo hiki kwamba hivi eka moja tunavuna kiasi gani cha chakula? Kama unavuna kwa eka moja gunia tatu au tano, sasa utalima eneo gani, ukubwa gani wa kupata chakula cha kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, tusingalie tu kwamba tuna mashamba, tuangalie na elimu ya kuwaelekeza watu wetu ili watumie eneo dogo kwa kuzalisha chakula kingi. Kama mnavyotambia sisi wafugaji, mnapenda kusema kwamba punguzeni mifugo muwe na mifugo michache yenye tija, mbona hamzungumzii eneo dogo la kuzalisha chakula kingi? Mnaona inawezekana kila mahali liwe ni shamba basi tuangalie na ukubwa wa shamba na mazao kwamba hili shamba linazalisha kiasi gani cha chakula, isiwe mashamba tu. Kwa sababu katika maeneo yetu ndivyo ilivyo, lakini kitaalam wanasema kwamba eka moja kwa magunia 30, hivi ni kweli eka zetu zinazalisha magunia 30, hata magunia 10 hayafiki. Kwa hiyo, ule wingi hausaidii mashamba yenu ni makubwa lakini hayazalishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mgogoro wa wafugaji na wakulima. Naona ni halali kwa mkulima kuwa na shamba kila mahali, yeye kwake ni halali, lakini kwa mfugaji sio halali kufuga kila mahali na kila bonde ni la mkulima. Naomba Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo, wakutane, wapange utaratibu, sio halali mkulima kwenda kumvamia mfugaji na kulima katika maeneo ya malisho, mnakosea sana na ninyi ndio mnatuletea migogoro kwa kumpa mtu mmoja uhalali wa kulima kila mahali kilimo ambacho hakina tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule Tabora, sijawahi kuona kilimo cha kuhamahama, mfugaji ndiyo anahama, unalima miaka miwili, unahama unakwenda kuanza shamba lingine, sijawahi kuona na kwetu hakuna mashamba ya kuhamahama, shamba lako ni hili ndio unalima kila wakati lakini wanaruhusiwa, wangukuwa wafugaji ndio wanahamama hivyo wangufukuzwa kama mnavyowafukuza sasa. Kwa hiyo, ninapenda tu kusema na huo utaratibu wa kilimo bora ambacho hakina tija kizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika baadhi ya Kata zangu ambazo ziko milimani hakuna namna ya kupeleka trekta huko, wao wanachotaka ni majembe ya kukokotwa na wanyama. Nawaombeni mtusaidie sisi majembe hayo. Nashukuru sana na naunga mkono. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Hii pointi ya mwisho ya kwamba eka moja watu wapate kingi, kwa kweli ni muhimu sana.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, tukirudi mchana, nakusudia kuwapa nafasi Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa John Lwanji na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Hawa ni wale waliozungumza mara mbili ndio watakuwa wameishia na baada ya hapo nitamwita Naibu Waziri dakika zake 15 halafu Waziri tunaendelea kama kawaida.

Waheshimiwa Wabunge akinamama, kuna *DVDs* yenu mkaichukue katika Ofisi ya *TWPG*. Mlifanya maonyesho wakati Fulani, mkachukue kule juu.

Halafu Mheshimiwa Chibulunje amepumzishwa Hospitali ya Mkoa anaendelea vizuri. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, sasa mkienda wote kule sio kwamba atapumzika mtamsumbua. Sasa nashauri asiende mtu mpaka jioni, sio mtamsaidia, mtamsumbua tu. Sisi tunawapa taarifa ya kiofisi kwamba anaendelea vizuri, mwacheni apumzike.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.04 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati nasitisha shughuli za Bunge leo asubuhi, niliwataja wafuatao kuwa ndiyo watakuwa wachangiaji wetu katika hoja hii. Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Paul Lwanji na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Mheshimiwa Malangalila karibu!

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii. Lakini kabla ya hapo, namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa ili na mimi nichangie hotuba ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuishukuru Serikali kwa namna ilivyokubali kutoa ruzuku katika pembejeo za kilimo. Jambo hili limezungumzwa muda mrefu sana. Nilianza kulizungumzia suala hili tangu mwaka 1996.

**NAIBU SPIKA:** Ukijaribu *microphone* nyingine inakuaje? Tumia *microphone* nyingine!

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nianze upya. Nimesema, kwanza, nikushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi hii na pili nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo imetoa ruzuku katika pembejeo za kilimo, nadhani kuanzia mwaka 1997 na 1998. Kwa kweli, tunaishukuru sana Serikali. Lakini pamoja na kutoa ruzuku hii, mwaka jana nilisema kwamba kwa upande wa mbolea, nadhani sehemu kubwa ya fedha hizi zilitumika kununulia mbolea ya Minjingu. Kwa Wilaya ya Mufindi, kwa kweli haikuwa na manufaa

kwa sababu mazao yaliyopandiwa mbolea ya Minjingu hasusani mahindi, hayakuwa mazuri hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati alipokuwa anajibu swali la Mheshimiwa Zamboni alisema Serikali haitatoa mbolea ya Minjingu kule Mbozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nikiwa Mbunge wa Mufindi Kusini, nadhani nilikuwa ni mtu wa kwanza kuiuliza Serikali juu ya mbolea ya Minjingu kwamba ni mbolea ambayo ilikuwa haisaidii chochote kwa wakulima wa mazao ya mahindi hususan katika Wilaya yetu ya Mufindi. Bado hoja yangu iko palepale. Sisi tulizoea kutumia *DAP* kupandia mahindi na miaka yote tumekuwa tukipata mahindi ya kutosha lakini tulivyoanza kutumia mbolea ya Minjingu, kwa kweli watu wote waliotumia mwaka huu hawana mahindi kabisa. Kwa hiyo, hii ndiyo ilikuwa hoja yangu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote hivi sasa tunalalamika kwamba hakuna chakula. Mataifa makubwa kama Marekani wanasema hawana nafaka za kutosha. Kaya zetu pia tumelalamika hatuna nafaka za kutosha na Taifa letu la Tanzania nalo linalalamika kwamba halina nafaka za kutosha. Sasa tunatakiwa tufanye nini katika mazingira kama haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyovyote, kama Tanzania yatupasa tutafute kila mbinu kuhakikisha kwamba tunazalisha chakula cha kujitosheleza sisi wenyewe. Tunazo *scheme* nyingi sana za umwagiliaji, Serikali ihakikishe kwamba inafufua miradi yote ya umwagiliaji katika nchi hii na pia inaanzisha miradi mipya ya umwagiliaji ili tuweze kuzalisha chakula chetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika Mikoa ambayo inasemwa ina chakula cha kutosha ukiwemo Mkoa wa Iringa, mimi sina hakika juu ya jambo hili kwa sababu kwa mfano Wilaya ya Mufindi, ina Kata karibu 28, nina hakika katika Kata hizi, kuna Kata nane hazina chakula cha kutosha. Nikianza na Ihowanza, Idunda, Itandula, Mtambula, Sadani hakuna chakula cha kutosha na baadhi ya Kata nyingine. Kwa hiyo, hizi taarifa ambazo Serikali inatuambia humu Bungeni, ninashauri wataalam wafanye utafiti wa kutosha. Kwa sababu unapoutangazia ulimwengu kwamba Mkoa wa Iringa una chakula halafu baadaye ije ithibitike kwamba chakula kile hakitoshelezi, hivi unawaambiaje watu wa mataifa mengine? Kwa hiyo, napenda Serikali inapoleta taarifa yoyote ndani ya Bunge hili iwe imejiridhisha kwamba taarifa hiyo ni ya kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo zamani tuliwahi kupata njaa tukatoa Azimio la Iringa. Azimio lile lilikuwa linasema 'Siasa ni Kilimo' na kweli viongozi walitoka maofisini, walienda kukaa vijijini, walihamishiwa huko. Mmoja wa viongozi waliohamishiwa huko ni Mheshimiwa Dr. Kigoda wakati huo alikuwa ana digrii moja. Alihamishiwa Njombe, alikaa mwaka mzima kule na wananchi walihamasika, wakalima mahindi ya kutosha si mahindi tu watu wa Dodoma walilima mtama wa kutosha. Baada

ya lile azimio tuliona manufaa yake. Sasa hili neno Kilimo Kwanza tuna mkakati gani kuhakikisha kwamba kweli tutazalisha mazao ya chakula ya kutosha? Kweli tutazalisha mazao ya biashara ya kutosha? Au ni maneno tu ambayo tumeyasema. Mkakati gani ambao Serikali imeuweka kuhakikisha kwamba kweli tutazalisha vya kutosha kutokana na hii kauli ya Kilimo Kwanza? Kwa sababu ni kauli nzito sana lakini tunaweza?

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia tulivyoweza katika elimu. Tumefanikisha kuwa na shule ya msingi moja au mbili katika nchi nzima. Kama tumefanikisha kujenga shule, naiomba Serikali ihakikishe kwamba kweli tunakuwa na mazao ya kutosha ya chakula na biashara pia. Namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze mkakati wa kweli na dhati kabisa ambao Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote tutatoka hapa tukifurahi kwamba Serikali imeweza mkakati wa kuhakikisha kwamba kuanzia mwakani tuna chakula cha kutosha na miaka mingine yote inayofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua hapo zamani tulipata njaa, tukawa tunakimbilia Marekani kuomba msaada wa chakula. Wamerekani wakawa wanatusaidia. Sasa hivi Marekani wenyewe wanasema hawana chakula cha kutosha, sasa tukipata njaa, hivi tunakimbilia wapi? Kwa bahati mbaya zaidi kama njaa inaingia watu wa kwanza kufa watakuwa wanakijiji, wakulima hawa maskini. Sio watu wa mijini na sisi Wabunge, wengi wetu tunawakilisha wakulima wale maskini wa vijijini. Kwa hiyo, naomba Wabunge wote tena kwa bahati nzuri hata Mawaziri nao wapigakura wao ni wakulima, kwa hiyo, naomba Serikali yote kwa sababu iko hapa imeelewa kwamba nia yangu ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na chakula cha kutosha kabisa kwa watu wa mijini na watu wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya zaidi, mwakani ni wakati wa uchaguzi, hivi umewahi kwenda kijiji kina njaa ukahutubia mkutano wa hadhara? Nimewahi kwenda kijiji kimoja kinaitwa Kiponda, ulikuwa mwaka wa njaa, wakaniambia hivi Mheshimiwa Mbunge umekuja kutafuta nini? Walivyokuwa wamekasirika, nikasema jamani nimekuja kuwatembelea tu. Wala sikufanya mkutano maana wangeweza kunirushia mawe pale. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wabunge wenzangu, maana sisi wote tuliomo humu ndani ya jengo hili na labda Mwanasheria Mkuu wa Serikali peke yake, napenda tuone kwamba hili ni jambo kubwa na lenye uzito mkubwa kabisa hususani Chama Tawala na mimi ni mmoja wa Wabunge wa Chama Tawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za nyuma, Mkoa wa Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma, tuliwahi kulima mahindi mengi sana. Kati ya mwaka 1997 – 2000, tulikuwa na mahindi mengi mpaka yakakosa soko. Napenda Taifa hili tufike huko. Tuzalisha mazao ya chakula mengi, tuwe tunahangaikia soko. Tuwe tunakula tunashiba, tukishashiba tunatafuta masoko, tuwauzie wenzetu wenye shida ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jamani mbona katika miaka kumi ya uhuru wa nchi hii, tuliwaita wakoloni waliotutawala waje watembelee nchi yetu, mbona hatuwaiti tena? Nadhani lipo tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie Maafisa Ugani. Hawa Maafisa Ugani, kazi yao kwa kweli ni kusaidia kuwafundisha wakulima kilimo bora vijijini. Lakini kwa bahati mbaya, hawana vitendea kazi na vyombo vya usafiri. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe kwamba Maafisa Ugani hawa wanapewa vyombo vya usafiri hususani pikipiki ili waweze kuwa na uwezo wa kutoka kijiji kimoja hadi kijiji kingine. Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Afisa Kilimo wa Wilaya awe anawakagua hawa, sio kwamba katika Kata anamwachia kila kitu. Mimi nakumbuka wakati nakua, hawa Maafisa Kilimo walikuwa wanatembelea mashamba ya wakulima na kama wakiona shamba lako bovu, mahindi sio mazuri anakuuliza kwanini na anakupiga hata faini lakini leo Maafisa Ugani sijui kama hiyo Sheria ipo. Afisa Ugani anaona shamba lako mahindi ya njano tu anakwambia bwana rekebisha hapa na hapa, haitoshi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ni hali ya mvua, watu wanashuhudia mvua zimekuwa haba sana. Sasa sijui tufanye nini. Mimi nakumbuka kule Isimani nilivyokuwa mdogo, tulikuwa tunalima na mtu wa kwanza kumwona akilima kwa trekta alikuwa babu yangu, marehemu Abdallah Malangalila. Sasa leo hii ukienda Isimani, hakika utatoa machozi, kuna alizeti zilichanua tu zikakauka.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikwenda Chamwino pale ukifika debe la mahindi shilingi 7,000/- na nikamuuliza mwananchi mmoja anasema mahindi mwaka huu yatafika mpaka shilingi 15,000/-. Chamwino ni kijijini si kheri yafike 15,000/- hapa Dodoma mjini, sasa mwanakijiji shilingi 15,000/- atoa wapi wakati leo ukimpa shilingi 200/- anataka apige magoti, akubusu kwenye miguu yako kwa sababu umempa hela nyingi sana, sasa shilingi 15,000/- itakuwaje? Ni dhahiri kabisa wanakijiji wetu watakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumwombe Mungu sana, yatupasa twende Makanisani na Misikitini tumwombe Mungu afungue milango ya mvua, mito na mabwawa yajae, ili neema ya Mungu ikashuke duniani na ishuke Tanzania, ikashuke Majimboni kwetu ili tupate chakula cha kutosha.

**MBUNGE FULANI:** Twende kwa Waganga!

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mimi sijasema waganga, nimesema watu wa madhehebu na watu wa dini zote yafaa tuombe Mungu ili kwamba afungue milango mvua inyeshe, Vinginevyo Taifa hili tutakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la mwisho. Naiomba Serikali isomeshe wataalam wengi wa kilimo. Nimeona katika hotuba... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nianze kwa kuwashukuru watoa hoja, Waziri na Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, kwa jinsi walivyoshughulikia matatizo ya tumbaku kule kwenye maeneo yetu tunayolima tumbaku ya Mgandu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalima tumbaku nzuri sana kule na wenzetu walikuwa na matatizo ya bei ya tumbaku na mwaka jana walikuja hapa, nilipata nafasi nzuri sana ya kumwona Waziri, wakarekebisha matatizo hayo. Mpaka ninapozungumza hapa, sijawaona tena wanakuja kunisumbua. Kwa hiyo, nitoe shukrani na habari nilizonazo ni kwamba wameridhia na sasa hivi zao hili wanaendelea kulilima vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zao hili linapigwa vita na wengi hawapendi kuona wenzao wanavuta sigara kwa sababu ya madhara mbalimbali. Lakini kuna haja ya kuwaelekeza hao watu wavute kwa busara ili mradi na zao hili liweze kulimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili zao naona limeingiliwa katika soko. Tunaanza kuona tumbaku ambayo si halisi, wavutaji wa tumbaku wanalalamika. Mimi bahati nzuri sivuti tumbaki lakini sasa hivi huko madukani kuna sigara aina ya *Portsmen* ambayo ina *brand* ya *Sportsman*, sasa sielewi kama ni *Sportsman* lakini imeandikwa *Portsmen*. Nembo na kila kitu ni *Sportsman* na ushahidi ni huu hapa ninao.

*(Mheshimiwa Mbunge alionyesha paketi ya sigara)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, watakuletea, imeandikwa *Portsmen* lakini nembo na kila kitu ni *Sportsman*. Haraka haraka ukinunua wewe unadhani ni *Sportsman*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hili hapa kwa sababu sidhani kama nitapata nafasi kwenye Wizara ya Viwanda kwa utaratibu huu tulionao sasa hivi kwa sababu ni mara ya tatu nachangia. Hili ni zao langu wasije wakaharibu soko hili la tumbaku yetu nzuri ikasusiwa nje tukarudi tena kwenye matatizo. Napenda kupata maelezo maana wavutaji wanasema wakivuta hii wanapata kwikwi na kunywa maji sana. Sasa hii tumbaku ni aina gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo kwa ujumla, takwimu sio nzuri na taarifa ya Umoja wa Mataifa ya *United Nations Millennium Development Goals*, inasema hivi, Tanzania ni mojawapo ya nchi kumi duniani zenye uchumi duni kwa kigezo cha mapato ya mtu binafsi *per capita income*. Uchumi wake unategemea sana kilimo ambacho nacho hakijaendelezwa. Kilimo kinachangia asilimia 40 ya pato la Taifa, *GDP*. Kinachangia asilimia 85 ya mauzo yote ya nje na kuajiri asilimia 80, wengi wao wakiwa wakulima wadogo wadogo na wafugaji. Kutokana na hali ya hewa, ni asilimia nne tu ya eneo linatumika kwa kilimo. Kilimo kikiendelezwa, kinaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza umaskini na hii inawezekana kwa kuelekeza sera sahihi kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kimiti, hapa alivyozungumza asubuhi kwamba wamepita Mawaziri 21 wa kilimo toka tumepata uhuru, hapa hatujawahi kuwa na sera sahihi hata siku moja. Hii sekta imesusiwa na Mkoloni alituachia kasumba mbaya sana, sijui ni kirusi gani walituwekea sisi, hatupendi kilimo. Hata mtoto unamsomesha,

unamwambia mwanangu kua uje uwe Mbunge, uwe Waziri, uwe Mkurugenzi lakini hata siku moja sijawahi kusikia unamwambia mwanangu soma uje uwe mkulima, hata siku moja! Kwa hiyo, *mind set* zetu hazipo kwenye kilimo hata siku moja. Sisi ni *for white collar jobs*, tai na koti na sasa hivi ndiyo kabisa. Sasa sielewi huyu mdudu tuliyeachiwa na huyu Mkoloni atatoka lini katika *mind set* zetu, haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa katika takwimu kuwa tuna heka milioni 29.4 za *arable land* lakini ni heka laki tatu na ndizo zinazolimwa na ndiyo hizo asilimia nne zinazolimwa nchi nzima. Kilimo kinachohusisha matrekta ni asilimia 10 na kilimo kinachohusisha *plough*, ni asilimia 20 na kilimo kinachohusisha jembe la mkono ni asilimia 70. Inaeleweka kabisa na tuna ng'ombe milioni 18 hadi 20. Nadhani sera sahihi ni kuwatoa hawa watu wa asilimia 70 kuja hapa kwenye asilimia 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kumekuwepo na uhasama kati ya wafugaji na wakulima na haturekebishi hali hii na kuwapatanisha. Mkulima anamwonea wivu mfugaji lakini mkulima angewezesha apate maksai wa kulima angekuwa rafiki wa mfugaji. Sasa nashindwa hata kuelewa, ile ripoti ya Jaji Chande ya Ihefu, sielewi walipendekeza nini. Lakini hakuna sababu hapa Tanzania kuwa na uhasama kati ya mkulima na mfugaji. Pesa hizi nyingi za kuagiza matrekta na *power tillers* hizi zingekwenda kununua *plough*, kila kaya ikagawiwa maksai wanne wanne hawa watu watafufuka kwa kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati nauliza swali, nilisema wananchi wangu wa Kitopeni wanahitaji umeme na nikasema ni matajiri, nilikuwa nina maana ya utajiri katika ulingo wetu kule. Hatuwezi kufanana sana na watu wengine lakini katika hali yetu ya kule wao wanatumia sana *plough*. Hakuna umaskini ndani ya nyumba hizo, wanakunywa maziwa, watoto hawana kwashakoo na Kitopeni ni kati ya kijiji ambacho kinatoa *the best students* katika eneo letu. Mwaka juzi walikuwa ndiyo wa kwanza Kimkoa kwa sababu watoto wametulia, wazazi wao wanalima vizuri. Sasa mimi naomba tutazame na tukazie zaidi kilimo cha maksai.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Blandes!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia Kanuni ya 68 ya Kanuni za Bunge na hapa tulipoingia jioni hii, nilijaribu kuangalia upande wa wenzetu wa Upinzani na wakati nasimama, walikuwepo wenzetu wawili na sasa hivi wawili ndiyo wanaingia lakini pia niliangalia Kiti cha Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kimekuwa wazi kwa muda wote. Sasa kwa kuwa ni mara ya kwanza kutokea, mimi imenipa shida sana pengine kuna tatizo limetokea. Kwa hiyo, ninaomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana. Kilichotokea ni kwamba hata ninyi wote mlikuwa hampo ndiyo sasa mnaingia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Lwanji, utaongezewa dakika zako.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nilikuwa nasisitiza juu ya umuhimu wa kilimo cha wanyama kazi. Kweli ndugu zangu ninawaomba mje muone hivi vijiji hata cha kwangu, kijiji cha Sanjaranda jinsi wanavyojishughulisha na kilimo cha maksai. Wao wameweka kaumoja, wanaalikana wakati wa kilimo, wewe leo tunakuja kwako heka zako kumi zinalimwa siku hiyo hiyo. Wewe unachotakiwa ni kuchinja kuku au mbuzi, ndiyo gharama. Sijawahi kusikia maksai wamefungwa *plough* halafu wanakwenda kituo cha mafuta kuweka mafuta, sijawahi kusikia. Mnyama anaamka asubuhi anafungwa, anakwenda *straight forward* shambani, hakuna haja ya kusema kwamba kuna tatizo la *spares*, ile *plough* ina *spanner* moja tu ya kukaza *nut* basi na kubadili ule ulimi unaolima, hakuna kitu kingine zaidi lakini tunakipuuza. Tunataka kufanana na nchi zinazoendelea kwamba ni lazima tuwe na matrekta, sasa unaambiwa juzi Mkoa mzima wa Tabora una trekta tatu, *can you imagine?* Ukichukua Wilaya muhimu kama Nzega, Igunga ambako kuna matajiri kule kuna matrekta matatu, tuliambiwa hapa. Zimekwenda wapi? *Definitely* trekta hizi ziko kwenye mawe wanashindwa kuzi-*service*. *Power tillers* zenyewe ni za muda mfupi tu baada ya hapo ikiharibika utapata wapi nyingine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiende mbali, tuwainue hawa asilimia 70 waje kwenye asilimia 30, hawa kumi tusihangaike nao, wenyewe watatafuta, watajua ni wapi watakwenda kuyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera nyingine sahihi ni hii ya juzi Mheshimiwa Rais alipokwenda kufungua mradi wa maji wa Ziwa Victoria. Huu mradi ndiyo mkombozi. Mimi nafikiri kwenye Mikoa yetu hii ya Tabora, Singida na Dodoma, mradi huu ufike ili watu waweze kutumia maji. Tatizo kubwa hapa ni ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwana mmoja katika kuepuka adha za Kariakoo kule, alikuwa Machinga, baada ya kukoswakoswa na marungu ya Askari wa Jiji, akaamua kurudi nyumbani. Nisiseme Machinga, samahani sana, ni biashara ndogo ndogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi alipoamua kurudi nyumbani, ana kamtaji kake, akaanza kilimo, haikuwa kwetu, kwetu Mungu ametujalia pale, lakini ilikuwa maeneo mengine. Basi akaenda kule kwao akanzisha kilimo kwa mtaji huo, basi mvua za kwanza zikanyesha lakini zikanyesha mvua mbili tu, kabla mazao hayajabeba, mvua zikaondoka na hazikurudi, ikabidi akumbuke tena Kariakoo. Wenzake wakamwambia, vumilia bwana, basi akavumilia. *This time* akaenda kutafuta sehemu ambayo si mwinuko sana, kwenye mbuga au bonde, maana aliona wenzake walipata. Akalima heka tano (5), mvua zilipokuja mwaka ule wa pili, zikakuta mahindi yameota vizuri na mtama na nini, ziliporudi mvua zikaja kubwa zikaosha kila kitu, hakupata kitu. Sasa huyo mtu yuko Kariakoo mpaka sasa hivi. Alirudi akasema afadhali nifie mjini, kuliko kurudi kijijini. Kwa hiyo, mtaona kilimo chetu ni cha kuku wa kienyeji. Hatuna tofauti, ni cha kubahatisha tu. (*Kicheko*)



Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikirudi sehemu ya kwetu ambayo tunalima sana alizeti pamoja na dengi, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, haya mazao mchanganyiko bado hawajayaangalia. Ukienda Kitopeni, Sengeranda, Ipande utakuta marundo kwa marundo ya dengi, soko ni meli moja kutoka India huwa inakuja mwezi Agosti na hivi sasa walanguzi ndio wanapita kule kununua kwa bei wanayoitaka wao lakini ikiishafika ile meli bei inapanda, ikiondoka ile meli bei inashuka. Walaji wa dengi ni wenzetu Wahindi kwa hiyo, hiyo meli inakuja mara moja, inatia nanga inakaa wiki mbili, tatu, inakusanya dengi zote, inaondoka lakini bei bado haieleweki.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ni-*declare interest*, mimi mwenyewe ninalima alizeti, ninayo nyingi sana safari hii. Mwaka jana niliwauzia hata wenzangu hapa mafuta ya alizeti lakini sasa hivi siwezi kuleta mafuta kwa sababu hakuna bei na siwezi kuja kuwadanganya Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa ili niwalangue, itakuwa si vizuri. Niwauzie hapa dumu au debe shilingi elfu arobaini (40,000) au elfu hamsini (50,000) halafu wapite sokoni wakute ni shilingi elfu Ishirini (20,000), nitaweka wapi uso wangu hapa? Kwa hiyo, inabidi sasa nihodhi, nisubiri na wale wanaotaka hayo mafuta, samahani sana msubiri mpaka labda mwezi wa kumi na mbili, mwezi wa kwanza mwakani tuweze kufanya biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namfahamu bwana mmoja kule kijijini, yeye amehodhi alizeti na dengi, ni mwaka wa pili sasa, ameweka nyumbani kwake, haiharibiki, tatizo ni panya tu lakini haiharibiki, anasubiri bei akiambiwa bwana bei iko pale, anasema aah hatuna uhakika, sasa tumeshauri Bodi ya Mazao Mchanganyiko iundwe hakuna, sasa Mheshimiwa tungependa kupata maelezo, kuna tatizo gani kuhusu haya mazao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Mkoa wetu, viongozi wote wamejaribu sasa kuhamasisha watu walime zao hili lakini inakuwa kitendawili, watu wana shida zao, wanataka kupeleka watoto shule, wanataka kununua mahitaji ya lazima, ada na nini lakini wanashindwa, kwa hiyo, inabidi wauze na wengine wanauza mazao yakiwa shambani, walanguzi wanapita pale wanauwauzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli kununua gunia la alizeti kwa shilingi elfu kumi (10,000), ni halali kweli? Mkulima ana *breakeven* vipi? Nguvu zake zinakwenda vipi? Mimi nafikiri tukabiliane na tatizo hili na kilimo chetu kigeuke, *revolution* ya hiki kilimo kiwe kilimo cha maksai. Naomba pia tatizo la ukame liangaliwe kwa undani sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana lakini tumekuwa tukisema mara nyingi kwamba, Msingi wa Maendeleo ni Ardhi, Watu, Siasa Safi na Uongozi bora, ndiyo tumekuwa tukisema hivyo. Hivi vyote tunavyo lakini sasa sielewi maana siku hizi mtaani wanasema sio vitu vinne ni vitano, ukiuliza cha tano ni kipi wanasema ni pamoja na mfadhili au wanaita Mzungu, unaona hiyo?

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwishakwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, nashukuru sana na hongera kwa kulima alizeti.

Sasa nitamwita Mheshimiwa Ruth Msafiri, kwa upande wa Bunge atakuwa mchangiaji wa mwisho kwa hoja hii.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja ya Wizara hii kwa jioni ya leo, nikiwa ndio mchangiaji wa mwisho kwa upande wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa Serikali, kwa majibu ambayo imenipatia kufuatia hoja niliyoitoa hapa Bungeni tarehe 3 Julai, 2009 nikiomba wale wananchi wa kule Rutoro kwenye Ranchi ya Kagoma ambao walikuwa wanafukuzwa, wafikiriwe. Serikali imenijibu kwa maandishi na kusema kwamba, wananchi wasifukuzwe mpaka kesi yao Na. 305 ya mwaka 2007, imalizike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili nikiwa namaanisha kwamba, wale wawekezaji ambao walikuwa wamekwishaweka matangazo kwamba, wananchi waondoke ifikapo tarehe 30 Julai, 2009, imekwishabatilishwa na barua ninayo, ni hii hapa na Wizara imeahidi kwamba itatuma Wataalam wake kwenda kulifuatilia suala hili kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, ninafurahi na ninaishukuru Serikali kwa sababu imewafikiria wananchi na mimi nilikuwa nashangazwa kwamba Serikali itawapaje nafasi watu 16 halafu ikasahau maelfu ya wananchi ambao wanaishi katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulisema hilo, kwa furaha basi sasa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kutoa hoja yake vizuri hapo jana na pia niwashukuru wenzangu waliotangulia kuchangia, kwa vyovyote wamegusia mengi ambayo nilikuwa nakusudia kuyasema lakini basi na mimi niseme machache kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nizungumzie kidogo hii Kauli Mbiu yetu ya Kilimo Kwanza. Kauli hii ni yetu Watanzania wote na kwa kipindi hiki tulichokuwa nacho, ni kipindi ambacho kwa kweli ni kigumu, uchumi wetu uko katika hali isiyokuwa ya kawaida na si Tanzania tu bali ni suala la kimataifa. Kwa maana hiyo basi sisi Watanzania tushikamane na tushirikiane kuona kwamba, kauli hii inakua ni ya tija kwetu sisi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika harakati hizi, naomba niwasilishe kilio cha akina mama. Asilimia kubwa sana ya chakula tunachokula nchini, ni chakula ambacho kinazalishwa kutoka vijijini, ni chakula ambacho wazalishaji wakuu ni akina mama.

Lakini akina mama hawa, ni wale ambao wamekaa huria, kila mmoja huzalisha jinsi anavyoona anaweza kuzalisha mwenyewe. Akina mama hawa ni wale wanaolangukiwa mazao yao yakiwa bado yako mashambani. Kwa maana hiyo, akina mama hawa wanauza mazao yao kwa bei ya chini kabisa kwa sababu bei inapofika sokoni inapanda kwa ajili ya yule msafirishaji aliyekuja kuuza jumla na kwa ajili ya yule anayekuja kuuza kidogo kidogo. Kwa hiyo, akina mama wamekuwa wanatumia nguvu zao nyingi kuzalisha ili kujikimu na kulisha taifa hili lakini wao wakifaidika kidogo. Naomba Serikali iwaangalie kwa namna ya kipekee akina mama nchini kwa upande wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kila tunapohitaji uwekezaji, iko ile dhana ya kudhani kuwa mwekezaji ni lazima awe mgeni katika maeneo husika. Lakini mimi naamini kabisa kuwa akina mama wakiwezesha, wanaweza kwa sababu ninayo mifano katika Jimbo langu akina mama wamejiundia vikundi vyao vidogo vidogo vya kuwezesha wao kwa wao. Kukiwa na mpango maalumu wa kuweza kuwasaidia akina mama hawa, nina hakika, wanaweza kabisa wakachangia sana katika hii Kauli Mbiu yetu ya Kilimo Kwanza ili wanawake hawa waweze kuzalisha kiasi kikubwa, waweze kuuza wenyewe katika masoko badala ya kuiuzia Halmashauri na waweze kupata bei nzuri isiyokuwa ya kuwalangua na kuwavunja nguvu mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo pia kundi lingine la vijana. Vijana wetu wa Tanzania kimsingi hawana mahali maalum wanapoweza wakasema hapa wapo kwa kuangaliwa kiuzalishaji. Wachache ambao wameweza kupata elimu ya juu, sasa hivi kuna walau namna ya kutafuta soko la kuwatafutia ajira. Lakini hili kundi kubwa ambalo limebakia, halijaweza kupata elimu nzuri, kwa kweli bado halina utaratibu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposema hivyo, ninadhamiria kuwasemea vijana wa Jimbo langu. Ninazo Kata takribani tano ambazo ni wakulima wazuri wa mananasi, ni wakulima wazuri wa mapesheni, ni wakulima wazuri wa nyanya na mazao mengine mbalimbali ya mbogamboga. Lakini hawa vijana wanahaingaika na mboga zao mikononi wakiwa wanakwenda kuuza kidogo kidogo, wanauza kwa bei ya chini sana, ya kutupwa kwa sababu wanakuwa wamezalisha mazao mengi ambayo hawana soko la pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hizi ni Bulyakashaju, Muhutwe, Kagoma, Izigo, Rushwa ya Kihaya kwa maana ya Kumbikumbi na Ngenge ambapo vijana wake ni wazalishaji wazuri wa mazao niliyoyataja lakini pia baadhi yao wana mashamba kwa hiyo wanazalisha hata kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kwa kiwango gani sasa hawa vijana wamewekewa mikakati ya kusaidiwa?. Naomba akina mama na vijana wawe na mfuko wao sasa unaokwenda kutaka kuwasaidia mahususi ili nao waweze kusaidiwa na nguvu kazi yao iweze kuonekana kwamba huu ni mchango wa akina mama, huu ni mchango wa vijana ambao unachangia kwa kweli katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, alizungumzia uanzishaji wa benki. Mimi napenda kuipongeza sana Serikali kwamba, sasa kutakuwa na

Benki ya Wakulima. Lakini mimi najiuliza hii benki itakuwa ni ya akina nani? Kwa sababu isijekuwa sasa benki hii ikaanzishwa halafu ikawa ni benki ya wafanyabiashara badala ya kuwa ni benki ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu tumetenga nchi yetu katika maeneo mbalimbali na sasa hivi kuna Mkoa michache ambayo imepewa nafasi kwamba hii ni Mkoa mikubwa ya kuzalisha ambayo ni sita. Bahati mbaya, Mkoa wangu wa Kagera haumo, zilitajwa Wilaya mbili kwamba zitapata mbolea ambazo ni Chato na Karagwe lakini Wilaya zingine hazimo katika utaratibu, lakini hii Benki ya Wakulima, isipoanzishwa kwa umakini wa hali ya juu sana, wale walanguzi na wachuuzi ndiyo watakuja kuishia kuwa ndiyo wateja wa benki hii ya wakulima badala ya wakulima wanaotakiwa kulima mashambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe kwamba, sasa inatenga maeneo mbalimbali. Kila Mkoa utenge maeneo yake kwa ajili ya kilimo ambayo yatapewa wawekezaji wa Kitanzania na kutokana na hayo maeneo yatakayokuwa yametengwa iwe ndiyo kigezo cha kuwawezesha kwenda kukopa katika hii Benki ya Wakulima, sio watu wajitokeze hivyo eeh, kwamba wanaenda kukopa matokeo yake tutakuta benki inaacha kazi ya kukopesha wakulima na itanza kukopesha masuala mengine na zaidi tutakuta wanaopata fedha hizo ni wafanyabiashara, maana sasa hivi watu wameshakuwa wajanja wakitamka kilimo tu neno moja yaliyobaki ni biashara zake basi anapatia hapo mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie suala hilo sana kwa maana kwamba, hata mikopo yetu iweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba walengwa wawe ndiyo wafaidikaji wakubwa wa mikopo yetu na taratibu zetu tunazozianzisha nchini kwa kweli zilenge kuwasaidia wakulima na zihakikishe kwamba kweli wameweza kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba barabara za vijijini zipewe uzito mkubwa sana. Asubuhi Mheshimiwa Seleli aliuliza Serikali nadhani alikuwa anaishauri kuhusu utengaji wa pesa za Serikali zinazotengeneza barabara. Serikali za Halmashauri za Wilaya ndizo zenye barabara nyingi sana zinazowezesha mazao kutoka vijijini kuja mijini lakini ni mbovu mno. Tatizo kubwa ni pesa ambazo *councils* zinapata kwa ajili ya kutengeneza barabara zake. Kwa hiyo na mimi naunga mkono kwamba ni vizuri sasa Serikali itafakari upya mgawanyo wa pesa ili pesa nyingi ziweze kwenda vijijini kutengeneza miundombinu ya barabara, ziimarisha madaraja ili wananchi waweze kuleta mazao yao mahali yatakapouzwa haraka na kupata faida kuliko kudhani kwamba sasa barabara zitengenezwe za lami tu ambazo bado zimeachwa zibebe mizigo mikubwa, reli iko inaangamia, kwa hiyo na barabara zetu za mijini nzuri zinaharibiwa kwa sababu ya mizigo mizito. Lakini hata zile ndogo za vijijini zinashindwa kutuletea mazao au kufikisha mazao mahali ambapo yatapata bei nzuri walau ya kuweza kuwasaidia hawa wakulima wetu. Kwa hiyo, Serikali ilianganalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalopenda kuzungumza, ni kuhusu uimarishaji wa mazao yetu ya biashara. Sisi Mkoa wa Kagera tunalima kahawa sana,

tulijaribu pia zao la vanilla na hata chai tunalima vizuri. Jimbo la Muleba Kaskazini, ndilo Jimbo pekee katika Mkoa wa Kagera linalolima chai, tena chai kwa wingi. Lakini bado hakuna ule msukumo wa zamani wa kwamba sasa ni kilimo, kwa sababu mimi eneo langu ni zuri kwa uzalishaji mzuri wa chai. Nani anasukuma hii chai iweze kuzalishwa? Wamejaribu sasa hivi kufufua mashamba lakini bado ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kahawa sasa hivi, watu wanaamua kuacha kabisa kwa sababu msukumo hakuna. Lakini bei ya mazao haya ndio tatizo kubwa sana. Haya mazao yanashuka bei msimu hadi msimu na hata katika msimu huu yameshuka tena. Hali hii haiwezi ikatoa nafasi kwa wakulima kuendelea kulima mazao haya. Naiomba Serikali kama ilivyoweza kufikiria wakulima wa pamba ikawaongeza bei, ninaomba na wakulima wa kahawa, wakulima wa chai katika Mkoa wa Kagera na wenyewe waangaliwe kuongezwa pesa katika zao hili ili na wao waweze kufaidika na kilimo hiki walichojikita nacho badala ya kuwaachia tu sasa kwamba itakuwa ni bei ya soko na wenyewe wameathirika katika mtikisiko huu. Ninaomba Serikali iwaangalie na Mheshimiwa Waziri Mkuu umesikia, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu, naomba mtusaidie na aseme kwamba na sisi mtatufikiriaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalotaka kuzungumzia, ni kuhusu matumizi ya mbolea ya samadi na mboji. Sisi ambao hatumo katika orodha ya hii mbolea ya viwandani, tunatumia samadi. Jamani naomba na sisi tusaidiwe, samadi lazima uwe na ng'ombe, mboji lazima uwe na chakula kingi, kwa sababu utapata wapi mboji kama huwezi kupata mchanganyiko wa vitu mbali mbali?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaitumia hii sana, ninaomba isitupwe, ikaonekana kwamba pale ambapo hakuna mbolea ya viwandani, basi uzalishaji hamna. Tunazalisha na tunaweza kupata chakula chetu na mazao yote ambayo nayazungumzia. Lakini suala la kutilia mkazo samadi na mboji limekuwa ni la chini sana. Naomba yapewe uzito na kimsingi vyakula vinavyozalishwa kwa samadi na mboji ndivyo vyakula vinavyofaa kuliwa kwa sababu havina sumu mwilini. Kwa hiyo, ni vizuri na lenyewe kulisemea, si kwamba sasa tumeishaingia mbolea za viwandani, tuisemee kabisa mbolea za mboji, tuiseme kabisa mbolea ya samadi. Kwa kweli, kwa namna moja au nyingine, inakatisha tamaa kwa wale wanaotumia hizi mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jioni ya leo nikushukuru, nisiendeze maneno mengi zaidi kwa sababu mengine yote niliyotaka kuyazungumza, wenzangu wameyazungumza. Labda niombe Serikali itoe elimu ili tuweze kutumia vizuri hizi pesa mbalimbali tunazoletewa kwa mfano kwenye *VADPs*, kwenye *DADPs* wananchi hawajaelewa na mara nyingi pesa zinakuja na zinaishia kujulikana kwa watalaam, wananchi wanakuwa hawazijui na viongozi wengine hawazijui ambao wangesukuma. Haya kwa pamoja, ninaamini yataweza kuleta mabadiliko na mapinduzi ya kilimo na kauli mbiu yetu inaweza ikafanikiwa kama sisi Watanzania wote tutajiunga pamoja na tutaipa nguvu Serikali yetu kuweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana! (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, huyu ndiye alikuwa msemaji wetu wa mwisho kwa kuchangia kwa kusema hapa ukumbini kwa upande wa Wabunge.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa kwa miaka kadhaa sasa Wilaya ya Karatu imekumbana na hali mbaya ya hewa na kumekuwa na ukame usiotabirika, kama mwaka huu ambapo mwanzo wa mwaka mvua zilichelewa sana, watu wakapanda, ikakauka, wakapanda ikakauka tena na baadaye mara ya tatu kukawa na matumaini. Lakini yakakauka wakati mabua yamekuwa makubwa:- Je,

- (i) Tathmini ya mara ya mwisho ya hali ya njaa imefanyika lini? Hali ya njaa Wilayani Karatu imesema nini (Tathmini)?
- (ii) Taarifa ya awali toka vijijini inaonyesha zaidi ya nusu ya Wilaya hali yao ni mbaya na tayari kuna njaa. Je, kuna utaratibu gani kuokoa wananchi hao ambao toka msimu uliopita hali yao tayari ni mbaya?

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kuamka salama huku tukiwa na imani katika nchi yetu niseme Allhamdullillah.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe pongezi zangu kwako, Naibu Spika pamoja na Wenjeviti wako kwa uvumilivu wenu katika Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mbele yetu kuna hotuba ya Wizara naomba nami uniruhusu nieleze yangu katika Wizara husika, kwanza napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu yake ambayo iliweza kuandaa bajeti yake kiufundi kabisa pia kuonesha nia ya kuinua uchumi wa nchi yetu ili kumwezesha mwananchi kuweza kuishi katika maisha bora. Niseme Mwenyezi Mungu awape uwezo ili waiokoe nchi katika omba omba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia bajeti ya Wizara ilivyo ni wazi utaona ni ndogo ukilinganisha na majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli mbiu ya Serikali ni Kilimo Kwanza. Historia inajionesha nia ya Serikali katika kukuza kilimo haikuanza leo. Tulitumia neno Siasa ni Kilimo. Ni wazi ni nia njema ya Serikali kutoa kipaumbele katika kilimo. Je, Siasa ni kilimo ilitufikisha wapi na leo tukatoa tena kipaumbele hiki cha kilimo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo. Kwa kuzingatia kilimo Watanzania walio wengi ni wakulima, kinachofelisha ni kukosekana kwa utaalam katika kilimo. Ili kufanikisha azma hii ya kilimo kwanza ni lazima Serikali ijipange ili kuleta kilimo cha sayansi katika kuboresha kilimo cha sayansi ni lazima papatikane wataalam yaani mabwana shamba wa kutosha, mbolea, mbegu bora pia tuondokane na kilimo cha mkono. Wizara italazimika kutoa elimu kwa kuwapatia mabwana shamba (Ogani) kila eneo. Mara nyingi tunakuwa na upungufu wa wataalam jambo ambalo hupelekea tunalima panatosha, tunavuna pamekwisha. Je! Serikali ili kuwapatia wataalam wakulima kwa kujiandaa kiasi gani kuhakikisha wakulima wanapata ushauri kila leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyuo vya kilimo. Bila shaka vyuo vyetu vinazalisha wataalam wazuri sana. Kumpata mtaalam unachukua muda. Je, kwa nini hatuwaandalii wakulima wetu kozi fupi ambayo itatoa elimu kwa mkulima? Kuendelea kumsubiri aliyepata Diploma hatuoni tutachukua muda kufikia malengo? Pia kuna upungufu wa kuwajua wakulima wetu huko Wilayani. Kutokuwajua wakulima ni wangapi katika maeneo husika ndio pale mkulima anapolima bila ya kusimamiwa na mtaalam. Je, Wilaya zetu zinajua idadi ya wakulima wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji (Irrigation). Tukizingatia kilimo cha umwagiliaji ni lazima tuangalie Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Morogoro una idadi ya mito mia moja na arobaini (140) ambayo haikauki. Lakini kilimo katika Mkoa huo hakijakidhi haja katika mkoa huo. Hii ni dhahiri Serikali haijawa tayari kukipa uwezo kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufikie malengo ya kilimo kwanza, naiomba Serikali itoe elimu kwa wakulima, iwaandalie wakulima wataalam wa kutosha, wataalam wawezeshwe na kuthaminiwa. Bei za pembejeo ziwe ni zile zenye unafuu, kwa kufanikisha haya, ni mategemeo yangu tutafikia azma yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitakia Wizara mafanikio. Ahsante.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa Bungeni wote tukiwa hai na wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wa Wizara na taasisi zake kwa juhudi wanazozifanya kuhakikisha kuwa Watanzania hawafi na njaa wakati wa ukame unapokuwa unaikabili nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kwanza ni jambo zuri lakini sasa kinachotakiwa ni utekelezaji wa kilimo kwanza. Serikali ni lazima iwe na mpango mkakati wa tafiti za mazao mbalimbali ili wananchi (wakulima) wapande mbegu ambazo zimefanyiwa utafiti wa kutosha ili kutambua na kupata mbegu nzuri ambazo zitatoa matokeo mazuri ambayo

yatapelekea wakulima kupata mavuno mazuri na kuwa na mazao ambayo hayashambuliwi na magonjwa mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kilimo chetu kiwe cha manufaa ni lazima wakulima wetu wawe na elimu nzuri, kilimo ni sayansi. Naishauri Serikali ule mpango wa elimu kwa wananchi hasa wakulima ufufuliwe ili wakulima wawe na elimu angalau namna ya kutumia mbolea, madawa, kupanda kwa nafasi. Katika shule zetu za Kata yaani za Sekondari ziwe na somo la kilimo ili mara wanafunzi wanapomaliza na kuhitimu Kidato cha Nne, wawe wakulima wazuri. Naishauri Serikali iwapeleke wanafunzi katika Vyuo vya Ualimu ambavyo vitakuwa na wakufunzi wa somo la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuajiri wataalam wa kilimo wa kutosha ili wawasaidie wakulima kupata tija katika ukulima na wapewe mshahara wa kutosha kulingana na kazi yao muhimu wanayofanya kuboresha ukulima na kukuza uchumi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima waweze kupata nafasi ya kukopa kutoka katika mabanki yetu na Serikali itambue kuwa taasisi za kifedha haziweze kutoa mikopo bila kuwa na dhamana. Je mkulima atakuwa na dhamana gani ili aweze kupata mkopo? Hata kama kutakuwa na benki ya wakulima watakaofaidi ni wafanyakazi. Naishauri Serikali iwe na mpango wa Kitaifa kuhakikisha kuwa kila mkulima nchini anamiliki ardhi kwa kuwa na hati miliki ili kila mkulima awe na uwezo wa kupata mkopo kutoka kwenye mabanki na taasisi mbali mbali za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tabia ya kuzuia chakula kutoingia Wilayani Tarime, chakula cha nafaka kama mchele au mahindi. Ni kweli kwamba wakati mwingine Serikali inakuwa na upungufu wa chakula, lakini ni lazima Serikali kulinda mipaka yetu ili chakula kisipelekwe nchi jirani lakini sio kuweka *Barrier* ndani ya Wilaya ni vema Serikali iweke *Barrier* mpakani Sirari, ambapo kwa sasa pale Sirari tayari kuna *barriers* mpakani. Uwekaji wa *barrier* ndani au kabla haujaingia Wilaya husababisha kupanda kwa bei ya nafaka isiyokuwa ya lazima. Naomba Serikali inijulishe kama huo ndiyo utawala bora na kwa tabia hii ya kuweka *barrier* ni kuwanyanyasa wananchi na kuwanyima haki wananchi wa Jimbo la Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hao askari polisi ambao huwasumbua sana wafanyabiashara kwa kuwatoza kwa lori moja zaidi ya laki tano (500,000/=) kutakoma lini? Kama kuna ulazima wa wafanyakazi kulipa basi Halmashauri isimamie kukusanya makusanyo hayo kuliko askari polisi kukusanya na kupata kwa manufaa ya biashara mazao mbalimbali kama vile kahawa, tumbaku, Serikali iwe inatoa bei elekezi ili wakulima wasiwe wanalipwa kiasi kidogo. Mfano, kuna kampuni ya kununua kahawa Wilayani Tarime (Mara *Coffee*) hutoa bei ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuwatafutia wakulima wa kahawa soko la kuuza kahawa zao, pamoja na kuwa na ushirika wa kulegalega, ni jukumu la Serikali kuwatafutia soko ili wakulima wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.



**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA :** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji kwa kuandaa hotuba, bajeti na hatimaye kusomwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika bajeti, naipongeza Serikali kwa kuongeza Tshs.80/= kwa kilo ya pamba kwa mkulima. Ni kweli nililozungumza na wakulima wamefurahi na kusema kweli Serikali inawajali na wameahidi kuendelea kulima kwa bidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekubali kuiweka Bukombe katika mfumo wa mbolea/pembejeo za ruzuku naipongeza sana. Ombi la pembejeo hizi ziwe na utaratibu mzuri, tuangalie zisije kuishia mikononi mwa wajanja. Ili kufanikisha kilimo kwanza, Bukombe ni vizuri tuangalie mfumo wa kuwakopesha pembejeo hasa *power tillers*, majembe ya ng'ombe na matrekta. Nasema hivyo kwa sababu sehemu kubwa ya wananchi hawana hati miliki za nyumba zao au mashamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, Serikali ngazi ya Taifa izishauri Halmashauri au Mkoa ukope vifaa kazi hizi ili wananchi wakulima wakope kupitia ama Halmashauri au Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itusaidie kusukuma ili *SACCOS* ya Vijana Masumbwe wapate *Power Tillers* za mkopo ambazo zitawasaidia. Napenda kushauri Serikali ihamasishe na itoe hela kwa ajili ya mabwawa, kwani Bukombe ambayo ni nzuri sana tena ni ghala la chakula Mkoa wa Shinyanga lakini haijawezeshwa kuwa na bwawa au mradi wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wilaya ambayo ni nzuri haina mradi wa umwagiliaji twawezaje kuendeleza kilimo kwanza? Naomba Serikali ifanye utaratibu wa kukusanya au kuwaunganisha vijana kila Kata, Wilaya au Mkoa na kuwapa maeneo na vitendea kazi ili waendeleze kilimo badala ya wao kukaa mijini na kufanya shughuli zisizoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena Serikali kushauri iangalie namna ya kuviwezesha vyama vya ushirika, mfano *SHIRECU* wapate mikopo haraka ya kununulia mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu *SHIRECU* wamekwama kupata fedha kwa muda mrefu za kununulia mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali isimamie upatikanaji wa fedha za mikopo *SHIRECU* na vyama vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Stephen Wassira Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Mathayo David Mathayo, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Katibu Mkuu pamoja na wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye lengo la kuinua kilimo pamoja na kuimarisha ushirika pamoja na masoko ya mazao ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nina imani na Mheshimiwa Wassira Babu yangu pamoja na Mheshimiwa Mathayo David Mathayo, mwanangu napenda kabla sijaanza kuchangia nitamke rasmi kuwa naunga mkono hoja hii na nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wao kwa maslahi ya wakulima wa nchi yetu wakiwemo wakulima wa Mkoa wa Singida. Wakati nikisubiri majibu au ufafanuzi wa hoja mbalimbali ndani ya mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiangaliza Serikali kuwa ufanisi wa kilimo kote nchini ni kuwa na Maafisa Ugani kuanzia ngazi ya kijiji kwani ndiko wakulima wengi walipo. Je, ina maana kuwa Maafisa Ugani wa Kata hupata taabu sana kwani eneo wanalohudumia ni kubwa hivyo naishauri Serikali wawepo pia Maafisa Ugani wa vijiji ili wakulima wengi waweze kupata elimu ya kilimo kuanzia kuandaa shamba, kulima, kupanda, kupalilia, masuala ya madawa, uvunaji hata uwekaji wa mazao kwenye ghala. Hii itasaidia sana wakulima kuvuna mazao bora kuliko ilivyo sasa. Naiomba Serikali kusomesha maafisa wengi ili waweze kukidhi haja kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu stakabadhi ya mazao, napenda kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Singida chini ya Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Parseko Kone kwa jitihada zao kubwa katika kuinua kilimo cha mazao ya nafaka Mkoani Singida. Mazao ya mahindi, mtama, uwele na kadhali. Vile vile niwapongeze kwa kuanzisha ushirika wa stakabadhi ya mazao Mkoani Singida mpango ambao utawasaidia sana wakulima kuwa na uhakika wa kuuza mazao yao na kuendelea kupata faida mara mazao yanapopata soko zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kusaidia mpango huu kwa kutoa fedha zaidi za kuendesha mpango huu kwani bila Serikali kutoa nguvu, ushirika huu wa stakabadhi hautaleti tija kwa wakulima wetu pamoja na nia yao njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyombo vya usafiri kwa maafisa ugani ni ukweli usiokwepeka kuwa Maafisa Ugani wetu pamoja na juhudi zao zote endapo hawatapata vyombo vya usafiri itakuwa kazi sana kuwasaidia wakulima wetu kwani maeneo wanayohudumia ni makubwa na mashamba yapo mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi ninaomba mpango wa pikipiki uwe endelevu na uwe kwa Maafisa Ugani wa Kata zote kisha wale Maafisa Ugani wa vijiji wapatiwe baiskeli. Hii itasaidia sana kutimiza wajibu wao ipasavyo. Nasubiri majibu tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji, naipongeza sana Serikali kuona umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji bali kilimo hiki cha umwagiliaji bado hakina tija kwani bado tuna skimu chache za umwagiliaji tena ufungaji wake mashine kuna dosari kwani mashine zimefungwa kwa pistonni moja tu, naomba Wizara hii kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika lengo la kukuza kilimo kwa njia ya umwagiliaji naomba skimu zote Mkoani zihakikiwe ili zitoe huduma ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *databank* ya ardhi iwepo Wizarani na Kituo cha Uwekezaji kwa kuwa tunataka kukuza kilimo chetu ili kauli mbiu yetu ya ‘kilimo kwanza’ iweze kuwa na mantiki ni vema Serikali kuwa na *databank* ili ifahamike kila eneo linafaa kwa kilimo cha mazao gani. Hii itasaidia wawekezaji wa ndani na nje kujua kila zao na maeneo yanayoweza kustawi, hivyo wawekezaji wenye nia ya kuwekeza kupitia mazao yanayostawi nchini watakuwa wanafahamu kila zao linastawi wapi. Naomba Mheshimiwa Wassira, babu yangu atoe ufafanuzi wakati akijibu hoja. Kwa hiyo *databank* iwepo Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na iwepo kwenye Kituo cha Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa miundombinu kwa wakulima ni ukweli usiojificha kuwa miundombinu ya barabara, reli na bandari ni muhimu sana kwa kukuza kilimo chetu. Hivyo basi, ni vema sana kuhakikisha barabara zinazokwenda kwenye vijiji vyenye wakulima wakubwa ziwe zinapitika muda wote wakati wa kilimo na wakati wa kuvuna na kusafirisha mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo itasaidia mazao kusafirishwa na kufikishwa eneo husika bila kuharibika mfano vitunguu vikikaa sana bila kuanikwa huanza kuoza. Hivyo usafiri wa reli pia ni muhimu hasa reli ya Dodoma hadi Singida ni vema mabehewa ya mizigo yawepo ya kutosha wakati wa mavuno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano kwenye kilimo naomba ifahamike kuwa kilimo cha sasa ni cha Kimataifa kwani wakulima wanatakiwa walime mazao huku wanajua soko liko wapi. Hivyo ni vema mambo ya simu, *Internet* na *E-Mail* yafikishwe kijijini ili wakulima wawe wanatafuta soko kabla hawajaanza kuvuna mazao yao. Tukiwawekea wakulima mtandao tuna haki kujivuna na kauli mbiu yetu ya kilimo kwanza. Naomba majibu kutoka kwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pembejeo za kutosha, suala la upatikanaji wa pembejeo bado ni tatizo kwani wafanyabiashara bado wanachelewa kupeleka pembejeo wakati wa masika. Tabia hii huwafanya wakulima kushindwa kukitumia kipindi cha kilimo ipasavyo kwani pembejeo huwa duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa Serikali kuwadhamini wafanyabiashara mapema ili waweze kupeleka pembejeo mapema ikiwa ni pamoja na mbegu bora kwa mazao mbali kadri *databank* iliyoonesha ustawi wa mazao na maeneo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia utafiti wa ustawi wa mazao, ili kilimo chetu kiende sambaba na kauli mbiu ya ‘kilimo kwanza’, ni vema tuwe na Kitengo cha

Utafiti kwa mazao mbalimbali ambayo tunaona yanaingizia Taifa letu pato kubwa ili wakulima wakubwa walioamua kuwekeza kwenye kilimo waelewe ardhi husika kwa zao analotaka kuwekeza liko Wilaya gani na Tarafa ipi kwa kila Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko la mazao bado kuna tatizo la wakulima kukosa soko kwa mazao mbalimbali yanayolimwa mfano, Singida tunalima sana alizeti ambayo hutoa mafuta mazuri ya kupikia tena mafuta haya hayana hata madhara kwa watumiaji. Naiomba Wizara hii iwaeleze wakulima wa alizeti soko la mafuta ya alizeti liko wapi kwani sasa hivi mafuta haya yamejaa Singida na hawajui wapeleke wapi zaidi ya kuuza rejareja – biashara ya kubahatisha tu. Naomba Mheshimiwa Waziri Babu yangu Wassira awaeleze wakulima wa zao la alizeti ili wapate matumaini ya mafuta haya ya alizeti ambayo ndio msimu wake sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, baada ya mchango wangu ambao nasubiri ufafanuzi wa Naibu Waziri na Waziri wakati wa majumuisho yao, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana wewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine wote wa Wizara hii, nawapongeza sana kwa kazi nzuri mnazofanya ndani ya mazingira magumu ya maeneo mengi kuwa kame, upungufu wa vitendea kazi, bei mbaya za mazao na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahia sana na kuunga mkono Serikali kuamua kutoa kipaumbele katika kilimo na kuja na maeneo ya 'kilimo kwanza'. Ninaloomba ni Serikali iongeze bajeti ya kilimo kwani hata hii iliyotengwa mwaka wa 2009/2010 bado ndogo sana ulikinganisha na wakulima tulio nao hapa nchini hasa wale wa Mikoa kame ambao mpaka sasa hawana mazao halisi ya mazao ya biashara kwani mazao waliyonayo mpaka sasa hayana msimamo wa bei kutokana na kukosekana kwa bodi inayosimamia mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaolima alizeti, mawese, vitunguu maji/vitunguu saumu, gilgilani, dengu, karanga na kadhalika mpaka sasa ndio wakulima wenye shida sana. Huko nyuma *GAPEX* ndio ilikuwa inasimamia maslahi yao na hawakuwa na shida kabisa lakini leo wanajuta na kusaga meno, maana wanatumia fedha zao, nguvu zao kulima lakini bei ya mazao yao wanapangiwa na walanguzi. Wakulima hawa wasaidiwe kwa kuanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko haraka iwezekanavyo, tunaomba sana Muswada uje bila kukosa Bunge lijalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirika, mpango wa stakabadhi za mazao ghalani ni mpango mzuri sana utaona umefanikiwa sana kwa wenzetu wenye bodi kama korosho. Tunakuomba sana usaidie na mikoa ambayo haina bodi ili ziweze kufanikiwa. Mikoa hii ni Dodoma, Singida, Shinyanga, Kigoma na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Mikoa kama ya Singida na Dodoma maghala ya kuhifadhi mazao yaliyokuwa yanahifadhi mazao wakati vyama vya ushirika vilikuwa

na nguvu mengi yaliharibika baada ya vyama vya ushirika kufa na Halmashauri zetu za Wilaya hazina uwezo wa kukarabati maghala hayo na pia kujenga mapya, naomba sana Wizara yake isaidie kwa kutoa fedha au kuzikopesha *SACCOS* kwenye yale maeneo zinakoendelea vizuri ilikufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ugani, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hatua anayochukua kuajiri maafisa ugani nchi nzima, lakini naomba kasi hiyo iongezeke kwani mahitaji ya maafisa hao bado kubwa sana kwa faida ya kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu zana. Wakulima wetu wengi bado wanategemea jembe la mkono, mbegu za asili na kadhalika. Wilaya ya Iramba asilimia kumi matrekta na asilimia tano jembe la mkono. Sasa hivi wale asilimia themanini na tano ni wanyama kazi, nusu yao wanaomba wakopeshwe matrekta. Naomba sana Serikali ihakikishe inaagiza *power tillers* na matrekta ya kutosha karibu na Maafisa Kilimo wa Wilaya ili wananchi wote wanaohitaji zana hizo wawe wanapata. Pia ihakikishwe mbegu bora na zinazovumilia ukame zinatafutwa kwa ajili ya wakulima wa mikoa kame. Tuna upungufu mkubwa sana wa Maafisa Ushirika, tunaomba nao waajiriwe wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu Ushirika. Huu ni mwaka wa sita toka Wizara ikubali kujenga soko la Kimataifa Iguguno – Iramba Mashariki nataka kujua ahadi hiyo itatekelezwa lini ?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Napongeza juhudi za Serikali hasa baada ya kusikia kilio cha wakulima wa pamba. Bonde la Mawonga linafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji hasa kwa zao la mpunga. Mto Manonga hupata maji mengi hasa wakati wa masika na hupotea bila ya matumizi ya kutosha ya umwagiliaji. Napendekeza Serikali ijenge mabwawa ili kuyavuna maji yasiptee bure. Kwa sasa yapo malambo madogo madogo ambayo hayakidhi kufanya umwagiliaji wa maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazotengwa kwenye miradi ya *ASDP (DADPs)* ni kidogo kulingana na uzito wa kilimo. Napendekeza pesa iongezwe maradufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya kilimo yashabihiane na upatikanaji wa watalaam angalau hadi ngazi ya kijiji. Mkazo uzingatie kupata Maafisa Kilimo ili kuwaelekeza wakulima kilimo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali inafanya upendeleo hasa katika utoaji wa mbolea ya ruzuku. Wote ni wakulima na ardhi imechoka, hivyo wanahitaji mbolea ili kuwa na kilimo cha kisasa na cha uhakika na mbolea iendane na upatikanaji wa mbegu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nawapongeza.

**MHE. ENG. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Steven Wasira na Naibu wake Dr. David Mathayo, Katibu Mkuu wa Wizara na wataalam wote wa Wizara kwa kazi mbalimbali wanazoendeleza pale Wizarani. Hakika kazi yao ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi inaonekana ina mafanikio tunayaona huku pia wakituongoza kwenda kwenye upeo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri na wataalam wake wanipe maelezo juu ya maeneo yafuatayo, angalau kwa kifupi tu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, je, Mheshimiwa Waziri anatueleza nini sasa juu ya matumizi ya utaratibu wa stakabadhi ghalani (WHRS) kwa mazao ya korosho, pamba na tumbaku, kwa msimu huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri anatueleza nini kuhusu matarajio ya kuwakwamua wakulima wa tumbaku kutoka katika kuyategemea makampuni ya ununuzi wa tumbaku katika kuendelea kuyategemea pia katika kuwaletea pembejeo? Je, kwa maendeleo gani hivi sasa katika kuisaidia *WETCO* kukopa *NMB* ili wakulima wapate pembejeo mapema mwaka huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, je, Mheshimiwa Naibu Spika, ni mkakati gani Wizara imeweka katika kukomesha utendaji wa tumbaku wa ardhi ya wakulima wasio waaminifu wanaokwama kulipa madeni yao ya pembejeo kupitia vyama vya msingi vya ushirika walikokopea pembejeo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maswali haya matatu, napenda tena kuipongeza sana Wizara na Serikali kwa ujumla na nitamke kuwa naunga mkono hoja ya Waziri na kwamba mimi na wana Tabora Kaskazini tuna mategemeo makubwa sana sasa ya maendeleo kupitia msukumo mpya wa Kilimo Kwanza. Ahsante.

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja. Ili kauli mbiu ya Kilimo kwanza ifanikiwe mambo yafuatayo yazingatiwe.

- (1) Elimu kwa wakulima na nia ya kutumia kilimo bora
- (2) Serikali isambaze pembejeo kwa wakati unaofaa.
- (3) Mabwana shamba wasambazwe nchi nzima hasa vijijini ili waweze kutoa ushauri wa kilimo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naiomba Serikali wawaruhusu wafanyabiashara waagize matrekta na wasamehewe kodi ili matrekta yaingizwe kwa wingi sana humu nchini ili wakulima waweze kununua matrekta hayo. Wakulima waondokane na kilimo cha kutumia majembe ya mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itilie makazo zaidi ukulima wa umwagiliaji ambao ndio ukombozi wa kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ifanye utafiti mpya kuhusu miongo ya mvua kwani inavyonekana kuna mabadiliko ya hali ya hewa, mara nyingi majira ya mvua yamebadalika sana, wakati mwingine mvua inawahi sana na wakati mwingine inachelewa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijitayarisha kwa ununuzi wa mazao ya wakulima, kwani mara nyingi wakulima wanalanguliwa sana mazao yao na wafanyabiashara matapeli.

**MHE. MOHAMMED SAID SINANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti nzuri na yenye kutia moyo. Naomba nichangie yafuatayo:-

Kwanza, kuhusu Kituo cha Utafiti cha Naliendele. Watengewe asilimia moja ya *Export Levy* ili shughuli za utafiti wa zao la korosho usiathirike

Nashauri asilimia moja ya *Export Levy* ittengwe kwa ajili ya zao la ufuta ambao baada ya kupatikana *export levy* hiyo unaweza ukaongezeka na kukidhi mahitaji ya mafuta ya kula hapa nchini. Itaongeza pia pato la wananchi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu zao la ndizi Mkoani Mtwara, wakulima wa Mkoa wa Mtwara hawana ujuzi wa zao la ndizi. Hivyo, nashauri Serikali iweke mkakati wa kutoa mafunzo na miche ya aina mbali mbali ya zao hilo. Maeneo mazuri ya kilimo cha ndizi yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu zao la muhogo Mkoani Mtwara. Muhogo unastawi sana Mkoani Mtwara na hivyo naomba Serikali itafute soko la zao hilo.

Mheshimiwa Waziri, nne ni kuhusu zao la minazi, minazi mingi inakufa kwa magonjwa. Naomba Wizara yako iwafahamishe na kuwaelimisha wakulima wa zao hilo ni magonjwa gani yanayoathiri zao hilo na utatuzi wake. Wananchi wengi hawafahamu magonjwa hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Kituo cha Utafiti cha Naliendele kifanye pia utafiti wa magonjwa hayo ya minazi. Vitalu vya miche ya minazi inayohimili magonjwa ingefaa ianzishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha Matrikta (*Power Tillers*). Uamuzi wa kununua *power tillers* inawezekana haukufanyiwa utafiti wa kutosha kwani mapungufu yafuatayo ni dhahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja. gharama yake ni kubwa mfano *tractor* aina ya kubota, jembe, *trailer*, *pump* na *padler* sawa sawa na USD 7000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, *acreage* kwa siku iko chini (3 – 5 *acres*).

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, haiongozi ajira ukilinganisha na *tractor* lenye *horse power* kubwa: *High acreage employment, driver, tingo*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, haliwezi kulima bila uharibifu (*breakdowns*) katika udongo wa mbuga) katika mabonde ya Ruvu, Rufiji, Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Bunda, Igunga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, hakuna maandalizi ya matengenezo hayo vijijini kama ilivyokuwa huko nyuma (*mechanization centres*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, Halmashauri zielekezwe kununua pia matrekta yenye *horse power* kubwa, na Halmashauri ziwe na *mobile workshop* ili kuhudumia matrekta hayo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Graduate Farmers*, hili limeshazungumzwa na Rais. Ufanyike mpango wa *Agricultural Graduate Farmers* wajiunge waende kampuni zao wapewe mitaji, wawekeze katika kilimo (*large scale farming*). Sasa hivi vipo vikundi kama hivi Dar es Salaam na Morogoro lakini hawana msaada wa Serikali.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mungu kunijaalia kupata furasa hii ili nichangie Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Stephen Masato Wasiri, Waziri mwenye dhamana, pia nimpongeze Mheshimwa Dr. Mathayo David Mathayo, Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, niwashukuru pia Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nitoe shukrani na pongezi kwa wakulima wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa jitihada zao ambazo wanazifanya katika kilimo, juhudi binafsi bila kutegemea msaada wa Serikali sasa kwa kiasi fulani wamedhibiti suala la njaa na wamejishirikisha kwa karibu sana kulima mazao ya biashara kama vile alizeti, karanga, pamba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri au niulize maswali ili Mheshimiwa Waziri anipe majibu wakati akijumuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri anipe ufafanuzi ni jinsi gani mpango kazi (*Action Plan*) walivyoandaa kwa Mikoa ya Singida, Dodoma na kadhalika, ili wakulima wa Mikoa hii nao wakaingia kwenye ukulima wa kisasa kwani mikoa hii haimo kwenye programu ya kupatiwa mbolea ya ruzuku, pembejeo na hata utaalam pia tofauti na Mikoa ya Kusini Nyanda za Juu.



Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kuendeleza kilimo cha mwaka mzima kwa maana ya umwagiliaji, Wizara ina mpango upi shirikishi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na TAMISEMI katika kuhakikisha miundo mbinu ya umwagiliaji inakuwepo na kufanya kazi muda wote wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atolee maelezo juu ya Maafisa Kilimo, kwa nini hadi sasa Wizara haina Maafisa Kilimo kwenye ngazi za Kata na Vijiji, Waziri haoni kutokuwa na maafisa kilimo kwa ngazi hizi tajwa kauli mbiu ya mwaka huu ya kilimo kwanza ni sawa na ndoto za Alnacha kwani kilimo kwanza hakiwezi kuja kwa kauli za uandishi mzuri wa mipango vitabuni bila vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kumekuwepo na kauli mbiu tofauti bila kufikia mwisho na kutathmini matokeo yake badala yake kila mwaka tunaanzisha kauli mbiu nyingine mfano mapinduzi ya kijani (*Green Revolution*) mafanikio yake yako vipi na nyingine nyingi zilizopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri anieleze Wizara ina mkakati upi wa kuendeleza zao la alizeti linalolimwa sana Jimboni Iramba Magharibi, mkakati wa Serikali uko vipi kutambua juhudi za wakulima hasa kwa suala la ushauri na hata mbegu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni nzuri iliyo na wakulima kwa asilimia themanini, hivyo nguvu ya uchumi wa wananchi unategemea kilimo. Naomba Serikali inapotoa ruzuku ya kilimo basi isiwe na upendeleo wa ukanda kwani kufanya hivyo ni kuwagawa wakulima na wananchi kwani Mikoa inakoelekezwa ruzuku kubwa bado hakuna faida yoyote tunayoiona katika mikoa ambayo haikupewa ruzuku inafaidika na nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa kwa ununuzi wa matrekta ni ndogo sana kiasi cha Shs.700,000,000/=, ni sawa na matrekta kumi hadi kumi na nne, mgawo wake utakuwa uko vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa *ASDP*, *PADEP* na *DADPs*. Mipango hii ni mingi lakini ujaji wake unawachanganya mno wakulima, ni vizuri mipango hii ikatekelezwa kwa awamu vinginevyo fedha za miradi hii zitatumbekezwa kwa watu (watendaji) wasio waaminifu na hivyo kutotoa maana halisi ya miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri anipe *outcome* ya matumizi ya fedha za ruzuku ya nyongeza 2008/09, zilizotokana na *EPA* kiasi cha billioni 40. Baada ya kutoa ruzuku ya mbolea, uzalishaji wa kiasi gani ulipatikana na thamani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, *power tiller*, matumizi yake bado ni adha kwa mkulima, vumbi linalotoka huku mwongozaji akiwa nyuma ni hatari kwa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiunga mkono hotuba ya Waziri wa Kilimo na Ushirika, hotuba nzuri aliyotoa yenye kuonyesha kuwa sasa Serikali imedhamiria kulisimamia suala zima la kilimo hali ambayo wananchi wanaiona kuwa itakuja kuwakomboa kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kumpongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa ushirikiano wanaouonesha katika utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutamka rasmi kuwa naiunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono hoja, napenda kuchangia katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Serikali kuchelewesha mbolea kwa wakulima ni kosa linalosababisha maeneo mengi yanachelewa kupanda mazao. Kwa mfano katika Mkoa wa Kigoma, mvua zitaanza kunyesha hivi karibuni, lakini cha kushangaza ni Serikali kuchelewa kufikisha mbolea kwa watumiaji. Utaratibu ambao umekuwa ukitumika umekuwa siyo wa kuridhisha. Ili kupunguza malalamiko na kuhakikisha mbolea inawafikia wadau, basi usimamizi uwe chini ya Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye naye atawahusisha Madiwani ili kuhakikisha kila Kata inapata mgao wake. Hii itaondoa malalamiko yaliyojitokeza msimu uliopita ambapo mbolea na hasa katika Mkoa wa Kigoma mbolea iliuzwa hadi nchi jirani

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kilimo kwanza kiende sambamba na mbegu bora. Wananchi wanahangaika kupata mbegu bora ambapo kwa kutumia mbegu bora, ni dhahiri uzalishaji ungeweza kupanda. Ni kwa mantiki hii naishauri Serikali kwamba, kama inavyohangaika kutafuta mbolea kwa ajili ya wakulima, ingefanyika hivyo pia katika kutafuta mbegu bora. Kipaumbele kingetolewa kwa Mikoa ile sita ambayo imeteuliwa kuwa mikoa ya kilimo ambayo ni Kigoma, Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Iringa na Morogoro. Ni wazi kwamba mikoa hii ikipewa mbolea ya kutosha na mbegu bora kutatokea mabadiliko makubwa katika kilimo na dhahiri nchi itapata chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nyenzo za kisasa nazo za kilimo ni jambo bora na la msingi. Mfano hai ni kuwa mikoa yote ambayo imeingizwa katika *G6*, ni mikoa ambayo wananchi wake wanatumia kilimo cha mkono. Mfano hai ni Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake ambapo wananchi wamekuwa wakitumia kilimo cha mkono na kuweza kujitosheleza kuwa na mazao ya kutosha kwa chakula na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iwatie moyo wananchi hao kwa kuwapatia nyenzo za kisasa za kilimo ili kuwa na mapinduzi katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, napendekeza kuanzishwa kwa maghala ya kuhifadhi chakula katika mikoa hiyo sita inayozalisha chakula. Kwa kufanya hivyo,

kutapunguza kwa kiasi kikubwa kuuzwa kwa mazao kwa nchi jirani kama vile Burundi, DRC na Rwanda. Utaratibu huo utamfanya kila mkulima kuhifadhi chakula katika ghala ambapo ataweza kukipata wakati wowote.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri Mheshimiwa Wasira na Naibu wake kwa kazi nzuri sana wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika , naoamba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Kilimo kwanza. Serikali ipige marufuku jembe la mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali ianzishe *centres* za kilimo hasa matrekta. Pale wakulima waende kuyakodi ili walimie na kupanda kisasa na baada ya mavuno Serikali ichukue ujira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Serikali ihimiza na kusaidia zaidi mazao ya chakula ambayo yanaweza kuwa mazao ya biashara. Mazao hayo ni kama mahindi, mpunga, karanga, alizeti na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Serikali iwahimiza wakulima wakubwa kutoka nje waje kuwekeza katika kilimo kwa masharti nafuu, wapewe ardhi ya kutosha ili tujitosheleze kwa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, ruzuku ya mbolea iwahi kuja kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie yafuatayo. Moja, Chuo cha Kilimo na Mifugo Tengeru – Arusha. Pamoja na chuo hiki kuwa kwenye hali mbaya hata vyuo vingine viwili haviridhishi ukizingatia kauli mbiu ya Kilimo kwanza, naona haitatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi Serikali ifadhili wanafunzi wengi (Maafisa Ugani) wakisomea ili waweze kuwasaidia wakulima kulima kilimo cha kisasa na ni lazima Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Maji ili kuweza kuwepo na kilimo cha umwagiliaji ambacho ni endelevu badala ya kutegemea mawingu (mvua).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima ihakikishe tunakuwa na (*Commercial Farm*) yaani wakulima wakubwa wakati na wadogo mfano mzuri ni Shamba la *TPC* Moshi Vijijini wale ni *commercial farmers* tunaona jinsi wananchi wa pale walivyofaidika kwa ajira, umeme, mashule, na kadhalika. Sio hilo tu kwa sasa hivi wanawasaidia *out growers*, wakashatumiwa yao wana uhakika wa soko, huwa wanakwenda kuuza pale kwenye kiwanda cha *TPC*. Huu ni mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wakulima, bila wakulima kupata benki ambayo wanaweza kwenda kukopa kwa ajili ya kilimo hawataweza kuwa na kilimo chenye tija wala mapinduzi ya kilimo. Je, Serikali imefikia wapi katika kuanzisha benki ya wakulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, pembejeo za kilimo, inabidi Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara washirikiane kuona ni jinsi gani ya kutengeneza vifaa vya kilimo kupitia *CARMATEC*, taasisi ambayo ipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Tayari taasisi hii inatengeneza pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri ni kwamba, Wizara ili kupata kilimo chenye faida ni vizuri pakaandaliwa mpango wa kupanda mazao yanayotokana na Mkoa huo kimkoa mfano, Kilimanjaro wanajulikana kwa zao la ndizi na kahawa basi Wizara ipeleke nguvu kule zao lile lizalishwe kitaalam, hivyo hivyo Rukwa wanalima mahindi kwa wingi basi nyezo zote zipelekwe kule. Hii itasaidia sana kupata mavuno mengi itakayopelekea kupata akiba ya kutosha na hata kuuza nje. Angalizo, lazima kuhakikisha tuna maghala ya kutosha kuhifadhi vyakula hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wengi wanauza mazao yao sababu hawana sehemu ya kuhifadhi nafaka. Hizi mbegu za kisasa zinaharibika mapema mfano mahindi yanabidi yahifadhiwe kwenye matanki kama mkulima hataki kuyatia dawa. *Tank* moja siyo chini ya 800,000/= kwa magunia 50. Hivi mkulima huyu ataweza kununua tank hilo? Kwa kule Kilimanjaro wanakimbilia kuuza Kenya sababu hata Serikali hainunui kwa bei nzuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima hawa na hifadhi za nafaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mbolea, katika nchi zilizoendelea kwa sasa hivi zana zote za vyakula wanahimiza watu kutumia *Organic food* lakini hapa kwetu bado tunahimiza kutumia mbolea za kisasa ambazo zinaharibu ardhi, kuichosha na hata mavuno yake sio mazuri kiafya kwa mlaji. Je, ni sababu zipi zinapelekea Serikali kuacha kuhimiza matumizi ya mbolea ya asili kama samadi za wanyama? Kwa kutumia samadi za asili itafanya mazao yetu yauzwe kwa bei ya juu na hatimaye kuinua uchumi wa Taifa letu na mkulima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hizi kauli mbiu za kilimo kwanza, kilimo uti wa mgongo, Azimio la kilimo Iringa, Mapinduzi ya kilimo ya kijani. Ilani ya CCM imetekeleza ipi kama si siasa tu? Tunahitaji matendo zaidi kuliko maneno.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye malengo sahihi yanayotoa matumaini makubwa kwa wakulima wetu. Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Lushoto hasa Jimbo la Lushoto, naomba ufafanuzi wa Waziri kuhusu namna ambavyo Serikali imejipanga kuwasaidia wakulima katika maeneo yafuatayo:-

Moja, kupanua na kuboresha kilimo cha chai Wilaya yote ya Lushoto zikiwemo Kata za Kwai, Mlola na Makanya, na kuharakisha utatuzi wa shamba la Kuni Sakare.

Mbili, kupanua na kuboresha kilimo cha mboga na matunda kwa kuwapatia wakulima miche bora ya *peas, plums, peaches, apples, mangoes, guavas, passion fruits* na uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mboga na matunda.

Tatu, kubaini kusanifu, kugharamia, na kujenga skimu ndogo za umwagiliaji katika mabonde ya mito Kata za Makanya, Ngwelo, Mlola, Malibwi, Kwai, Gare, Ubiri na Lushoto ili kuongeza uzalishaji na kuinua mapato ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kupata nafasi ili nitoe mchango wangu katika bajeti hii, nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ya maandalizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni uti wa mgongo bajeti yake kwa kuangalia ni ndogo lakini imegusa maeneo mengi kama utekelezaji wa maeneo mengine watatekeleza vizuri mfano TAMISEMI wanazo pesa za ujenzi wa barabara vijijini kwa ajili ya kurahisisha usombaji wa mazao ya wakulima kupitia *DASP* kama usimamizi utakuwa mzuri kilimo kitakua kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo mkakati wa jumla wa kufuatilia ni muhimu ili matunda yaonekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani kwa Serikali hii ya Awamu ya Nne, imekuwa sikivu sana kwa wananchi wake kupitia Wabunge wao, yapo mambo mbalimbali yamekuwa yakitekelezwa mara tu baada ya taarifa kutolewa hapa Bungeni mfano ni nyongeza ya bei kwa zao la pamba kutoka 360 na kuongeza Tshs.80/=, ongezeko hilo ni picha tosha kuwa ni sikivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri hayo, lakini elimu itolewe na Bodi ya Pamba iliyopewa jukumu la kuwalipa wanunuzi baada ya wanunuzi kupeleka ripoti Bodi ya Pamba kitu ambacho tusipotoa elimu kupitia vyombo vya habari na redio mara kwa mara wakulima watapoteza haki zao. Vile vile Serikali za Wilaya katika maeneo husika wafuatilie kwa karibu haki hii ya wakulima kwani Serikali imetoa kwa nia nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanunuzi walionunua pamba mwaka jana na kupata hasara Serikali hii na Mheshimiwa Rais alipowahutubia wazee wa Dodoma na Waheshimiwa Wabunge kwa pamoja aliainisha kuwa watalipiwa madeni yao ili wakopesheke tayari kwa kuanza msimu mapema cha kusikitisha wanunuzi hao hawajaruhusiwa kukopa benki hadi sasa akiwemo *SHIRECU*. Hali hii ni hatari sana kwa Chama cha Ushirika na wafanyabiashara wengine kwa sababu wasiponunua mapema

watashindwa kukamilisha mikataba waliyoingia na waliowauzia marobota. Kwa taratibu za siku zote hadi leo hii baadhi ya robota zilitakiwa ziwe bandarini kwa kusubiri meli ya mnunuzi, mikataba mingi ya kuanza kupakia ni kati ya Agosti na Septemba. Ukichelewa unalipia au anakutoza faini ambayo inakuletea hasara, hivyo Serikali ilione hilo kama kuna utata, ni vema wakaahirisha vinginevyo hasara kubwa watapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyama vilivyoruhusiwa kupewa pesa kama *NCU*, alikubaliwa bilioni tatu. Amepewa bilioni moja alipoipeleka vyamani wakulima walipeleka pamba yao na kuwa na ziada ya kilo ambazo zinahitaji milioni 600 ili kuwalipa wakulima cha ajabu benki imewataka waisombe kwanza pamba, watu ambao hawajalipwa wanakataa kusomba mpaka wawalipe benki imekataa hilo ni tatizo. Cha kujiuliza kwa nini kama mkopo waliosaini Bilioni tatu kwa nini masharti ni magumu hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi au ushauri Serikali isimamie benki ili pamba hiyo ifike *Ginnery* ichambuliwe na robota zipelekwe kwa wanunuzi kama ni Dar es Salaam au popote mkopo uanze kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu nilielezea tatizo kubwa la watumishi wa Chuo cha Utafiti Ukiliguru na Chuo cha Mafunzo hapo Ukiliguru juu ya maji sasa ni zaidi ya miaka 25, watumishi hawa wana tatizo hilo hufuata maji jijini Mwanza kwa gari ambayo ni gharama. Je tatizo lao limepatiwa ufumbuzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema tukapata ufafanuzi wa ufumbuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Pembejeo ni Mfuko unaostahili kupewa kipaumbele ili waweze kukopesha wengi na suala la uzalishaji litaongezeka. Mfano wa Mfuko huu ni wa ajabu ukilinganisha na Mifuko mingine, sasa ni vema Serikali itilie maana Mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile watendaji wa Mfuko wawezeshwe na wawe wanawatembelea wateja wao mara kwa mara na kuwasaidia inapobidi ili mikopo yao iweze kurudishwa kwa wakati yapo matatizo ya ukame, uharibifu wa *treder* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wa ushirika yaani maafisa ushirika ni wachache Serikali iajiri wa kutosha ili wasaidie wakulima katika suala ufufuaji wa ushirika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Mazao ni muhimu sana kwa usimamizi, hivyo ipo haja ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko ianzishwe haraka ili mazao kama choroko, dengue, mahindi na kadhalika yaweze kuingiza pesa za kigeni na kuboresha maisha ya wakulima wa mazao mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kutoa pongezi kwa Waziri kwa usimamizi bora, juhudi ziendelezwe kwa ushauri nilioutoa upo, unaohitaji uamuzi wa haraka mfano,

ni ununuzi wa zao la pamba msimu huu kwa Vyama vya Ushirika kupewa mkopo na masharti yapunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. FRED T. MPENDAZOE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja hii. Aidha, napenda kwa namna ya kipekee nimpongeze Waziri wa Sekta hii, Mheshimiwa Wasira kwa jinsi anavyojituma katika kutekeleza majukumu yake. Pia nampongeza Naibu Waziri na watendaji Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati nampongeza Mheshimiwa Wassira kwa jitihada alizofanya na kuweza kufanikisha kuwafidia wakulima wa pamba kwa Tsh. 80 kwa kilo kama ilivyowafidia wanunuzi wa pamba

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mvua za msimu huu kutonyesha vizuri mazao mengi ya chakula yalikauka katika maeneo mengi. Mazao yaliweza kunusurika, ni yale yaliyotokana na mbegu za kisasa. Hii ina maana kwamba ipo haja ya Serikali kuwapatia mbegu bora wakulima, mbegu zilizofanyiwa utafiti lakini uzalishaji wa mbegu pia uliathirika sana kutokana na ukame mkubwa uliotokea maeneo mengi nchini. Je, Serikali haioni ni muhimu sana kuwasaidia wakulima wa mbegu za mazao ya chakula ili waweze kuendelea na uzalishaji wa mbegu? Serikali iwaongeze bei au Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha mbegu bora zinapatikana au zinaendelea kuzalishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, madawa ya pamba, ununuzi mdogo wa madawa ya pamba umesababishwa na uwezo mdogo wa wakulima kununua madawa hayo kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani ambao umesababisha bei ya mwaka huu iwe Tshs.440 kwa kilo badala ya Tshs.500 kwa kilo kwa mwaka jana, je, Serikali inachukua hatua gani mwaka huu ili kuwaongezea uwezo wakulima wa pamba ili waweze kununua madawa ya kuulia wadudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukipa kipaumbele kilimo katika dhana ya kilimo kwanza napendekeza mambo yafuatayo yazingatiwe:-

Moja, suala la mabadiliko ya tabia nchi – *climate change* lizingatiwe. Ipo haja ya kuwepo ushirikiano wa karibu kati ya Wizara ya Maji, Miundombinu na Mazingira. Suala la mabadiliko ya tabia nchi litaleta changamoto kubwa kwenye sekta ya kilimo.

Pili, mkazo utiliwe kwenye miradi ya umwagiliaji. Miradi iliyopo mifano mradi wa Itilima, Talaga, Ngeme na Masanga Wilaya ya Kishapu ipewe kipaumbele.

Tatu, utekelezaji wa programu ya *ASDP* inachelewa kutekelezwa hasa kutokana na upungufu wa wataalam wa kilimo kwenye baadhi ya Wilaya ikiwemo Kishapu. Wilaya zinazochelewa kukamilisha miradi ya *ASDP* zipewe msukumo na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kishapu ni moja ya Wilaya yenye ukame, lakini ina mito mikubwa ambayo inaweza kufaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Naiomba

Wizara ifuatilie ahadi ya Rais wa Awamu ya Pili aliyeahidi kujenga bwawa kubwa kwa ajili ya umwagiliaji katika Mto Manonga kwenye Kata ya Ngofila, Kijiji cha Kalifu. Wananchi wanakumbushia ahadi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri utekelezaji mwema.

**MHE. KHADIJA SALIM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema nimshukuru Mungu kwa kunipa uwezo wa kufika Bungeni na kuweza kutoa mchango katika Wizara husika. Pia napenda kutoa pongezi zangu kwako wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, pamoja na Wenyevitani wako wote kwa imani yako kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilicho mbele yetu ni hotuba ya Wizara husika ambayo ina nia njema kwa ukuzaji wa uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mara nyingi Serikali inatenga fedha nyingi kwa ajili ya kilimo, kinachotufelisha ni ufanisi wake kuwa mdogo, hii inatokana na Wilaya zetu kukosa idadi ya wakulima waliopo katika Wilaya zao. Hatuwezi kugawa bila kujua idadi. Leo hatuna utaratibu wa kujua idadi za wakulima, tutaweza vipi kuwahudumia? Tukumbuke walio wengi katika nchi yetu ni wakulima. Wakulima ambao wanalima bila utaalam, wanalima kwa majembe ya mkono. Tunategemea nini hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tuna nia ya kulima kilimo cha kisayansi na tukafanikiwa, hii itasaidia kukuza uchumi wetu. Katika kuboresha kilimo cha kisasa ni lazima tutumie sayansi, mbegu bora, pembejeo, mabwana shamba wa kutosha, hapa tutaweza kuzalisha kilimo cha biashara na kuinusuru nchi yetu katika omba omba.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kwa wakulima ni muhimu, wakulima wetu bado hawana elimu ya kutosha, hivyo tutalima sana na mazao madogo. Wizara inapaswa kutoa elimu kwa wakulima wetu, ili waweze kulima kilimo chenye tija. Mara nyingi Wizara inawapangia wakulima wataalam, lakini wataalam hao hawawasaidii wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini sasa elimu hii inayomhusu mkulima hapewi yeye mwenyewe? Hiyo ni elimu gani ambayo mkulima wetu hawezi kuifahamu? Tukiendelea kumsubiri mtaalam mwenye Diploma tutafika lini katika maendeleo ya mavuno mazuri kwa wakulima wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Stephen Wasira, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. David Mathayo na Katibu Mkuu wa Wizara kwa kuleta bajeti yao Bungeni.



Mheshimiwa Naibu Spika, katika dira ya bajeti hii Wizara imepewa jukumu kubwa la Kilimo Kwanza, nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wao, naamini wamejipanga vizuri na hakutakuwa na matatizo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri afafanue suala linalotusibu wakulima wa korosho kuhusu pembejeo. Sisi tunategemea zaidi dawa za salfa, biofidan na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya zao hili halikuwa linapata fedha za ruzuku, ni mwaka 2006/2007 tu ndipo ruzuku ya kwanza ilitolewa kwa kununulia dawa za korosho, toka hapo fedha zake zinatolewa kwa shida kweli, mara nyingi zinachanganywa na fedha za *export levy*, fedha ambazo kisheria ni mali ya Halmashauri za Wilaya zinazolima zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iwe na mpango unaoeleweka wa kusaidia dawa za korosho kutokana na ughali wa dawa zenyewe. Fedha za ruzuku ya korosho zieleweke wazi kuwa ni kiasi gani na uwakala wake uwe wazi kama hakuna uangalifu watakaonufaika ni mawakala na sio wakulima, wao wanaweza kununua kwa bei ya chini na kuuza kwa bei ya juu kwa wakulima jambo ambalo linawaumiza wakulima, pia uzalishaji wa korosho nao unaathirika. Ni vizuri Mheshimiwa Waziri, katika dhana ya Kilimo Kwanza awe na mpango madhubuti wa fedha za ruzuku kwa madawa ya korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umwagiliaji bado halijawa safi katika usimamizi wake. Sioni mantiki ya sekta hii kuwa katika Wizara mbili tofauti. Napendekeza Idara ya Umwagiliaji iliyopo Wizara ya Maji irudi Kilimo ili teknolojia yake ihusishwe na utaalum uliopo kilimo. Hata hivyo, nasisitiza umwagiliaji uwepo zaidi wakati wa kiangazi badala ya wakati wa mvua. Katika maeneo ya Mto Lukuledi na Ruvuma katika Jimbo langu la Masasi kuna maeneo mengi ambayo yangeweza kutumiwa kifuku na kiangazi lakini hakuna mipango ya kilimo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ugani sina haja ya kulirudia zaidi kwani ni mwiba katika maeneo mengi. Maeneo mengi hayawezi kujiendeleza kutokana na huduma duni za ugani, kilimo endelevu lazima kiambatane na utaalum wa ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara isikilize maoni ya Wabunge na kuhakikisha kuwa taaluma na teknolojia inawafikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza ni dhana nzuri ikiwa itatekelezeka. Tatizo lililopo Tanzania ni wingi wa kauli mbiu zinazobadilishwa kila mwaka. Nikianza na kauli mbiu chache ninazozikumbuka tulikuwa na Kilimo ni Uti wa mgongo, Siasa ni Kilimo, Azimio la Kilimo la Iringa, Mapinduzi ya Kijani na mengine mengi. Lakini hali ya kilimo chetu bado ni dhaifu tena maeneo mengi waliyokuwa wakitegemea kilimo, kilimo kimekufa au kupungua kasi

yake. Mfano, kilimo cha kahawa Mkoani Kilimanjaro kimeshuka sana tofauti na miaka ya nyuma. Huo ni mfano mmoja lakini ipo mingi tu. Hivyo sioni haja ya kubadili kauli mbiu kila kukicha wakati kilimo kinaendelea kudidimia wakati wananchi zaidi ya asilimia 70 ni wakulima lakini bado kilimo chao ni cha jembe la mkono na wengi hulima kwa ajili ya kujikimu na si kibiashara au kilimo cha ziada, maana kila msimu unapoisha wa kilimo nao huwa hawana hata ziada na matokeo yake ikitokea njaa basi huathirika na tatizo hilo. Hizo kauli mbiu haziwasaidii yahitaji matendo yaendane na kauli mbiu na sio maneno peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha Tanzania kinategemea mvua kwa kiasi kikubwa. Mvua inapochelewa au isipokuwa ya kutosha maana yake ni kwamba wakulima hupata hasara kwani mazao yao hufa kwa kukosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi Serikali iongeze utekelezaji wa kilimo cha umwagiliaji na tuache maneno yasioonekana kwenye *field*, maana tumekuwa tukisikia kilimo cha umwagiliaji bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile inabidi Serikali itoe mafunzo ya kilimo cha kisasa kikiwemo cha umwagiliaji kwa teknolojia rahisi na njia za kisasa zaidi ili wajiiinue katika kazi yao ya kila siku ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuvuna maji kipindi cha mvua ndefu na nyingi, badala ya nchi kupata tatizo la mafuriko bora wananchi wapewe mafunzo ya jinsi ya kuvuna maji ambayo yanaweza kutumika katika shughuli mbalimbali ikiwemo ya kilimo kipindi cha ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni uchache wa maafisa ugani, bado vyuo vya kilimo ni vichache. Kauli mbiu ya kilimo kwanza haiwezi kutekelezeka kama hatuna wataalam wa kutosha wa masuala ya kilimo wawezao kufanya tafiti mbalimbali. Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza vyuo na kusomesha wataalam wengi zaidi ili wasaidie hicho kilimo chetu kuliko kubadilishiwa kauli mbiu zisizo na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni nchi hii kuendelea kununua pembejeo za kilimo kutoka nje zikiwemo zana mbalimbali za kilimo yakiwemo matrekta. Ufike wakati nchi au Serikali ione umuhimu wa kuzalisha zana zake za kilimo. Inasikitisha Serikali kununua zana China na India na bil. 12 zimetengwa kwa ajili hiyo, hivi Serikali haioni kuwa inatengeneza ajira kwa nchi nyingine? Kwanini viwanda kama ZZK, Mbeya na UFI, Dar es Salaam visihuishwe ili vifanye kazi ya kutengeneza zana zetu wenyewe, kwanza tutaongeza ajira. Pili, zana za kilimo zitapatikana kirahisi. Tuna Kiwanda cha Nyumbu cha Jeshi ambacho kingeendelezwa vizuri kingetoa matrekta makubwa na madogo lakini ni kama kimekufa, matokeo yake tunaendeleza viwanda vya nje kwani tunaendelea kununua nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kwanza hakiwezi kuwa kwanza kama hatuna viwanda vya usindikaji, matunda na bidhaa nyingi huoza kwa kukosa *processing industries*, matokeo ya Watanzania wanakunywa juisi za makopo na maboksi kutoka nchi

za Uarabuni ambako kuna ukame (jangwa). Vile vile matunda mengi yanauzwa Kenya ndio watengeneze juisi huko, kwa maana hiyo Watanzania tunaendeleza viwanda vya nchi nyingine na kutengeneza ajira badala ya kuanzisha vya kwetu, hii ni aibu. Nchi yetu ina rasilimali nyingi sana hatushindwi, kuanzisha viwanda vidogo na vikubwa kwa ajili ya mazao yetu na tuache tabia ya kuuza malighafi kwa bei ya kutupa, matokeo yake kununua bidhaa kutoka nje kwa bei ghali wakati malighafi inatoka kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitaka Serikali ituambie ni jinsi gani kauli mbiu ya Kilimo Kwanza itatekelezeka maana tumezoea kusikia maneno matamu, utekelezaji hafifu. Tatizo ninaloliona ni bajeti ndogo ya asilimia saba (7%) sawa na ya mwaka jana kwani ilikuwa hivyo hivyo asilimia saba (7%) ingawa ipo tofauti ndogo ya kiwango cha pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kujua *project* za *ASDP* wanazi-*coordinate* vipi na kauli mbiu hii, pamoja na *project* zingine zote za kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kufahamu, tafiti za kilimo zinasaidiaje kilimo maana kilimo chetu hakikui na kinazorota ingawa tumepitia kauli mbiu nyingi zilizojaa maneno ya kisiasa lakini matunda hayaonekani.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara kwa kuandaa hotuba yenye kuonyesha mwelekeo wa Wizara kwa kipindi hiki cha mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wa – Dodoma tunayo mazao ya biashara ambayo ni yakiwepo yale aliyoyataja Mheshimiwa Waziri yakiwa ni karanga, ufuta na alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali itambue zao la zabibu kuwa ni zao la biashara ambalo linapaswa kupewa umuhimu na kuweka utaratibu wa jinsi ya kuwawezesha wananchi waweze kuendeleza zao hilo katika Mkoa wa Dodoma. Vile vile tunaomba Wizara ifanye utafiti wa zao hili ili kupata mbegu nzuri zaidi na madawa ya kutibu magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Serikali itoe maelezo ni mpango upi uliwekwa na Serikali wa kuendeleza zao hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mwingi Tanzania tumetegemea mvua kwa kilimo chetu, wakati sasa hali ya hewa na uchumi umebadilika na sisi lazima tubadilike, twende sasa kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tanzania tuna eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji hekta milioni 29.4 sawa na asilimia 31.1%, lakini linalotumiwa ni hekta milioni 0.25, ni sawa na

asilimia 0.3% Kitaifa. Nchi yetu ina mabonde, mito ya kudumu, maziwa na hata mvua ikinyesha unyevu unyevu hubakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutegemea mvua kwa mwaka huu, tunategemea ukame mkubwa sana utatokea, kiu cha maji, njaa kubwa na mahangaiko ya chakula cha njaa. Lakini katika Mkoa wa Lindi kama suala la kilimo cha umwagiliaji lingezingatiwa kwa siku za nyuma, wala tusingepata shida kwani tuna mabonde ya umwagiliaji kwa Wilaya za:-

(1) Ruangwa kuna mabonde ya:-

- Chikoko
- Chinokole
- Mkowe
- Chiimbila A
- Chiimbila B
- Likunja
- Chienjele

(2) Lindi Vijijini

Rutamba Kubwa

(3) Liwale

Mito

(4) Kilwa

Bonde La Makangaga,

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni mabonde makubwa ya unyevu mwaka mzima.

- Mkoa wa Lindi una eneo hecta elfu 11,218 kati ya hekta milioni 29.4 nchini zinazofaa kwa umwagiliaji Tanzania. Lakini zinazotumiwa ni hekta 727 tu ambazo ni asilimia 6% ya eneo nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali, ili kuokoa njaa ya chakula Mkoani Lindi tunaomba hatua za haraka zichukuliwe kwa:-

- Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji;
- Kuwa na wataalam wa kilimo cha umwagiliaji;
- Kuwapa nyenzo za kufanyia kazi za shughuli za kilimo cha umwagiliaji (usafiri, tractor, vyombo vya kisasa); na
- Mikopo ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwe na benki ya wakulima ili wakulima waende wakakope ili waweze kulima mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Mazao zamani zilikuwa zinajitegemea, lakini sasa wanatengewa pesa, wanapewa kidogo tu ambazo hazitoshi kwa kusimamia mambo ya kilimo kama Bodi ya Pamba, pia ya kilimo cha korosho zina mambo mengi:-

- Kuhimiza suala la mfumo wa maghala kitu kipya Lindi, inabidi elimu itolewe;
- Upandaji miche mipya;
- Elimu ya ubanguaji korosho;
- Upangaji wa korosho madaraja; na
- Ufuatiliaji wa pembejeo

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiambia Wizara hii kwamba ndiyo mbebaji wa kauli mbiu ya kilimo kwanza. Dunia katika mtikisiko huu wa uchumi ambapo Tanzania ni sehemu hatuwezi kubaki bila kuguswa. Hata hivyo, ukombozi wetu unaweza kupatikana, kama kweli tutaweka nguvu, bidii na maarifa katika kilimo bora kinachozingatia taratibu za kilimo na matumizi ya viwango vya pembejeo. Tukitumia vizuri pia wataalam wa ugani wa sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa kilimo kwanza hatuwezi kutegemea kilimo kinachosubiri msimu wa mvua kwamba tutafanikiwa, la hasha! Majira ya mvua nayo sasa yamebadilika, vinaweza kuwa vifupi ama vikachelewa tofauti na zamani kutokana na kuongezeka kwa joto duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itilie mkazo kilimo cha umwagiliaji. Kilimo hiki pia kitaathiriwa maana mvua ni haba. Kwa hiyo iko haja ya kubajeti uchimbaji visima virefu, vifupi na mabwawa au malambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeiteua mikoa michache ambayo yote inasifika kwa uzalishaji wa mazao hasa ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiarifu Serikali kuwa na Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa yenye mvua nyingi na udongo wenye rutuba. Udongo huu unaweza kuzalisha mazao yote ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la Mkoa wa Kagera sasa ni uvamizi wa maeneo mapya yanayopandwa miti ya mbao na karatasi kwa wingi na kuwaacha hasa wanawake ambao ndio wazalishaji wakuu wa chakula bila maeneo ya kulima. Baadhi ya viongozi

wasio waaminifu wameshiriki kinyemela kuuza maeneo ya wazi ya vijiji kwa watu binafsi, hali inayopunguza uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo pale wanapolima wananchi wanaweza kuzalisha kahawa, vanilla, ndizi, mhogo na mazao mengine ya msimu. Tatizo ni soko kwa mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasemaje kuhusu soko la uhakika la zao la kahawa? Ni ahadi ya Rais kwamba ataboresha soko la kahawa. Hili soko bado halijaboreka. Wananchi walianza kuzalisha vanilla, bado soko linasumbua sana. Ndizi na mhogo ni mazao ya chakula yanayompunja sana mkulima maana hununuliwa shambani. Je, Serikali inasaidiaje wakulima wa mazao ya chakula hasa ndizi na mhogo wasipunjwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kutokana na bajeti yake na pesa za *EPA* walizopewa kuinua kilimo, yaanzishwe mashamba darasa kila Wilaya na yafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, semina na mafunzo yanayotolewa kwa watumishi wa Wizara yaachwe (labda pale ambapo kuna watumishi wapya au mbinu mpya). Badala yake yaanzishwe mafunzo ya wakulima wenyewe huko huko mashambani. Aidha, wataalamu wa ugani wawepo wa kutosha. Pale ambapo hawapo, utaratibu wa dharura kama uliotumika kwa walimu ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wilaya ya Muleba yenye eneo kubwa linalofaa kwa umwagiliaji kandokando ya mto Ngono, lipewe umuhimu kwa kupata mradi wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wapewe mbinu mpya za uzalishaji katika kilimo na wasaidiwe kupata masoko ya mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mikopo itolewe kwa vikundi vya wanawake na vijana kwa mpango maalum. Serikali ikitegemea wanawake na vijana wakakope katika benki kwa taratibu za kawaida, hawatawahi kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake na vijana ndiyo nguvu yetu katika uzalishaji wa chakula na mazao ya biashara, lakini hawana dhamana zao wenyewe matokeo yake wanaokopeshwa ni wale walanguzi na wachuuzi. Hii inaathiri sana kilimo chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. HAWA A. GHASIA :** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Stephen Wasira kwa juhudi zake pamoja na timu yake kwa uongozi mzuri na msukumo wake katika kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo binafsi kwa jitihada zake za dhata katika kuhamasisha, kusimamia na kuendeleza utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani, utaratibu huu umeleta ukombozi mkubwa kwa wakulima hasa wakulima wa zao la korosho ambao wamenyonywa kwa muda mrefu na wafanyabiasha wababaishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi nzuri zinazofanywa na Wizara ipo haja ya kuhakikisha kuwa utaratibu huu unasimamiwa kwa karibu na wataalam wenye kuufahamu vizuri utaratibu huu pia wenye uzalendo na wanaoupenda utaratibu huu na si walioajiriwa tu kusimamia utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kuwa ununuzi wa korosho kwa msimu uliopita Vyama vya Msingi vya mazao ya korosho na Vyama Vikuu vya *MAMCU* na *TANECU* Mkoani Mtwara vimepata hasara iliyotokana na benki za NMB na CRDB kuwakata riba kubwa kwa vyama hivyo kati ya Shs. 25 hadi 137 kwa kilo kiasi ambacho ni kikubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na riba kubwa vyama vimeshindwa kulipa ushuru wa Halmashauri, vimeshindwa kuendesha mikutano ya mwaka na hivyo kushindwa kufanya maandalizi ya ununuzi wa korosho msimu unaotegemewa kuanza mwezi wa kumi mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani mtikisiko wa uchumi uzisaidie Benki kutengeneza *Super profit* na Vyama vya Msingi vya Ushirika kutengeneza hasara. Hii inaweza ikaua kabisa utaratibu huu kwa zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, *MAMCU* walishaandika barua kwa Mkurugenzi wa Ushirika, Wizara ya Kilimo. Hata hivyo, haijapata majibu, namwomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Wasira kufuatilia suala hili kama ilivyofanyika kwenye zao la pamba ili kauli mbiu ya Kilimo Kwanza ipokelewe na wakulima wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Rorya, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wakurugenzi, mameneja, wataalam, wenyeviti na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba yenye matumaini na mipango mikakati ya kukomboa wakulima kwa kuongeza tija na kupunguza umaskini. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwa kutoa ushauri/ombi katika maeneo machache ya hotuba hii ya kihistoria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa109 – Mazao ya Bustani, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kutambua na kuwakumbuka vikundi vya wakulima wadogo wa bustani kwa kuandaa programu itakayoanisha maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, katika Wilaya mpya ya Rorya wakulima wadogo wa bustani wa mboga wanaendesha shughuli za kilimo katika vijiji mbalimbali kando ya ziwa. Jumla ya vikundi 28 vyenye wanachama 228 vimepatiwa mashine za umwagiliaji aina za MP (*Motorized pump*) na aina ya *Trodle pump*, jumla 27.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika programu ya Wizara kama ilivyoelezwa kwa hotuba ya Waziri Kif. 172 ukurasa 109 itambue vikundi nilivyotaja ili vikundi viweze kuhimiza kutumia fursa zitakazopatikana kutokana na programu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri anijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 117 kuhusu matumizi bora ya Ardhi. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, na timu yake kwa kuandika mpango kabambe wa Kitaifa wa matumizi bora ya ardhi (*National Agriculture Land use planning and Management Master Plan*) itakayotoa mwelekeo wa matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 185 zimetajwa Wilaya ambazo Maafisa Ugani watapatiwa mafunzo kuhusu kanuni za matumizi bora ya ardhi na kudhibitiwa mmonyoko wa udongo Tarime imetajwa kama mmojawapo wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya Aprili 2008, Wilaya ya Rorya na Tarime zilikuwa zimehesabiwa kama Wilaya ya Tarime. Ushauri wangu ni kwamba, kwa kuwa Wilaya ya Rorya inayo Mkuu wa Wilaya na shughuli zote za kiutawala na kiuchumi zinaendesha kutoka Rorya. Naomba kati ya Maafisa Ugani 22 watakaopatiwa mafunzo wale wa Tarime baadhi wapangwe Wilaya ya Rorya. Naomba Mheshimiwa Waziri azingatie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 119, Mipango ya kuhifadhi mazingira katika kilimo. Ushauri wangu ni kwamba, naomba Wilaya ya Rorya ipatiwe mafunzo ya hifadhi ya mazingira kupitia mamlaka zinazohusika. Kamati za Hifadhi Mazingira kutoka Wilaya ya Rorya katika Kata hadi vijijini zinafanya kazi nzuri kuhifadhi mazingira. Halmashauri ya Rorya katika mwaka 2009/2010, ishirikishwe katika shughuli za hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametoa hotuba ya kuhistoria na ya kimapinduzi. Ni matumaini yangu kuwa utekelezaji wa hotuba hii utafanywa kwa nguvu na kasi inayolingana na yaliyomo ndani ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa uwepo kwa Vyama vya Ushirika. Naamini katika mikoa mingine vyama hivi vimefanya vizuri na wakulima wamefurahia sana utendaji wake.



Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ifike Mkoa wa Lindi na kukiangalia Chama Kikuu cha Ushirika Ilulu kama utendaji wake unafanana na utendaji wa vyama vya mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu stakabadhi ghalani, mikoa mingine kama vile Mtwara wamefanikiwa, ingawaje kuna baadhi ya Wilaya wamekuwa wakilalamika kwamba kiandikwacho katika risiti ya mkulima hakifanani na kile kilichoandikwa katika leja ya Chama cha Ushirika. Mara nyingi hunyofoa vikaratasi vya madaftari na kumpatia mkulima ambaye ameacha mazao yake vikiwa na thamani ya mazao hayo pungufu ya mazao halisi aliyoacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ilianganalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mazao kama vile ufuta hayana bodi. Ni kipi kikubwa ambacho kinawakataza wananchi wasiuze mazao yao kwa wafanyabiashara wengine ambao wako tayari kununua kwa bei ambayo mkoa umepanga au Chama cha Ushirika kimepanga? Wakati mwingine wafanyabiashara hao huhitaji kununua kwa bei kubwa zaidi ya iliyopangwa lakini huzuiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika hii imekuwa kero kubwa kwa wakulima. Kikubwa mno ni pale hata Halmashauri hukosa mapato kwa sababu wananchi hutorosha mazao hayo kwa njia za panya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wakusanyaji wa ushuru katika vizuio vya maliasili, kipindi hiki ndicho kwao ni muda wa kujitajirisha. Kunakuwa mitandao, kati ya kizuio kimoja hadi kingine kwa njia ya simu na siyo risiti kwani kwa kutumia risiti huchelewa kukamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao hawana fedha za kumpa mtandao huo ndio hurudishwa hadi Wilayani na hadi kufikishwa Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, wakati wa msimu wa mazao haya niliyoyataja, hasa ufuta wafike Mkoa wa Lindi na kuchunguza haya niliyoyasema hapa ili kuondoa kero hii hasa Wilaya ya Kilwa, (Mandawa na Malendego).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ya kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero kubwa inayotukabili Manyoni Magharibi ni:-

Kwanza, ukame. Kauli mbiu ya Kilimo Kwanza haitakuwa na maana kama hakuna maji, mvua zimekuwa kitendawili katika baadhi ya maeneo. Maji ya Ziwa Victoria yaekelezwe Mkoa wa Singida pia. Vinginevyo kauli mbiu hii ya Kilimo Kwanza itabakia kitendawili. Sisi tunadhani kauli mbiu iwe maji kwanza ili kufufua kilimo.

Pili, kuhusu bei ya Mazao. Eneo letu wanalima mazao mchanganyiko ya alizeti, dengu na nafaka za mahindi, mtama na uwele. Lakini pindi mavumo yanapoanza bei huanguka na walanguzi hutawala kununua mazao kwa bei ya kutupwa wakiwa-*exploit* wakulima maskini kwa sababu ya shida zao.

Tatu, ni kuhusu Kilimo cha Maksai (Wanyamakazi). Eneo hili ni mahodari kwa kilimo hiki lakini wengi wanakosa majembe ya plau. Serikali inaonekana kusisitiza zaidi kilimo cha matrekta na *power tillers* wakati sehemu kubwa ya wananchi wanatumia jembe la mkono. Takwimu zinazoonyesha asilimia 70 ya wakulima wanatumia jembe la mkono, asilimia 20 plau na asilimia 10 matrekta. Napendekeza hatua za makusudi zifanywe kusambaza plau nyingi ili kuinua kilimo bila gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha nyingi zinaonyeshwa kwenye bajeti kuelekezwa kununua zaidi nyenzo za kazi maofisini kwa ajili ya kusimamia, kuratibu na kununua vitendea kazi yakiwemo magari. Napendekeza fedha nyingi zitengwe kwa kununua ma-plau na maksai kwa ajili ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za wataalam zinaonyesha kuwa eka 29.4 million ya ardhi ya Tanzania ni *arable land* inaweza kulimika lakini ni eka 30,000 tu ndizo ziko *under cultivation*. Kama ni kweli, nchi hii si nchi ya kilimo, watu wanajishughulisha na biashara ndogo ndogo tu na kukimbilia mijini wakitanga tanga bila shughuli maalum. Hivyo si kweli tunaposema kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifugo, takwimu zinaonyesha tuna ng'ombe kati ya 18 – 20 milioni, lakini hatutumii mifugo hii kutuletea mageuzi ya kilimo. Ng'ombe wametumika kukuza migogoro baina ya wakulima na wafugaji, badala ya kutumika kuwaunganisha, imetumika kuwafarakanisha na kuleta mtafaruku usio na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Kuanzishwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko uletwe haraka Bungeni.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na wakurugenzi wote kwa hotuba nzuri yenye kuzingatia maudhui ya kilimo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti katika Kilimo. Napenda kuipongeza Wizara kwa kuweka mkazo mkubwa katika utafiti wa mazao ya kilimo sambamba na kutilia mkazo wa mazao ya kilimo cha kisasa na upatikanaji wa mbegu bora, utafiti utatusaidia sana katika kuongeza tija katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa mradi wa kuanzisha kituo cha utafiti wa ubora wa hali ya juu (*Rice Centre of Excellence*) wa zao la mpunga ambao utatekelezwa chini ya programu ya kilimo ya kuendeleza Tija na uzalishaji katika Afrika Mashariki (*Eastern Africa Agricultural Productivity Programme*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo hicho ambacho kitakuwa katika Kituo cha Utafiti cha *KATRIN* – Ifakara katika Jimbo langu kitasaidia kuleta msukumo kuhusu uzalishaji wa zao la mpunga, pamoja na magonjwa ambayo zao hili huwa linakabiliwa nayo. Kwa mfano, katika mwaka uliopita wa 2008/2009 licha ya jitihada za wananchi za kulima vizuri na kuwahi majira, mpunga ulikabiliwa na ugonjwa wa kukauka, ugonjwa ambao wenyeji tunauita *Kimyanga*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwepo kituo hiki cha Utafiti cha *KATRIN* ambacho kitaongoza na kuratibu shughuli za utafiti kikishirikiana na vituo vyote vya utafiti katika kanda saba za utafiti, vyuo vya mafunzo ya kilimo na chuo Kikuu cha Sokoine, ni matumaini yangu kuwa matatizo ambayo hayana majibu yatapatiwa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hali hiyo, iko hali ambayo mimi na wenzangu wa Kamati ya Kilimo, Maji, Mipango na Uvuvi tumeiona ambayo Wizara itabidi iingalie, nayo ni wataalam wa utafiti walio wengi kuwa katika umri wa kustaafu, bila kuwa na watu walio na ujuzi karibu yao kwa ajili ya kuwarithi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu katika kipindi cha miaka 10 ajira haikuwepo (awamu ya tatu) kiasi cha kukosekana *succession plan* ya watafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ifikirie kuwa-retain watafiti hao *on contract terms* kwa miaka miwili hadi mitatu ili waweze ‘kuwa-*train successors* wao. Tusipofanya hivyo, wakati bajeti ya Vyuo vya Utafiti imeongezwa tija yake haitaonekana kutoka kwa hao watafiti wapya watakaojiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya msukosuko wa hali ya uchumi duniani katika mazao ya kilimo, bei ya mazao ambayo hayakuathirika na msukosuko huo ni pamoja na *cocoa*. Bei ya dunia inafikia dola takribani mbili hadi tatu kwa kilo, (May, 2009).

Mheshimiwa Naibu Spika, zao hili kama nilivyowahi kuuliza swali halina Afisa Ugani na katika Wilaya ya Kilombero wananchi wameanza kulilima zao hili bila utalam wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la *Pods* za *cocoa* kusinyaa baada ya kufyonzwa maji maji yake na wadudu na wakulima hawajui dawa yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wafanyabiashara wanunuzi binafsi wanaonunua zao hili. Ukiwaeleza tatizo hili wao wanasema wasingependa tutumie dawa yoyote. Tunaomba msaada juu ya ugani wa zao hili na ikibidi kama nilivyowahi kuomba, wapelekwe maafisa kilimo nchi za Cote de Ivoire, Ghana ili wakirudi waweze kuja kutuenezea elimu ya ugani katika maeneo tunayolima zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Satellite Agricultural Colleges*. Sasa hivi tuna zana hizi ndogo ndogo za kilimo ambazo zinaenea kwa kasi sana huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza tuwe na vyuo vidogo vidogo vya kilimo katika ngazi za Kata ambavyo siyo lazima vianzishwe na Serikali bali Serikali iwadhamini watu binafsi au mashirika ya watu binafsi kwenye mablenki ili waazishe vyuo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vyuo hivyo pawepo na karakana, madarasa mawili au matatu, mabweni mawili (wasichana na wavulana) na shamba lisilopungua ekari 100 kwa ajili ya kilimo cha vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vyuo hivi, mashine kama *power tillers*, *planters*, *threshers*, zitafundishwa utendaji kazi wake kinadharia na katika karakana kivitendo, kwa kuweza kufungua na kuzifunga ili teknolojia hii rahisi iweze kufika vijijini kama elimu ya ufundi wa baiskeli ulivyoenea vijijini.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kuipongeza sana Serikali kwa kutambua umuhimu wa kilimo na kutoa kipaumbele cha kwanza Kilimo Kwanza katika bajeti ya Serikali mwaka 2009/2010. Pamoja na pongezi hizo naomba nichangie mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikoa yote nchini wakulima wamehamasika sana kulima mazao ya mbegu za mafuta na hivi sasa kufikia hatua ya kujaribia kutosheleza mahitaji ya Taifa. Pamoja na juhudi hizo za wakulima nchini Serikali haijachukua hatua za dhati za kuwalinda wakulima hawa. Serikali bila kujali maslahi ya wakulima imekuwa ikiruhusu uingizwaji wa mafuta ghafi na yaliyosafishwa kutoka nje na hivyo kusababisha mazao ya wakulima kukosa soko. Hivi sasa kuna mazao mengi kama alizeti, karanga na ufuta ambayo yamekosa soko katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Iringa, Morogoro, Mbeya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukame uliotokea nchini kote mikoa iliyoathirika sana na ukame ni pamoja na Mkoa wa Dodoma. Mkoa wa Dodoma hivi sasa unakabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula katika Wilaya zote hivyo Serikali iandae chakula cha msaada hususan cha bei nafuu, chakula bure na nguvu kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dodoma ni moja ya mikoa kame sana nchini. Hata hivyo, mkoa huu una ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo cha mazao mengi. Aidha, ardhi ya mkoa huu haihitaji mbolea za chumvi chumvi ila mbolea ya samadi na mboji. Kwa kuwa tatizo ni ukosefu wa unyevu, tunaomba Serikali itoe kipaumbele katika kilimo cha umwagiliaji ili wakulima wa Mkoa wa Dodoma nao wajitegemee kwa chakula. Napenda kuisitiza kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma kuwa mpaka sasa Serikali haijatoa msaada wa kutosha kuwasaidia katika kilimo chao kama inavyofanya katika mikoa mingine. Kama mikoa ya korosho, pamba, chai, kahawa na

mahindi inapewa ruzuku na pembejeo mbalimbali, Mkoa wa Dodoma unasaidiwa nini hadi sasa? Serikali lazima ibadilike, Mkoa wa Dodoma nao unahitaji msaada wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha wakulima cha muda mrefu ni uundwaji wa Bodi ya Mazao mchanganyiko. Serikali iharakishe kuunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko ili kuwasaidia soko wakulima wa mazao mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni uongozi wa Mkoa wa Dodoma umeanzisha kilimo cha zao la korosho. Hata hivyo, wakulima wengi wana mashaka kama zao hili litastawi na kuzalisha mazao ya kutosha kuwanufaisha wakulima. Kwanza mashaka yao ni kama utafiti wa kutosha umefanyika. Pili, kama mbegu wanazopewa wakulima ni bora. Tatu, kama kuna wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri awahakikishie wakulima wa Dodoma kuhusu kilimo cha korosho mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu naomba kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

**MHE. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David; Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya na hotuba yao nzuri. Kwa hiyo, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru sana kuingiza Wilaya ya Serengeti kuwa Wilaya zitakazopatiwa mbolea ya ruzuku. Wilaya ya Serengeti ina ardhi nzuri na mvua za kutosha, hivyo tukipewa mbolea ya ruzuku na mbegu bora tutaongeza mazao katika hekta na hii itaondoa umaskini. Tunaomba sasa tuwekewe SGR ili wakulima waweze kuuza mazao yao kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni muhimu sana katika kuwapatia chakula wananchi na pia mapato ambayo huingia mfukoni mwa mkulima moja kwa moja na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuongeze *production per hectre*, tunahitaji kutumia kilimo cha kisasa. Kilimo hiki kitahitaji tujue katika eneo langu udongo wa aina hii ni zao gani linatakiwa kupandwa, mvua kiasi, ni zao gani linastahili kupandwa huko, tarehe gani tupande, tuweke mbolea, tupalilie, tuweke dawa na tuanze kuvuna. Pia, itakuwa muhimu kutumia mbolea kiasi gani na wakati gani. Ni lazima kabisa kutumia mbegu bora inayo-*respond positively* kwa mbolea na ambayo inahimili magonjwa na ukame.

Kwa sasa hivi mbolea inapewa kipaumbele zaidi ukilinganisha mbegu bora. Lakini mbolea lazima iambatane na mbegu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kilimo kinufaishe wananchi soko la uhakika na lenye kumpatia mkulima bei nzuri ni lazima. Kama wananchi watalima halafu wauze mazao yao kwa bei ndogo watakata tamaa na kuacha kulima.

**MHE. DR. IBRAHIM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Hali ya chakula sio nzuri katika Jimbo la Kibaha Vijijini. Hii inatokana na ukosefu wa mvua ya kutosha. Kata karibu zote zilikumbwa na ukame, Mlandizi, Soga, Ruvu, Kwala na Magindu. Nashauri suala hili lifuatiliwe kwa karibu ili wananchi wa maeneo husika wapate msaada wa chakula pale itakapobidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli mbiu ya Kilimo Kwanza ni muhimu. Hata hivyo msisitizo uwekwe katika upatikanaji wa vifaa vya kisasa – *tractors* na Maafisa Ugani kufanya kazi kwenye mashamba ya wananchi. Hivi sasa Maafisa Ugani tulionao wanafanya kazi kwa mazoea, wako ofisini muda mwingi na wengine hawaishi katika Kata wanazozihudumia. Ni vema Wizara ije na mpango wa kujenga nyumba za Maafisa Ugani katika vijiji wanavyovihudumia, hata ikibidi kwa mtindo wa *operation*, kama ilivyokuwa katika ujenzi wa shule na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazap. Kibaha Vijijini katika Kata ya Soga pamekuwa na ukulima wa mkonge kwa miongo mingi. Pamoja na kuzorota katika kipindi kilichopita, hivi sasa ukulima huu unafufuliwa kwa kasi. Ni vema Serikali ikatoa msaada wa kuhakikisha kilimo kinashamiri. Suala moja linalorudisha nyuma nguvu za wafanyakazi wa mkonge pale *Alavi Sisal Estate* ni ukosefu wa malipo ya kiinua mgongo na mengineyo wakati shamba lilipouzwa kutoka kwa mwenye mali wa zamani – Karimjee hadi wa sasa, Mohamed *Enterprise Limited*. Wafanyakazi waliachwa solemba, hawakulipwa mafao yao hadi leo, zaidi ya miaka mitano sasa. Naomba Serikali ifuatilie dhuluma hii ili wafanyakazi wapate haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu korosho. Zao hili linahitaji msukumo wa kipekee ili uzalishaji ukue. Napongeza utaratibu wa soko wa ghala. Naamini, mpango huu utakapoanza Pwani utasaidia kukuza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao mengine kama vile mananasi, maembe ya kisasa, minazi na kadhalika, yatiliwe mkazo kwa kutoa mikopo kwa nguvu kazi hasa vijana.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake iliyoelezea kwa umahiri mkubwa, ikijumuisha maeneo mbalimbali ya sekta ya kilimo. Napenda pia kuwapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu, Wakurugenzi na watendaji wakuu wa Taasisi mbalimbali za Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Kilimo Kwanza haikuja kama ajali bali ni mnyumbuliko wa dhana za awali ya Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa letu. Kwa hali hiyo, kwa sababu hadi sasa dhana ya awali ya Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa letu ilikuwa inabaki kama wimbo tu midomoni na masikioni mwa watu wengi kwa kutopewa msukumo mkubwa, sasa ni wakati muafaka wa kutekeleza kwa vitendo dhana ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado sioni ni jinsi gani lengo la dhana ya Kilimo Kwanza linaweza kufikiwa yaani kuondokana na umaskini wa kipato na njaa miongoni mwa wananchi wetu. Lengo la kwanza la millennia limekuwa likitukumbusha juu ya kuondoa umaskini na njaa iliyokithiri kwa asilimia 50 kati ya mwaka 1990 na 2015. Mpaka sasa hapa tulipo bila juhudi na maarifa ya ziada hatuwezi kufanikisha lengo hili. Tunahitaji uwekezaji wa nguvu wa rasilimali watu, nyezo na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na kuchezea kwa upana namna ya kufanikisha lengo la Kilimo Kwanza inabanwa na ufinyu wa fedha na upungufu mkubwa wa wataalam na Maafisa Ugani. Ili kufanikisha mpango huu inabidi maeneo mengine ya utekelezaji kwenye Wizara zingine yapunguzwe vipaumbele vyao kwa muda wa miaka kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la zana na pembejeo za kilimo katika mapinduzi ya kilimo ni muhimu sana. Kumekuwa na namna kadhaa za kuhakikisha upatikanaji wake, lakini pamoja na yote hayo, katika sehemu mbalimbali imekuwa vigumu kumfikia mkulima kijijini. Mpango wa vocha na utaratibu wa kumfikia mkulima kwa miaka ya nyuma ulikumbwa na kashifa ya mawakala kufanya udanganyifu mkubwa. Kwa msimu uliopita Serikali ilifanya utaratibu mzuri sana wa kumfikishia mkulima pembejeo za kilimo zikiwemo mbegu na mbolea. Hata hivyo, kwenye Halmashauri chache, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Watendaji wa Kata kwa kushirikiana na mawakala walihujumu mchakato huu kwa kuuza pembejeo hizo kwenye Kata zingine kabla ya kuwafikishia wakulima. Malalamiko ya matukio hayo yalipokelewa toka Kata za Chilulumo (ambako mtendaji wake tayari kafikishwa Mahakamani), Chitata na Kamsamba Jimboni Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukomesha uhuni huu ni vizuri Serikali kuu (kupitia Wizara hii) iwe inatuma wataalam wake kufanya ukaguzi (*Audit*) ya usambazaji wa vocha za ununuzi wa pembejeo hizi kwenye ngazi ya Wilaya, Kata na hata Vijiji kwani hata huko kuna ufisadi dhidi ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jinsi hotuba iliyowekwa wazi mpango mzima wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, nalazimika kuunga mkono hoja pamoja na kuomba *exemption* ya wananchi wa Wilaya ya Mbozi kuruhusiwa kuuza mazao na viazi nje ya nchi ambako bei yake ni nzuri sana.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kutoa ruzuku kwa wakulima wa pamba nchini. Lakini kwa kuwa mojawapo ya mazao yaliyoathirika kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani ni pamoja na kahawa. Bei ya kahawa imeshuka sana kiasi kwamba wakulima wasipopewa ruzuku hawataweza kurudisha gharama walizozitumia na hivyo kushindwa kuzalisha kahawa. Naomba na kushauri Serikali ijitahidi kuwapatia ruzuku wakulima wa kahawa ili kuwakomboa katika janga hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu benki ya wakulima, nashauri benki hii ipewe kipaumbele. Mikopo yenye masharti nafuu na ya muda mrefu itolewe kwa wakulima na wafugaji. Matawi ya benki hii yafunguliwe Wilayani kote ili huduma hii iwafikie kwa urahisi wananchi wa vijijini na mijini. Pia wananchi wapewe elimu ya kutosha kuhusu benki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli mbiu ya Kilimo Kwanza naiunga mkono. Lakini napenda kushauri kuwa mapendekezo yote yaliyotolewa na wadau katika mkutano wa Kilimo Kwanza Kunduchi *Beach* Hoteli yafanyiwe kazi kwa asilimia mia moja, kinyume na hapo tutakwama tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE: HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa S. Wassira. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kamilifu ambayo ninaunga mkono kwa asilimia mia moja. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. D. Mathayo, kwa kazi nzuri na kwa kujibu maswali kikamilifu Bungeni. Pia nawapongeza Katibu Mkuu na wataalam husika wa Waziri hii. Nawaomba wataalam hao wasaidie kikamilifu utekelezaji wa yale yaliyokusudiwa katika hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika michango yangu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Maliasili nimeeleza kuhusu Wizara hii na hali halisi ya Jimbo langu la Liwale, hivyo sina sababu kurudia. Hata hivyo, tatizo nililonalo hivi sasa katika Mkoa wa Lindi hususan Jimboni kwangu Liwale ni kusuasua kwa manunuzi ya zao la ufuta. Bei ilikuwa, TShs.1,000/= kwa kilo, sasa ni Tsh.800/= kila kilo. Lakini ununuzi wa zao hilo unasuasua sana kwa madai kwamba *CRDB* inasita kutoa fedha kwa Chama cha ILULU. Kwa vile maelezo hayo hayawasaidii wakulima, Serikali inawasaidiaje wananchi hao hivi sasa hasa tukizingatia kwamba kipindi hiki pia kuna njaa katika maeneo hayo? Naomba sana Waziri atusaidie kupata ufumbuzi kwa zao hili ili wananchi wa Liwale au Mkoa wa Lindi wapate kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. DAMAS PASCAL NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Steven Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yake



nzuri. Pia nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Mathayo David Mahayo kwa kazi nzuri ya kumsaidia Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania kwa kusimamia suala la kilimo kwa kauli mbiu mpya ya Kilimo Kwanza ambayo ni katika azma ya kuleta *New Impetus* kwenye mapinduzi ya kilimo. Ilibidi Mheshimiwa Rais aitische mkutano maalum wa Viongozi Wakuu ndani ya Serikali na Bunge kuonyesha uzito anaouweka kwenye kilimo. Sasa kazi ni kwetu sisi wadau wengine wote tunaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuende mbele vizuri katika kilimo kuanzia hapa tulipo ni lazima kuangalia nyuma tulikotoka; kwa nini hatukufanya vizuri na tujifunze kwa makosa ya uzoefu. Nashauri wataalam wa kilimo sasa wafanye kazi kwa bidii, kwa kujituma, kwa uaminifu na kwa uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pembejeo lipewe umuhimu mkubwa, Serikali ilianzisha mpango wa *voucher* kwenye mbolea na mbegu msimu uliopita, Jimboni kwangu Babati utaratibu huu haukupokelewa vizuri kwa sababu ulionyesha ubaguzi fulani, kuchagua baadhi ya au aina fulani ya mbegu na kuacha aina nyingine. Pia utaratibu mzima haukueleweka na kusababisha kero nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba elimu ya kutosha itolewe kuhusu mpango wa vocha kwa pembejeo na kuwe na udhibiti wa kutosha kuepusha matumizi mabaya ya ruzuku hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri na wote wahusika katika Wizara hii kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kwamba zao la zabibu limesahaulika/limepuuzwa kabisa katika hotuba, kwa hiyo halipo pia katika mipango ya maendeleo ya Wizara hii. Wizara lazima itoe sababu za msingi kwa nini maendeleo ya zao hili ambalo limeanza kufufuka (baada ya enzi ya *DOWICO*) yamepuuzwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa notisi kwamba sitaunga mkono hoja hii kama Waziri hatatoa maelezo ya mipango aliyonayo ya kuliendeleza zao hili muhimu.

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Kilimo; Naibu Waziri, Mheshimiwa Mathayo David Mathayo pamoja na Katibu Mkuu, watendaji wote wa Wizara kwa juhudi kubwa wanazozifanya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia themanini ya Watanzania ni wakulima na takribani asilimia kubwa kati yao bado wanalima kwa kutumia jembe la mkono bila

kutumia teknolojia ya kisasa na ndio maana pamoja na ardhi kubwa tuliyonayo na mito mizuri bado hatujaweza kujitosheleza kwa chakula katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sasa Watanzania tujiulize kwa kauli mbiu tunazojiwekea kwa mfano kauli mbiu ya Siasa ni kilimo, mapinduzi ya kijani na sasa kilimo kwanza. Tulisonga mbele hatua/asilimia ngapi kwa kauli mbiu ya siasa ni kilimo? Je, mapinduzi ya kijani yamemsaidiaje mkulima wa Kitanzania na hasa mkulima mdogo anayetakiwa kuachana na kilimo cha mazoea na kulima kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Maafisa Ugani utendaji wao wa kazi upimwe kwa ushauri wanaoutoa kwa wakulima, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda alijionea mwenyewe alipotembelea Mkoa wa Dodoma jinsi baadhi ya Maafisa Ugani wasivyotekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutenga shilini bilioni 12.8 kuziwekesha Halmashauri za Wilaya kununua matrekta madogo ya mkono. Ukombozi wa mkulima mdogo ni *power tiller*, mkulima mdogo ana uwezo wa kukopa na kurejesha. Viongozi kuanzia ngazi ya kijiji kuwahamasisha wakulima kukopa *power tiller* ili kujikomboa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutumia nguvu kazi ya vijana kwa kuwashirikisha katika kuendeleza kilimo. Programu hii ikifanikiwa vijana wengi wataacha kukimbilia mijini kutafuta kazi kwani ajira zitakuwepo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zifanywe za kuhakikisha kuwa mazao yao yanapata soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania walio wengi hawana uwezo wa kujijengea miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji na ndiyo sababu kilimo cha umwagiliaji hakimnufaishi Mtanzania. Nashauri wawekezaji watafutwe kujenga miundombinu ya umwagiliaji na kisha kuwakodisha wakulima wadogo wadogo kama inavyofanyika kwa wakulima wa Mbarali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Dodoma wamekumbwa na baa la njaa kutokana na mvua kutonyesha kwa kiasi cha kuridhisha. Naomba Serikali kuwasaidia wananchi kwa kugawa chakula cha njaa kwa Wilaya zote za Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kusema naunga mkono hoja hii. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendeleza kilimo hapa nchini. Pamoja na pongezi hizi napenda kuwasilisha maombi ya watu wa Manyoni kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni kuboresha Skimu za Kilimo cha Umwagiliaji – Manyoni. Tunashukuru kwa hatua zilizomo katika bajeti ya Wizara yao ya kusaidia skimu hizi kwa pembejeo za ruzuku. Hata hivyo, wananchi wangependa skimu tano zilizopo Manyoni ziboreshwe kwa kujengwa mabwawa ili walime hata katika msimu wa kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunaomba skimu mpya ya Chitalala ambayo ilifanyiwa upembuzi mwaka 2008/2009 mwaka huu ianze kujengwa kwa kushikiriana na Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu upugufu wa chakula. Japokuwa katika Mkoa wa Singida na sehemu mbalimbali za Wilaya ya Manyoni kuna chakula cha kutosha lakini eneo la Bonde la Ufa hasa Tarafa ya Kintinku lipo tatizo kubwa sana la upungufu wa chakula. Hali ni mbaya! Hivyo Waziri aitazame vizuri tathmini ya chakula katika Wilaya ya Manyoni ili kubaini tatizo hili na Tarafa hiyo ya Kintinku iwemo katika maeneo yatakayoletewa chakula cha msaada mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, narudia kusema naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa hotuba nzuri. Imejibu maswali mengi kuhusu kilimo. Pongezi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mikakati ya Kilimo Kwanza, imbatane na uwekezaji, uvunaji, na utunzaji maji. Kwa hiyo tuwe na mikakati ya kila kijiji kuwa na mradi wa ujenzi wa mabwawa kama sehemu ya kuthibitisha umuhimu wa maji. Hatuwezi kufanikisha bila maji kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Njombe tunaomba tujengewe masoko ya mazao katika maeneo ya Kipulapula, Kata ya Taweta na Lungemba, Lupembe na Makambako penyewe. Tuko tayari kuchangia hiyo asilimia tano katika ujenzi. Makambako Mjini hatuna soko la mazao. Licha ya maneno ya siku nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lupembe inahitaji soko kwa sababu zao la mahindi halistawi huko. Ili kufanikisha ndoto zetu katika kilimo kwanza Serikali ichukue maeneo ya kilimo yaliyo wazi kwa nchi yote (katika kila Wilaya) ili watu wakitaka maeneo yaliyo wazi wayapate kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chakula (mazao) tutaje mazao yote na siyo mahindi tu. Pia mifugo itengewe maeneo badala ya kuendelea kupiga chenga.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri bajeti ya kilimo imeongezwa karibu mara mbili. Ni vizuri bajeti ya kilimo ikaendelea kuongezwa hadi kufikia asilimia kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapinduzi ya kilimo yanaenda sambamba na kukua kwa maendeleo ya viwanda lazima kuwe na *horizontal* na *vertical linkages*, hivi ndivyo *industrialization* ilivyofanikiwa katika nchi za Ulaya na kadhalika. Ikiwa tutasafirisha pamba nje na kuridhika na pia wakulima wakishalipwa fedha za kutosha watosheke hatuwezi kwenda mbali. Siku zote tutaagiza nguo kutoka nje, juisi, viatu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu *raw material* ibadilishwe kuwa *finished products*, lazima suala la kuongeza thamani – *add value* litiliwe mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya nafaka ni muhimu sana, lazima Serikali kuhakikisha mazao hayaendi nje. Nchi jirani hivi sasa inashusha shehena za chakula ili kuweka, kwa kuwa mwaka huu kuna ukame Tanzania iwe na chakula na hifadhi ya chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kwanza hakiwezi ku-*take off* bila ya kilimo cha kisasa. Lakini kilimo cha umwagiliaji, bila ya maji hakuna kilimo, kama ni kutegemea mvua hakuna uhakika wa kilimo, kwa hiyo suala la umwagiliaji lazima lipewe nafasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya kilimo ni budi itolewe bila ya urasimu. Ni vizuri mabenki yakaelezwa hivyo. Na kuwa na *window* kwa ajili ya mikopo ya kilimo ambayo itakuwa ya muda mrefu na yenye *invest* ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usindikaji mazao huu umekuwa wimbo wa muda mrefu sana. Tatizo ni nini? Unavyokwenda kwenye *shopping markets* unakuta *juices* kutoka nchi za nje. Sasa umefika wakati tufanye mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo muhimu kuwa kilimo cha matrekta kinatiliwa mkazo na kuwawezesha wakulima kununua matrektra madogo madogo. Hakuna mapinduzi ya kilimo kwa kutumia jembe la mkono. Hii itakuwa ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Ushirika ambavyo vingi vimekuwa na matatizo baada ya Serikali kuwalipia madeni na hivyo kutokuwa na madeni ni muhimu viimarishwe, kwa njia mbali mbali. Tujifunze historia ya ushirika jinsi ulivyofanya vizuri. *SACCOS* ziimarishwe na viongozi wapewe mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara lazima iwe na ushirikiano na Wizara ya Maji na *Vice President Office* upande wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, pesa za Serikali zinazopelekwa katika Halmashauri zinatumiwa vibaya sana kwa watendaji kulipana posho, viburudisho, chai na kadhalika hasa pesa za miradi ya *DADPS, ASDP, DASIP* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tumeamua kilimo kwanza, ni vema tukawa makini kufuatilia pesa zinazokwenda kwenye Halmashauri zetu ili kuhakikisha kuwa pesa hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tena ni vema malengo yenyewe yakawa ni kumsaidia mkulima na kukisaidia kilimo chenyewe na sio posho, viburudisho na kadhalika. Nyie mnasema kilimo kwanza lakini huku kwenye Halmashauri wanachekelea na sasa wanasema, Posho kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana mfuatilie pesa za miradi ya kilimo na umwagiliaji mlizopelH ili kujua *value for money*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Naibu Waziri, katibu mkuu na watendaji wote kwa maandalizi ya hotuba nzuri iliyosheheni mikakati mingi itakayowezesha dhana ya kilimo kwanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata maelezo au ushauri na kutoa mapendekezo kama ifuatavyo:-

Kwanza, mfumo wa Maji Chuo cha Kilimo/Utafiti Mlingano. Naipongeza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kusimamia utekelezaji wa mradi wa maji toka Pongwe kwenda Mlingano. Mabomba na tanki la maji Ngomeni ujenzi unaenda vizuri. Hata hivyo lipo tatizo la umeme eneo la mradi kuwezesha mtiririko wa maji kwenda vizuri hadi Mlingano. Tumeendelea kushauriana na *TANESCO* kutoa kipaumbele utekelezaji wa mradi wa umeme kwa mpango wa *MCC* kwa eneo la Ngomeni na Bagamoyo ili kupunguza gharama. Hata hivyo, utekelezaji unaweza kuchelewa na hivyo kuchelewesha ukamilishwaji wa mradi huu wa maji kufika Mlingano. Kwa msingi huu nashauri Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika iendeleze jitihada za kuwezesha kugharamia uwekaji wa umeme kutokana na makadirio ya *TANESCO*, ili mradi ukamilike.

Pili, ahadi za Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa ziara Mlingano 2008. Mheshimiwa Rais aliahidi kama ifuatavyo:-

(a) Hali ya watafiti (wafanyakazi). Mheshimiwa Rais aliagiza kwamba mfumo wa mishahara na upandishwaji vyeo watafiti wa Mlingano utazamwe upya na kufanyiwa marekebisho walingane na wataalam wengine nchini. Nafahamu mkakati uliandaliwa kuangalia hilo. Je, marekebisho yamefanyika

(b) Uchakavu wa matrekta. Mheshimiwa rais aliona umuhimu wa Chuo kupatiwa matrekta mapya badala ya kukarabati yaliyokuwepo yenye umri wa zaidi ya miaka 15.

Je, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imefanya jitihada gani kutekeleza pendekezo hilo la kukipatia chuo matrekta mapya?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kukarabati Chuo na Ofisi za Utafiti Mlingano na kuwapatia magari mawili katika bajeti hii 2009/2010.

Tatu, Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukuimarisha utafiti. Utafiti katika sekta ya kilimo ni muhimu na wa lazima. kwa kuwa agizo la Mheshimiwa Rais ni kutenga asilimia moja ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya utafiti na kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha Bungeni leo tarehe 21/7/2009 kwamba fedha zilizotengwa ni 0.4%. Je, Wizara ya Kilimo imepata kiasi gani kwa utafiti na fungu hilo limepitia wapi? Ni vizuri Wizara ikafuatilia kwa makini mgao halali wa fedha za utafiti kwa ajili ya sekta ya kilimo.

Nne, mbegu bora za mpunga na michungwa.

(a) Mbegu za Mpunga. Wilaya ya Muheza inatekeleza mradi mkubwa wa umwagiliaji wa Misozwe na miradi mingine ya Mashewa na Antakae, kwa zao la mpunga. Miradi hiyo itakuwa tayari ndani ya mwaka 2010/2011. Kwa kuwa Serikali imepanga kutoa ruzuku tani 2,102, Wizara ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kusaidia vikundi vya umwagiliaji katika miradi hiyo na kuwapatia wakulima hao mbegu bora za mpunga.

(b) Mbegu bora za Michungwa: Wilaya ya Muheza kwa sasa inaongoza hapa nchini kwa kilimo cha michungwa na kuuza katika masoko ya ndani na nje ya nchi hasa Kenya na Uganda. Zipo aina nyingi za machungwa yanayolimwa, zaidi ya aina nane. Hata hivyo, aina tatu zifuatazo ndio zinazoonekana bora kidogo. Aina hizo ni Nairobi, Washington na Valensia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingi kati ya aina za machungwa hayo hazina mvuto mkubwa sokoni kwa vile zina rangi ya kijani wakati chungwa likiwa limeiva badala ya rangi ya njano na pia kuwa na mbegu nyingi na maji kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha kilimo cha michungwa kwa masoko ya nje na kwa viwanda vya usindikaji mbegu bora ni muhimu sana. Miaka ya 60 zilikuwepo mbegu za machungwa yaliyokuwa na rangi ya njano na yasiyokuwa na mbegu katika maeneo ya Kata ya Songa na eneo la Shamba la Muheza *Estate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika isaidiane na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuendeza utafiti wa aina bora ya mbegu za machungwa kuzizalisha kwa wingi na kuhamasisha wakulima wa Wilaya ya Muheza na Wilaya nyingine kuzipanda na kuziendeleza. Wataalam waanzilishi wa aina ya mbegu za michungwa isiyokuwa na mbegu bado wapo na Wizara ya Kilimo inawafahamu. Wanaweza kusaidia sana katika mpango wa utafiti na kufuatilia maeneo ya awali yaliyokuwa na mbegu bora. Itakuwa vema pia kuangalia na kutafiti mbegu bora ya michungwa zinazozalishwa katika nchi kama Afrika Kusini, na Israel.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU**, Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti hii muhimu ya Wizara hii ambayo wakulima wanaitegemea sana. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wake wote wa Wizara hii kwa kuandaa bajeti hii na leo imeweza kuwasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania zaidi ya asilimia themanini ni wakulima ambao kwa, muda mrefu wamekuwa wakifanya kazi yao hiyo ya kilimo katika mazingira magumu sana na kufanya maisha yao kuendelea kuwa magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa Tanzania ni maskini kwa sababu mazao yao wanayojitahidi kulima yanakosa masoko na kujikuta wanauza mazao yao kwa bei ndogo sana pamoja na nguvu nyingi wanazotumia kulima kwa jembe la mkono, umefika wakati sasa wa kuwasaidia wakulima wetu kwa dhati kama kweli tunataka kuleta mabadiliko ya kweli katika kilimo ili dhana ya kilimo kwanza ya itimie kwa kufanya hayo yafuatayo:-

- (1) Kupata pembejeo za kilimo kwa wakati.
- (2) Wapattiwe masoko ya mazao yao wanapovuna mazao yao tusiwaachie hao walanguzi kupunja wakulima wetu.
- (3) Tuwe na Maofisa Ugani wa kutosha na wawe na nyenzo zitakazoweza kuwafikisha kwa wakulima kuwapa elimu, waache kukaa maofisini.
- (4) Tuachane na jembe la mkono, wakulima wawezeshwe kutumia matrekta. Hayo yakifanyika naamini umaskini utapungua katika njia yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa kamati ya Laac na Kamati yetu tunakagua miradi inayopelekwa katika halmashauri zetu ila jambo linalonisikitisha ni fedha zinazopelekwa kwenye miradi ya kilimo (*DADPs, DASIP, ASDP*) fedha hizo hazitumiki vizuri na hazitaleta mabadiliko ambayo tunayotegemea kama utaratibu ndiyo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa hizo zinaishia kwenye semina, posho, chai na kadhalika, ukiangalia pesa inayokwenda hasa kwenye kilimo ni ndogo sana na ukiuliza wanadai ni maelekezo toka Wizarani. Sasa tunamwomba Waziri atueleza taratibu za matumizi ya fedha hizo, vinginevyo tutaendelea kunufaisha watu wachache ambao si walengwa na wakulima wetu wakaendelea kufanya kazi yao ya kilimo bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo nategemea kupata majibu hasa kwenye pesa hizo za miradi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii, kilimo kwanza kitawezekana, kama wakulima watawezesha kwa kupata mikopo ili wawe wakulima wa kisasa waachane na kilimo cha kizamani.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Kilimo ni wachache sana wakulima wanahitaji mafunzo kwa ajili ya kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanahitaji mkopo kwa ajili ya kilimo pamoja na pembejeo na zana za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwezesha Halmashauri za Wilaya kutoa utaalum na mafunzo ya kilimo cha kibiashara kwa wanawake na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya usindikaji mbogamboga na matunda, masoko hakuna, wajasiriamali wanapata masoko mahali popote, sasa tunaomba Serikali itafute masoko ili wajasiriamali wapate faida na kilimo chao.

**MHE. MARGARET S. SITTA,** Mheshimiwa Naibu Spika, hongera kwa mpango mzuri ambao naamini utafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mbolea ziwahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakulima wasaidiwe masoko ya mazao yao.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napongeza kazi nzuri ya Wizara pamoja na hotuba murua. Ni bajeti nzuri kasoro kiwango cha fedha hakilingani na majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mwaka jana kule Morogoro nilikuwa *Septical* sana juu ya utaratibu wa ruzuku ya mbolea. Na kweli matatizo kadhaa yalijitokeza lakini nafurahi kuwa kwa kiwango yalikabiliwa. Kilichobaki ni kufanya valuation kwa lengo la kuweka utaratibu mzuri zaidi. Ningeshauri zaidi kwamba Wabunge na Halmashauri tuhusiswe zaidi, hasa kwa vile hotuba inapanua wigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, papo hapo, mbolea ya Minjingu ni mpya na inahitaji elimu hasa aina ya udongo unaokubali mbolea hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nilichangia bajeti ya Waziri Mkuu nilisema idadi ya matrekta ni vitrekta (*power tillers*) ni ndogo mno kulinganisha na changamoto ya kilimo kwanza. Nilishauri ikibidi tutumie Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *as short term investment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe, nashauri mnetumia *Investment Centre* kutuletea viwanda vya zana za kilimo na spea zake, hata kama ni kuunganisha tu kama *TAWICO* ya zamani.



Mheshimiwa Naibu Spika, nne, pamoja na kifungu kilichotangulia nashauri Wizara iweke mkazo katika viwanda vidogo vidogo vya mazao (*Agro-based industries*). Mpango aina hiyo utapanua soko na hatimaye kuongeza kilimo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kwa sababu ya historia mbaya ya ushirika huko nyuma, si rahisi kuhamasisha Vyama/SACCOS. Nashauri Wizara ijipange upya kufanya mabadiliko mapya ili kuvutia wakulima na kuvunja *projedices* zilizojengeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, naunga mkono hoja hii.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu na Waziri wetu wa Kilimo, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, endelezeni jitihada za kuhimiza mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea ya ruzuku, naipongeza sana Serikali kwa ongezeko la wigo wa watu watakaopata mbolea hii. Nchi yetu ina idadi ya watu milioni 34 na karibu asilimia themanini ni wakulima wadogo, hivyo wigo wa watu milioni moja na nusu ni kundi dogo sana kuleta mabadiliko ya dhati, nchi ya Malawi yenye idadi ndogo sana ya watu takribani milioni 11, uwezo wao mpaka sasa ni kwa watu milioni moja na laki mbili. Tusiridhike na wigo huo, tuendeleo kuongeza wigo ili tuwe na uwezo wa kuzalisha chakula kingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni bei ya mbolea, tupunguze bei kwa wakulima wetu ili kila mkulima mdogo awe na uwezo wa kumudu bei hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha pamba, Mbeya. Nilijenga hoja mwaka 2004 juu ya kuzuia kilimo cha pamba Mbeya, kwa maelezo ya kuwepo kwa *red boll worm* (funza mwekundu) naomba maelezo kwa nini mpaka sasa sijapata majibu ya utafiti huo. Viwanda vingi vya Mbeya vimekufa kwa sababu ya kukosa malighafi ya pamba na mbegu za pamba. Kuna kigugumizi gani katika kutoa majibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Utafiti Uyole/Chuo cha Kilimo. Nazipongeza taasisi hizi mbili, zimekuwa mkombozi kwa wakulima wa Mbeya, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti ya utafiti ili wananchi wanufaike na matokeo ya utafiti huo. Napenda pia nikumbushie ahadi ya Waziri Mkuu alipotembelea taasisi hizo kwa pamoja, aliahidi trekta na kuboresha barabara ya kutoka Uyole Kati kupitia Chuoni mpaka daraja la reli, pia kutoka Chuoni mpaka barabara kuu karibu na Mwaji *Group*, naomba ufuatiliaji wa ahadi hizo kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupatiwa mbolea ya ruzuku ushirika wa Umwagiliaji Uyole. Tulipongeza mimi na Mheshimiwa Waziri aliniahidi kuwa wananchi wa bonde la Uyole, wenye Ushirika wa Umwagiliaji, watapatiwa mbolea ya ruzuku kwa wanachama wao hasa baada ya kuona juhudi kubwa waliyonayo wana ushirika hawa. Tayari wana ushirika wanaleta barua rasmi ya maombi yao. Naomba jambo hili lizingatiwe, ili kuwapa moyo wa kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, trekta ndogo (*power tillers*). Nashauri Serikali iagize matrekta haya moja kwa moja toka Uchina gharama yake ni Tshs, million moja tu *CFU*, Dar es Salaam, lakini, ukiagiza kama una-*assembled parts* bei inapungua mpaka shilingi laki 800 *CFU* – Dar es Salaam. Hali hii ingetusaidia sana kukopi teknolojia hiyo na kuiboresha zaidi. Katika mapinduzi ya kilimo ni vema tukachukua hatua za kimapinduzi kweli kweli, nashauri kiwanda cha ZZK Mbeya, kitumike kama eneo la kuunganishia matrekta madogo – *power tillers*. Naomba tuthubutu katika hili. Serikali ichukue hatua katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na bajeti kutoashiria kilimo kwanza, wala kutofikisha kiwango cha asilimia kumi za bajeti kama makubaliano ya nchi za *SADC* yalivyo. Naridhika na *thrust* ya viongozi wa Kitaifa, Waziri, Naibu Waziri na wataalam, kwamba dhamira yao inatosha kuashiria kilimo kwanza, tuwape ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa mara ya pili.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Matrekta madogo. Nianze kwa kutoa shukrani kwa Serikalii kwa kutoa matrekta 30 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara. Natumaini hizi trekta zitatumika kuboresha kilimo katika Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo na biashara, zamani Ngara ilikuwa maarufu kwa zao la Kahawa. Kwa sasa hivi Ngara inazalisha kahawa kidogo sana. Sababu ni kwamba kilimo cha kahawa kimedorora hakuna utaratibu wa kueleweka ambao ungeliwawezesha wakulima wafaidike na kilimo cha kahawa. Naomba Serikalii iweke utaratibu wa kupatikana kwa miche ya kahawa ili wale waliopenda kulima kahawa waweze kupanda miche na wavune kahawa nzuri na ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia matatizo ya kuuza mazao. Wapo wakulima ambao wana zao la mihogo lakini ikija wakati wa kuuza inakuwa kuna kudhibiti mpakani hasa mpaka wa Kabanga Border. Wananchi wanaomba hicho kizuizi kiondolewe ili mazao hasa yale yanayoweza kuharibika basi yaweze kupelekwa Burundi ili waweze kupata pesa kutokana na mazao yao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maafisa Ugani, kuna upungufu mkubwa katika Halmashauri ya Ngara. Hawa wale waliopata uwezo wao ni mdogo sana. Tunaomba wapewe mafunzo ya kilimo cha kisasa ili waweze kuwasaidia wananchi. Vile vile wananchi wanaomba maafisa ugani wapewe vitendea kazi hasa pikipiki ili waweze kusimamia kilimo kwa uadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ASDP*, huu mradi wa kuboresha kilimo katika Wilaya ya Ngara haujafanikiwa sana. Sababu ni kwamba inachukua muda mrefu sana kufanya

tathmini ya mradi wenyewe. Inachukua karibu miaka miwili kuomba pesa za mradi mpaka kuzipata. Tatizo ni kwamba wakuu wa idara inaonekana wana uwezo mdogo wa kuchanganua miradi.

Tunaomba maafisa wenye uwezo mkubwa ili wananchi wa Ngara waweze kufaidika na mradi huu wa *ASDP*.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote katika Wizara hii kwa kazi nzuri zinazoendelea kufanyika katika Wizara hii. Aidha, napenda kutumia fursa hii kwa hotuba ya bajeti ya mwaka 2009/10 waliyoiwasilisha Bungeni asubuhi hii. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Naipongeza sana Serikali kuwakumbusha wananchi na wakulima kuwa serikali yao inawakumbuka na inatambua umuhimu/mchango wa kilimo kwa ustawi na maendeleo ya taifa hili. Juhudi mbalimbali za viongizi wa kitaifa (Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, katika vikao, mikutano na mazingira mbalimbali kuhusu kilimo ni ishara tosha kuwa wanatambua umuhimu na uzito wa utashi wa kisiasa katika mapinduzi ya kijani. Kauli mbiu – ““Kilimo Kwanza”” ni ishara nyingine pia.

Hata hivyo ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri atumie muda kidogo kuonesha tofauti ya umakini (Seriousness) kwa kauli mbiu za nyuma kama kilimo cha kufa na kupona, kilimo ni uti wa mgongo n.k. Vilivyo vilivyotanguliwa na mikutano mikubwa, kauli za viongozi na matumizi makubwa ya fedha kama inavyoonekana hii, kauli mbiu ambazo hazikutufikisha mahali popote katika kilimo. Ni vema Mheshimiwa akatueleza kauli mbiu za nyuma zilipungukiwa na yapi hata vikaishia ukutani kama mbizo za...ni vema wananchi wakaelezwa na kuelewa udhaifu wa mipango na taratibu za nyuma ili makosa yasije yakarudiwa katika kauli mbiu hiyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri aelewe kuwa anawaeleza wananchi wengi waliozoea kulima na kula mwaka, wakapata wanatumia mpaka kiishe. Ni wananchi wenye malengo kupata chakula cha kutosha kutumika kuvuna hadi mavuno mengine, na ikitoa bahati ya zaida ni ya kuuza siyo ya kuhifadhi. Anawaeleza wananchi wengi wanaojua kuwa mvua zikianza kunyesha mtu anatakiwa kuanza kulima, kulima vyovyote ili mradi alime tu hadi pale mvua zitakapokatika na kwao hayo ndiyo maisha – akipata – chakula kheri asipopata heri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anaongea na watu ambao kwanza hawajui kama lipo tatizo na kilimo chao na maelengo ya kilimo chao.

Wakati Mheshimiwa Waziri anafikiri kuwa wanajua kuwa kuna tatizo wakati wenyewe hawajui Mheshimiwa Waziri anataka kusaidia watu waondokanae na tatizo ambalo wenyewe hawajua kama ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri asaidie kutufahamisha kama utashi huu wa kisiasa uliopelekea kauli mbiu hii unaeleweka kwa wananchi.

Jambo la msingi hapa ni kujua je Malengo ya wananchi, wakulima kwa kilimo chao yako sahihi? Je nini malengo ya Serikali na viongozi wake kwa kilimo cha wananchi wake.

Je, pengo lililopo kati ya malengo ya vikundi hivi viwili unamvuto kiasi gani kushawishi wananchi kuliziba? Maswali haya ni muhimu kwa kuwa bila wananchi wakulima kuwa na malengo ya juu kuliko waliyoyazoea – kauli mbiu hii haitakuwa na msaada.

Ni vema wananchi wakafundishwa mambo yaliyopungua katika yale wanayoyafahamu. Ni muhimu wakawa wazi na tunakotamkiwa kufika na jinsi ya kufika huko.

Ni vema tukajiuliza *ASDP* ni matunda ya nani, je wakulima 80% ya watanzania wamechangia kwa kiwango gani kwa dhati katika mpango huu. Je *ASDP* ni matokeo ya watu fulani kuwa hurumia wakulima au je, *ASDP* au ni matunda ya madai ya wakulima? Maswali haya ni rahisi kuyajibu, kwa haraka sana mtu anatakiwa kuiangalia bajeti ya mpango wenyewe, katika wale asilimia 80, ni wangapi wanafikiwa moja kwa moja na hiyo bajeti au ni asilimia ngapi kati ya hao wanaomaliza mwaka mzima bila kunufaika hata kidogo na bajeti hiyo, hivyo mwaka mzima unapata bila kutatua hata tatizo moja la sehemu kubwa ya bajeti hiyo.

Kwa mfano, tuna ruzuku mbalimbali ni asilimia ngapi ya wakulima wanaonufaika na ruzuku hiyo? Tukiwa makini na takwimu kama hizo tutaweka mantiki katika kauli mbiu yetu na kuifanya itekelezeke kwa vitendo na kuchangiwa na wengi katika ufikiaji malengo yaliyofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo kipi Kwanza? Katika kauli mbiu ya “Kilimo Kwanza” tumekuwa wazi kwa mapana mno

- a) Kilimo cha kutegemea mvua?
- b) Kilimo cha Umwagiliaji?
- c) Kilimo cha wakulima wakubwa? au
- d) Kilimo cha wakulima wadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri awe wazi ni kilimo kipi tunachokijenga?

Kwa kuona kwangu bajeti iliyotolewa ni ndogo sana japo yaonekana kwa macho na kwa kulinganisha na bajeti za Wizara zingine kuwa kubwa kwa kilimo bila kujiwekea

mipaka kwa makusudi ni ndogo sana. Ni vema tukawa wazi ni maeneo yapi tunalenga kujikita. Bila kufanya hivyo fedha hii tutaisambaza mwisho wa mwaka tushindwe kutoa taarifa ya kuungana na fedha hiyo. Siyo vema tukagusa kidogo kidogo kila sehemu kwa nia ya kupaendeleza mwisho wa mwaka kisione kane kilichofanyika!

Kwa mawazo yangu, ili mradi wananchi wetu ni wakulima wagogo wadogo, nguvu kubwa tungezielekeza kwao.

- a) Kuwasaidia wakaachana na jembe la mikono;
- b) Kuwasaidia wakatambua umuhimu wa kutumia bila kusukumwa mbolea za samadi na mboji;
- c) Kuwasaidia kutambua umuhimu wa kupanga mbegu kwa mstari na kuacha umbali unaotakiwa; na
- d) Kuwasaidia kufanya hayo ya juu kwa kuwa karibu na Maafisa Ugani kila mara wanapowahitaji.

Kwa kuwa nchi yetu ni kubwa na wakulima hawa wanapambana na matatizo yaliyomo katika mazingira ili mradi lengo letu ni wakulima wadogo basi lengo letu lisibadilike tuendeleze kuwa nalo, wakulima wakubwa waachwe wajitegemee. Kwa muda na kila wakulima katika kikundi fulani wakijitokeza wanasaidiwa kuingia kwenye kikundi cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zana za Kilimo. Naipongeza sana Serikali katika eneo hili. Ninachoomba ni Serikali kuongeza kasi ya kusambaza elimu ya zana hizi na ya zana hizi kwa ardhi kama zipo ni vema vikatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado ninazidi kusisitiza kuwa ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Waziri hii kwa kazi nzuri zinazoendelea kutendeka chini ya Wizara hii pamoja na hotuba nzuri ya bajeti 2009/10 ya Wizara hii. Aidha, nasema kuwa naunga mkono hoja. Naomba niendeleze mchango wangu katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo. Kwa mwaka ni kiasi gani kilitengwa kwa pembejeo na zana za kilimo zilizopekwa katika mikoa iliyopelekwa pembejeo na zana hizo. Ni katika uwiano upi wakulima na wakala, ukurasa wa 28 wa kitabu cha bajeti inaonesha kuwa ni wakulima 737,000 tu ndiyo walionufaika waliokuwa wakihudumiwa na mawakala 1684 ikionesha kila wakala alikuwa akihudumia wastani wa wakulima 438. Je, kiasi hicho nacho kilikuwa katika uwiano huo? Je, kiasi hicho cha fedha ilikuwa ni asilimia ngapi ya bajeti yote na wakulima walionufaika ni asilimia ngapi ya wakulima nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri ni vigezo vipi vinavyotumika kwa Mkoa kustahili kupata ruzuku hiyo. Hivyo ndivyo vigezo vinavyoiondoa mikoa ya Shinyanga na Mwanza katika stahili hiyo? Naomba maelezo.

Binafsi nilifikiri kiwango cha ruzuku ya pembejeo ingewekwa ili kila Mkoa uweze kupata elimu ya matumizi ya pembejeo husika, yapo maeneo katika Mkoa yanayohitaji matumizi ya mbolea hivyo yanastahili ruzuku ya pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu bora, hapa ningependa kujielekeza katika Wilaya yangu ya Kwimba. Mbegu za dengue ni zao la pili la biashara katika maeneo mengi ya Kwimba. Kwa kipindi cha miaka kadhaa sasa zao hili limekuwa likishambuliwa na aina fulani ya vikungu (*fungus*) inayosababisha mimea isinyae au idumae na kuathiri sana mazao. Hii ni mara yangu ya pili kuulizia maradhi haya ya dengue. Wizara ilishanipatia jibu kuhusu kisababisho cha ugonjwa. Ukiriguru wanalifahamu tatizo hili, leo nauliza je, ugonjwa huu wa dengue hauna dawa kama ukimwi? Kama dawa ipo mbona Serikali iko kimya? Nauliza dawa ipo au hakuna dawa? Je, kwa kubadilisha mbegu ugonjwa huu unaweza kukwepwa? Naomba majibu. Wananchi wajue ili waendeleo kulima dengue au wasiendeleo kupoteza nguvu, muda na fedha. Kwa nini Zao la dengue halikutajwa kabisa katika Kitabu kizima, halijatambuliwa na Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu ucheleweshwaji wa kuletewa mbegu bora. Ni mara nyingi sana mbegu bora za mazao mengi huchelewa sana kufikishwa Kwimba ikiwa ni pamoja na za watu binafsi. Ombi langu kwa wakulima wa Wilayani Kwimba mbegu bora za mazao mbalimbali ziwe zinaletwa mapema. Kuletwa kwa kuchelewa sana kunasababisha gharama isiyokuwa ya manufaa kwa wakulima na uharibifu wa mbegu bora bila sababu hasa kwa kuzingatia ukweli kuwa mbegu huzalishwa kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu skimu ya umwagiliaji nifahamavyo kusudi kubwa la skimu hizi ni kuwa wakulima wasiathirike kwa mazao yao kukosa maji. Skimu hizi zinazojengwa kwa fedha nyingi zinaposhindwa kuwatofautisha wakulima nje na ndani ya eneo la skimu inasikitisha. Hii inatokea kama skimu hizi zina kuwa na manufaa tu wakati wa mvua, mvua zikikatika kwa wiki mbili, tatu mashamba yanakauka, katika Jimbo langu nina mifano miwili, skimu ya Luhala na skimu ya Mahiga. Skimu zote hizi zimekuwa na manufaa kwa wakulima kipindi tu cha masika. Mara nyingi na leo naomba tena skimu hizi zijengewe mabwawa makubwa yanayoweza kuhifadhi maji kwa muda mrefu kwa ajili ya matumizi ya umwagiliaji na kunywa binadamu na wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya utafiti ni muhimu sana kwa maendeleo yoyote, kazi za vitafiti hazitakiwi kufanywa kwa kubahatisha. Kuzitaka Halmashauri zichangie katika shughuli za utafiti wowote ni kuziweka hatarini. Hii ni kutokana na ukweli kuwa:-

- Halmashauri za wilaya nyingi ni tegemezi kwa sehemu kubwa.

- Mapato yao ni duni na ni ya kubangaiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri fedha kwa ajili ya utafiti itolewe yote na Serikali kuu. Si vema vyanzo vya shughuli hizo zikatoka sehemu nyingi kwa kuwa makusanyo yake yatasumbua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa hekima yake iliyotumia ya kuangalia njia mbalimbali za kunusuru zao la pamba kwa kuchukua hatua muhimu zifuatazo:

- i) Kuwafidia na kuwadhamini wanunuzi walionunua zao hili msimu uliopita na kupata hasara kutokana na msukumo wa fedha duniani licha ya madeni waliyokuwa nayo katika Mabenki. Hii imewapa moyo wanunuzi hao wa kuweza kununua pamba toka kwa wakulima katika msimu huu.
- ii) Kuwaongeza bei wakulima iliyokuwa chini sana, hii itawatia moyo waweze kulima tena zao hili mwakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE BENT KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kahawa yetu ni nzuri inahitajika lazima tuipangie bei elekezi bila kuachia Vyama vya Ushirika peke yake. *TCB* kwa kushirikiana na Wizara wahakikishe kuwa kahawa ya Tanzania inakuwa na *Brand New* ya Kilimanjaro. Tuwe na *copyright* ya jina hilo Kilimanjaro *coffee*. Jina hili linatumika kwa manufaa ya watu wa nje ambao hawalimi kahawa hiyo. E thiopia wamefanya hivyo, nangojea jibu la Wizara ikiwa ni pamoja na mbegu zote zilizogunduliwa hapa nchini ikiwa ni pamoja na miche bora ya Kahawa tuwe na *copyright*.

Pia mazao yetu kama mchele wa Kyela, Mchele wa Magugu yalindwe na tuwe pia na *copyright* ama hati miliki.

**MHE. DR. GETRUDE MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza ni mpango ambao utafanikiwa tu kama maafisa kilimo nao watakuwa *serious* na kama watakuwa na upeo na wabunifu. Njaa iliyoko Ukerewe imetupa fundisho kwamba Wizarani na taasisi zinazopaswa kuona *early warning signs*, magonjwa ya mihogo yalivyoathiri muhogo ambao ni zao kuu la chakula wilayani lingeweza kupata *quick response* ya kutoa mbegu mbadala. Kupata mbegu za mtama ambayo tulifikiria itasaidia ilichukua muda mrefu na urasimu wa kuudhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chakula cha njaa ni kidogo na kinasababisha kero katika ugawaji

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu ni kwamba, mbegu za mazao mbadala yatufikie mapema kabla ya Mwezi Octoba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iangalie watumishi wasio na uwezo kasi ya mapinduzi ya kilimo.

Mwl J.K. Nyerere aliwahi kusema: “Hata Maafisa Kilimo wote wasipokuwepo pengo lao litaonekana”, sasa ni wakati wa kubadili hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu za mtama ziwe ni zile ambazo hazishambuliwi na ndege kama vile mtama mwekundu mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Ukerewe kuna njaa na hili lishughulikiwe haraka.

**MHE. DKT. FESTUS LIMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote Wizarani, taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara kwa hotuba nzuri sana, iliyopangiliwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana na kuishukuru pia Serikali kwa kusikia kilio cha wadau wa sekta ndogo ya pamba na kukubali ushauri uliotolewa wa kufidia hasara ya wafanyabiashara wa pamba kutokana ma mtikisiko wa uchumi wa dunia. Pamoja na fidia hii, Serikali imemwongezea pia mkulima Sh. 80 kwa kilo na hivyo kuipandisha bei ya mkulima kutoka Sh. 360 hadi Sh. 440/= kwa kilo. Hatua hii ni ya kupongezwa sana na wananchi wamefurahishwa sana na hatua hii. Wakulima wamehamasika sana na wametiwa moyo wa kuendelea kulima tena pamba msimu ujao. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wako wote kwa kumshauri Mheshimiwa Rais vizuri na kwa ufasaha hadi akaridhia juu ya hatua hii ya kimapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimu wa Pamba umeanza tarehe 22 Julai, 2009 hadi leo hii ni wafanyabiashara wachache sana wenye pesa wameshaanza kununua pamba. Nafikiri si zaidi ya Makampuni manne tu yameanza kununua pamba. *CRDB* bado hawajatoa pesa. Kwa nini wanachelewa kutoa fedha? Hali hii inasaidia kuleta ushindani usiokuwa na uwiano, wenye pesa wanahunua sana hivi sasa na kwa bei ya chini 360/= Tatizo litakalotokea mara tu *CRDB* watakapotoa fedha ni kwamba:-

- (a) Ushindani utakuwa mkubwa maana kila mnunuzi atataka anunue kiasi kikubwa cha pamba mara moja.
- (b) Bei ya pamba itapanda ghafla (pengine inaweza kupanda ghafla hadi 550/= kwa kilo). Wakulima waliouza kwa 440/= kwa kilo hawatakuwa wametendewa haki na soko. Naomba Serikali iwashinikize *CRDB* wawahi kutoa:-
  - (i) fidia kwa kampuni zilizopata hasara; na
  - (ii) mikopo kwa kampuni husika.



Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina mpango gani mahsusi kuhusiana na wanafunzi waliosomeshwa kupitia programu maalum kwenye chuo cha Ukiriguru na vingine, waliomaliza *Form Six*? Wanafunzi hawa wamemaliza chuo na walitarajiwa au waliahidiwa kwenda kufanya kazi au kuajiriwa moja kwa moja. Wanafunzi hawa wako *frustrated* na hawajui kinachoendelea. Wizara au Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Serikali kuondoa kodi ya asilimia kumi kwa mafuta ghafi ya kula yanayoingizwa nchini toka nje ya nchi, ni dhahiri bei ya mazao ya mbegu za mafuta itashuka (ikiwemo bei ya pamba). Hatua ya kuondoa kodi hii ni kuwakatisha tamaa wakulima wa alizeti na ufuta. Nashauri Serikali ilione hili na ichukue hatua mapema ili uzalishaji wa mazao haya usishuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana Serikali kwa hatua inazochukua kuimarisha ushirika nchini. Imechukua madeni na hivi sasa Chama cha Ushirika cha NYANZA kimepata mkopo *CRDB* ni hivi sasa kinanunua pamba. Nashauri jitihada hizi ziendelezwe. Ushirika (*NYANZA/SHIRECU etc*) usimamiwe vizuri hasa kipindi hiki wanapopewa fedha nyingi kununulia mazao kuepuka ufujaji wa fedha hizi za mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa chakula, Jimbo la Magu ni mojawapo wa maeneo nchini ambayo yamepata upungufu wa chakula. Kata zifuatazo naomba zifikiwe kupatiwa chakula cha msaada; Kata za Kisesa, Lutale, Bajeshi, Kongolo, Nyanguge, Kitongosima, Kahangara, Nyigogo, Mwamabanza na Sukuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Tarafa moja tu ya Ndagalu ndiyo ilipata chakula cha kutosha. Tarafa zingine za Itumbuli, Kahangara na Sanjo zote zina upungufu mkubwa wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha biashara, Wizara ifanye sensa ya wataalam wa Kilimo na ufugaji nchi nzima ili kujua nani yuko wapi na anafanya nini. Lengo la sensa hii ni kuwabaini na kujua wanafanya nini ili Wizara ione itawawezeshaje na kuwahamasisha ili waweze kuanzisha kilimo kikuu cha kibiashara. Wafanywe watumie taaluma zao kwa maendeleo ya nchi. *Hypothesis* yangu ni kwamba wataalam wengi sana wa kilimo wamekata tamaa; wanaonekana kuwa *neglected* na wanafanya kazi zingine ambazo hazihusiani na taaluma yao. Pengine wanahitaji tu *enterprenership exposure*, wakishapewa ardhi na mtaji ili watumie fursa zinazotolewa na soko. Nashauri hii ianze kama *pilot project*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kila la kheri na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na kuweza kufika hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti yao hapa bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kauli mbiu ya sasa ni Kilimo Kwanza. Je, Serikali imejiandaa vipi ili kauli mbiu hii iweze kuleta mabadiliko katika kilimo tofauti na kauli mbiu zilizopita kama vile kilimo uti wa mgongo, kilimo cha kufa na kupona na kadhalika, ni mabadiliko gani yanayotarajiwa katika Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuhakikishe kwamba kilimo chetu kinatosheleza kwa chakula pamoja na kupata ziada tuweze kuuza nje ya nchi na hivyo kukuza uchumi na kupata maendeleo. Serikali inapaswa kuwa makini katika kuhakikisha lengo hilo linafikiwa vinginevyo tutaendelea kukabiliwa na njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna mazao mbalimbali hasa ya matunda ambayo huozea shambani au majumbani kwa wakulima, Serikali inapaswa kutilia mkazo suala zima la ujenzi na uimarishaji wa viwanda vya kusindika matunda na mbogamboga ili kuwakomboa wakulima ambao wanapata hasara kila msimu kutokana na kuharibikiwa na mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji ndio mkombozi halisi wa mkulima wa Tanzania pamoja na Tanzania kwa ujumla hasa ikizingatiwa kwamba nchi yetu ina miti mingi isiyokauka kwa mwaka mzima, ina maziwa makubwa pamoja na vyanzo mbalimbali vya uhakika. Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kwamba inavitumia vyanzo mbalimbali vya maji katika kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati gani wa uhakika utakaowezesha kupatikana kwa wagani wa kutosha wenye sifa (*diploma*) watakaonea nchi nzima katika maeneo ya kilimo hasa ikizingatiwa maslahi bora kama motisha ya kuwafanya waende katika sehemu watakazopangiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mbolea ni pembejeo muhimu ili kuongeza uzalishaji. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vya mbolea katika maeneo mbalimbali hapa nchini ili mbolea iweze kupatikana kwa wakati na kwa bei nafuu badala ya kutegemea mbolea kutoka nje ambayo inakuwa ghali na inachelewa kuwafikia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana ndio nguvu kazi kubwa ya Taifa na kwa kuwa kauli mbiu ya sasa ni Kilimo Kwanza. Je, Serikali ina mpango gani au mikakati gani ya kuwawezesha vijana kushiriki katika shughuli za kilimo huko vijijini badala ya kuwaacha vijana wakimbilie mijini kwenda kutafuta ajira ambazo hazina uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo cha kutegemea jembe la mkono hakiwezi kukaa na kuleta maendeleo hivyo ni lazima matrekta ya kutosha yapatikane ndiyo kilimo kitaweza kukua na kuwa endelevu.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza ni jambo jema sana kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, mafanikio yake yatahitaji sana utashi wa kisiasa. Hofu yangu ni kwamba, isiwe ni mwendelezo wa kauli mbiu ambazo tumekuwa tukisikia tangu uhuru katika nchi hii na hakuna mabadiliko ya msingi katika Kilimo, lakini badala ya kukata tamaa tuanze tunaweza kufanikiwa kama tuna utashi wa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kidogo juu ya tumbaku. Lengo la nchi ilikuwa kilo milioni moja ifikapo 2010 kama alivyoagiza Waziri Mkuu aliyetangulia. Ukiangalia ukurasa wa 41 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kiasi kilichoongezeka ni kama kilo 3345 mpaka kilo 55357 hadi 58702 ni pamoja na kupanua maeneo ya uzalishaji, hivi tutaendelea hadi lini kupanua maeneo badala ya kuongeza uzalishaji kutoka katika eneo dogo, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufikia malengo na kuongeza uzalishaji ni lazima tufahamu matatizo ya msingi katika zao la tumbaku, ni pamoja na gharama kama tunaweza kupunguza, kusimamia zao lenyewe, hatuwezi kuwasaidia wakulima wetu kwa kuachia makampuni pekee na mashamba darasa ambayo hakuna mabadiliko makubwa na lazima kuongeza wataalam wa zao la tumbaku na kuimarisha Chuo cha Tumbi. Aidha, matokeo ya tafiti ya zao hili zifikiwe kwa wakulima wetu badala ya kuishia katika makabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni ya tumbaku ni tatizo lingine, tulianza vizuri kwa kuruhusu biashara ya ushindani, nataka kufahamu kwa nini makampuni haya ambayo yamesajiliwa nchini huruhusiwa kuanzisha *aliance* yao na kujisajili kama *ATTT* na sasa hakuna ushindani katika zao la tumbaku, lakini msimu uliopita Chunya ilipata kampuni nyingine na imetoa changamoto hata bei inaweza kuongezeka na kufikia dola mbili kwa kilo. Naipongeza sana. Sasa nataka maelezo katika mambo yafuatayo:-

Moja, je, Serikali sasa ipo tayari kufuta usajili wa *ATTT* na kubakia na makampuni yenye ushindani?

Pili, ni kwa nini na sababu gani kampuni ambayo ilinunua tumbaku msimu uliopita Chunya hairuhusiwi kununua tumbaku Mpanda, nani amekwamisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufafanuzi wa mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nilipenda kufahamu kwa nini mbolea ya *earthfood* imeshindwa kufikishwa sokoni, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Taifa liweze kujitosheleza kwa chakula ni pamoja na kuongeza nguvu katika kilimo cha umwagiliaji na kama tukiwa na mipango

madhubuti na ya kutekelezeka mabonde ya Wilaya ya Mpanda, Kigoma, Kagera, Kilombero na Rufiji tungeweza kutengeneza miundombinu imara, tungeongeza sana uzalishaji wa chakula kwa kuwatumia hawa wakulima wetu wadogo wadogo, ambao wakati fulani waliweza kutosheleza Taifa chakula na kuwa na ziada bila ya kutegemea hao wakulima wakubwa ambao tunadhani ndio ufumbuzi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuisihi Wizara hii wasiwadharau wakulima wadogo wadogo na itazame wapi tumekosea. Waliweza kulisha Taifa na wanaweza bila wakulima wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile mifugo hususan ng'ombe imesambazwa karibu nchi nzima pamoja na maeneo ambayo kwa kawaida si ya wafugaji, mpango wa usimamizi (*Management plans*) kwa matumizi ya ardhi ya kilimo na ufugaji uwe kwa nchi nzima badala ya Wilaya chache zilizoordheshwa katika Kif. 187 ukurasa 118 wa kitabu cha bajeti.

Kadhalika tathmini ya athari ya mazingira ya shughuli za maendeleo ya kilimo na mabadiliko ya wananchi kwenye mazingira ifanywe kwa nchi nzima na siyo katika wilaya chache zilizoordheshwa katika kifungu 118, ukurasa 119. Hii iwe pamoja na kutoa elimu kwa Watanzania wote kuhusu sheria ya mazingira na siyo kwa Halmashauri chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hifadhi ya udongo na matumizi bora ya ardhi inayotajwa katika kifungu 191 ukurasa 120, je ni vigezo gani vimetumika kuchagua vijiji hivyo 12 kwa ajili ya mafunzo hayo na malengo ya mafunzo hayo ni nini kwa Halmashauri chache hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani ni mzuri sana, si tu kwa mazao ya korosho na pamba tu, naamini hata za mazao mengine kama mahindi na mpunga. Waziri aeleze ni kwa nini amelenga mazao ya korosho na pamba tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itangaze bei ya mahindi msimu huu kwa ajili ya *NFRA*, licha ya kupanga kununua tani 165,000 za nafaka iseme ununuzi utanza lini?

Mwisho, mamlaka ya mbolea tuliyoiondika sheria mwanzoni mwa mwaka huu imefikia wapi?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naipongeza hotuba ya Wizara kwa jinsi gani ilivyoandaliwa na hasa kwa kulihakikishia Taifa kuwa hakuna mtu atakayekufa kwa njaa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango mkakati wa kuzingatia Kilimo Kwanza kwa kipindi hiki, ningeomba Mheshimiwa Waziri azingatie yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pembejeo na mbegu bora. Miaka ya nyuma mikoa ilikuwa na vituo rasmi vilivyokuwa vinajihusisha na uuzaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali. Inashangaza sasa hivi havipo. Vituo hivyo vilikuwa karibu na wananchi. Naiomba Serikali kurejesha utaratibu huo na kama uzalishaji wa mbegu nchini ulisimama basi urejeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu Benki ya Wakulima. Pamoja na kuwa na msemo kuwa Benki ni maeneo ya matajiri na si kimbilio la maskini – katika benki ya wakulima ni kimbilio la maskini. Kuharakishwa kwa benki hii kutawawezesha wakulima waweze kukopa kutoka katika benki hiyo na niombe yafanyike yafuatayo:-

- Itolewe Elimu ya matumizi ya benki hiyo mapema.
- Wananchi wahamasishwe ili kujua utofauti wa benki hiyo na benki zingine.
- Benki ijiandae kutoa mikopo pia ya vifaa vya kilimo yaani pembejeo na zana za kilimo

Mheshimiwa Naibu Spika, naliunga mkono suala au tamko la Kilimo Kwanza, lakini suala la kujiuliza:-

- Mbona bajeti ni ile ile ya 2008/2009 na 2009/2010, ukwanza wake utaonyeshaje tofauti?
- Kama wakulima wataitikia tamko hilo la Kilimo Kwanza, je, Serikali imejiandaa vipi kuyapokea mazao yao mfano kuwa na soko la uhakika?
- Mheshimiwa Waziri akumbuke kuwa, Kilimo ni vijijini, je, Maafisa Ugani watakapopatikana wa kutosha na kilimo ni vijijini, kuna maandalizi gani ya kutosha kwa wataalam hawa mfano usafiri na nyumba?
- Serikali inapojiandaa kuwapimia wawekezaji ardhi, niombe pia wanapojitokeza wananchi wazalendo wa nchi hii nao wapimiwe ardhi zao

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha zao la pamba si kigeni nchini na hasa Mkoa au Mikoa ya Kanda ya Ziwa hasa Mwanza na Shinyanga. Nampongeza sana sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuongeza bei ya Pamba na wananchi kuifurahia. Tunasema ahsante kwa Serikali, ila ninachoomba:-

- Pembejeo na zana za kilimo zipatikane za kutosha na kusambazwa nchini kwa wakati.
- Elimu ya ubora wa zao hili ili wakulima waweze kuvuna na kuuza kwa ubora wake, itolewe na Maafisa Ugani iwezekanavyo. Nasema hivyo kwa sababu

wakulima huongeza mfano, maji, mchanga na kadhalika kwenye zao hili, hivyo kukosa soko zuri nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza ni *theme* ambayo itahamasisha wananchi kushiriki katika kilimo ili kujiongezea tija ya chakula cha kutosha, akiba na chakula cha biashara. Lakini kilimo hapa nchini petu kinategemea sana mvua na kumekuwa na mabadiliko ya tabia nchi na uchafuzi wa mazingira ambapo mvua hainyeshi vya kutosha. Je, katika hali hii tumejipangaje aidha, kutumia mabwawa na mito kuanza kilimo cha umwagiliaji ili kukidhi lengo hili la Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo bora si mvua peke yake, ni pamoja na pembejeo, mbegu bora, mbolea na zana za kilimo kama vile matrekta. Asilimia kubwa ya wakulima ni wale ambao wanatumia jembe la mkono. Je, Serikali imejipangaje sasa kuachana na kilimo cha jembe la mkono na kutumia matrekta? Je, matrekta ya kutosha yatanunuliwa na kusambazwa kwa wananchi kwa lengo la kuwarahisishia shughuli zao za kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii imekuwa na Mikoa ambayo mvua ni ya kutosha, yenye ardhi ya kutosha tena yenye rutuba ya kutosha, sasa rai yangu hapa ni kwamba, Serikali iendeleze mikoa hii kwa kuwapatia mambo yote yale ambayo yanaifanya iweze kuzalisha zaidi na kuwa ghala la chakula kwa nchi nzima kulikoni kuzigawa rasilimali nchi nzima. Mkazo zaidi uwe katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo hakiendi bila wataalam. Hivyo lazima tuwe na mshamba darasa ambayo wananchi watasoma kwa lengo la kupata elimu zaidi. Mabwana Shamba waachane na tabia ya kukaa ofisini, wapatiwe vitendea kazi pamoja na usafiri ili waweze kufanya kazi zao ipasavyo ili wawasaidie wakulima wetu ili tija ionekane katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea ni msingi katika kilimo, hivyo ni lazima ipatikane kwa wakati na ya kutosha tena kulingana na Mkoa na Mkoa. Utafiti ufanyike kuangalia ni aina gani ya mbolea ambayo inafaa kutoka sehemu moja ya nchi na sehemu nyingine ya nchi ili kuwa na mizania kati ya udongo, mbolea na mimea.

**MHE. PINDI CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja na kupongeza kazi nzuri za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze kwa kuwasaidia sana wakulima kama kuwafidia wakulima wakati wa *Financial Crisis* na ruzuku za pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kilimo Kwanza, naomba kushauri kama ifuatavyo. Mapinduzi ya kilimo yanatuelekeza kuwa upo umuhimu wa kuwa na viwanda vya majembe na mbolea je, hadi leo viwanda vya majembe ya mkono na mbolea nchini

ni vingapi na je, vinatosheleza? Nini mpango wa Wizara katika kuboresha maeneo hayo? Aidha, ningependa kujua kwanini bei ya mbolea wakati wa kilimo inakuwa tofauti na wakati wa kiangazi ambapo hupungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri ni kwamba, suala la umwagiliaji ni muhimu sana je, Wizara ina mpango gani wa kuweka kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mto Ruaha wa Iringa. Bado matumizi ya mashine za kilimo ni madogo mfano matrekta, mashine za kupukuchua mahindi, mashine za palizi katika kilimo, Serikali ina mpango gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya kuweka sera ambao zitawalinda wakulima wetu pamoja na utandawazi na soko huria mfano, mazao ya chai, kahawa na matunda kwanini tunaruhusu viwe *imported*. Tuweke *Import tax* kubwa ili kulinda soko la ndani la malighafi. Michele Mbeya iko mingi sana, unga, *apples* tuweke mipaka ya soko huria ili kuwalinda wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi iliyopo Halmashauri husaidia sana lakini *capacity* kwenye *Councils* bado ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi yaliyokuwa yanalimwa sana enzi hizo sasa hayapo, mfano, Ismani iko wapi leo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Mazao ambako watu wanaweza kuweka mazao (kupitia hotuba hii naomba wataalam wa mazao (kuanzisha benki za mazao) waje Iringa hususan Ludewa kutuelekeza. Benki ya mazao iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vocha, ugawaji wa vocha ni muhimu ukashirikisha wadau wote baadhi ya maeneo walisahau kuwashirikisha Madiwani ambao husaidia kuelimisha hususan pale ambapo vocha ni chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuwasilisha

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa na kuwasilisha bajeti vizuri, lakini hasa kwa kuendesha Wizara ambayo inawezesha Watanzania kula na pia kuweza kujiletea pato kwa wale walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu aina ya Kilimo. Nawaasa tuendelee na msukumo wa kubadili kilimo toka jembe la mkono kwenda katika matumizi ya *power tillers* na matrekta. Itasaidia kungeza wingi wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mnyauko wa Migomba. Mashamba ya migomba ya wananchi wa Wilaya ya Karagwe yameshambuliwa na ugonjwa wa mnyauko. Serikali ngazi ya Wilaya inajitahidi, lakini suala hili limekuwa zito sana. Tunaomba Serikali ngazi ya Taifa iongeze nguvu katika kushughulikia tatizo hili ama sivyo baada ya muda si mrefu kutakuwa na tatizo la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi nzuri na kutoa kipaumbele cha Kilimo Kwanza, bajeti imeongezeka hatuna budi kuishukuru Serikali kwa ongezeko hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu wa kuwepo viwanda vya pembejeo na kuwapatia wakulima soko na bei nzuri kwa mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima, kwa kufungua mashamba darasa kwa kuwapatia hao wataalam pikipiki ili waweze kuwafikia wakulima kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia ihakikishe wataalam wa ugani wanapatiwa nyumba kama wataalam wengine wanavyojengewa mfano, walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie Kilimo cha Umwagiliaji, kwa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza kilimo kimepewa kipaumbele, basi Kilimo cha umwagiliaji kitiliwe mkazo mwelekeo ubadilike kwa kuwa na mashamba makubwa yaliyopimwa, watu watawekeza pesa zao humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikupongeze wewe pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo chakula na Ushirika aliyetoa hotuba yake. Vile vile niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kwa kuwa mbolea ya ruzuku mwaka jana katika Mkoa wa Kigoma vocha zilicheleweshwa na kupelekwa mwezi wa 11 wakati huo mahindi yalikuwa si ya kuwekewa mbolea tena. Kwa kuwa mwaka jana vocha zilichelewa kwani zinatakiwa zifikishwe mwezi wa Nane au wa Kumi je, mwaka huu vocha zitafikishwa mapema ikiwezekana? Ahsante.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa dhati pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wakiwemo viongozi wa Bodi za Mazao kwa jitihada zao na kazi nzuri katika kipindi hiki kigumu cha hali ya hewa isiyotabirika, msukosuko wa uchumi na kuporomoka kwa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia kwa hotuba safi yenye kuzingatia changamoto dhidi ya kilimo na kwa kuweka mikakati yenye matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya jitihada zao zinarejeshwa nyuma na mgao mdogo katika bajeti za kila mwaka, chini ya lengo la asilimia kumi ya tamko la Maputo. Kwa mfano, mwaka 2008/2009, kati ya bajeti nzima ya Sh. 6,258.8 bilioni,



Kilimo, Mifugo na Uvuvi vilipangiwa Sh. 155.2 bilioni sawa na asilimia 2.5. Kwenye bajeti hii, mgao ni Sh. 173.12 bilioni sawa na asilimia 2.2 ya bajeti nzima ya Sh. 7,224.7 bilioni. Kwa hiyo, mbali ya kuwa chini sana ya Azimio la Maputo, ingawa mgao wa mwaka huu ni ongezeko la asilimia 45, ikilinganishwa na bajeti nzima umeshuka kutoka asilimia 2.5 hadi 2.2. Katika hali hii, kauli ya Kilimo Kwanza na msimamo au wa *Agriculture for Development for food security* yanabaki maneno tu. Si makosa ya Wizara bali Taifa liwape nguvu zaidi ingawa sasa tunajaribu kushirikisha sekta binafsi, yapo maeneo ambayo yataendelea kutegemea zaidi bajeti za Serikali, nayo ni Mafunzo ya Maafisa Ugani; Ruzuku kwenye pembejeo; Uzalishaji wa mbegu bora; Utafiti; Usimamizi wa usambazaji pembejeo; Usimamiaji mashamba darasa na mengineyo. Haya yote yanahitaji fedha na watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umwagiliaji limetajwa chini ya kauli mbiu Kilimo Kwanza (Ibara 118 – 121) na katika Ibara 135 – 136. Kwa kuzingatia janga ya mabadiliko ya hali ya hewa na kutokutabirika mvua, hotuba ingezama zaidi katika suala hili. Pana haja ya kuunganisha mipango ya Wizara yako na ile ya Wizara ya Maji, Ardhi na Maliasili na Mazingira kuibua miradi mikubwa ya umwagiliaji. Katika hili nashauri kwenye hizo skimu 40 zinazotajwa iwepo miradi kando kando ya Mto Ruvu kwa manufaa ya Wilaya za Kisarawe, Kibaha na Morogoro Vijijini hasa baada ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka ya 2007/08 hadi 2008/09 zao la Korosho limeshuka kwa asilimia 20.22. Pamoja na sababu nyingi, upungufu wa pembejeo na kushindwa kwa wakulima kumudu gharama zake, kumechangia sana. Kwa bahati mbaya, baada ya kutetereka zao la nazi (minazi kufa hovyoy), tegemeo kubwa la ukanda wa pwani kwa zao la biashara ni korosho pekee. Kwa hiyo, kutetereka kwa zao hili ni pigo kubwa kwa wakulima wa ukanda wa pwani ya Hindi. Ipo haja ya Serikali kuchukua hatua thabiti za kuwezesha pembejeo ziwafikie wakulima kwa wakati na za kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hasa wadogo wadogo hawana nafasi ya kupata mikopo yenye masharti nafuu. Kwa hiyo, uamuzi wa uanzishaji wa Benki ya Kilimo ni wa busara. Nchi nyingi zimenufaika sana kutokana na kuwepo benki za kilimo. Ushauri wangu ni kuwa, ule mpango wa kuwa na Dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali (*TIB*) utekelezwe haraka. Pia dirisha hilo lisiruhusiwe kudumu muda mrefu. Vinginevyo *TIB* ataona ugumu kuliachia dirisha liende kwa benki kamili. Vile vile, Serikali iruhusu uwepo wa taasisi nyingine za kukopesha wakulima ili pawe na ushindani kwa manufaa ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi ya Mazao na ukusanyaji wa Mapato. Hivi karibuni Serikali iliamua kusitisha Bodi za Mazao kukusanya ushuru wa mazao yao. Badala yake kazi hiyo ifanywe ne *TRA* na pia makusanyo hayo yawasilishwe hazina. Gharama za uendeshaji wa Bodi zote za Mazao zinabebwa na Serikali. Uamuzi huu una kasoro zifuatazo:-

a) Umeondoa motisha kwa Bodi kufanya bidii ya kuongeza upatikanaji wa faida kwani haziwajibiki kugharamia matumizi yao.

b) Sasa Hazina inabeba mzigo wa kumudu gharama za mazao kama ilivyokuwa siku za nyuma Mashirika ya Umeme yalipokuwa yanasongamana na Hazina kufuatilia fidia ya hasara zao. Naishauri Serikali ilitafakari hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushuru wa korosho zisizobanguliwa. Siku za nyuma ushuru huu ulikuwa ukikusanywa na Bodi ya Korosho kwa matumizi ya bodi. Leo hii ushuru huo unakusanywa na *TRA* na makusanyo hayo yanagawiwa kama ifuatavyo:-

- Asilimia 5.5 wilaya zinazozalisha korosho.
- Asilimia 1.0 zinaenda kwenye tafiti ya utafiti wa Naliendele.
- Asilimia 3.5 inapelekwa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini asilimia 3.5 isirejeshwe kwa wakulima, sielewi. Nashauri hiyo asilimia 3.5 sasa irejeshwe kwa wakulima wa Korosho ama kwa njia ya kuongeza ruzuku kwenye pembejeo au ruzuku (*subsidy*) kwenye bei ya kununulia korosho kutoka kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwombea Waziri kila la kheri afanikishe suala la kuhamisha asilimia 3.5 kwa manufaa ya wakulima na Taifa kwa jumla na naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliohusika kuandaa makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Tanzania kwa utashi wake wa kisiasa ambao umewezesha kilimo kuwa kipaumbele cha Taifa na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Naipongeza hotuba hii kwani inalenga kuendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa CCM, inayosema kuwa kilimo ndio msingi wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Kilimo kwani pamoja na matatizo yaliyoikumba nchi yetu ya ukame na mtikisiko wa kiuchumi, sekta ya kilimo imeweza kukua kwa asilimia 4.6, kuchangia pato la Taifa kwa asilimia 25.7 na kutupatia fedha za kigeni asilimia 30.9. Hii ni ishara tosha kuwa kwa kuwa Watanzania walio wengi ni wakulima, kutafsiri kauli mbiu ya Kilimo Kwanza kwenye vitendo, kweli ndio njia pekee itakayokuza uchumi wetu kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amesema utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta ya Kilimo (*ASDP*) utaendelea kutekelezwa kupitia *DADPs* katika ngazi ya Wilaya. Ili hili liwezekane inabidi mambo yabadilike. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Mahesabu za Serikali za Mitaa, ukaguzi wa programu ya *DADPs* unaonyesha kuwa fedha nyingi hata zaidi ya 40% watu wanafanya semina, wanalipana posho, viburudisho

na kadhalika. Kinachohitajika sasa ni uwekezaji wa kina katika sekta hii. Hivi miongozo ya *DADPs* unasema asilimia ya semina, posho, viburudisho, mafuta ni asilimia ngapi ya miradi mzima? Fedha nyingi zinazopelekwa kwenye Halmashauri, za kilimo hazionyeshi mabadiliko kwa sababu zinawanufaisha watendaji wachache. Naiomba Wizara ya Kilimo ipitie miongozo hiyo ili fedha za nchi hii zitumike itakiwavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndizi kwa wakazi wengi wa Mkoa wa Kagera ni zao la kudumu la chakula na biashara. Kwa kiasi kikubwa uchumi wa Mkoa wa Kagera unajitegemea kwa ndizi. Hivi sasa, katika Mkoani Kagera Halmashauri saba kati ya nane zimeathiriwa na ugonjwa mbaya wa migomba uitwao ugonjwa wa unyanjano wa migomba (*banana Bacterial wilt BBW*). Ugonjwa huu ni hatari na unasambaa haraka sana, kwani unasababishwa na vimelea vya bakteria, majani huwa njano, hubabuka, ndizi huwa na mabaka, ndizi huwa ngumu, huiva kabla ya kukomaa na haifai kwa matumizi ya binadamu au wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa huu kwa haraka unaangamiza uchumi wa Mkoa wa Kagera, lakini haupewi kipaumbele. Hata katika hotuba ya bajeti hii, wakati Waziri anajadili udhibiti wa magonjwa, visumbufu vya mimea na mazao ya kilimo, ugonjwa huu wa unyanjano wa migomba (*banana bacteria wilt*) haukutajwa. Naleta kilio cha wana Kagera na naomba Waziri anieleze katika bajeti hii, kuna mipango gani ya makusudi na ni kiasi gani cha fedha vimetengwa ili kuudhibiti ugonjwa huu wa kunusuru Mkoa wa Kagera kutokana na janga hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mkulima aweze kunufaika na kilimo chake inabidi apate soko la uhakika na bei nzuri. Watanzania wa Kagera wengi hupendelea kuuza kahawa zao kwa Waganda kuliko kuuza hapa nchini kwa sababu Waganda wana bei nzuri zaidi. Hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa sana na sera za masoko zilizopo. Tanzania mnunuzi lazima anunulie kwenye vituo, akoboe, *A grade*, asafirishe, aweke kwenye makasha, atoe *sample* ziende Moshi kwenye Bodi, majibu yarudi baada ya kama wiki mbili hivi, ndipo huyu mnunuzi aweze kuuza kahawa yake kupitia Auction. Mtanzania aliyechukua mkopo benki akanunua kahawa, hadi kulipwa inachukua muda wa miezi miwili hadi mitatu. Mganda mzunguko ni mfupi anachukua wiki mbili hadi tatu. Hivyo fedha alizokopa zinazaa haraka zaidi.

Vile vile Uganda sera zao zinawaruhusu *ku-process* kahawa kufuatana na matakwa ya soko. Uganda wanunua hata kahawa mbivu, mbichi, na kadhalika na *ku-process* kufuatana na matakwa ya mteja (*washed, semi-washed, steamed, Honey* na kadhalika) Uganda hawawezi kodi au ushuru wa Halmashauri hawalipi *port wharfage charges* pale bandarini na vile vile wanaruhusiwa kuuza kahawa (*export*) moja kwa moja bila kupitia kwenye mnada. Kwa sasa kahawa ya *Robusta* ya maganda Uganda inanunuliwa kwa sh. 650/= au 700/= wakati Mtanzania anauza kwa sh. 450/= kwa kilo. Ni lini sasa wataalam wa kilimo na masoko wataingilia utaratibu huu mrefu wa Tanzania ili mkulima aweze kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siku ya leo kuamka hali nikiwa mzima. Pia Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi zangu kwako wewe binafsi, Naibu wako pamoja na Wenyeviti wako kwa hali ya upendo mlio nao kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hali ya bajeti ya Wizara unaweza ukaona ama kusema kutokana na majukumu ya Wizara utaona Serikali bado haijawa tayari kuboresha sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli mbiu ya Serikali iliyopewa kilimo, nasema hili lilitendeka na kusema Siasa ni Kilimo, Kilimo ni Uti wa Mgongo. Mafanikio ya siasa ni kilimo hayakuonekana. Napata wasiwasi juu ya nia ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu mkubwa katika Wizara hii juu ya kutoa elimu kwa wakulima. Wakulima wetu ambao ndio asilimia kubwa wanalima patosha na huvuna pamekwisha. Hii inatokana na ukosefu wa elimu kwa wakulima wetu. Muundo wa kilimo cha sasa ni lazima kilimo chetu kiwe cha kisayansi. Kufanya hivi tunamwondoa mkulima katika kilimo cha kutumia jembe la mkono na kutegemea mvua ambayo huna uhakika na mvua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuwa na kilimo chenye nia ya biashara ili kukuza uchumi wetu ni lazima tumwandae mkulima kwa kumpa elimu, pembejeo, mbegu bora, Mabwana Shamba wa kutosha na pia kumwondolea jembe la mkono. Tukifanya hivi tutaweza kufikia malengo ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maafisa Ugani, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na Mabwana Shamba wa kutosha, tunaweza kupiga hatua tatizo sugu juu ya watu hawa ni Serikali yenyewe kutowajali, jambo ambalo walishindwa kufanikisha majukumu yao na hatimaye wakulima wetu kukosa kilimo kielimu. Pia ni wachache sana, bado ni kidogo kulinganisha na *geography* ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi za Mazao lengo la Serikali juu ya Bodi za Mazao ilikuwa ni njema sana. Mfumo wa Bodi huu ulikuwa wa kujitegemea. Mara tu baada ya Serikali kutoa ahadi juu ya bodi hizi kuhusiana na malipo yao. Serikali iliahidi kulipa asilimia mia moja juu ya watendaji hao. La kusikitisha Serikali haikuweza kuwalipa wafanyakazi hao kama ilivyopanga na sasa bodi hizo zimepooza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kilimo cha Umwagiliaji, nchi yetu imetenga mikoa sita ambayo ndiyo iliyopewa kipaumbele katika kilimo. Mkoa mmojawapo ambao ni tajiri kwa maji ni Mkoa wa Morogoro. Mkoa huu una mito si chini ya mia moja na arobaini 140, mito mingi ambayo ina uwezo wa kuwa na maji kwa mwaka moja. Ni kitu gani kinachopelekea Mkoa huu kukaribia kukumbwa na njaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, naiombea Mungu Wizara hii ipate mategemeo yake ili iweze kufanikisha azma yake.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze hotuba ya Waziri na naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Wananchi wa Pangani wamehamasika sana katika kilimo, kinachohitajika na wasaidiwe sasa waondokane na kilimo cha jembe la mkono. Katika mpango mzima wa Kilimo Kwanza Serikali izingatie mambo yafuatayo:-

- Serikali iweke mikakati ya makusudi ili kuhakikisha wananchi wanapimiwa mashamba yao ili wapate hati miliki na hati za kimila, kwani ndio msingi wa wao kupata uwezo wa kutumia rasilimali zao na kupata mikopo ili waendeleze kilimo.
- Wahamasishwe wakulima kwa kutumia trekta na *power tillers* na wakopeshwe kwa masharti nafuu hata kutoa ruzuku wa *power tillers* ili wazalishe kwa wingi.
- Watoe kipaumbele na kutoa pesa za kutosha kuimarisha miradi ya umwagiliaji. Wilaya ya Pangani imeomba fedha za ziada za *DIF*, tunaomba Serikali itusaidie katika hili ili tuweze kukamilisha miradi ya umwagiliaji katika Wilaya ya Pangani. Pamoja na mchango huu naambatanisha barua iliyo kwenda Wizara ya maji ili yenye maombi ya ziada ya Sh. 290,051,120/= ili tukamilishe miradi hii.

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote waliotayarisha hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu napenda kuanza kwa kutoa maoni yangu kuhusu kuendeleza na kukuza kilimo hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufanikisha azma hiyo ni lazima sasa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kutekeleza kwa vitendo mipango yote iliyotoa katika hotuba hii ya bajeti na isiishie kwenye vitabu na maneno matupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ninaloishauri Serikali ni kubaini mazao ambayo kila Mkoa au Wilaya ndio yanastawi vizuri ili kuweza kuwapa pembejeo mahsusi wakulima wa maeneo husika kwa mazao hayo ili waweze kufanikisha uzalishaji unaoridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo muhimu sana kuandaa masoko kwa mazao yetu ambayo wakulima watayavuna ili kutowakatisha tamaa kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha azma ya Serikali ya kuzidisha pato la Serikali katika kilimo ni lazima sasa tubadilike kwa kuuza bidhaa zetu nje ya nchi zikiwa ghafi kwa sasa tuziuzwe zikiwa zimeongezwa thamani kwa kuzisindika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami niungane na wenzangu kuchangia hoja iliyo mbele yetu ambayo ni muhimu sana Kilimo Kwanza. Awali ya yote naomba niwapongeze, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote waliohusika katika kuandaa utaratibu mzima. Sasa naomba nijikite kwenye kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakumbuka kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliuteua Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la chakula la Taifa lakini pia Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa mikoa sita maalum ya uzalishaji wa chakula hapa nchini. Mradi huu wa kuzalisha chakula katika Mkoa wa Morogoro unajulikana kwa jina la *FAMOGATA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ni mkubwa sana (kamambe) ni mradi wa Kitaifa. Sasa cha kushangaza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikuona mahali popote kuhusu mradi huu wa kitaifa, tunasema Kilimo Kwanza na wakati huo huo hakuna mpango madhubuti au mkakati wa Kitaifa unaoonyesha jinsi *FAMOGATA* itakavyotekelezwa ili tulime vya kutosha na kuzalisha chakula cha kutosha kwa ajili ya nchi yetu na kuuza nje ya nchi. Hata hivyo, pia sioni mikakati kamambe ya kuisaidia hii mikoa sita maalum yaani Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa na Kigoma. Je, katika mazingira haya tutafanikiwa kuhusu Kilimo Kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapojumuisha kujibu hoja, naomba sana nipate maelezo ya kina kuhusu jinsi Serikali itavyotekeleza mradi huu wa *FAMOGATA* wa Mkoa wa Morogoro lakini pia kuhusu hiyo mikoa sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nawatakia kazi njema.

**MHE. DR. CYRIL AUGUST CHAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kazi nzuri sana, ukisaidiwa kwa karibu na ndugu yangu Dkt. Mathayo David na watendaji wako chini ya mchapakazi Mohamed Muya. Ninalo ombi moja tu. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vyama vya Ushirika (vya Msingi) haviendeshwi vizuri. Mapato yatokanayo na mirahaba ya ukodishaji wa mashamba yanatumiwa na viongozi wa vyama hivi peke yao na hata pale nilipowaeleza katika semina kuwa fedha hizo zinapaswa kutumiwa kwa shughuli za jamii yote, nilishutumiwa sana na viongozi hawa. Wengi wamefikia hadi hatua ya kuweka mikakati ya kumleta mtu atakayegombea ubunge ambaye hatawabugudhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muimulike Halmashauri hii hasa Vyama vya Msingi vya Jimbo la Moshi Vijijini ili wananchi wote wanufaike na fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Kilimo na Chakula kwa bajeti yake nzuri na muhimu sana kwa Taifa. Nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa

ujumla wao. Lakini pia kwa umuhimu nimpongeze Waziri Mkuu pamoja na Serikali kwa pamoja kwa kutoa kipaumbele katika suala zima la Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu zao la kahawa. Ni kweli kwamba zao hili la kahawa kwa sasa hivi limekosa kabisa maana, kwa maana kwamba soko lake linazidi kabisa kudidimia na kwa kuwa Mikoa inayotegemea zao hili limekuwa likiwasaidia sana wananchi katika uendeshaji wa maisha ya kila siku. Naiomba Serikali iangalie ni jinsi gani zao hili linapatiwa ufumbuzi ili kuweza kuwasaidia wananchi wanaotegemea zao hilo. Lakini ningependa niseme kuwa kama nchi jirani mfano Uganda wanaweza kununua zao hili na wananchi wanapata pesa nzuri, basi Serikali ione umuhimu wa kuruhusu wananchi waishio jirani ili waweze kuuza zao hilo kwa uhuru na amani kuliko sasa hivi wanavyouza huko kwa kificho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamechangiwa na wenzangu na hili likiwemo, lakini nimeona nilirudie tena kwa kuwa wananchi wanaolima zao la kahawa sasa wamekata tamaa na wanaona hakuna msaada wowote unaoonekana kuchukua na kuchukuliwa na Serikali. Naomba Serikali iangalie zao hili kwa macho mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Stephen M. Wasira; Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. David Mathayo David; Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri sana na inafurahisha. Ombi langu ni kuwa, mipango yote hii isimamiwe vizuri ili tupige hatua kubwa ya kuendeleza kilimo na kuondoa umaskini kwa wananchi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakulima na hali zao zimekuwa hazibadiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba:-

Kwanza, uanzishwaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko ni muhimu sana kuwasaidia kuwa na masoko ya uhakika.

Pili, kwa kuwa tathmini ya hali halisi ya chakula iliyofanywa na Serikali nchi nzima inaonekana kuwa kuna upungufu wa chakula katika maeneo mengi au katika mikoa mingi. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikafanya mapema ugawaji wa chakula kwa kujua ni kiasi gani kitapelekwa kwenye kila eneo lenye upungufu wa chakula ila kisubiri usambazaji tu. Hii itaondoa usumbufu ambao umekuwa ukitokea kama dharura.

Tatu, ugawaji wa mbolea kwa kutumia vocha ni mzuri sana, lakini utekelezaji wake inabidi uboreshwe zaidi. Pia ni muhimu viongozi kama Madiwani wakapewa elimu na washirikishwe kwa ukaribu, hasa kwa Wilaya ambazo hazijaanza kutumia utaratibu huu, mwongozo wa jinsi ya kutumia utaratibu huu upelekwe kwanza ili kuondoa matatizo yaliyojitokeza katika Wilaya kama Mbarali na kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ombi kwamba, Vyama vya Ushirika na wananchi binafsi kutoka Mbarali walikopa pesa kwa taasisi ya *SCULT* kwa ajili ya kusaidiwa kuagiziwa *power tiller* (matrekta madogo), ni karibu mwaka mmoja umepita hawajapata matrekta hayo na nimekuwa nikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi hao kuwa wamekuwa wakifuatilia bila mafanikio. Naelewa utendaji mzuri wa chombo hiki na umuhimu wake katika kutoa elimu na uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika. Ninachoomba kwa Wizara ni kujua nini kinachotokea kwa *SCULT* mpaka wameshindwa kukamilisha ahadi hiyo kwa wakulima kama walivyoahidi, inawezekana wameshindwa kulipia kwa waagizaji. Naomba msaada wa Wizara kwa hili aidha, kwa kuwasaidia *SCULT* ili waweze au kwa kuwasaidia waweze kupata mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la wakulima wadogo wadogo la Maalbino linahitaji watalaam wenye uzoefu na utalam kwa ajili ya kuwasimamia wakulima waliopewa maeneo ili kuongeza uzalishaji wa eka tofauti na ilivyo sasa. Kuna malalamiko kutoka kwa wataalam wachache walio pale Madibira kuwa bajeti au pesa wanazopewa ni kidogo sana kiasi kwamba wanakosa hata pesa kwa ajili ya matengenezo madogo madogo ya miundombinu na hata usimamizi unakuwa mgumu sana kwao kwa kukosa magari ya usafiri ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Ubaruku wananchi baada ya shamba la Mpunga la Serikali kuuzwa walitafuta eneo lenye kubwa wa hekta 5000 na wameanza kujitahidi kwa shida sana kutengeneza miundombinu itakayowawezesha waanze kulima kilimo cha mpunga. Hadi sasa kiasi cha zaidi ya Sh. 25,000,000/= zimetumika kutokana na michango na nguvu za wananchi, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alipotembelea Mbarali na Mheshimiwa Waziri Mkuu pia alipotembelea wananchi au wakulima hawa wamekuwa wakiwasilisha maombi yao ya kuomba msaada wa kuungwa mkono na Serikali, lakini bado jibu kamili halijapatikana. Je, Serikali inaaahidi nini au inatoa jibu gani? Kama kuna utaratibu wowote wa kufuata naomba tupewe ili kuharakisha kabla ya msimu wa kulima mwaka 2009/2010 haujaanza.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Kilimo kwa kazi yao nzuri ya Kilimo Kwanza kwa lengo la kuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza, napenda kujua Serikali ilivyojipanga kupeleka fedha kwenye ukulima badala ya kilimo kwa kuanzisha vikundi vya ushirika wa kilimo na kuwakopesha zana za kilimo na kutengeneza miundombinu hasa ya umwagiliaji ili kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua Wizara imejipanga vipi kuondoa vikwazo vya kuzuia chakula kwenda Mjini Musoma ili kupunguza mfumuko wa bei.



Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ukurasa wa 86 amesema skimu zote za umwagiliaji zitapata ruzuku ya pembejeo. Napenda kupata ufafanuzi, hizi ni pamoja na wilaya ambazo hazikutajwa kupewa ruzuku kama Wilaya ya Bunda na Magu au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuanza kulipa madeni ya wakulima wa pamba Mkoani Mara. Ombi langu ni kwamba, wapo pia waliokuwa wanaiuzia Mara *Co-operative Union* vifaa mbalimbali ambao walikuwa wazabuni, bado hawajalipwa, tunaomba nao pia waweze kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. HASSAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na ya kuleta matumaini. Naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia tisini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kumwagilia maji ulioko Makangaga bado mpaka leo huo mradi haujakamilika na unasuasua. Hapa tunasisitiza Kilimo Kwanza, lakini miradi muhimu ya kumwagilia maji haikamiliki. Je Mheshimiwa Waziri ni lini huu mradi utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wawekezaji wakubwa kwenye kilimo bado uwekezaji uko ovyo na hauzingatii chakula kwa kuwa hao wawekezaji hawataki kulima chakula, wanazingatia mibono. Naomba Wizara kuwabana ili wapate kulima chakula kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo makubwa kupewa wawekezaji bila kuyaendeleza. Je, kanuni zake zinamtaka kuendeleza maeneo kwa muda gani? Naomba ufafanuzi hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kwa wakulima ni muhimu kwa kuzalisha zaidi. Bado nina wasiwasi katika upatikanaji mikopo na riba kuwa nafuu na muda mrefu. Naiomba Wizara kupitia hazina kuangalia upya mikopo kwa wakulima.

Je, mpango wa kuanzisha Benki ya Wakulima imefikia wapi”?

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza mpango wa (*one un joint programme*) kwa mikoa ya Lindi na Mtwara, mafunzo kwa vikundi 50 na kupatiwa matrekta na mashine za kusindika muhogo. Hii italeti tija na kuzalisha chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara kuwashawishi na kuwapa agizo kununua mbegu bora na kuhimili ukame hususan Halmashauri zote nchini kufanya hivyo, hilo litasaidia wakulima kupata mbegu hizo kwa karibu na haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naipongeza Wizara kwa mpango huu naona kama tukizingatia tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii ambayo inabeba jukumu kubwa la kulisha nchi, kuipatia fedha za kigeni na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni namna gani tunawapa (*attitude*) wakulima wadogo wadogo wenye vishamba vidogo na zana duni. Kwa maoni yangu si vema kuwavusha hawa wakulima kwenda kwenye matrekta kwa maana hawana uwezo huo. Pengine ni bora kuboresha kazi zao kwa kuwapatia mafunzo na ushauri wa ugani ili wazalishe zaidi. Pia matumizi ya mboji ambayo ni nafuu na *economical* kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya *Exports bag*. Nawapongeza *TCB* kwa kutoa uhuru wa wakulima kutumia *Sisal* au *Jute Bags*, si haki kwa mkulima wa kahawa kukulazimishwa kununua *sisal bag* ambayo ni ghali na haitumiki kwa muda mrefu maana inaishia pale tu bandarini. Katani ina matumizi mengi na inaweza kutoa mazao mengi kama mazulia na kadhalika, kwa nini ulazima upo wenye *coffee exports bags* tu, kwa nini kiwanda hiki kimeng'ang'ania *export bags* tu. Je, kwa kipindi ambacho kahawa imesafirishwa na pale ambapo inauzwa kiwanda hiki kinazalisha mazao gani? Napenda sana kulinda viwanda vyetu lakini ulinzi huu uwe wa ushindani ulio sawa na si wa uonevu tu. Wakulima wa mahindi, pamba na mazao mengine wanatumia magunia na mbona hakuna ulazima huo? Kama Serikali ingekuwa inahudumia viwanda hivyo ingelinda viwanda vyetu vya fanicha hapa nchini. Mbona hakuna maagizo ya kutumia samani za hapa nchini. Naiomba Wizara iunge mkono hatua iliyochukuliwa na *TCB* maana ni ya kizalendo na inaleta usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji mashamba na kuwa na Mabwana Shamba. Sheria ya Kahawa ya 2001 bado haijatekelezwa na Bodi ya Kahawa mpaka sasa. *Impact* ya *TCB* kwenye uzalishaji wa kahawa haionekani. Wizara isaidie *TCB* kufanya kazi hii kwa kusaidiana na Halmashauri husika. Pengine ni vema kufungua ofisi za *TCB* pia katika maeneo ya wakulima wa kahawa. Bila hivyo wakulima wa kahawa wanahangaika sana na wanaonekana hawana baba wa kuwaangalia. Ni vema kuona utaratibu wa kuiwezesha *TCB* ili itimize majukumu yake. Njia moja na kuweka ushuru kwenye leseni kwa wanaoshiriki mnada.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana ahadi ya Mheshimiwa Waziri juu ya kuufanya ushirika wa *MBIFACO* ufanye kazi ya kununua kahawa mwaka huu ili kuleta ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema kwa mwaka wa fedha.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Wizara hii kupitia Wizara na Naibu wake pamoja na Katibu wake. Mchango wangu wa kwanza ni kuishauri Wizara kuzingatia yale yote yaliyoibuliwa na Serikali katika hoja ya Kilimo Kwanza katika

awamu hii ya nne. Kwa kuwa kilimo kimeongelewa sana katika awamu zilizopita lakini kiwango kilichofikiwa hakikuwa cha kuridhisha, basi tunaomba Mheshimiwa Wassira, Waziri na timu nzima iweke historia katika kuandaa program nzuri ya ulimaji na uzalishaji mkubwa wa kutosha soko la ndani na kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia katika hili lazima, Wizara iandae mbegu zenye ladha ya mvuto kwenye mchele kwa ajili ya kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kilimo kiweze kutoa picha ya uhalisia wa kasi lazima Wizara hii ishirikiane na Wizara ya umwagiliaji ili mipango hii iendane na kubana matumizi katika maandalizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huu wa kuasisiwa umeenda sambamba na nchi ya Malawi kwani Malawi nao tayari wametangaza Kilimo Kwanza, hivyo tuchukulie changamoto ya ushindani na tujigeze baada ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeelekezwa na Mheshimiwa Rais kwamba Morogoro iwe ghala la chakula, lakini kwa mtazamo wangu Mheshimiwa Rais alikuwa na nia nzuri sana. Lakini kauli yake ilipokelewa katika udhaifu kwani kasi haiendani na uhalisia wake, wala hatuelezwi tatizo ni nini, hii inapelekea hofu hata mpango huu wa Kilimo Kwanza huenda ukasuasua, kwa uzoefu wa kutotimiza dhamira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu juu ya Vyama vyetu vya Ushirika, lazima vifanyiwe mabadiliko, naomba kushauri, hivi sasa muundo wake uwe katika mtindo wa kampuni, hivyo vyama viajiri wataalam wenye ujuzi na *management* inayokubalika na mikataba ya utumishi kwa wote watakaokubalika katika uendeshaji wake, kwani kufanya hivyo kunaweza kuwapeleka Mahakamani pindi watakapoonekana wamekwenda kinyume na maadili ya kazi.

Mwisho, naishauri Wizara iwe inatoa ripoti ya Kilimo Kwanza kila baada ya miezi sita ili tuone tathmini yake na kuendelea kushauri, hii ni kwa sababu ya uzito wake. Ahsante.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ni jambo lililo dhahiri kwamba maendeleo ya nchi yetu yanategemea kilimo. Napenda kuzipongeza juhudi za Serikali katika mipango na lazima yake kubadili aina ya kilimo chetu ili kiwe na tija zaidi. Ili kufikia lengo hilo, suala la zana bora, mbegu bora, matumizi ya mbolea na kufuata kanuni za kilimo bora ni mambo ya msingi sana. Serikali imeshatoa maagizo ya ununuzi wa matrekta na *Power Tillers*. Inajitahidi kuagiza mbolea ya kutosha, aidha, tafiti za mbegu zinaendelea vizuri. Tatizo kubwa ni suala la ugani, Maafisa Ugani ni wachache na wengi wao wana mpango wa maarifa na ujuzi. Wengi wao wamekaa katika vituo vyao kwa muda mrefu na wamejenga mazoea na kusahau wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tufanye mageuzi makubwa kwa upande wa Maafisa Ugani. Na hapo wapatiwe Refresher course wa wapangwe upya ili kuamsha ari

yao. Nako tuone uwezekano wa kuanzisha vituo vya mafunzo ya kilimo kwa kila Wilaya/Tarafa, vituo ambavyo wakulima watakwenda hapo kujifunza elimu ya kilimo bora na ufugaji wa kisasa. Tumeweza kuwa na shule ya Sekondari kwa kila Kata, tutashindwa vipi kuwa na kituo cha mafunzo ya kilimo kila Tarafa na chuo cha Maafisa Ugani katika kila Wilaya? Nashauri Serikali ifikirie suala hili na naamini itawezekana.

Nchi yetu inahitaji sana mbolea, uko wapi mradi wa Kilameo? Je, gesi ya Songosongo haitoi tena mali ghafi inayofaa kutengenezea mbolea? Nini kilisababisha mradi huu kufa bila kuugua? Naomba nipate maelezo, Serikali ina mipango gani kuhusu ujenzi wa viwanda vya mbolea.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nashauri vocha za ruzuku ya mbolea izidishwe katika mbolea ya Minjingu ambayo imeonekana inafaa sana katika Mikoa ya Iringa na Ruvuma. Hii itasaidia sana kuendeleza utaalam mzuri uliotolewa na Serikali mwaka jana na kwamba mbolea hii inafaa kupandia. Tangazo hili lilifanya Kiwanda cha Minjingu kuzalisha zaidi na hivyo mwaka huu kwa kuachia soko huria au kwa kuipa *DAP* ruzuku kubwa, kutasababisha kiwanda kufa. Hii itakatisha tamaa wawekezaji wengine katika viwanda vya mbolea nchini. Pia itaonekana Serikali haifanyi utafiti wa kutosha kabla ya kutangaza jambo. Zaidi ya hayo kwa kutoa ruzuku kubwa kwa mbolea ya Minjingu kutaisaidia *TFC* kuuza mbolea hii ambayo imerundikana katika *godowns* zake baada ya mwaka jana kulazimishwa na Serikali kununua tani nyingi na ikaishia kununua tani 25,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, zilizoununuliwa hadi sasa ni tani 7000 tu! Hata hivyo, kwa mwaka mmoja kutangaza *TFC* kama ni muuzaji pekee wa mbolea hii na ghafla mwaka mwingine kutangaza soko huria, je, si kusababisha Kampuni hii kufa kwa sababu ya hasara kubwa iliyopatikana hasa kwa sababu ililazimishwa na Serikali kununua na ku-*stock* mbolea nyingi wakati ule bei ilikuwa kubwa sana? Niki-*declare interest* kama Mwenyekiti wa Bodi ya *TFFC*, uamuzi wa soko huria kwa kuingiza *DAP* ishindane kwa viwango sawa na mbolea ya Minjingu imetupa mshtuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba ruzuku ya mbolea iwahi katika mwezi wa Nane ili kusitokee uuzaji wa vocha kama ilivyotokea mwaka jana kwa baadhi ya maeneo. Hii ilitokea kwa sababu mbolea ya ruzuku waliipata baada ya kupanda mbegu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niendeleo kuikumbusha Serikali juu ya kuanzisha Benki ya Wakulima nchini, mpango ambao utasaidia sana wakulima kuwa na benki yao ambayo itawasaidia kuweka fedha zao wanazozipata kutokana na kuuza mazao yao wakati wa msimu wa mavuno. Vile vile itasaidia kuwaunganisha wakulima kuwa na umoja wao, kubwa zaidi wakulima wataweza kununua hisa na kukopeshwa wakati muda wa kilimo ukifika ili waweze kununua pembejeo, mbegu na matumizi mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wakulima wanania sana na mpango huu wa kuanzia Benki ya Wakulima vema Serikali ikasema lolote wakati wa majumuisho tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya mifuko aina ya Jafafa (*Jute bags*). Nina habari sio rasmi kuwa Serikali imeruhusu mifuko ya aina ya Jafafa (*jute bags*) kwa ajili ya kufungia zao la kahawa badala ya magunia ambayo yanazalishwa hapa hapa nchini. Vile vile nimesikia kuwa *jute bag* inapunguza ubora wa zao la kahawa kwani mifuko hiyo haina sehemu ya kupitishia hewa hivyo inasababisha kahawa yetu kuvunda. Naomba maelezo ya Serikali ili kutoa utata huu kwa wakulima na kwa nini magunia yasiendelee kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kubwa na Waziri pamoja na Naibu Waziri, hivyo nitapewa fafanuzi wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Naipongeza Serikali kwa kuwajali wakulima na kukuza uchumi wa Taifa kupitia kilimo. Kwa mazao mbalimbali yana bodi zake ambazo husaidia kusimamia uzalishaji wa mazao hayo pamoja na kutafuta soko la uhakika

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko mfano, alizeti, karanga, ufuta na kadhalika. Vile vile Mheshimiwa Waziri akinipa Ujumbe wa Bodi hiyo hakika nitamsaidia kwa uwezo wangu wote. Ni mara chache mtu kujiombea bali mimi ni muwazi siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya kilimo cha kisasa kwa wakulima. Bila elimu kwa wakulima wetu juu ya kilimo cha kisasa, uzalishaji kwa mazao mbalimbali utaendelea kuwa duni. Sasa ni Kilimo Kwanza, hivyo lazima mkulima apate elimu na hapo tutakuwa tumedhamiria kukuza kilimo cha Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiojificha mishahara ya Maafisa Ugani ni midogo sana kulingana na kazi zao zilivyo ngumu huko vijijini hata vyombo vya usafiri hawana.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii na nawapongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kitabu cha maendeleo, Wizara hii imetengewa kiasi cha Sh. 92,694,254,000/=, kati ya fedha hizo Sh. 90,177,545,000 sawa na asilimia 97.285 (97.285%) ya fedha zote za maendeleo ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uchumi wa dunia hivi sasa unayumba na kwa kuwa wachangiaji wetu au wahisani wetu tunaowategemea sana katika bajeti hii nchi zao ni miongoni mwa nchi zilizokumbwa na kuyumba kwa uchumi wa nchi hizo, je, endapo wahisani hao watashindwa kuchangia kwenye kapu la fedha zilizopangwa kwa miradi hii ya kilimo, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa malengo ya Kilimo Kwanza hayatakuwa na hivyo kuwa ni porojo la siasa tu bila vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nionavyo ni kwamba, bajeti hii ni tegemezi kutokana na fedha nyingi iliyopangwa kwenye miradi yake ya maendeleo inategemea sana *basket fund* (pesa za nje).

Mheshimiwa Naibu Spika, bila wafadhili inaonekana kabisa miradi hii ya maendeleo haitekelezeki, ni vema sasa Tanzania kwa maana ya Serikali ya Tanzania ianze kuwa na utamaduni wa kutenga fedha zake za ndani zaidi ili kuondokana na utegemezi vinginevyo kauli mbio ya Kilimo Kwanza itabaki wimbo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki ya wakulima ni muhimu sana kwa wakulima wetu, wakati umefika wa kuanzisha benki hii ili wakulima wetu wapate mikopo ambayo itawawezesha kununulia zana za kilimo na kuboresha kilimo chao, mikopo hiyo pia itawawezesha wakulima wetu kujijengea wenyewe miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga mitaro hasa kwa wakulima walioko kwenye maeneo inakopita mito.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wetu hawana masoko ya uhakika ya ndani kwa kuwa Serikali imekuwa ikiwabana kuuza mazao yao nje ya nchi hasa mazao ya chakula na hivyo kusababisha malalamiko mengi miongoni mwao. Ni vema Serikali ikatafuta jinsi ya kupunguza malalamiko hayo ikiwa pamoja kwa Serikali yenyewe kununua mazao yao kwa wingi na kumhusu kiasi fulani kwa mazao hayo kuuzwa nje ya nchi. Aidha, ni wajibu pia wa Serikali kutoa elimu kwa wananchi wetu juu ya uhifadhi wa mazao ya chakula ili kujikinga na njaa badala ya kuyauza mazao yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti za kilimo zilizofanywa ambazo matokeo yake mazuri hayajaendelezwa ni vizuri zikaenda sambamba na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza na taasisi zinazofanya tafiti hizo zishirikishwe kikamilifu ili kupata matokeo mazuri zaidi ya uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yako ya mwaka jana pamoja na ile ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema kujengwa kwa Kiwanda cha Mbolea huko Mtwara. Je, kiwanda hicho kitaanza kujengwa lini maana Mheshimiwa Waziri hajasema lolote kwenye hotuba hii.

**MHE. ARCH. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Wasira, Mheshimiwa Naibu Waziri D. Mathayo, Katibu Mkuu na watendaji pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kutuletea hotuba nzuri licha ya ufinyu wa bajeti, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuweza kuwafidia wafanyabiashara wa mazao makuu ya biashara kutokana na mtikisiko wa uchumi dunia pamoja na wakulima wa pamba. Ushauri wangu pia ni kuwaangalia wakulima wa kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia ile Benki ya wakulima ambayo tumekuwa tukizungumzia kwa muda mrefu ianze kwani ni mojawapo ya majibu ya haraka katika kuwakomboa wakulima wetu iwe ni pembejeo au zana kwa mapana yake. Kuna umuhimu mkubwa kwa pembejeo kufika kwa wakati wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sana tunavyowashawishi wakulima wetu kuongeza bidii katika uzalishaji wa mazao na wanaitikia na kujitahidi sana shida kubwa inakuja pale wanapovuna wanazuiliwa kuuza mazao yao nje ya nchi. Nashauri kwa sababu ni uhaba wa mavuno katika maeneo mengine, basi Serikali inunue hayo mazao kutoka kwa wakulima kwa bei nzuri kama ambavyo wangeweza kupata nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutamka mchakato wa uanzishwaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko, rai yangu ni uanzishwaji wa haraka wa hiyo bodi kutokana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti ni gharama, lakini tusichoke kutenga pesa kwa ajili ya utafiti pamoja na kuwalipa watafiti wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhimize *Agro-processing* zaidi ili tupate zaidi pamoja na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 136 takwimu siyo sahihi kwani haijaongezwa pamoja na kuwa na upungufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nasisitiza uwajibikaji kwa kila mmoja wetu kwenye nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa hotuba nzuri ambayo imelenga utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za bajeti zinazopitishwa na Bunge zikiwemo zile za ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha za maendeleo 2,516,709.000 za ndani na 90,177,545,000 za nje, hizi za nje kwanini ziwe nyingi kiasi hiki. Naiomba Serikali kuliangalia kwa kina suala hili hasa kwa vile tuna mategemeo ya Kilimo Kwanza. Hivi

hizi za kutoka nje na zimewekwa nyingi kiasi hiki hivyo kama nje hawakutupatia hizo fedha tutaweza kuwa katika mategemeo gani?

Serikali lazima iangalie uwezekano katika kipindi kijacho kutenga fedha za maendeleo kutoka ndani ziwe nyingi kuliko zile za nje.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam kwa hotuba na bajeti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa chakula cha msaada unaotolewa katika maeneo yaliyokumbwa na ukame, Wilaya ya Kiteto ikiwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa mbegu na mbolea kwa wakati uzingatiwe. Pia kiasi cha kutosha kitolewe ili wakulima zaidi waweze kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa *DADPs* uratibiwe kwa karibu zaidi katika ngazi ya wilaya na iwe *monitored* kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *VADPs* ienezwe katika vijiji zaidi

Mheshimiwa Naibu Spika, *PADEP* katika ngazi ya wilaya ijengewe uwezo zaidi katika kutoa utaalam na mafunzo ya kilimo chenye tija.

**MHE. GERTRUDE RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo kwa hotuba nzuri.

Pongezi kwa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri ni kwamba, wakulima wapewe ardhi ya kutosha ili wazalishe mazao ya chakula na ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima Wasaidiwe kuunda vikundi vya Ushirika ili wawezeshwe na matrekta na mbegu bora na mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuandae *programmes* za kufundisha wananchi umuhimu wa Kilimo Kwanza (mashamba Darasa). Pia wakulima wasaidiwe kupata masoko ya mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujenge viwanda vingi kutengeneza mbolea nchini na tuboreshe miundombinu ili mazao yaende kwenye Mkoa ya njaa

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu wake na Wakurugenzi wetu kwa hotuba mzuri inayotia matumaini. Kilimo Kwanza ni ukombozi.



Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa chakula. Kwa ajili ya ukame mkubwa kuna njaa kubwa katika nchi yetu. Wilaya ya Rufiji Kata za Utete, Mkongo, Ngorongo, Mwaseni na Mtwara hawana chakula kabisa. Nimetoka Rufiji jana tarehe 21.7.2009, kuna njaa kali na watu wanakula matunda ya porini aina ya mkoche.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na kuomba uwakomboe wananchi wetu kwa kupeleka chakula haraka huko Rufiji. Katika kitabu cha hotuba ukurasa 138, Rufiji haijatajwa na ukitazama ukurasa 10, kuna wilaya zilizokwisha pata chakula cha msaada, Rufiji haipo. Sasa tunaomba Serikali ipeleke chakula Rufiji kwa haraka sana ili kuokoa maisha ya wananchi au wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matrekta, Rufiji inahitaji matrekta. Tunaomba Benki ya Kilimo itakayokuwa na masharti nafuu (riba ndogo sana mkopo muda mrefu miaka mine mpaka mitano ili wanunuwe matrekta kwa vile trekta hufanya kazi kwa zaidi ya miaka mitano, mkopo wa matrekta hayo utarejeshwa bila tabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umwagiliaji, ardhi ya Rufiji ina rutuba nyingi na ni kubwa. Mto Rufiji una maji mengi sana pamoja na mabwawa ya asili makubwa mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, sasa Serikali iache kigugumizi ipange mipango mikubwa ya umwagiliaji katika Wilaya ya Rufiji. Kufanikiwa kwa kilimo Tanzania ni kuanza kilimo cha matrekta na umwagiliaji mkubwa katika Wilaya ya Rufiji.

Serikali inatumia fedha nyingi kwa ununuzi wa mbolea kila mwaka na kupata asilimia kumi zao lakini mvua zikikosekana basi njaa inatuathiri kila mara. Historia ya Misri, Sudan na India hawa hawategemei mvua, wanamwagilia tu na hawana njaa. Tuachane na njaa kwa kuanzisha *mechanized farming* na umwagiliaji mkubwa Rufiji na tuachane na kumwagilia kidogo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. DR. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa natoa pongezi na hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Kilimo kwa kazi nzuri Wizara inayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa pongezi kwa wananchi wa Morogoro pia na Ruvuma kwa kazi nzuri wanayofanya ya kilimo. Wananchi wanajituma sana katika kilimo mpaka miko hii, imependekezwa kuwa katika miko sita kwa kutekeleza Kilimo Kwanza. Nawaomba wananchi hawa waendee kujituma kuzalisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo wanalia sana ni kupunguziwa au kuangalia ruzuku ya mbolea. Wakulima wamepokea kwa moyo mmoja vocha za

pembejeo, tatizo bado wanapata tabu ya kulipia hizo vocha licha ya kusaidiwa na Serikali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anaombwa aliangalie jambo hili ambalo naamini analiamini na kuliafiki na analifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo wakulima wanaomba ni kufika mapema kwa pembejeo hasa mbolea na mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkoa wa Ruvuma, tunaomba mbolea na mbegu zitufikie mara tu baada ya bajeti hii kupitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri fedha za kununua nafaka hasa mahindi kwa (SGR) ya Taifa zitumwe haraka iwezekanavyo, kwani walanguzi wananunua mahindi (hasa kutoka Ruvuma) kwa fujo na kasi, licha ya uongozi wa Wilaya na Mkoa kuweka sheria ndogo za kuwabana. Kwa hiyo, naomba kushauri na kuomba pia kuwa fedha tunazoziomba kama tulivyokwishandika barua Wizarani zitumwe haraka, zikatumike kununua mazao hayo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Waziri wa Kilimo, kuwa mambo yote yaliyoagizwa na Serikali tutayatimiza kama yalivyoagizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nawaomba wananchi wa Mkoa wa Morogoro na Ruvuma, wajitume na wazidi kuzalisha kwa bidii zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni Songwe kuna matatizo yafuatayo:-

Kati ya Kata 10 ni Kata tano tu ndizo zilizopata yale malipo ya madai ya wakulima na pamba. Fedha za Kata tano zilirudishwa Wizarani kwa sababu majina ya wadai hayakuwemo kwenye orodha iliyofika Wizarani. Nashauri utaratibu ufanyike kuwalipa wale wakulima wa pamba wanaoendelea kudai.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya chakula kwenye Jimbo la Songwe iendelee kufanyiwa tathmini kwa sababu baadhi ya maeneo yatakuwa na upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi utatuzi wa migogoro kati ya wakulima na wafugaji ni kutumia nguvu za dola, yaani hakuna mikakati mingine inayowezekana. Mfano, kwa nini Serikali isipeleke miundombinu kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho kwa mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. TEDDY L. KASELLA -BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kama wote tukienda kwenye vitendo na si maneno sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana wakulima wetu ambao wanalima katika hali ngumu na nyenzo za mwaka arobaini na saba, hasa wanawake wenzangu kwani bila chakula, hakuna mtu hata mmoja anaweza kusimama akafanya kazi, akafanya siasa na kadhalika na hakuna mtu atakusikia au atasikia kitu akiwa na njaa. Hivyo jambo la muhimu hapa, ni Kilimo Kwanza na vitengo hasa Kilimo Kwanza kwa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa tunapotaka Kilimo Kwanza ni kuipanga hii ardhi yetu, tugawe ardhi ya kilimo na ardhi ya mifugo na kadhalika kwa misingi hiyo, naamini mtu akipewa ardhi apewe na hati miliki ili mashamba yawe na hati miliki ya miaka 99 au 33 na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu akijua kwamba ardhi au shamba hili ni lake, akifa ni la wanae na wajukuu au watukuu zake, atalitunza. Naamini kabisa mkulima akiwa na shamba lenye hati miliki na apate wataalam wa kumuonyesha au apewe elimu ya kilimo, naamini, kilimo kitakuwa Kilimo Kwanza kwani hakuna mtu au mkulima au familia yake, atahama kuacha shamba lake, wakulima watalima kitaalam na vijana hawatatoka vijijini au shambani kwa sababu tayari hii ni ajira tosha kwao wanaorithi toka kwa wazazi wao na inawapatia chakula, ajira na mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtiririko huo huo hapo juu, wakulima wetu wapate elimu ya kilimo cha kisasa, wapate mbolea kwa wakati, wapate mbegu kwa wakati, naamini kabisa tutaikwamua nchi hii kwani asilimia sabini ya Watanzania ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba pia Wizara kwa kuwa ina fedha za kutengeneza barabara za kutoa mazao shambani kupeleka sokoni. Kwa misingi hiyo, naomba basi fedha hizi zisaidie barabara ya Jimboni kwangu, kutoka Maambali, kupitia Semembela kwenda Chambo Kahama. Naomba barabara hii itengenezwe ili mazao toka Maambali na Semembela, yapelekwe Chambo hadi Kahama na kuendelea Shinyanga , Mwanza au Dar es Salaam au Kahama mpaka Burundi. Vinginevyo basi zitengenezwe barabara zingine za aina hii kwa Majimbo mengine Tanzania, lengo kupeleka mazao toka shambani hadi sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hawa wanawahitaji sana wataalam kwa misingi hiyo, naomba ili kazi hii ya Kilimo Kwanza inoge, wataalam hawa walipwe mishahara na maslahi mazuri, ili wafurahie kazi yao na wala wasiwe wamangimeza, watoke wafanye kazi na wakulima. Mabwana Shamba wawe vijijini au shambani, sio mezani pamoja na marupurupu, mishahara minono. Naamini wataalam wetu wawe *practical* yaani watoe mafunzo na wafanye kazi, walime na wakulima wetu kitalaam. Hivyo tutafikia lengo la Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia na naomba kuwasilisha.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuchangia mjadala huu. Awali ya yote nampongeza sana Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na pia kutulelea hotuba nzuri. Pamoja na nia nzuri ya kutaka kuunga hoja mkono, naomba ufafanuzi kwa machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza, awali ya yote napongeza kwa dhiti kabisa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Baada ya pongezi hizo naomba ufafanuzi kwa haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kuwafikia wakulima vijijini ili kufufua mashamba yao? Ni maeneo gani yametengwa kwa kilimo kikubwa na cha kisasa kwa wawekezaji wakubwa ukiondoa ile mikoa sita? Kuna mkakati gani wa pamoja na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuendeleza Bonde la Ruvu, Kibaha na kwingineko?

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee njaa Kilimanjaro. Mwaka huu Mkoa wa Kilimanjaro umekumbwa na njaa. Naomba kupitia Bunge hii Tukufu Mheshimiwa Waziri awatangazie wananchi wa Kilimanjaro kiasi cha chakula kitakachopelekwa, Same, Mwanga, Rombo, Moshi vijijini, Hai na Siha. Tamko hili ni muhimu sana lifanyike mapema kwani hali halisi huko ni mbaya sana. Endapo Serikali haitafanya hivyo wale wanaobeza Serikali watalipatia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ushirika naomba kumfikishia Waziri kero ya kuanzisha *SACCOS* za kina mama huko Kilimanjaro. Binafsi nimekumbana na matatizo mengi sana wakati wa kuhamasisha uundwaji wa *SACCOS*. Kina mama wamekosa msaada kutoka kwenye ofisi husika na kukimbilia kwenye *VIKOB*A. Mfano kule Rombo Afisa Ushirika amekataa kuandikisha *SACCOS* ya akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Wizara hii itajitosa kutoa elimu kwa ratiba maalum ili wanawake wengi zaidi wajiunge kwenye *SACCOS*? Naomba majibu ya kina wakati wa majumuisho kwani sio nia yangu kusimamia kifungu cha mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Malipo ya wastaafu *TCB*. Ni zaidi ya miaka minne sasa wastaafu wa *TCB* hawajaweza kulipwa mafao yao. Jambo hili nililifuatilia kwa Mheshimiwa Waziri mwaka jana lakini hadi leo hakuna mafanikio. Wengi wa wastaafu hawa ni wanawake na tena ni wajane. Ni vema nitaje majina ya baadhi yao, mama Kimaro, Mama Kajembe, Mama Riwa na wanaume wachache. Naomba jambo hili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mbolea ya samadi. Kilimo cha Mkoa wa Kilimanjaro kwenye maeneo ya mlimani kinatumia zaidi samadi ya ng'ombe. Hapa natoa ombi rasmi la wakulima hao wadogo wadogo kupatiwa mbolea hiyo kwa wingi kwani ardhi sasa imechujuka sana. Kilimo hiki ni cha mseto *intercropping* ndizi na kahawa kwa pamoja. Tunaomba msaada wa mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa limetangaza sera ya Kilimo Kwanza na katika kukazia hilo taifa pia limeamua kuwa Mkoa wa Morogoro uwe ghala la Chakula kwa msimamo huu, maana yake Morogoro lazima sasa iweke mkazo katika mtindo wa kulima na kufanya mapinduzi katika zana za kilimo. Halikadhalika, Mkoa lazima sasa upange jinsi ya matumizi ya ardhi ya Mkoa wote. Ingawaje Mkoa mzima una miti mingi sana, mito hii haitumiki katika ukulima wa umwagiliaji maji. Hii itawezesha kulima wakati wa kiangazi. Jambo lingine muhimu kwa Morogoro ni kuhakikisha kwamba wananchi wa Morogoro wapate ardhi ya kutosha kwa kila mwananchi wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata ardhi lazima mkulima huyu apatiwe elimu juu ya kilimo bora na ufugaji bora zaidi. Kilimo bora ni pamoja na utenganisho wa ardhi ya kilimo na kufuga. Wananchi wa Morogoro siyo wafugaji, wafugaji wake ni wahamiaji wa Morogoro. Kama hawa wafugaji hawaendi Morogoro katika utaratibu unaofahamika basi juhudi hizi za kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la chakula ni ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wa Morogoro ni watu maskini sana. Hivyo, hawa wakulima wadogo maskini wakipelekewa matrekta makubwa na madogo hawawezi kununua zana hizo. Lazima kwa muda wa miaka fulani wananchi walime kwa *centre* za zana za vyombo vya kulimia kwa kukodishiwa vyombo hivyo kwa kulimiwa na kukatwa gharama wakati wa mavuno ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kuzingatia juu ya kilimo ni aina ya mazao. Ardhi hii ya Mkoa ina uweza wa kuzalisha aina nyingi ya mazao. Bahati nzuri Mkoa huu wa Morogoro una vituo vya kilimo vingi. Hali kadhalika kuna Chuo Kikuu cha *SUA*. Mkoa una vituo vya taasisi za utafiti vingi. Hivyo utalam huu wote ukitumiwa, hakuna sababu wazi ya Mkoa kushindwa kulima mazao ya aina aina katika Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada ya kulima vema lazima tukaribishe sekta binafsi. Kuna mambo mengi ambayo sekta binafsi ingeweza kusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ghala la Chakula kusiwe na maana ya mazao ya chakula tu, lazima hii iende sambamba na kuzalisha mazao ya biashara ili wananchi wa Morogoro waweze kutokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Morogoro wanaweza chini ya usimamizi wa busara kugawa aina ya mazao. Huu sio tu ushauri wa aina ya mazao bali pia mazao ambayo ni ya aina ya chakula na mazao ya biashara. Hii itaondoa njaa na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema nikazungumzia *FORMAGATA* ambayo ni msimamo wa Morogoro kuwa ghala la chakula. Lakini *FOMAGATA* kuweza kufanikiwa, lazima Serikali Kuu ianze kwa kuwekeza kwa kiasi kikubwa. Udongo wa Morogoro haulimiki kwa *power tiller*, hivyo hapa uzito utiwe kwenye matrekta makubwa. Matrekta haya ni ghali lakini Serikali inaweza kupangilia vema jinsi ya matumizi ya zana hizi. Hali kadhalika lazima Mkoa uitumie sana *SUA* na vyuo vingine vyote ambavyo vipo Mkoani humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikoa iliyoamuliwa kuzalisha mazao kuweza kujaza Ghala la Taifa lazima bei za mazao yao iangaliwe vema. Bila ya motisha ya bei basi wakulima hawatapata hamasa ya kulima zaidi na kushiriki vema katika *FOMAGATA*. Lazima mkulima mwenyewe aione *FOMAGATA* ni mali yake na Serikali inasaidia tu katika kuiendesha *FOMAGATA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya watumishi wangu wa Jimbo la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa M. Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. David Mathayo kwa kazi nzuri inayofanyika katika Wizara hii. Kipekee naipongeze sana hotuba nzuri na uchambuzi wa kina ambao umetolewa katika hotuba hio.

Ningependa pia kuchukua fursa kuipongeze sana *TACRI* yenye Makao yake Makuu Wilayani Hai – huko Lyamungo kwa kazi nzuri inayofanywa na taasisi hii. Ni maoni yetu sisi watu wa SIHA kwamba kazi inayofanywa na *TACRI* chini ya Prof. Terry ni yenye kutia moyo na kupongezwa sana. Tumenufaika sana na matokeo ya utafiti yanayotuelimisha kwa karibu namna ya kufufua zao la kahawa kwa kutumia miche ya kisasa ambayo inastahimili magonjwa kama *CBD* na *leaf rust*.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yetu ni kwamba Sh. 700,000,000/= zilizotengwa kwa ajili ya taasisi hii hazitoshi. *TACRI* inafanya utafiti wa kilimo cha kahawa nchi nzima. Wakati huo huo wanaandaa vitabu vya kuwapatia wananchi miche bora nchini kote. Kuna gharama za uendeshaji na kadhalika. Ni maoni yangu/yetu kwamba kuzingatia majukumu makubwa waliyonayo *TACRI* pamoja na yale ambayo sikuyataja, kama vile pembejeo na kadhalika, kuna haja ya kuwapatia angalau Sh. 1,000,000,000/= ili waweze kuboresha na kutekeleza majukumu mazito waliyonayo.

Kwa mara nyingine narudia kutoa pongezi kwa Wizara kwa kazi nzuri.

**MHE. CLEMENCE BEATUS LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Kilimo, Chakula, na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kuiandaa hoja ya bajeti iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, itekelezwe na itoe matunda, ni budi Serikali iamue, maeneo yanayofaa kwa kilimo cha mazao tu yatumike kwa kilimo tu, yanayofaa kwa kilimo na mifugo, yatumike kwa kilimo na mifugo na maeneo yanayofaa kwa mifugo tu, yatumike kwa mifugo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hii, katika mpango wa mradi wa *FAMOGARA*, Mkoani Morogoro, ukweli ni kwamba Wilaya ya Kilosa inafaa iamuliwe moja kwa moja kuwa na eneo la kilimo cha mazao ya chakula tu. Mifugo ya kibiashara isiruhusiwe isipokuwa ile ya wafugaji asilia walioishi miaka mingi. Wafugaji hawa wanajulikana kwa majina na idadi ya mifugo yao na wafugaji hawa wa asili endapo idadi ya mifugo yao imezidi kiwango kulingana na eneo walilopewa kwa malisho hawana budi kulazimishwa wapunguze idadi ya mifugo iliyozidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia hii eneo linalofaa kwa kilimo cha mazao ya chakula au biashara litazalisha mazao kwa ufanisi mzuri na kufanikisha sehemu yao ya uzalishaji mazao chini ya mpango wa *FAMOGATA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, ilisimamie suala la kuwaondoa wafugaji waliozidi katika eneo Wilaya ya Kilosa. Napenda kumwuliza kama Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika ana taarifa kuwa miundombinu ya skimu umwagiliaji ya kilimo cha mpunga katika shamba la Kilangali (Kata ya Kilangali) ambayo Wizara ilikarabati mwaka 2006/2007 kwa gharama ya zaidi ya Sh. 120 milioni imeharibiwa yote, vibaya sana na wafugaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa skimu hii, wakulima wanaweza kulima mpunga misimu miwili na kuzalisha mpunga kwa wingi sana. Huu ni mchango mkubwa sana katika uzalishaji wa mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na athari za uharibifu uliofanywa na wafugaji namwomba sana Mheshimiwa Waziri alithibitishie Bunge lako Tukufu kama anajua uharibifu uliotokea katika skimu ya umwagiliaji Kilangali na hatua ambazo atachukua kurekebisha uharibifu uliotokea ili kuongeza uzalishaji wa mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili wananchi wengi nchini waweze kuelewa na kutambua kuwepo kwa Mfuko wa Pembejeo na taratibu za kukopa fedha katika Mfuko huo, Wizara ya Kilimo iongeze kuutangaza zaidi katika *Radio*, runinga na magazetini.

Matangazo haya yataongeza hamasa miongoni mwa wananchi na hasa vikundi vya kiuchumi ambao wengi hawajui sana kuwepo na taratibu za Mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi katika maeneo mengi pamoja na Jimbo la Mikumi wanalalamika kuhusu urasimu mkubwa kuhusu mlolongo mrefu na vikwazo mbalimbali katika kufuatilia kupatikana kwa pembejeo tangu mwombaji anapokamilisha vigezo vyote vya kumruhusu kufikiwa hadi atakapoupata mkopo huo. Namwomba Mheshimiwa Waziri, akitupie macho kitengo kinachohusika na Mfuko huu, ili kuwahimiza na kuwaonya juu ya malalamiko dhidi ya utendaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadri muda unavyoendelea hivi sasa, bila Serikali kutoa uamuzi kuhusu kurejeshwa tena zoezi la kuwahamisha wafugaji waliozidi katika maeneo ya Kilimo cha Mazao ndivyo kiwango cha uharibifu wa mazingira unavyoongezeka na mazao ya wakulima yanavyozidi kuliwa na upungufu wa chakula unavyoongezeka pamoja na vurugu baina ya wakulima na wafugaji. Namwomba Mheshimiwa Waziri asisitize suala hili Serikalini ili uamuzi wa kurejeshwa zoezi la kwaondoa wafugaji waliozidi katika maeneo waliyovamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni katika kijiji cha Kikenke katika Wilaya ya Kilosa, kijana mmoja mkulima kapigwa na wafugaji na kujeruhiwa vibaya sana bila sababu ya msingi. Inasemekana watuhumiwa wamekamatwa. Hali kadhalika katika kijiji cha Kilangali, Bwana Shamba akiwa anaendesha pikipiki akitoka kazini, alikimbizwa na wafugaji waliokuwa pia wakiendesha pikipiki na kumsababishia atumbukie katika mtaro na kuumia vibaya. Hali hii ni mbaya, wakulima na wananchi katika maeneo ya wakulima wanaishi kwa hofu kubwa na kusita kwenda kuhudumia mashamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza, kweli kitafanikiwa? Huku wingu la hofu limetanda katika mioyo ya wakulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii haiwezi kuvumilika, ni budi Serikali itambue umuhimu wa kufikia haraka uamuzi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni nimepokea ombi toka kwa baadhi ya wakulima wa miwa kutoka Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa, niwasilishe lalamiko kwao kuwa, kiwanda kinawapunja sana malipo yao ya miwa. Wakulima wa Mtibwa wanadai kuwa wanalipwa bei ya tani ya miwa ambayo ni pungufu kwa zaidi ya sh. 10,000/= ikilinganishwa na bei kwa tani wanayolipwa wakulima wa Kilombero *Sugar Company Limited*. Si hilo tu, bali malipo yao hucheleva hadi miezi mitatu kwa wastani.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo kuhusu hali hiyo ili iboreshwe kwa lengo la kuinua kilimo cha miwa ili kupunguza upungufu wa uzalishaji wa sukari nchini. Naamini Mheshimiwa Waziri atazingatia mapendekezo na ushauri uliomo katika mchango wangu. Kwa maana hiyo, naunga mkono hoja.



**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii pamoja na mashirika yote yaliyo chini ya Wizara kwa matayarisho mazuri ya hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Kilimo Tabora – Tumbi, ni moja ya Vyuo vya utafiti chini ya Wizara ya Kilimo hapa nchini ambacho kinafanya kazi nzuri. Naomba kiwezeshe kwa kuwa na bajeti ya kutosha kukidhi mahitaji yake muhimu hususan miundombinu mbalimbali pale chuoni kama vile madarasa, mabweni, maktaba, upatikanaji wa maji safi na salama kwa haraka. Chuo hiki kimekwama kuanzisha mradi wa kilimo cha kumwagiliaji kama sehemu ya somo kwa wanafunzi. Tatizo ni fedha kwa ajili ya mradi huu. Naiomba Wizara ikisaidie chuo kuweza kukamilisha mradi wake wa kilimo cha umwagiliaji pale chuoni haraka iwezekanavyo

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za matrekta, napendekeza Wizara isimamie kwa karibu upatikanaji wa matrekta katika maeneo mbalimbali kwa kupitia vituo maalum vitakavyoanzishwa kwa ajili ya matrekta ya kukodisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima katika Jimbo la Tabora Mjini wanalalamikia utaratibu wa kutoa mbolea ya ruzuku katika baadhi ya maeneo hapa nchini ambayo Tabora haimo. Naomba sana mwaka huu Tabora nayo ipatiwe mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kilimo na Viwanda. Kilimo Kwanza bila viwanda haiwezekani. Kuna mahusiano ya karibu sana baina ya baadhi ya viwanda na kilimo. Ili kilimo kiendeleo haraka ni lazima viwanda vinavyozalisha mahitaji ya sekta ya kilimo navyo viendelezwe. Baadhi ya viwanda hivyo ni viwanda vya zana za kilimo, viwanda vya pembejeo mbalimbali, viwanda vya bidhaa mbalimbali ambavyo ni mahitaji muhimu ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbolea ya Minjingu inalalamikiwa na baadhi ya Wabunge kuwa haifai. Je, Wizara inasemaje juu ya malalamiko haya? Je, vyuo vyetu vya utafiti kilimo vimekwisha utafiti ubora wa mbolea hii? Kama vimekwishafanya utafiti wa mbolea hii, nini matokeo ya tafiti hizo? Nashauri Serikali ishughulikie suala hili kisayansi na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina bahati ya kuwa na mbolea ya Minjingu ambayo inaweza kutumika kama mali ghafi kwa kutengeneza aina nyingine hapa nchini kwa kuichanganya na gesi asilia. Tuhakikishe utengenezaji wa mbolea ya aina nyingine kama vile Minjingu pamoja na gesi asilia unatekelezwa haraka kwa manufa ya uchumi wetu. Hatuna haja ya kuendelea kuagiza mbolea hizi toka ng'ambo.

**MHE. MAGDALENA A. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kusimamia Wizara hii na kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya mbolea, Serikali ihakikishe inatumia wataalam wake kufanya utafiti kabla ya matumizi ya mbolea ya aina yoyote kwa zao lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo mengi ardhi imekuwa inaharibika na kupoteza rutuba yake baada ya matumizi ya mbolea za viwandani. Wakulima wa matunda na mboga mboga kwa kutumia mbolea wamekosa masoko kwenye mahoteli ya ndani hata ya nje kwa sababu ya chumvi chumvi zinazokuwepo kwenye mazao hayo. Mbolea nyingine zimetumiwa zikakausha mazao mashambani na hivyo kuletea wakulima hasara kubwa. Haya yote yanaonyesha kwamba bado Tanzania tupo nyuma katika suala la utafiti. Tusilime kwa kujaribu au kwa majaribio, tuwe na uhakika na kilimo chetu. Je, sisi ambao ni walaji wakubwa wa mbogamboga na matunda yanayozalishwa kwa kutumia hiyo mbolea tunapata athari gani kiafya?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za *ASDP* kwa miaka 3 sasa zimetumika bilioni 198.6 sawa na asilimia 34.42 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya bilioni 578.6 kwa kipindi hicho. Kwa *speed* hii hatuwezi kuleta mapinduzi ya kilimo tunayoyategemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za *DADPs* haziendi kwa walengwa. Zaidi ya 808 inaishia kwenye posho, semina, makongamano, mafuta na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mashamba darasa yanayoanzishwa kama mifano hai kwa wakulima kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wa kilimo kwenye Halmashauri pamoja na Wakurugenzi hawasimamii vizuri fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri wanasema Serikali Kuu ndio wametoa mwongozo wa matumizi ya fedha hizo. Kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuleta mapinduzi ya kilimo huku wanatoa miongozo isiyokuwa na tija kwa fedha za kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo cha Mibono (jiotrofa) hapa nchini kimeanza kushika kasi. Maeneo makubwa, ardhi yenye rutuba yameanza kulimwa mibono. Je, Serikali imefanya utafiti wa kutosha hususan na zao hili la nishati? Tuna uhakika kwa kilimo hiki kitakuwa endelevu? Tusije rukia tu mpango huu tukajikuta tunaharibu ardhi ya mazao ya chakula kwa ajili ya mibono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetamka hapa Bungeni kwamba bei ya tumbaku kwa Tanzania imepanda kwa asilimia mia moja. Hili siyo kweli kwa maeneo yote. Kwa Wilaya ya Iramba na Mkoa wa Tabora bado bei ya kilo ya tumbaku wastani ni Sh. 2500/= hadi 2200/=. Hapo bado hajakatiwa gunia, kila belo moja anakatwa 500/= kwa ajili ya gunia. Bado hajakatiwa miche ya miti ya magunia, kila mfuko mmoja wa mbolea anakatwa Sh. 100/= kwa ajili ya mche wa mti. Tatizo hapa ni Makampuni ya tumbaku ambayo Serikali imeendelea kuyalea na hivyo kuuza mbolea bei wanayotaka, kununua tumbaku bei wanayotaka. Mikataba hii mibovu lini itarekebishwa? Serikali iondoe *monopoly* kwa biashara ya zao la tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa tumbaku Wilaya ya Urambo hawajalipwa fedha zao tangu mwezi wa tano 2009 hadi leo. Wakulima wa Kata ya Usinge, Kiloleni na kadhalika. Wamefuatilia kwa muda mrefu bila mafaniko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo ya kwanza walikatwa pembejeo, soko la pili wameuza hakuna hela. Kwa muda wa mwaka mzima mkulima anategemea auze mazao yake apate pesa. Leo kwa nini Makampuni haya yanakopa wananchi maskini? Watalipa lini?

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nampongeza sana Waziri Mheshimiwa Wasira kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Wizara hii nawapongeza Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu bila ya kuwasahau watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla kwa kujitahidi kutuma ndege ya kuangamiza ndege wajulikanao kama Kwelea kwelea katika Wilaya yetu ya Singida. Kwa kiasi fulani ndege hiyo iliwapa afueni wakulima wetu ingawa haikutatua tatizo kwani ilikaa muda mfupi ikaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo inaelekea ni ndege yenyewe kuwa ni moja tena naambiwa ni ndege ya kukodisha, hivi Serikali haioni umuhimu wa kununua ndege zetu wenyewe angalau tatu au nne? Hivi Serikali haijui athari kubwa inayowapata wakulima kwa mazao yao kuliwa na kwelea kwelea? Hivi tutaendelea kukodi ndege hadi lini? Naomba sana Serikali inieleze, ina mpango gani wa kununua ndege ya kuangamiza ndege waharibifu? Aidha, ndege aina ya Silingu bado ni tatizo kubwa la muda mrefu. Wananchi hawaoni jitihada za Serikali kuhusu ndege hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Singida tumeanza kufaidika na zao la alizeti kama zao la biashara. Naomba wakulima wasaidiwe mbegu bora, utaalam pamoja na soko la nje ili wananchi wanufaike zaidi. Je, ni lini Bodi ya Mazao Mchanganyiko itaundwa? Kwani ikiundwa itawasaidia wananchi kiutaalam pamoja na kutupatia bei nzuri na soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Maofisa Ugani ni tatizo kwa maana ya kwamba ni wachache katika Kata na Vijiji hawatoshi. Aidha, baadhi yao hawapendi kukaa vituoni mwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DANIELI N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha kilimo cha Bugaga, *Status* yake ikoje? Ni kiasi gani Wizara imetenga kwa ajili ya kituo hiki? *Bugaga Agriculture Centre* inafanya utafiti, inasambaza mbegu na kufundisha wakulima. Kwa kuwa ni kituo cha Kitaifa, napenda kufahamu *strategy* ya kuendeleza mazao mapya ya biashara, mboga, matunda na viungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao jipya Numbu lilimwalo katika Wilaya ya Kasuli . Tafadhali Wizara ifanye utafiti wa zao hili ili lisipotelee na ni zao zuri la chakula na kiburudisho. Nashauri Wizara kupitia Halmashauri ya Wilaya kufanya utafiti wa kina juu ya zao hili litumwe kibiashara na baadaye tuliuze nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nguzo 10 za kuharakisha Mapinduzi ya Kijani. Nguzo hizo kumi zipo wapi? Naomba sana Wizara iainishe nguzo hizo na tuletewe Bungeni ili iwe ni elimu kwa Wabunge, maombi yaliyoainishwa uk 75 -78 ni wazi siyo nguzo bali ni mambo ambayo yataweza kusaidia Mapinduzi ya kijani kwa mfano Kilimo Kwanza, kutambua kuwepo viwanda ndiyo moja ya nguzo hizo? Nafikiri Wizara iainishe mambo ya msingi yanayoweza kutusaidia kutoka hapa tulipo kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za ugani na kuanzisha *ward agricultural resource centres*. Fikra hii ni muhimu sana, wekezeni katika eneo hili. 2.52 bilioni za kuwezesha au kuratibu, Sekretarieti za Mikoa wekeza katika huduma za ugani na 21.9 billioni pia katika ukurasa wa 79 wa hotuba.

**MHE. ADAM K.A. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa idhini yako nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mzee Wasira na Naibu wake Mheshimiwa Dr. David Mathayo kwa kazi nzuri sana wanayofanya. Aidha, naomba nimpongeze Katibu Mkuu Bwana Mohamed Muya na watendaji wote wa Wizara hii na sekta hii katika ngazi zote. Aidha, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kukubali kufika Jimboni kwangu na kuzungumza na wananchi wa Kata ya Magawa kwa ajili ya kujionea matatizo yanayowasibu wakulima wa korosho kwa sababu ya matatizo katika mauzo ya zao la korosho na matatizo mengine yote husika ya zao hilo kwa wananchi wa Mkuranga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la korosho Mkuranga ni tatizo la Mkoa wa Pwani. Kama wazalishaji wakuu wa zao hili kuu la Mkoa wetu, usugu wa tatizo hili miaka hadi miaka umewafanya wananchi wa Mkoa wa Pwani kukosa imani na mfumo na vyombo vinavyosimamia zao hili. Hali hii ni ya kuhuzunisha sana kwa kuwa Mkoa wa Pwani una uwezo wa kuzalisha mpaka tani 50,000 za korosho kwa kuchukua hatua za makusudi za kuwekeza kwenye mbegu bora, pembejeo na elimu ya umma, badala ya uzalishaji wa sasa wa tani 15,000 tu.

Mfumo wa kugawa pembejeo, unachangia kuzorotesha uzalishaji kwa kuwa kila msimu sisi wa Mkuranga na pwani, tunapokea *sulphur* mwezi Septemba wakati matumizi ya *sulphur* yanatakiwa yaanze miezi ya Juni na Julai. Aidha, Bodi ya Korosho inaonekana kuwa na kazi kubwa zaidi katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Wilaya Tunduru. Naomba Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi wa Mkuranga na wakulima wa Pwani kwamba Bodi ya Korosho, itaelekeza nguvu za ziada msimu huu ili kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa stakabadhi ghalani ambao unatumika kuuza mazao, haswa zao la korosho kusini umepata mafaniko makubwa. Waziri wa kilimo ametoa kauli hadharani kwamba mfumo huu utanza kutumika Mkoa wa Pwani

mwaka huu wa 2009/2010. Naomba Waziri anihakikishie na wananchi wa Mkuranga na Kisarawe, Rufiji, Kibaha na Bagamoyo kwamba Wizara itatenga pesa kwa ajili ya kuendesha elimu kwa umma ili mfumo huu usipate matatizo katika utekelezaji wake msimu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze na wananchi wasikie kule Mkuranga, kwamba taasisi ya Naliendele kitengo cha kuboresha zao la korosho kitapatiwa fedha na utaalim ili kuzalisha mbengu bora (miche ya kisasa) ya korosho siyo chini ya milioni 1 na Halmashauri zetu zikopeshwe miche hiyo na waagizwe Maafisa Ugani wasimamie elimu na upandaji wa miche hiyo Mkuranga, ambapo tuna maeneo na Kaya za kutosha. Miche milioni mbili ikisimamiwa vizuri ndani ya miaka minne itakuwa imezalisha kati ya tani 40,000 hadi tani 50,00. Thamani ya kuzalisha miche milioni moja ni shilingi za Tanzania bilioni 2.5. Tani 40,000 za korosho kwa bei za mwaka huu (kwa wastani wa Sh. 550/= kwa kilo) ni shilingi bilioni 22.5. Naomba kwa maana hiyo, niombe Wizara iwekeze fedha hizo za kiasi cha shilingi bilioni tatu kwenye zao la korosho, Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Mkuranga, nikisisitza kwamba ndani ya miaka minne wakulima watakuwa wamerejesha fedha zilizotumika kwenye uwekezaji, hata kwa njia ya tozo kwenye zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nimsihi Waziri wa Kilimo atenge fedha na utaalim ili kuunga mkono mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mazao mbadala, ya matunda na haswa maembe ya kisasa ambayo yana soko la uhakika nje ya nchi pamoja na zao la mhogo, ambalo nalo lina soko kubwa la wazi Ulaya na nchi za Asia. Wananchi wa Mkuranga wana asili ya kilimo cha mazao hayo na ya matunda kama mazao mbadala ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ifanye jitihada ya makusudi ya kusimamia matatizo ya ushirika na udhaifu unaojitokeza wa viongozi wa vyama hivyo hali inayodumaza juhudi za wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapa ndiyo mwisho kwa kuchangia kwa upande wa Wabunge.

Sasa Mheshimiwa Lwanji, amemletea Mheshimiwa Spika hii paketi ya sigara inaitwa *Portsman*. Yeye anasema ilikuwa inaitwa *Sportsman*. Sasa bahati nzuri hili Bunge lina watu wa aina zote, kuna Mheshimiwa Victor Mwambalasa yeye amekuwa mfanyakazi wa Kampuni ya Sigara Tanzania kwa miaka 30, amestaafu mwaka huu. Anasema Kampuni imeamua kutohusisha michezo na sigara, hivyo jina la *Sportsman* limebadilika na kuitwa *Portsman*. Kwa hiyo, hiyo sigara ni sahihi, ni ile ile. Kwa hiyo, napenda ijulikane kwamba hakuna sigara *fake*, ni sigara ile ile, wamebadilisha jina lao kutoka *Sportsman*, wameamua iwe *Portsman*. Kwa hiyo, naomba tu watu waiamini, labda kule kunukia, kama hujui kuvuta, hujui inanukia vipi. Kwa hiyo, ni sigara halali, naomba hii ieleweke hivyo msije mkaharibu soko la watu la biashara hii, ni sigara halali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, naona nimwalike sasa Mheshimiwa Naibu Waziri aendelee na kuanza kujibu hoja za Wabunge, yeye atapewa dakika 15.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na busara za kuweza kuwa kiongozi katika *level* yangu hii na kuwa Mbunge wa Jimbo la Same Magharibi. Namshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniingiza kwenye siasa, namshukuru Waziri Mkuu, kwa kutuongoza kila siku na Waziri wangu, Mheshimiwa Wassira, kwa kuwa kiongozi wangu wa karibu na kiongozi wangu mzuri na kiongozi wangu kwa kweli anayejali maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Same Magharibi, kwa kuniingiza Bungeni, nashukuru pia familia yangu kwa kuwa nami kila siku na kunitia moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaenda moja kwa moja kwenye hoja kwa sababu muda niliopewa, ni mdogo kwa taratibu zetu tulizojiwekea humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja kwamba huduma za ugani ziimarishwe, nadhani sisi sote katika Bunge letu hili tunaelewa kabisa kwamba Serikali inaendelea na mkakati wake wa kuendelea kuajiri na kufundisha Maafisa Ugani kusudi ifikapo mwaka 2011/2012, tuwe na Maafisa Ugani 11,700 ambao wameajiriwa au ambao wamefundishwa kusudi tuweze kupata Maafisa Ugani 15,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitendea kazi, *DADPs* inaendelea kuwapatia Maafisa Ugani hususan pikipiki. Kwa mfano, mwaka 2008/2009, zilinunuliwa pikipiki 248, baiskeli 710, magari 10 pamoja na nyumba 58 zilijengwa. Hadi Juni mwaka huu, walijiriwa Maafisa Ugani 1058 ambao wamepelekwa katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini. Wizara yetu hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika inahimiza Halmashauri kujenga Vituo vya Rasilimali kwa ajili ya kuwaelimisha wakulima mbinu na taratibu bora za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Prof. Sarungi, aliomba kupatiwa Maafisa Ugani, napenda kumfahamisha kwamba tutampatia Maafisa Ugani 10 kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, tutawaandikia barua mapema iwezekanavyo kusudi naye aweze kupata 10 kule Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, tunanzisha na tunaendelea na Mashamba Darasa ambayo yalishakwisha kuanzishwa na mwongozo kuhusiana na Maafisa Ugani pamoja na Mashamba Darasa, tayari unasambazwa kwenye Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwapatia wahitimu mazoezi kwa vitendo, yaani wale wanaomaliza sasa hivi wapatiwe mazoezi kwa vitendo, napenda kulifahamisha Bunge kwamba mwaka huu tutapeleka wahitimu 1,999 katika Wilaya 64 na kwenye Mikoa 14 kwa ajili ya kupata mafunzo, lakini pia kutoa maelekezo kwa wakulima, mbinu bora na taratibu bora za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwapatia Maafisa Ugani *uniform*, Wizara yangu pamoja na TAMISEMI, tutashirikiana tuangalie ni jinsi gani Maafisa Ugani hawa watapatiwa *uniform* ili waweze kufanya kazi zao kwa usalama zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchakavu wa vyuo na vitendea kazi pamoja na mitaala dhaifu ya Vyuo vyetu vya Kilimo, napenda kulifahamisha Bunge letu Tukufu kwamba katika kuwafundisha hawa watalaam wa ugani, tunahakikisha kwamba Vyuo vyetu 14 vyote tunaviboresha kwa maana ya kukarabati, kuvipanua na kuvipatia zana bora za kufundishia. Kwa hiyo, suala hilo tulishalianza tangu tuanze Programu hii mwaka 2007/2008. Mpaka sasa hivi tumeishapata wahitimu 1,402 na mwaka huu wa 2008/2009, tunategemea kupata wahitimu 2,327.

*(Hapa minong'ono ya Wabunge ilisikika)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, punguzeni namna ya kuongea, sasa inakuwa kama tunashindana na anayetoa majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010, tunategemea tutapata wahitimu 3,000. Vile vile sasa hivi bado tunaendelea kuchukua wanafunzi ili waweze kusoma katika Vyuo vyetu hivyo 14 nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mabwana Shamba kusambazwa nchi nzima, kama nilivyosema tutawapeleka 1,999 nchi nzima katika *practical* zao, lakini pia kutoa maelekezo kwa wakulima katika Mikoa 14 na Wilaya 64.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha *Horticulture* Tengeru kuwezesha, tumezingatia suala hili na tunakikarabati, tunaajiri Wakufunzi na tunaandaa mitaala mipya na vifaa vya kufundishia vinapelekwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Mkakati uwepo wa Tafiti za Mazao mbalimbali ili kusaidia kuongeza uzalishaji wa mazao. Napenda kulifahamisha Bunge letu Tukufu kwamba Wizara imeishaanzisha Mifuko ya Utafiti ya Kanda na kila Kanda imeweka vipaumbele katika mazao ambayo yanazunguka maeneo hayo. Mifuko hiyo inaitwa *Zonal Agricultural Research Development Funds*.

Mheshimiwa Naibu Spika, zabibu katika Mkoa huu wa Dodoma, Wizara kupitia Kituo chake cha Utafiti kilichoko Makutopora, inafanya utafiti wa aina bora ya mizabibu. Lakini pia mwaka 2007/2008 aina mbili za mizabibu ziligunduliwa ambazo zinaitwa Cheni Nyeupe pamoja na Makutopora *Red*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa mfumo wa upatikanaji wa maji Ukiriguru, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa mradi huu wa maji uliokuwa unagharamiwa na *Stabex* ulianza mwaka 2006/2007, lakini viwango vyake vilikuwa vya chini sana. Kwa hiyo, kukawa na tatizo kidogo, kukawa na kaugomvi kidogo. Sasa hivi taratibu za kupatanisha Wizara ya Fedha pamoja na Mkandarasi huyu zinaendelea. Punde zitakapokamilika na tuna uhakika kwamba mwaka huu ujenzi wa mfumo huo wa maji utaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mlingano katika Chuo chetu cha Kilimo kule Tanga, ni kwamba fedha shilingi milioni 52 zimeishapatikana na ameishalipwa *TANESCO*. Kwa hiyo, ujenzi wa *Pump House*, tunatazamia utakamilika katika bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Funza Mwekundu kule Kusini, utafiti ulianza mwaka 2004 na sasa hivi umeshakamilika na matokeo ni kwamba Funza Mwekundu bado yupo na kwa hiyo, Uchambuzi wa Kiuchumi (*Cost Benefit Analysis*) umeonyesha kwamba mkulima akilima bila dawa, kwanza atapoteza mazao yote, lakini pia akitumia dawa hataweza kurudisha gharama zake. Kwa maana hiyo, mpaka sasa hivi Funza Mwekundu huyo yupo, maeneo hayo hayafai kulima pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa ya mihogo, kuna magonjwa yanaitwa Batobato na Michirizi Kahawia, utafiti umeonyesha kuwa mbegu saba zina ukinzani wa Batobato na mbegu mbili kati yake zina ukinzani dhidi ya Michirizi ya Kahawia na utafiti bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa Mnyauko wa Migomba, utafiti unaendelea katika Kituo chetu cha Maruku kule Kagera na tunaziomba Halmashauri zitenge fedha za mafunzo kwa ajili ya wakulima ili waweze kuelimishwa vizuri ni jinsi gani tunaweza tuka-*control* ugonjwa huu usisambae zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Waziri Mkuu kuboresha barabara ya kutoka kwenye barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya kuelekea kwenye Chuo cha Kilimo cha Uyole, itatekelezwa mwaka huu. Barabara hiyo itakarabatiwa vizuri kusudi Chuo kile kiweze kufikika kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge alipenda kujua kiasi gani cha fedha kimetengwa kwenye utafiti mwaka 2009/2010. Kiasi hicho ni shilingi bilioni 25. Kimeongezeka, kama nakumbuka tarakimu za mwaka jana zilikuwa chini kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya mbolea ya Minjingu, kama nilivyokuwa ninasema hapa na kama vile nilivyokwishasema hapa Bungeni siku za nyuma, ni kwamba mbolea hii, kirutubisho kinachotakiwa pale ni *Phosphorus* sawa na ile *Phosphorus* inayopatikana kwenye *DAP*. Kinachotakiwa katika mbolea hii ya Minjingu ambayo inaitwa *Rock Phosphate* kwa sababu inatoka kwenye *rocks*, ni kuhakikisha kwamba tunatumia mbolea hii maeneo ambayo *PH* yake iko chini ya 5.5. Watalaamu wetu wa



Kilimo katika Halmashauri zetu, wanaelewa hili kwa sababu tulishazijulisha Halmashauri zote kupitia kwa ma-RAS wote tangu mwaka jana. Kwa hiyo, maeneo ambayo hayafai mbolea hii ya Minjingu, yatapelekewa ruzuku ya *DAP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utafiti lazima ufanyike, tusikatae mbolea yetu hii ambayo tunaizalisha ndani ya nchi na ni kiwanda pekee ambacho tunacho, ni lazima tulinde viwanda vyetu vya humu ndani. Tulinde kwa kuboresha lakini siyo kulinda kwa kukataa. Utafiti unaendelea katika maeneo yale ambayo yalionekana kama hayafai kwa mfano kwa maeneo kama ya Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa minazi, kuna ugonjwa unaitwa *Leffo Disease*, kituo chetu cha Mikocheni sasa hivi kimekwisha shughulikia. Tumepata miche mizuri ambayo inaukinzani wa magonjwa katika kituo chetu cha kule Bagamoyo. Miche hii inapatikana na ninazishauri Halmashauri ambazo ziko kwenye maeneo wanayolima minazi basi waweze kutoa fedha kutoka kwenye *DADPS* ili kutoa mafunzo pamoja na kuanzisha vitalu vizuri kwa mbegu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za kuendeleza zao la korosho. Tutaendela kutoa ruzuku katika zao hili na Bodi ya Korosho pamoja na Naliendele wataendelea na utafiti kwa ajili ya kuendeleza zao hili katika maeneo ya Dodoma, Singida na Kigoma. Tutaendelea pia kutoa mafunzo ya kubangua korosho kwa vikundi vidogo vidogo hata kwenye viwanda vikubwa ili kusudi tuweze kuuza korosho yetu ikiwa imeshabangukiwa kuongeza *value* na kuongeza bei zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa stakabadhi wa mazao ghalani bado utaendelea mwaka huu na tunaziomba *DADPs*, zisaidie kuendeleza zao hili la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za *export revenue*, zinachanganywa na ruzuku ya pembejeo. *Export revenue* ni mali ya Halmashauri lakini Halmashauri husika pamoja na wadau wa maeneo hayo, katika kikao cha wadau kilichofanyika Mei mwaka 2005 na February mwaka 2009, waliomba kwamba fedha hizi za *export revenue* zinavyorudi Halmashauri zisaidie kuendeleza zao la korosho kwa maana ya kuongeza pembejeo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha ruzuku kinachotengwa na Serikali kiwekwe wazi. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Bodi hutangaza kiasi cha fedha za ruzuku zinazotolewa kwa ajili ya korosho. Bodi hutangaza pia zabuni lakini Halmashauri huteua mawakala ambao watapeleka pembejeo maeneo yanayohusika na zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya korosho ni ndogo au haieleweki. Bei ya korosho haipangwi na Serikali. Bei ya korosho inapangwa na soko, ile *pressure* ya soko ndio inayopanga bei. Kama bei ya soko la dunia ni nzuri basi hata bei ya korosho hapa nchini itakuwa nzuri kwa sababu bei inapangwa na soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa stakabadhi wa mazao ghalani, nao utatusaidia katika kupandisha bei kwa sababu korosho inapowekwa ikisubiri bei maana yake ni kwamba ushindani utakuwepo kwa wale wanunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Mazao ziruhusiwe kukusanya ushuru ili iwe motisha kwa kukusanya mapato zaidi. Serikali inapokea na tutaufanyia kazi ushauri huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha mkonge kifufuliwe, napenda kukujulisha kwamba tunaendelea kwa nguvu kabisa kupitia Bodi yetu ya Mkonge kukifufua kilimo hiki na tunahamasisha wakulima wadogo wadogo kujiunga na tunafufua kilimo hiki Kanda ya Ziwa na tunatayarisha *Programme* mbalimbali kwa kutumia *OXFAM* kule Shinyanga ili tuweze kuongeza uzalishaji wa Mkonge. Kama tunavyoelewa sasa hivi tuzalisha umeme kwa kutumia mkonge na tunaendelea kusaidia wazalishaji kutafuta soko nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwatafutie malipo ya kiinua mgongo wafanyakazi wa shamba la *Alavi Sisal Estate*. Tunafanya utararibu huu ili kujua gharama na kiasi gani, kusudi tumshauri yule mwekezaji aweze kuwalipa wakulima hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga bei ya majani mabichi ya chai. Bodi ya Chai itapanga bei elekezi kwa kuzingatia gharama, tutashirikiana na Vyama vya Ushirika. Lakini tunawashauri wakulima wawe na hisa katika viwanda vilivyopo pamoja na kuanzisha viwanda vingine vipya. Mpaka sasa hivi tangu mwaka 2001, tumeshatoa miche milioni 5.9 ya chai na mwaka huu tunategemea kutoa miche milioni 1.6 ya chai ili kuweza kuongeza uzalishaji zaidi wa chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, utatuzi wa shamba la kuni Sakare, Serikali imeanza taratibu za kubatilisha umiliki wa shamba hilo ambalo kisheria linamilikiwa na Bwana Humfrey Luu toka mwaka 1963 hadi mwaka 2062. Taratibu zikikamilika, Halmashauri ya Lushoto na Korogwe watapanga matumizi ya shamba hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la dengi tunalifanyia kazi. Kuna ugonjwa unaoitwa mnyauko fuzari. Mbegu kinzani zimekwishapatikana mbili na madawa bado yanatumika kwa ajili ya kuzuia magonjwa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao ya nishati, tunaandaa mwongozo kusudi tusiruhusu wawekezaji wa ndani na nje kulima mazao ya nishati kama *jiotropa* maeneo ambayo yatafaa kwa mazao ya vyakula mfano maeneo ya Iringa, Ruvuma, yale ni maeneo ambayo yanazalisha mahindi na si maeneo ya kupeleka *jiotropa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendeleza zao la cocoa, Mheshimiwa Waziri amekubali atakwenda kule kwa Mheshimiwa Mwakyembe kwa ajili ya kuangalia zao hilo lakini pia *DADPS* zitusaide kuendeleza zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushuru wa Bodi ya kahawa urudishwe, tukirudisha ushuru huu utaongeza gharama kwa wakulima. Kwa hiyo, *regulatory functions*

zitaendelea kugharamiwa na Serikali lakini uendelezaji wa zao utaendelea kugharamiwa na wadau na kusaidiana na Serikali na Tanzania *Cofee Authority* tayari imekwisha kubali kutoa shilingi milioni 500 mwaka huu kwa ajili ya kuendeleza zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Kahawa na Ushirika wapange bei...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru, kwa kunipa fursa hii ya kuhitimisha hoja ambayo iliwasilishwa hapa jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao muda mfupi wa kuweza kuhitimisha hoja na kwa sababu hiyo, itakuwa vigumu kujibu hoja zote ambazo tumezipokea. Pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Wabunge wote ambao wameshiriki katika mjadala huu. Nataka kuwahakikishia kwamba hakuna hoja hata moja ambayo tunaiona kuwa haikuwa ya msingi. Mwanzo ni mawazo, unaweza ukasema hili lingoje hili litekelezwe, lakini mawazo ni sahihi kabisa kuyatoa hata kama yanapingana na ya kwako, nayo ni mawazo, kwa hiyo, hakuna ubaya wowote kwa sababu haiwezekani watu wote wakawa wanafikiri sawa, wakifikiri sawa, itakuwa ngumu sana, nchi hii inaweza ikawa kama Jeshi ambalo watu wakisema mguu pande wanapiga mguu pande, nchi haiendeshwi namna hiyo. Kwa hiyo, nawashukuru wote waliotoa mawazo hata kama unafikiri yanapingana na yale ambayo sisi tunafikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kujibu hoja, nilitaka nitumie fursa hii kuwatambua watu ambao wametoa mchango wao.

**NAIBU SPIKA:** Ila muda wa kuwatambua hatutauhesabu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Nakushukuru sana.

Kwanza hii hoja imejadiliwa na Waheshimiwa Wabunge 33 kwa kuongea halafu imejadiliwa na Wabunge 101 kwa kuandika. Wale wengine ambao nitawataja hapa, nitawataja kwa idadi bila kuwasoma, ni wale walitoa mchango wao wakati ule Wizara ya Fedha inawasilisha bajeti ya Serikali. Walikuwa Waheshimiwa Wabunge 35 ambao walizungumza kilimo, nataka kuwahakikishia kuwa hoja zao zote tunazo na tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale waliojadili kuhusu kilimo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, walikuwa Waheshimiwa Wabunge 55. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni karibu nusu ya Bunge limetoa mchango kwa masuala yanayohusu kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa niwatambue wale waliochangia kwa kauli nao ni Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Oscar Mkasa, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Geofrey Weston Zambi, Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda, Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mheshimiwa Mtutura Abdalah Mtutura, Mheshimiwa Ruhaga Mpina, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Danieli N. Nswanzugwanko, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila na Mheshimiwa Omari S. Kwaangw'. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi, ni Mheshimiwa Dr. Willibrod P. Slaa, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Charles N. Mwera, Mheshimiwa Emanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Diana N. Chilolo, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Capt. Damiano Komba, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Balozzi Abdi H. Mshangama na Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Naibu Spika, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mheshimiwa Felister A. Bura na Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Margaret S. Sita, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Balozzi Dr. Getrude Ibengwe

Mongella, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Mohammed A. Chomboh, Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo na Mheshimiwa Mohammed A. Abdulaziz. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Msolwa C. Msolwa, Mheshimiwa Maida H. Abdallah, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Hamza Mwenyegoha, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Ibrahim M. Sanya, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Adamu K. A. Malima, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Aziza S. Ally na Mheshimiwa Ame Pandu Ame, hao ni wale wa mwisho mwisho, ndio mambo yalikuwa hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusoma na kuwatambua wote waliochangia, sasa nataka nitumie nafasi hii, kutoa maelezo kuhusu mambo ambayo yamezungumzwa hapa na ushauri ambao tumeupokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, walioandika hii karatasi ya waliochangia, walisahau, kulikuwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambaye sikumtaja lakini majibu yake yapo hapa na vile vile msemaji wa Kamati, hakuwa ameorodheshwa, naomba radhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kutumia nafasi hii, kutoa majibu kama ifuatavyo:-

Kwanza, yako mambo ya jumla ambayo yamesemwa na Wabunge wengi sana. Kwa sababu muda ni mfupi, nafikiri nianze na hayo kwa sababu, kwa kuyasema hayo, nitakuwa nimeweza kujibu angalau hoja za wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamehoji juu ya dhana ya Kilimo Kwanza, wanasema mkakati wake uko wapi na wengine hasa hasa rafiki yangu Mheshimiwa Kwaangw', alisema sasa hii na MKUKUTA tofauti yake iko wapi, sasa nataka kusema tu kwamba dhana ya Kilimo Kwanza, msingi wake ni kuweka msisitizo kwamba uchumi wa Tanzania hauwezi kukua bila kilimo kukua! Hilo ni jambo ambalo huwezi kukataa kwa sababu ikiwa kilimo kinaajiri 80% ya watu wote na uchumi unakuzwa na watu wanaozalisha viwandani au katika mashamba au kwa kutoa huduma za namna mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu asilimia kubwa ya watu wako katika kilimo, uchumi wa Tanzania unaweza ukakua ikiwa kilimo kitaboreshwa na pato linalotokana na kilimo litaongezeka. Huo ndio msingi mkubwa na ukikubali msingi huo, unakubali dhana ya Kilimo Kwanza na kwamba sasa kwa sababu asilimia 80% ya watu wetu wako kule na uchumi wa nchi hii hauwezi kukua bila kilimo, kilimo lazima kipewe nafasi ya kwanza kwa kufikiriwa katika kila fani, huo ndio msingi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nimesema katika hotuba yangu Kilimo Kwanza kinashirikisha wadau wengi. Wapo wakulima wadogo mashambani, wako watu ambao wangependa kulima mashamba makubwa lakini hawajayalima, tunawaambia na ninyi mshiriki na tunawawekea mazingira ambayo yanawawezesha kuwekeza kwa njia ya sheria au njia ya kuwapa vivutio katika uwekezaji wa sekta ya kilimo, hao tunawaambia lakini zipo sekta nyingi ambazo zinaweza zikafanya mambo yakasaidia kilimo na hayo ni sehemu ya mfumo mzima wa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Wizara ya Miundombinu, ikitengeneza barabara kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga, kwa kweli inatekeleza dhana nzima ya Kilimo Kwanza kwa sababu unafungua eneo ambalo linalima lakini mazao hayafiki sokoni kwa urahisi na kwa sababu hiyo, unawawezesha wananchi wa maeneo yale kupanua kilimo. Kwa hiyo, Wizara ya Miundombinu, wanakuwa wadau muhimu katika kutekeleza dhana nzima ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni mifano na ni rasharasha tu kwa sababu muda hautoshi, lakini nataka niseme kwamba ili tuweze kujielimisha vizuri, nimeshauriana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na tumekubaliana kwamba katika kikao kijacho tufanye semina ya Wabunge wote, tuzungumzie Kilimo Kwanza, ili tuelewane kwa sababu sisi Wabunge ni wadau wa jambo hili na tukielewa sisi, Watanzania wote wataelewa kupitia kwetu. Kwa hiyo, tutaitisha semina ambayo itatuwezesha sisi wote kushiriki. Tutaleta na jamaa kutoka katika sekta binafsi tuje tukae nao, tuzungumze na tuwasikilize wao wanasemaje na sisi tunasemaje ili tuweze kuelewa dhana ya Kilimo Kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa ujumla, tunachosema hapa, nimesikia, Waheshimiwa Wabunge wanasema mbona bajeti ni ndogo, mimi kama Waziri wa Kilimo, siwezi kusimama hapa nikasema bajeti inatosha au ni kubwa maana ninapenda kubwa zaidi. Ni kawaida tu kuwa watu wengi wanapenda vitu vikubwa zaidi kuliko walivyo navyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kupanga ni kuchagua, siku za nyuma kwa mfano tuliamua wenyewe kwamba tutajenga sekondari katika kila Kata. Sasa huwezi kusema Kilimo Kwanza ghafla tu ukasema sasa hakuna kujenga sekondari au kuzimalizia, naamimi uwekezaji katika elimu kadri tunavyomaliza majengo, tumalize maabara na kadhalika, mahitaji ya fedha huko kwenye sekta ya elimu yatakuwa yanapungua na mahitaji kwenye sekta ya kilimo yanaongezeka. Naamini kwamba muda si mrefu tutafikia lile Azimio la Maputo la asilimia 10% ya bajeti ya Serikali. Lakini hata tukifika 10%, bado tutakuwa tunahitaji fedha zaidi kutokana na mabenki, kutokana uwekezaji ili

kilimo kiweze kupiga hatua zaidi. Ndio maana jambo moja kubwa ambalo limeamuliwa katika mfumo huu wa Kilimo Kwanza, ni kuanzisha *Bank* ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Msafiri akisema hii benki inaweza ikachukuliwa na wafanyabiashara lakini tumesema kilimo kiwe cha kibiashara na cha kibiashara maana yake siyo kuchukua hela za Benki ya Kilimo kwenda kununua ili uuze, unachukua kwa ajili ya kwenda kulima. Kwa hiyo, naamini ile benki itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunasisitiza juu ya *SACCOS* na kupitia *SACCOS*, Benki hii inaweza kufikisha mikopo kwa wakulima wadogo na hiyo itakuwa imewawezesha wakulima wote wakubwa, wa kati na wa wadogo kuweza kuendeleza kilimo chetu na kukigharamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la jumla linahusu uuzaji wa mazao nchi za nje, hili nalo limezungumzwa sana. Kwanza nataka niseme, Serikali haina Sera ya Kudumu ya Kuzuia Uuzaji wa Mazao ya Chakula Nje ya Nchi, haipo! Serikali inachofanya ni kutazama hali halisi na hii nayo siyo ngumu sana kueleza kwa sababu kama wewe ni mkulima, mahitaji yako wewe ni magunia saba kwa mwaka halafu umelima ukapata matano na ndio unayohitaji ili ule mwaka uishe usije ukafa, utayauza? Utayauza au utaweka akiba? Hiyo ndiyo hoja! Kwa hiyo, uitazame Tanzania kama familia maana nchi zilizotuzunguka ambazo hazina chakula zipo, ukisema uzeni nje, kwanza tunasema yasiende nje bado yanaenda sasa ukisema yaende, yatabaki? Tuulizane tu, hakitabaki chakula hapa na kisipobaki, hoja inakuwa kubwa, kwa nini hakuna chakula, Serikali iko wapi, maana binadamu sisi tuna sura nyingi sana, wanasema chakula kiuzwe kikiisha, unaulizwa kiko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waingereza wanasema, ‘huwezi kula keki yako halafu tena ukabaki nayo, ukauliza ile keki yangu imekwenda wapi wakati umeila mwenyewe’. Kwa hiyo, hili ni jambo nyeti, kama kuna kitu umewahi kusikia kinaitwa Usalama wa Taifa, chakula ni sehemu muhimu ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kumsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja alikuwa anasema tulime zaidi ili tusije tukaenda kwenye uchaguzi wakati kuna njaa na mimi nakubaliana naye kabisa. Ukienda kwenye uchaguzi kuna njaa, hamna chakula, wale wapiga kura wanakasirika, wanadhani wewe ndio umefanya njaa iwepo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, katika hili, lazima tukubali kwamba kuna mambo mengine itabidi tufanye kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea ni nini? Tumetoa mbolea kwa Mikoa ya Kaskazini na Kusini na mtu mmoja amesema hii mbolea tunayopeleka, je, tunapata manufaa? Mimi nasema ndiyo kwa sababu Mikoa minne tu ya Kaskazini mwaka huu imezalisha tani milioni 5.4, kama Kaskazini ingezalisha tungekuwa na *surplus* maana mahitaji yetu ya nafaka ni tani milioni sita, kama Kaskazini ingezalisha mwaka huu

tungeuza *surplus* nchi za nje na kusingekuwepo na tatizo lakini Kaskazini mvua haikunyeshwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Lekule Laizer, alikuwa kule, akanipigia simu, anasema usipoleta chakula leo hii, kuna watu watakufa hapa. Nikasema eeh Laizer, leo hii hii? Sasa katika mazingira hayo, unaruhusu chakula kiuzwe? Halafu kikiuzwa, hao wa Longido wafe?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia rafiki yangu mmoja anasema bei ya Longido ni shilingi 70,000 kwa gunia, mimi nikauliza, hiyo ni bei ya gunia kwa mahali ambapo hakuna mahindi na huwezi kutumia bei ya njaa ikawa ndiyo msingi wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wachumi wanasema kuna *effective demand* na *demand* tu, sasa tulipotangaza shilingi thelathini elfu kwa gunia rafiki yangu Mheshimiwa Kwaangw' anasema hiyo ni bei ya mezani, lakini nataka nimwambie huko Rukwa leo hivi ninavyoongea, bei ya mahindi ni shilingi 22,000 na kuna watu wananunua. Nawatangazia wananchi wa Rukwa, kama kuna mtu ananunua kwa bei ya shilingi 22,000 mimi nakuja huko kununua kwa shilingi elfu thelethini. Kama huyo aliyekuwa akinunua elfu ishirini na mbili akisikia kauli hiyo, akapandisha, naomba apandishe maana mimi shida yangu ni wale wakulima wapate nafuu, ndiyo Uwaziri wenyewe wa Kilimo kuwa na *productivity*. Hali ndiyo hiyo, tunanunua huko na mwaka jana tumenunua kwa ajili ya akiba ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na rafiki yangu Mheshimiwa Ngasongwa alipokuwa anasema ni lazima iwepo *Government intervention* kuliko kutumia *administrative mechanism*, ndiyo maana tunaunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko na Bunge lako Tukufu litakuja kuuzungumzia Muswada huo labda kikao kijacho ili tuunde bodi ambayo itakuwa ina-*intervene* kwenye *market* ili ku-*regulate* bei ili mkulima anufaike na aendeleo kuzalisha kwa manufaa ya nchi yetu, tukizalisha *surplus*, hamna tatizo kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wamesema kwamba Malawi ni nchi ndogo lakini inazalisha zaidi *surplus*, safi sana, lakini ni ndogo kweli, maana *surplus* inayozalishwa katika Mikoa mine ya Tanzania, ni kubwa zaidi kuliko *surplus* ya Malawi. Malawi mwaka jana wamezalisha *surplus* ya laki tatu lakini *surplus* ya Mikoa hiyo minne ya Tanzania inafikia laki tisa. Tofauti ya Malawi na Tanzania, Tanzania kuna sehemu kubwa ya watu hawana chakula, kwa hiyo *surplus* kama ndiyo ingekuwa kale ndiyo ka-Malawi ketu tungekuwa tumezidi Malawi mara tatu pale. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuache tu kutazama, tusikatae kufikiria mambo yanayofanikiwa na sisi tunaendelea vizuri mambo si mabaya, inyeshe tu mvua muone mambo ya *surplus*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa ruzuku za vocha, nakubaliana na wale wote waliotoa ushauri. Mheshimiwa Zamboni anasema alisoma kwenye Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwamba kuna *loss* ya shilingi milioni 30 mbolea haijulikani ilienda



wapi. Lakini hii ilikuwa ni ripoti ya mwaka 2007/2008, hayo matatizo aliyokuwa anayazungumza ndiyo yalifanya tukatoka kule tukaja kwenye vocha. Kwa sababu wafanyabiashara walikuwa wanapeleka halafu wakiturudishia *return* tunasema tunatoa ruzuku lakini hatuna ushahidi kama kweli mkulima amepata mbolea, tukasema hapana tupeleke vocha moja kwa moja kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisemi vocha kwa mkulima hazina matatizo, yapo matatizo lakini mifumo hii ya wanadamu hakuna ambao ni *perfect* na hapa panaitwa Bongo ni ngumu sana. Lakini naamini tutaboresha zaidi kwa mwaka huu ili tuone mfumo huu unafanya kazi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya jumla, Kamati yetu imetupa ushauri mzuri sana, mimi sina matatizo na ushauri uliotolewa na Kamati, Kamati chini ya Mheshimiwa Gideoni Cheyo, tunafanya nao kazi vizuri sana, inatushauri, wakati wowote ikituhitaji, tunaenda kuzungumza nao. Jambo hili la sekta ya kilimo, linahitaji maelezo na linahitaji msaada wa watu wengi, hakuna mtu mmoja anaweza kusema anaweza ku-*move* sekta ya kilimo peke yake na ikaleta mabadiliko, hii kitu ni *vast*, halafu kilimo chenyewe ni cha Kiafrika, unahitaji maoni ya watu wengi ili yaweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina maelezo zaidi isipokuwa kuwashukuru sana Kamati, nitapata fursa tena ya kuzungumza na Kamati hii kupitia maoni yao ili tuweze kuona utekelezaji unavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, rafiki yangu kutoka Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, safari hii hakuwa na makuu kusema kweli, tena nadhani anaendelea kuelewa dhana ya Kilimo Kwanza maana tupo naye kwenye Kamati siku zote, hata kama hutaki kuelewa lakini kila siku unasikia mwisho utaelewa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yeye alikuwa anasema kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza kauli ya Kilimo Kwanza, ni kidogo, ni kweli kama kila mtu anavyosema, lakini usitazame Kilimo Kwanza katika bajeti ya mwaka mmoja. Kilimo Kwanza ni dhana ambayo inataka kulipeleka Taifa letu kutoka hapo lilipo mpaka kufika mahali fulani. Kwa hiyo kila mwaka tutafanya maendeleo kuelekea huko, huwezi kusema kwa kuwa mwaka huu hamkutoa hela basi Kilimo Kwanza imekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapitisha Azimio la Kilimo Kwanza bajeti ilishatengenezwa na Mheshimiwa Hilda Ngoye, alieleza vizuri, alikuwepo. Kwa hiyo, nasema hazitoshi lakini ndiyo tunaendelea na maelezo nimeshayatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kunusuru uchumi, fedha shilingi bilioni ishirini, mbona haziko kwenye bajeti? Huo mpango wa kunusuru uchumi unasimamiwa zaidi na Waziri wa Fedha, yeye anajua katika mifuko yake, hizi pesa zitatoka wapi. Kwa hiyo, kwa kweli ukiniuliza mimi na mimi naenda kumwuuliza Mheshimiwa Mkulo, lazima yeye anazo, unajua Jungu Kuu halikosi ukoko, sasa huyu Bwana ndiyo Jungu Kuu na mambo yake yeye anasema yamekaa vizuri, nafikiri Mheshimiwa Khamis tutazungumza naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile fedha alizoeleza Mheshimiwa Rais, hazipo kwenye bajeti ndiyo hizo nimeshajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema *ASDP* hadi sasa tumepata asilimia 7.3, hapana, hiyo *statistic* siyo sawasawa, lakini unajua takwimu watu huwa wanazitengeneza ili kujenga hoja ili zilingane na zikubali. Lakini asilimia ya fedha hizi ambazo zimeshatumika ni asilimia 34 kwa fedha ambazo zilitakiwa ziwepo kwa miaka mitatu, hiyo ni kweli na hazitoshi. Lakini tuna mpango kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja la Mataifa, kukaa na *donors*, tutajaribu kufanya kikao hicho mwaka huu ili kuwapa motisha *donors* waanze kuingiza pesa zaidi ili kwa miaka iliyobakia tuweze kupiga hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Khamis, anasema je, kutoa ruzuku ya shilingi milioni 29 kwa Mikoa sita umefuata utaratibu wa *ASDP*? Nasema ndiyo, tena unajua *ASDP* inasimamiwa na sisi wenyewe lakini tuna uhusiano mkubwa sana na *development partners* na wao wana *interest* kujua. Kwa hiyo, tunatumia utaratibu uliokubalika na nchi hizi na *development partners* wetu na hizi pesa tumepeleka kule kwa ajili ya ku-*stimulate* kwa sababu licha ya kuwa tunapeleka mbolea lakini tunataka kupeleka miundombinu itakayosaidia kukuza zaidi uzalishaji wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ishiriki kikamilifu katika miradi hii, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Khamis na tunashiriki, tuna kitengo ambacho kinafuatilia na vile vile tunafikiria kuweka *coordinators* katika kanda ili tuwe karibu zaidi na utekelezaji wa miradi hii, kwa sababu si watu wote wa *Council* wana-*interest* za kufanana, wengine wanalala wanahitaji kuamshwa. Tunaimarisha *secretariat* za Mikoa ili ziwe karibu, ziweze ku-*supervise*, tunafanya kazi hiyo yote kwa ajili ya kuongeza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khamis alikuwa anazungumzia kuhusu bei ya mazao na wengine wapo ambao wamezungumza suala hili la bei, kwa hiyo, niki mjibu hapa nitakuwa nawajibu wote pamoja na suala la ruzuku. Kwanza, niseme tu kwa sababu ya udogo wa bajeti yetu, Serikali haina Sera ya kutoa ruzuku kwa mazao ya chakula, hatuna uwezo huo. Ilipotokea mtikisiko wa uchumi, yapo mazao yaliyoathirika zaidi na yapo mengine ambayo yameathirika lakini si kwa kiwango kile kile. Kwa mfano, mazao yetu ni mengi lakini ukichukua tumbaku wakati wa mtikisiko wa kiuchumi ilikuwa inaendelea kusimama, sasa huwezi kusema tupeleke ruzuku huko pia. Wakati wa mtikisiko unatokea korosho zilishanunuliwa zote na kuuzwa. Lakini zao ambalo limeathirika sana ni pamba ambayo imeshuka kutoka senti 72 mpaka senti 45 halafu hakuna dalili ya kupanda na iliposhuka wakulima wa pamba waka-*react* ndiyo maana nimesema kwenye hotuba yangu pamba itashuka kutoka marobota laki tatu themanini na sita elfu mpaka laki mbili na hamsini elfu na kwa sababu pamba inalimwa kila mwaka ni rahisi sana kwa *reaction* ile kuathiri kabisa uchumi. Bei ya soko tunayomlipa mkulima, ni shilingi 360 ukilinganisha na shilingi 450 mpaka shilingi 540 mwaka jana. Kama tukiendelea na *trend* ile bila kumpa motisha mkulima wa pamba, tutakuwa hatuna pamba na umaskini katika maeneo ya pamba utaongezeka sana. Kwa hiyo, Serikali pamoja na

kwamba haina uwezo iliamua katika mfumo ule ule wa *stimulus package* kufanya *saving* ya shilingi ishirini bilioni ili kumwongezea mkulima shilingi 80 na bei yake itoke kwenye shilingi 360 mpaka 440. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Mheshimiwa Khamis alikuwa amekosea aliandika shilingi 380 na shilingi 460, nikaona kama anataka kufanya mambo kama Mheshimiwa Cheyo ambaye alikuwa anatangaza bei kabla haijatangazwa, leo hayupo, lakini kimsingi ndiyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mazao kama kahawa iliathirika lakini dalili za kahawa ni nzuri. Habari nilizonazo leo ni kwamba bei ya kahawa imeanza kupanda, imefika sasa dola za Kimarekani 128 kwa mfuko wa Arabika wa kilo 50, zimeongezeka zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Hata Robusta imepanda kidogo ukilinganisha na Arabika. Kwa hiyo, kwa sababu hatuna uwezo, tunabembeleza soko la kahawa litujalie, lakini pamba ilikuwa na hali mbaya ilikuwa lazima tufanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nilieleze hilo na watu wa pamba vile vile nilitaka wajue kwamba hili ni jambo la mwaka mmoja siyo kwamba ni la kuendelea, matumaini yetu ni kwamba uchumi wa dunia ukifufuka hali ya pamba itaendelea kuwa kama ilivyokuwa huko nyuma. Nataka nitumie nafasi hii kuwataka wanunuzi wa pamba huko waliko, mipango itakapokamilika ya mabenki, ya *transfer* na urasimu wa mabenki, wale wakulima ambao walikuwa wameshauziwa pamba kwa shilingi 360, wawasilishe risiti zao na wakati ukifika wawafidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwishazungumzia suala la chakula na suala la pamba nimemaliza, nataka nimjibu rafiki yangu Nswanzugwanko, yeye alikuwa anasema tunatumia shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kitu kinachoitwa uratibu, lakini siyo kweli tunatumia shilingi bilioni 21 katika mambo hayo aliyoyasema tena hayo anayoita uratibu ni shilingi bilioni mbili tu kati ya hiyo shilingi bilioni 21. Shilingi 21 bilioni ni fedha zote za *ASDP* zinazobaki za kilimo ambazo zinatumika kwa ajili ya uratibu, kwa ajili ya kusomesha wanafunzi, kuimarisha vyuo na kununua vifaa vingi sana ambavyo vinafaa kwa ajili ya mambo ya utafiti na kadhalika. Kwa hiyo, siyo kwamba ni fedha za uratibu, zina kazi nyingi sana, ingekuwa kuna muda, ningesoma kila *item* lakini Mheshimiwa Nswanzugwanko nitampa mimi habari hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie nafasi hii, nimwambie kwamba kile kituo alichokisema, nimeshaonana naye pale kwenye *corridor*, nimemwambia kile kituo chake, kinaitwa Ligaga, ni kituo chetu na tumeamua sasa kukikabidhi kwa *agency* ya mbegu ili kizalishe mbegu kwa ajili ya ukanda wa Kigoma, siyo kwamba tumekitupa. Namwomba sasa atuunge mkono bila shida kwa sababu kazi ile tutaifanya kabisa bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua utapiga kengele nyingine sasa hivi, nirudie tu kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na ninawaahidi kwamba tutajibu kwa maandishi na tutawapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimsaidie ndugu yangu Mheshimiwa Killimbah kitu kimoja kidogo tu. Leo nimesikia redioni, nimemsikia rafiki yangu Killimbah anasema unajua bajeti hii haikunufaisha Jimbo lake, lakini nataka kumwambia, Mkoa wa Singida katika *vote* 84 imepewa shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuendeleza *ASDP*. Kwa hiyo, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge tuwe tunaenda kule kwenye Majimbo, tujue zile hesabu au kama hawatupi tuje huku tuzichukue ili twende kule tunazijua. Maana sisi kazi yetu moja ni kusimamia, ukisimamia unajua inakuwa vizuri zaidi. Kwa hiyo, pesa zipo kwa ajili ya Singida na hakuna Mkoa hata mmoja ambao umenyimwa fedha na mwaka huu katika ruzuku tumeweka Wilaya mbili za Mkoa wa Singida ambazo zitakuwa zinapata ruzuku, huko ambako kuna upungufu wa chakula, maeneo yanayoweza kuzalisha yazalishe zaidi ili kupunguza gharama ya kusafirisha chakula kutoka eneo moja kwenda lingine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, tumia *microphone*. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na kwa sababu *microphone* nayo inaleta taabu, naomba kutoa hoja (*Kicheko/Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna Mheshimiwa mmoja ameniandikia *ki-note*, anasema hii *microphone* inawafaa watu wafupi kama Mheshimiwa Hawa Ghasia lakini Mheshimiwa Wasira, anaonekana kipara tu lakini usoni haonekani. (*Kicheko*)

### **KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu nafahamu hii Wizara tumezungumza siku mbili lakini Waziri amepewa muda wa dakika 30 tu kujibu, kuna mambo mengi sana mliyozungumza hamkupata majibu, kwa hiyo hasira zote zinaweza zikaishia kwenye vitabu na mshahara wa Waziri. Kwa hiyo, tutatumia kanuni ya 104(1) ya kuongeza muda wa nusu saa baada ya saa ya kuahirisha Bunge, lakini pia tutatumia Kanuni ya 104(2) iwapo tutakuwa na dakika kumi kabla hatujamaliza.

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **FUNGU 43 - WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**

Kif. 1001 *Administration and General* ...Shs. 2,703,556,000/=

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza na Mheshimiwa Nswanzugwanko, Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shibiriti, Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Mkumba, Mheshimiwa Seleli, Mheshimiwa Dokta Siyame,

Mheshimiwa Dokta Mzindakaya, Mheshimiwa Waziri na wewe pia, Mheshimiwa Margaret Sitta. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Kimaro, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Chilolo, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Dokta Mpanda, Mheshimiwa Kigwalilo, Mheshimiwa Kayombo, Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Janguo, Mheshimiwa Msambya, Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Owenya, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Mheshimiwa Malangalila, Mheshimiwa Salum Hemed na Mheshimiwa Mwera. Tunaanza na Mheshimiwa Mwera.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye mchango wangu wa maandishi ...

**MWENYEKITI:** Naomba *statement* zetu ziwe fupi, hadithi msinipe maana sitazisikiliza.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sina taarifa zingine, ni kwamba kwenye mchango wangu wa maandishi, kulikuwa na kampuni zilizokuwa zikinunua kahawa pale Tarime na zimekuwa zikinunua kwa bei ya chini, nataka kujua bei elekezi inaweza ikawekwa kwenye mazao hayo ili wakulima wetu wasiweze kupunjwa?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Bodi zote zimeweka kifungu ambacho kinaziwezesha kuweka bei elekezi. Sasa ndugu yangu Mwera pale anasema zilikuwa zinanunua kwa bei ya chini. Kama bei ni ya chini ni ya chini kiasi gani? Lakini ninachojua mimi kwa mfano bei ya kahawa ilipoanza msimu huu ilianza kwa shilingi 350/- kahawa ya Robusta. Tarime wanalima Robusta na Arabica wanachanganya lakini bei ilikuwa ni hiyo. Kwa Arabica kwa Mkoa kama Kilimanjaro ilifika shilingi 1000/- na Robusta ilikuwa ni shilingi 350/- hata kule Karagwe lakini imeendelea kupanda, sasa hivi kule Karagwe Vyama vya Ushirika vinanunua kwa shilingi 450/- na kwa kweli watu binafsi wanaanza tena kupandisha baada ya vyama vile kupandisha lakini vilianza na shilingi 350/-. Kwa hiyo, Bodi ya Kahawa inaruhusiwa na sheria kuweka bei elekezi kama zilivyo Bodi zingine zote.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi sina haja sana ya kushika mshahara wa Mheshimiwa Waziri, nataka kupata ufafanuzi kuhusu mazao ya Mkoa wa Mbeya.

La kwanza, katika mchango wangu niliipongeza sana Wizara na Serikali kwa kuwalipa wakulima wa pamba Wilayani Chunya baada ya kusitisha kilimo cha pamba mwaka 1994/1995 na walikuwa wanaudai Ushirika wao uliokufa. Sasa nikamwambia Mheshimiwa Waziri kwamba kuna Kata ambazo hazijalipwa kabisa mfano Kata ya

Ifumbo, Galula, Totoe, Mbuyuni na Kata ya Namkukwe, je, watalipwa mwaka huu hawa ambao hawajalipwa?

Lingine kuhusu mazao ya Mkoa wa Mbeya...

**MWENYEKITI:** Aah, aah, swali moja Mheshimiwa!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya mazao kwa wakulima yalikuwa yanatokana na hesabu zilizofungwa mwaka 2004 yaani mwaka ule baada ya kufanya utafiti chini ya Wizara iliyokuwa ikiitwa Ushirika na Masoko. Walipofunga yale mahesabu, ndiyo waliorodhesha wakasema wapi tunalipa na tulikuwa hatulipi kwa Kata, malipo yale yalikuwa yanakwenda kwa Vyama vya Ushirika maana walikopa kwa kuuza kwenye Vyama. Sasa inawezekana Kata moja au mbili wakawa wanauza kwenye Chama kimoja, kwa hiyo, wale ambao madeni yao yalikuwa yameorodheshwa na kuthibitishwa katika mahesabu ya mwaka 2004 chini ya hiyo Wizara ya Ushirika na Masoko, ndiyo tumeyalipa. Tumetumia shilingi bilioni moja na laki sita kwa ajili ya kulipa wakulima katika maeneo yote ambayo tulikuwa tunadaiwa. Sasa kama kuna matatizo yametokea na kuna wakulima ambao wanadhani walistahili kulipwa lakini hawakulipwa, tunachoweza kufanya ni kufanya uhakiki tu kuona kama walikuwemo halafu hawakutendewa haki. Lakini tukikuta hawakuwemo itabidi tuwaambie ukweli kwamba hawakuwemo na kwa hiyo hakuna deni ambalo linaweza likalipwa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kajaribu kutafuta hizo habari zihakikiwe.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Kitabu hiki cha hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ukurasa wa sita, Kambi ya Upinzani imekuwa ikifuatilia uzalishaji wa kilimo kwa muda wa miaka minne kwenye kilimo cha umwagiliaji na imegundua kwamba kwa muda wote wa miaka mine, kila mwaka kuna ongezeko la hekta lakini uzalishaji wa mazao kwa hekta haujapungua wala kuzidi hata pointi moja. Sasa kwa akili ya kawaida katika utaalum wa kilimo jambo hili huwa haliwezekani. Sasa tuna wasiwasi kuwa hesabu hizi zimetengenezwa au zimepikwa kwa maana nyingine. Sasa kwa kuwa Waziri wa Kilimo ni mtaalam na kwa kuwa sisi wenzake wakulima hatuamini hili, atuhakikishie ilikuwaje hali hii ikajitokeza au ni makosa ya kibinadamu?

**MWENYEKITI:** Ni wenyewe wakulima au wewe mwenyewe Hemed? Mimi nadhani ni wewe Hemed.

**WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *figure* za Mheshimiwa Hemed, huwa ni ngumu kweli. Kwa mfano, moja aliyokuwa ameandika mle alisema mhogo haukuongezeka ukilinganisha na idadi ya watu. Sasa Watanzania wapo milioni 40 halafu si wote wanaolima mhogo, kwa hiyo, ukichukua mhogo halafu uutumie kulinganisha na ongezeko la watu, huwezi kupata jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii anayoisema kwamba kila mwaka uzalishaji hauongezeki, mimi siwezi kujibu hapa nikasema ndiyo au hapana. Lakini kama angekuwa ameniambia zao fulani, hajasema zao, sijui ni zao gani Mheshimiwa Khamis ambalo haliongezeki miaka yote wakati uzalishaji wa jumla unaongezeka au kupungua kulingana na mazingira yaliyopo, mvua kukosekana na kadhalika.

**MWENYEKITI:** Hili lilikuwa swali pana mno. Mheshimiwa Mushashu.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia ugonjwa ambao umeibuka katika Mkoa wa Kagera, ugonjwa wa migomba unaitwa unyanjano, *banana bacteria wilt*, utafiti umeshafika na inaonekana ule ugonjwa unasambaa haraka sana sasa hivi Halmashauri saba kati ya nane, migomba imeshaambukizwa, kwa hiyo, hili ni janga la Mkoa. Nikawa nimeomba basi kwa nini kama tunavyokwenda kushughulikia viwavi jeshi na ndege kama Kweleakwelea, Wizara ikatenga hela ikaenda kushughulikia tatizo hili ili kunusuru wana Kagera kwa sababu tunajua wanategemea ndizi wasije wakaingia katika janga la njaa na umaskini? Je, Serikali iko tayari kufanya hivyo kuliko kuziachia Halmashauri kwa sababu hali ya Halmashauri tunajua kwamba hazina hela na ugonjwa unaenea haraka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo, tunakubaliana naye kwamba ni suala linalohitaji uangalifu wa dharura na kwa sababu ni ugonjwa ambao kusema kweli ni mpya kulinganisha na yale magonjwa tunayoyaelewa, mara moja baada ya bajeti hii, tutatuma watalaam lakini kabla ya hapo tutatumia Chuo cha Maruku kwa ajili ya kutupa taarifa zaidi kuhusiana na ugonjwa huo, halafu mara moja tutalishughulikia hilo suala. (*Makofi*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia suala la makampuni ya tumbaku ambayo yameendelea kuhodhi biashara ya kununua tumbaku kutoka Mkoa wa Tabora na nikasema pamoja na kuendelea kutoa bei ndogo tofauti na Serikali ilivyotangaza hapa juzi kwamba bei imeongezeka bado Urambo wanapokea shilingi 2,700 mpaka shilingi 2,500 *average* kwa bei ya tumbaku kwa kilo na mbaya zaidi sasa hivi yale makampuni yameanza kukopa tumbaku kutoka kwa wakulima. Wameuza tangia mwezi wa tano mpaka sasa hivi wanahangaikia mapato yao hawajalipwa chochote. Mazao ya kwanza wamechukua pembejeo zao, waliyoendelea kuuza hawajalipwa mpaka sasa hivi. Ninapenda Mheshimiwa Waziri aweze kutupa ufafanuzi kwamba kwanza kwa nini wanakopa wakulima kwa sababu wamelima kwa mwaka mzima wakitegemea watanufaika na pili watalipa lini hela za wananchi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la tumbaku ni miongoni mwa mazao ambayo yana *grade* nyingi sana, zinakaribia 60 au zaidi. Sasa wanalipa *average* shilingi 2,500 mpaka shilingi 2,700, inategemea hizo *grade* na bei zake zinaleta *average* kiasi gani. Lakini jambo ambalo mimi nalijua na ambalo tumelishughulikia na ambalo wakulima wa tumbaku watakubaliana na mimi ni kwamba ingawa kampuni ilikuwa inanunulia kupitia Vyama

vya Ushirika lakini yalikuwa yanapeleka pembejeo na kusaini mikataba ambayo ilikuwa haijulikani riba yake itakuwa kiasi gani. Kwa hiyo, wanapokata zile fedha zao za pembejeo kiwango kinachobaki kwenda kwa mkulima walikuwa wanawapunja. Serikali tumechukua, hatua tumeondoa makampuni haya katika biashara ya pembejeo. Tumevisaidia Vyama vya Ushirika sasa vinakamilisha mipango yao ya kupata mikopo kutoka CRDB na NMB. Kwa hiyo, mbolea ya tumbaku mwaka huu sasa itapitia kwenye Vyama vya Ushirika ili tutenganishe soko la mazao na soko la pembejeo. Hiyo inaweza ikatupa unafuu zaidi na mimi nina imani kwamba baada ya kuondoa mgogoro huo, zao la tumbaku linaweza kuwalipa vizuri zaidi wakulima kwa sababu makampuni hayatakuwa na mikataba ya kushindana, badala yake yatakuwa yanashindana yenyewe kwa yenyewe katika kutoa bei kwa mkulima. (Makofi)

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mimi hoja yangu inatokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu hoja pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana dhana ya Kilimo Kwanza, kwa bahati nzuri Mkoa wa Kigoma ni moja katika Mikoa sita ambayo Taifa limechagua iwe katika ile Mikoa ambayo inatakiwa ihimiza kilimo. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kwamba lipo eneo moja wamepewa Mafisa Ugani 10 sasa ningeomba Wizara ituambie maeneo mengine kwa hii dhana ya Kilimo Kwanza ili kiende vizuri tutapata Maafisa Ugani wangapi au watano ili na sisi tuweze kulima kisayansi na hasa Mkoa wa Kigoma na Jimbo langu Kigoma Kusini? Ahsante. (Makofi)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikiri kwamba bado tunalo tatizo la upungufu wa Maafisa Ugani, hiyo ni kweli lakini ziko jitihada za kuwasomesha wengi zaidi. Ili kuweza kusimamia mwaka huu, kama alivyokuwa anatueleza Mheshimiwa Paul Kimiti ambaye yeye ni Bwana Shamba *by profession*, tunapeleka vijana kutoka vyuoni 1,900 na tumewesambaza katika Wilaya 60 ambazo programu hii inakwenda ili waende wakasimamie, ili kazi ya upelekaji wa pembejeo iende sambamba na mafunzo kwa mkulima, kilimo kitakapomalizika tutawa-*withdraw* kuwarudisha Chuoni halafu wenzao watakuja tena.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mimi nataka kujua tu kwa vile mwaka jana mbolea zilikawia kufika Kigoma mwaka huu, ni lini sasa zitaweza kufika kwa wakati muafaka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hata mimi nauliza hivyo hivyo. (Kicheko)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukujibu wewe pamoja na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba kama ifuatavyo:-

Hivi sasa tunakamilisha *voucher* mapema, *actually* wachapaji wameshachapa na karibu zinaingia nchini tutazipeleka sehemu husika. Lakini tumeshazungumza na wadau wote wanaosambaza mbolea ili wazipeleke kuanzia sasa ili mbolea ziweze kufika kule wakati zinapohitajika. (Makofi)



**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilisema kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani, inapelekea kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Dhana nzima ya Kilimo Kwanza, ni kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Lakini Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anajibu alisema, tutegemee mvua itanyesha tu. Lakini katika bajeti ya Wizara sijaona fungu lolote lililotengwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Ninapenda nipate ufafanuzi, fungu hilo liko wapi na bila fedha, tutaweza kweli kufanikisha Kilimo Kwanza bila umwagiliaji? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilikwishapitisha bajeti yake na fedha zimo mle ndani ya hiyo Wizara kwa ajili ya umwagiliaji. Sisi tunachofanya ni kufuatilia pale ambapo miundombinu imekwishatengenezwa na Wizara ya Maji kwa ajili ya kutoa utalaam juu ya uendelezaji wa mazao katika skimu zile. Kwa hiyo, fedha tulizonazo sisi ni za kuendeleza uzalishaji katika zile skimu lakini siyo kuweka miundombinu.

Halafu nilivyosema mvua ikinyesha kwa sababu hakuna nchi duniani ambayo kilimo chake chote kiko chini ya umwagiliaji. Hapa tuna hekta 44 milioni ambazo zinaweza kulimika lakini kati ya hizo ni 29 milioni ambazo ni *potential* kwa *irrigation*. Kwa hiyo, kwa namna yoyote hata ukifanya *irrigation* bado utaomba mvua ili iweze kukusaidia kule ambako *irrigation* haijafika.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nilichangia kwa maandishi, nadhani kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Waziri hakupata muda wa kujibu. Katika miaka 1988 mpaka 1990, tulikuwa tumeanzisha mradi ambao kwa wakati ule ulikuwa unaitwa *PADEP* lakini sasa hivi tumebadilisha jina imekuwa Kilimo Kwanza. Mradi ule ulifanya vizuri sana na mara nyingi tumekuwa tunajifunza kwa majaribio lakini miongoni mwa vitu vingi ambavyo vilifanikishwa ni kuwa na ratiba na huduma za ugani kwa Mabwana Shamba na watalaam wa kilimo kijijini. Katika kitabu cha Waziri, hajaeleza sana mikakati ambayo anaweza akafanikisha huduma hii ikaenda mpaka vijijini. Je, Waziri analiambiaje Bunge kuhakikisha kwamba Kilimo Kwanza kinaweza kufikia miaka ya 1988 ambapo tulifanikisha vizuri zaidi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na mpango unaitwa *PADEP* ambao bado upo na unamaliza kipindi chake Desemba mwaka huu. Lakini nafasi ya *PADEP* na *methodologies* zake zote zinahamia kwenye *ASDP*. Kwa hiyo, siyo kwamba *PADEP* inatoka inaacha uwazi hapana. Kwa hiyo, tunawatumia na watalaam wale wa *PADEP* na utalaam wao na umahiri wao walioutumia wakati wa *program* hii waende wasaidie *ASDP* kwa njia ya kuweka *coordinators* katika kanda ili wasaidie kusukuma zaidi *ASDP* ili kazi ile ambayo ilikuwa inafanywa na *PADEP* iendeleo kufanyika. (*Makofi*)

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, rejea ukurasa wa 34, ibara ya 50 ya kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa katika juhudi zake za kuendeleza Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Chakula la Taifa, Serikali msimu

uliopita iliweza kuupatia Mkoa huo zana mbalimbali yakiwemo matrekta madogo na makubwa, mashine za kusukumia maji, mashine za kupandikiza, kuvuna na hata kupura mpunga kwa ruzuku ya asilimia 50 ya bei ya ununuzi wa mashine hizo. Je, Serikali kwa mwaka huu, inaweza ikafanya hivyo hivyo kwa yale maeneo mengine nchini ambayo ni ya kilimo hicho hicho zikiwemo skimu za umwagiliaji za Naming'ongo, Iyendwe na Chilangu Jimboni Mbozi Magharibi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulipeleka zana za kilimo katika Mkoa wa Morogoro, lakini zana hizi tulikuwa tumepewa zawadi na Korea Kusini na nyingine tulipewa na China. Kwa sababu Mheshimiwa Rais alishasema Mkoa wa Morogoro uwe Ghala la Taifa, tuliona namna moja tunaweza kuchangia ni kuusaidia Mkoa uanze kupata zana za kuongeza uzalishaji. Sasa kule anakokusemea ndugu yangu Siyame, namshauri kupitia *DADPs* tumempelekea *power tillers* na kwa kweli kwenye skimu za umwagiliaji ambako wanalima mpunga *power tiller* inafanyakazi nzuri hata kuliko trekta kubwa. Kwa hiyo, mimi nashauri wapate *power tiller* ambazo wanagharamia kwa kulipa asilimia 20, tena ni asilimia 20 wala siyo 50% kama Morogoro. Kwa hiyo, itakuwa nafuu kwa skimu anazozungumzia.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia, nilizungumzia suala la uhaba wa watumishi. Lakini moja ya jambo ambalo kwa kweli linaweza likasababisha uhaba huu uendelee kuwa mkubwa hasa maeneo ya vijijini, ni kutokuwa na makazi. Sasa naiomba Wizara, labda nimwombe Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi hapa kwamba Wizara, ama Serikali imejiandaa vipi kuwaandalia makazi hawa watumishi hata wale ambao amesema kwamba watakwenda vyuoni baadaye watarudi kuja kuwatumikia wakulima huko vijijini?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba niliyoitoa hapa Bungeni jana, nilieleza idadi ya nyumba ambazo zitajengwa vijijini. Kwa kweli tunachoweza kusema ni kwamba ile *ASDP*, Halmashauri za Wilaya ndiyo zinaamua bajeti na zinaweza zikatenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za watumishi kwa sababu zinaruhusiwa kutumika kwa kazi hiyo. Kwa hiyo, naiomba Wilaya ya Mheshimiwa Mbunge, ifikirie suala hilo la kuwajengea Mabwana Shamba nyumba na sisi tunaunga mkono suala hilo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nilichangia kwa maandishi na nilizungumzia zaidi uhaba wa Maafisa Ushirika na nikatoa mfano kwamba Wilaya ninayotoka ya Iramba, tuna Afisa Ushirika mmoja tu na sisi wananchi wetu wanataka sana kufanyakazi kwa ushirika. Sasa tunataka Waziri atuambie wana mpango gani wa kuwafundisha Maafisa Ushirika kama vile wanavyowafundisha hawa Maafisa Kilimo wengine ili waende na kule Iramba Mashariki ambako hatuna hata mmoja?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunao mpango, chini ya mpango wa modenizesheni ya ushirika, kusomesha lakini akiulinganisha na ule wa Mabwana Shamba kutakuwa na tofauti kwa

sababu tangu zamani Mabwana Ushirika wao wanakaa zaidi Wilayani, Mabwana Kilimo wanakwenda mpaka kijijini. Lakini tunafundisha na kwa kweli Wilaya zinazotaka kuwaajiri wakati wowote zinaweza zikawaingiza kwenye bajeti na tukapata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili tuwaajiri, tuongeze *capacity* ya kutoa huduma ya ushirika.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina matatizo na Mheshimiwa Waziri upande wa vyombo vya fedha pamoja na wanunuzi wa mazao. Tatizo langu kubwa ni kwenye Chuo cha Ukiriguru, majibu niliyopewa hapa kwa kweli ni rahisi mno wakati tatizo ni kubwa sana na ni la muda mrefu na sasa hivi linaonyesha tu kwamba litashughulikiwa. Je, Waziri hawezi akatupa muda maalum ili watumishi hao wa Chuo cha Ukiriguru waweze kujisikia vizuri? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu tatizo la mradi wa maji wa Ukiriguru. Tatizo hili limechelewa kwa sababu kulikuwa na mkandarasi pale ambaye hakufanya kazi yake vizuri. Yule mkandarasi alipoondolewa, tulikuwa tumekusudia kutumia JKT na tulishazungumza na JKT ili wafanye kazi ile ya kumaliza ule mradi na kuhakikisha Ukiriguru inapata maji. Yule mkandarasi alikwenda Mahakamani akaweka *injunction* kuzuia ule mradi usiendelee mpaka kesi yake iishe. Sasa tunajaribu kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo. Lakini tukishamaliza kupata ufumbuzi, JKT tutawatuma waendeleo na kazi hiyo na sisi Wizara tuko tayari kugharamia kazi ya kupeleka maji Ukiriguru.

**MHE. JENISTA j. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sina tatizo na mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Ni ukweli usiofichika kwamba wananchi wa Jimbo la Peramiho kulingana na Sera ya Taifa ya kuhakikisha Taifa linajitosheleza kwa chakula, wamejikita kweli katika suala zima la kuzalisha mahindi na Mheshimiwa Waziri analifahamu hilo vizuri. Lakini tatizo kubwa ni kwamba mradi wa *ASDP* unalenga katika maeneo muhimu ambayo yanapewa vipaumbele kwenye Taifa letu. Mbaya zaidi kwa kuwa sasa wananchi wale wanalima zaidi chakula, lakini wameona ni bora walime na zao la biashara kwa kuwa mahindi yao mengi yananutuliwa moja kwa moja na Taifa. Hivyo tumekuwa tukipata shida sana ya kuendeleza zao letu la miwa ukizingatia hela za *ASDP* kupitia miradi mingine ambayo ni shirikishi katika Wilaya, hazitoshelezi katika mradi ule mkubwa sana wa miwa kama zao la biashara. Sasa ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kila siku nimekuwa nikilisema hili, hebu leo awape matumaini wananchi wa Jimbo la Peramiho, Wizara itafanya nini ili iweze kuendelea kuwapa moyo, wakazalishe chakula kwa ajili ya Watanzania lakini wakawa na zao la biashara la kupunguza makali ya bei ya mazao ya chakula, wakawa na mazao ya kuwaletea kipaumbele katika maisha yao ya kila siku na kuwaondolea umaskini? Ningeomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Jibu miwa sasa huko.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni miwa sasa. Tunajua tatizo la miwa katika Jimbo la Peramiho. Niliwahi kutembelea Mkoa wa Ruvuma. Nilipokuwa nazungumza na uongozi wa Halmashauri ya

Wilaya ya Songea, walisema kuna vikundi vya vijana ambao wameanza kupanda miwa kwa nia ya kutaka baadaye wapate mashine za kutengezea sukari kwa *simple technology*. Kwa hiyo, tukazungumza nao na kweli katika Mkoa ule, Paramiho ile pamoja na Songea imezungukwa na Wilaya ambazo zina mazao ya kudumu. Mbinga wanalima Kahawa, Namtumbo wanalima tumbaku, halafu kule Tunduru wanalima Korosho, sasa hawa wamebaki pale katikati. Kwa hiyo, mimi nilisema Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Songea na kupitia Bodi ya Sukari ambapo moja ya kazi yake ni ku-*promote* kilimo cha sukari, tuone jinsi tunavyoweza kuwasaidia. Kwa hiyo, tutawasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Songea tuone yenyewe iko tayari kuchangia kiasi gani na sisi tuwasaidia kiasi gani. (*Makofi*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma ni moja ya Mikoa sita ambayo Serikali imeamua kuwa ghala la Taifa. Lakini ukiangalia jiografia ya Kigoma ilivyo, unakuta kuna ardhi kubwa sana kama maeneo ya Rwiche, Titie kule Rungwa Mpya, *River Basin* ya Malaragasi, tusipofanya *irrigation* pale, hatuwezi kupatumia kwa maana ya kupata uzalishaji mkubwa zaidi. Kwenye Wizara ya Umwagiliaji, jambo hilo halikujitokeza kabisa. Sasa nikasema angalau nisubiri Waziri wa Kilimo labda na yeye atalionga hilo kwamba tusipofanya umwagiliaji tunalo tatizo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na Mheshimiwa Peter Serukamba kwamba lile Bonde la Rwiche, tukiweza kuwekeza na tukatumia lile bonde kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya chakula, tunaweza kupata manufaa zaidi kama ambavyo tunaweza kupata kutoka kwa mabonde mengine. Mimi nadhani tatizo tulilionalo ni rasilimali za kuwekeza katika maeneo haya. Mipango ipo, kisichokuwepo ni rasilimali kwa sababu hata kwa Wizara ya Maji, najua mwaka ulioisha tulikuwa tumeweka kule shilingi 13 bilioni sasa 13 bilioni kwa miradi ya umwagiliaji kusema kweli unaweza kumwagilia sehemu ndogo sana. Kwa hiyo, mimi nafikiri katika mpango huu wa Kilimo Kwanza na kwa mipango yetu ya kati na ya siku zinazokuja, nadhani ni vizuri kutazama uwezekano wa Rwiche lakini mimi kwa sasa siwezi kusema ni lini hilo linawezekana.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nifanye sahihisho kidogo kabla ya kuuliza swali langu, naomba ridhaa yako unipe ruhusa hiyo.

**MWENYEKITI:** Muda mfupi sana lakini.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Ndiyo dakika tatu zile zile.

Mheshimiwa Waziri alisema kwamba ni kijiji cha Ligaga kile ambacho kinahamishiwa kwenye mpango wa mbegu, kile kijiji kinaitwa Bugaga, ni Kituo cha Kilimo cha Bugaga na kiko katika Wilaya ya Kasulu, Kijiji cha Ligaga ni kitu kingine kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nina swali dogo tu. Wakati Mheshimiwa Waziri ananijibu, amesema nilikosea kuangalia vizuri. Lakini ukurasa wa

79 wa hotuba yake, naomba tuweke rekodi vizuri tu, labda Mheshimiwa Waziri naye rekodi zake zimejichanganya. Zile shilingi bilioni 52 zilizotengwa kwa mfuko wa *ASDP* na baadaye shilingi 21.8 bilioni, shilingi bilioni 2.5 ni za kuimarisha sekretarieti za Mikoa halafu fedha zilizobaki Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 79, 80, na 81 wameainisha kazi za kufanya. Katika zile kazi, hakuna mafunzo wala hakuna kuimarisha vyo vya kilimo. Sasa Mheshimiwa Waziri aliponijibu, nilishtuka, nikasema labda tunazungumza vitu viwili tofauti. Mimi nazungumzia fedha hizi ambazo kwa tafsiri yangu mimi zinapaswa zipelekwe kwenye uwekezaji wa kilimo siyo kwenye uratibu na *item* (i) - (x) zinazungumza uratibu tu, unaweza ukazitazama ziko pale. Sasa nasema Mheshimiwa Waziri labda ni rekodi tu, naomba tuweke rekodi sawa sawa kwamba katika zile *item* 10, hakuna *training* wala hakuna kuimarisha mafunzo ya kilimo, ni ulaji na ni uratibu tu. Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Naomba uondoe neno ulaji.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena hapa tunazungumza habari ya uandishi tu lakini ukweli ukienda kwenye vitabu na namna zile fedha zilivyogawanywa, kwa sababu *ASDP* pale tumeeleza, tumetoa shilingi 56 bilioni kwa Wizara zote ambazo zinasimamia kilimo, ambazo ni za sekta ya kilimo, ikiwemo mifugo na uvuvi, viwanda na masoko, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wote kwa pamoja ndiyo tuko katika *ASDP*. Sasa hakuna fedha zaidi ya zile shilingi 21 bilioni zilizokwenda Wizara ya Kilimo. Lakini Wizara ya Kilimo inatumia fedha za *ASDP* kuendesha yale yote niliyoyasema ambayo ni pamoja na uratibu ambao rafiki yangu Mheshimiwa Nsanzugwanko anauita ulaji. Lakini nadhani hata yeye anajua kuratibu siyo kula, kuratibu ni kusimamia. Lakini mimi ninamwambia zinatumiwa katika kusimamia lakini zinazotumiwa kwa kusimamia ni shilingi bilioni mbili mchanganuo tunao, zingine zinakwenda kwa ajili ya mafunzo, zingine ziko kwenye utafiti, maana *ASDP* inakwenda katika maeneo yote hayo. Sasa naomba Mheshimiwa Nsanzugwanko aniamini kama hotuba uandishi ulikuwa umemfanya akaona hivyo, sasa ninampa hali halisi kwamba fedha zile ni kwa ajili ya mipango ya *ASDP* inayosimamiwa Kitaifa.

**MWENYEKITI:** Hotuba haikuweka *breakdown* lakini Waziri nadhani kwenye randama zake ndiyo amefanya *breakdown*.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wango wa maandishi, nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu namna ya kuelimisha wanawake katika *SACCOS*. Mara nyingi tumekuwa tukipata shida sana Mkoani Kilimanjaro wakati akina mama wameshachangisha hela zao, wako tayari kufungua *SACCOS* yao lakini tukifika katika Ofisi za Ushirika, wale Maafisa Ushirika baadhi wanasema kwamba umoja huu una harufu ya kisiasa. Nimemweleza katika maandishi, nimemtajia Wilaya husika na nikamwomba basi katika mpango huu, sikuona pale kwenye ukurasa wa 71 wakati anapozungumzia *SACCOS* wala katika ule ukurasa wa 123 na 124 anapozungumzia kuhamasisha Vyama vya Ushirika na *SACCOS*. Swali langu lilikuwa je, katika mpango mzima, imetengwa fedha yoyote ya kuelimisha akina mama ili

waweze kujiandikisha kwenye *SACCOS* ili waweze kunufaika katika kupata mikopo ya kujiendeleza?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango yetu inayopitia *DADPs*, katika Halmashauri za Wilaya kuna fedha zinazotengwa kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ushirika na kuimarisha *SACCOS*. Kwa hiyo, nashauri ya kwamba ikiwa kinachotakiwa pale ni elimu, Maofisa wetu wa Ushirika walioko katika Wilaya ya Moshi Vijijini kama ni Moshi au katika Wilaya nyingine yoyote ya Mkoa ule, watumie fedha za *DADPs* zilizotengwa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vikundi vinavyotaka kuanzisha *SACCOS*, kwa sababu kuanzisha *SACCOS* ni kuanzisha ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu hii ya kusema kwamba kikundi kinanuka harufu ya kisiasa, mimi siielewi vizuri maana vikundi hivi ni kwa ajili ya uchumi zaidi na havichagui chama, wala havichagui itikadi. Ni watu wanaungana kwa ajili ya kufanya kazi za kiuchumi pamoja. Kwa hiyo, kama tatizo hilo litaendelea hata baada ya maelezo haya, kwa kweli nataka kutumia nafasi hii kuwataka Maafisa Ushirika kote nchini, wasaidie vikundi hivi na hasa vikundi vya akina mama, kwa sababu mahali popote ambapo akina mama wamejiunga kwenye *SACCOS*, *SACCOS* zao zinafanya kazi vizuri sana. Zinafanya vizuri kwa sababu kwanza wakikopa hawachelewi kulipa. Kwa hiyo, nafikiri Maafisa Ushirika wasaidie vikundi vya akina mama waweze kujikomboa kupitia mfumo wa *SACCOS*. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba ni-*declare interest* kwani katika ufafanuzi nitakaomba, ni mdau katika eneo hili.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 125, naomba kumnukuu, alisema:-

*“Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Tumbaku, tutafanya uchambuzi wa madeni ya pembejeo yanayodaiwa na makampuni ya ununuzi wa tumbaku na kuanza kuyalipa”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana baada ya wakulima wa tumbaku kusikia kwanza wameshukuru sana. Lakini waliniomba ufafanuzi kuhusu madeni yao ya nyuma yanayokatwa katika msimu huu wa uuzaji wa tumbaku, walitaka kujua, je, haya madeni huyakuwekwa katika utaratibu huu wa kuyachambua na kulipwa na Serikali kwa fedha zilizotengwa au utaratibu wake utakuwaje? Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukishirikiana toka mwanzo kwenye hili, naomba ukiwa kama Waziri mwenye dhamana, naomba uwatolee ufafanuzi moja kwa moja. Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumesema katika hotuba yetu kwamba tutafanya hivyo na nilikwishaeleza kwamba tunafanya hivyo kwa sababu ya kutaka kuwasaidia wakulima wa tumbaku. Hili ni tatizo ambalo limedumu kwa muda mrefu lakini tumesema kwenye hotuba tutafanya uchambuzi. Sasa tutachambua, lakini kama kuna mtu ana uwezo wa kulipa leo, alipe ili uchambuzi ule uje ulimlipie lililobaki lakini asikwepe deni wakati ana

uwezo wa kulipa. Ila tutachambua ili madeni yale mengi ya nyumba ambayo yamelimbikizwa ambayo yalikuwa yanafanya yale makampuni yanasema hamwezi kutoka kwenye mkataba kwa sababu mnadaiwa, mimi nikawa nasema sasa hawa kweli wakulima wa tumbaku hawa Wanyamwezi hawa wanaweza kuwa watumwa wa Wazungu, kwa hiyo, tulikuwa tunajaribu kufanya ukombozi pale na tutaufanya. Lakini kwa sasa waendeleo na *process* halafu uchambuzi utafuata tujue gharama gani imebakia.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika mchango wangu wa maandishi niliambia Serikali jinsi wakulima wa Mkoa wa Singida walivyofanikiwa kupata mvua za kutosha mwaka huu na wamelima alizeti kwa wingi sana. Tumekuwa tukiomba soko la alizeti humu Bungeni mara nyingi sana, nitapenda kujua jitihada za Serikali zimefikia wapi kuwatafutia wakulima wa Singida soko la alizeti.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba niliyoitoa hapa, tumeeleza jinsi tunavyokusudia kutilia mkazo ukulima wa mazao ya mafuta, mafuta haya ya kula na ni kweli kwamba kwa sasa hivi alizeti inanunuliwa kwa soko huria na kwamba hatuna utaratibu wa kuingia kwenye lile soko ili kuweza kuwaokoa walima wa alizeti. Lakini Bunge hili linakusudia kutunga Sheria ya kuanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Siku za nyuma kwa historia kulikuwa na Shirika lilikuwa linaitwa *GAPEX* ambalo lilikuwa linanunua ufuta, linanunua alizeti na mazao mengine ya mafuta lakini kwa sababu liliondoka na hatujaweka mbadala, sasa tunaunda hiyo Bodi ili iweze kusimamia ununuzi lakini itakupoanza sisi tunadhani wakulima wa alizeti wanaweza kufaidika zaidi.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi naomba niseme kwenye ukurasa wa 91, Programu ya kushirikisha vijana katika kuendeleza kilimo. Mheshimiwa Waziri alizungumza kwamba Serikali inatambua kwamba asilimia 60 ya vijana ni nguvu kazi ya Taifa. Lakini vile vile kwenye kifungu cha 139 akasema kuna baadhi ya vikundi katika Mikoa ambayo ameitaja kwenye hicho kipengele kwamba Halmashauri zitashirikishwa kuwezesha vikundi vya vijana katika kilimo. Nilipokuwa nachangia nilimweleza vijana wa Jimbo la Muleba Kaskazini, katika Kata tano zinazolima nanasi, pasheni na mboga mboga. Sasa vijana hawa walioorodheshwa kwamba wataingizwa katika miradi na mafunzo, wao hawamo na hawa wanatumia kilimo hiki katika kujikimu na kuendesha maisha yao. Je, wenyewe wataenda wapi na watapata msaada gani?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumesema hivyo na tumetaja maeneo lakini hiyo haina maana ya kwamba katika maeneo ambayo hatukuyataja hakuna wanachoweza kunufaika, kwa sababu mipango ya *DADPs* inaamuliwa Wilayani na vikundi hivi vya vijana vinaweza vikasaidiwa kupitia mpango wetu wa *DADPs* na kwa kweli ninapenda niseme tu kwamba kilimo chetu, moja ya matatizo yake makubwa ni kwamba wanaolima sasa ni watu wazima tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi ninapenda tufanye juhudi zozote kupitia *DADPs* kushirikisha vijana na pale inapowezekana na hata kupitia Mfuko wa Pembejeo kama kuna vijana wameandaliwa vizuri na wanaweza kudhaminiwa na *SACCOS* au kudhaminiwa na Halmashauri ya Wilaya, tunaweza tukaeneza vitu kama *power tillers* kwa vijana hao ili waanze kulima. Kwa sababu vijana wale wanachokimbia ni jembe la mkono sisi tunajua, maana vijana hawa ni watoto wetu tunawajua sisi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasema tuweke msukumo ili vijana mahali ambapo wameji-*organize*, Kigoma kule wameanza, vijana wa Kigoma pale Mkuu wa Mkoa anawapeleka miezi mitatu JKT, anawatoa JKT anawapa shamba, anawapa *power tillers* wanalima. Kila Mkoa ukifanya kama wanavyofanya wenzetu wa Kigoma, tutakuwa tumeanza vizuri katika kuwashirikisha vijana kwenye kazi ya kilimo.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika mchango wangu, nilisema kwamba Jimbo la Kilwa Kaskazini, limekumbwa na ukame sana na wananchi sasa hivi wanapewa kibaba yaani robo ratili, robo pishi tu. Sasa Mheshimiwa Waziri sijui utawasaidiaje ili wapate angalau debe ili waweze kujikimu katika maisha yao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Anasema kibaba hicho kwa wiki mbili, tatu hivi. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Kibaba kweli kwa wiki mbili wangukuwa bado wapo? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani wanapewa msaada. Lakini labda niseme tu kwamba kwa chakula hiki cha msaada tuna utaratibu ambao tunaufuata. Kwanza, tumepeleka wataalam wetu wanaotafiti juu ya hali ya chakula nchini. Tunapata takwimu, na mahali pale ambapo takwimu zimebadilika wakati wale vijana wametoka kule, tunaomba Ofisi za Wakuu wa Wilaya watuletee taarifa kamili juu ya mahitaji na hali halisi ya mahali wanaposema. Kwa kweli hakuna chakula cha kuweza kulisha kila Mtanzania lakini tunaweza kuwapa familia zile ambazo hazijiwezi kabisa na zile ambazo zinaweza kununua tunawapa vile vile na kazi hii tunashirikiana na Kamati ya Maafa ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika hotuba yangu nimesema kwamba tumetoa tani 36,000 kwa ajili ya kusaidia maeneo yenye upungufu na tumesema kwamba tumehamisha chakula kutoka maeneo ya Kusini kupeleka Kaskazini ili kiwe karibu zaidi na maeneo ambayo yanaweza kuathiriwa na njaa. Kwa hiyo, kama liko tatizo Kilwa na Mheshimiwa Mbunge Dr. Mpanda analisema, sisi tunalichukua, tutawasiliana na wenzetu wa Kilwa ili waweze kuchukua hatua kwa sababu hatuwezi kuruhusu watu wa huko waweze kupata maafa yale ya kula kibaba anachokisema wakati nchi inaweza ikawapa msaada wa chakula.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeelezea jinsi bei ya



ufuta ilivyosuasua kwa Wilaya ya Liwale na Lindi kwa ujumla. Lakini kuanzia jana kupitia juhudi yake wakati anasoma bajeti yake, hali inaanza kubadilika na kwamba vijiji vingi vimefikiwa na pesa jana na leo. Nina wasi wasi kwamba, je, leo tukipitisha bajeti yake hali hii itaendelea kwa kupata ushirikiano huo? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kigwalilo anajua kwamba sisi tumekuwa tunashirikiana vizuri sana na Mkoa wa Lindi katika kumaliza matatizo ya masoko katika eneo lile. Tumeshirikiana na Lindi miaka miwili iliyopita tukaondoa tatizo kubwa sana la ununuzi wa zao la korosho, sio Lindi tu lakini na katika Mikoa mingine yote ya Kusini na Pwani. Kwa hiyo, mradi pesa zimefika na hazikufika kwa amri ya Waziri kwa maana ya kuwa na bajeti leo, ndiyo zimefika na kwa kweli zitaendelea kuja tu, kwa sababu mimi ninajua kinachoendelea pale, Chama cha Ushirika cha Ilulu kimekopeshwa na CRDB kununua ufuta, lakini ni baada ya CRDB kuwa imehakikishiwa kwamba kuna mnunuzi kutoka nje ambaye anakuja kununua ule ufuta na kwa bei nzuri ndiyo maana wame-*release* zile pesa na baada ya kuwa sisi tumezungumza na CRDB vile vile. Kwa hiyo, mimi namhakikishia Mheshimiwa Kigwalilo, ndiyo mambo yanamnyookea huko sasa.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Serikali iliahidi wananchi wa Mbinga kuwapa umeme na umeme sasa Mbinga unawaka. Serikali pia iliahidi kulipa madeni ya MBIFACU, shilingi milioni 106, Serikali imefanya hivyo. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alifika Mbinga mwezi wa 10 na akahutubia Baraza la Madiwani na akaahidi baada ya kufanya mazungumzo naye kwamba bei ya kahawa inayumba akasema mbadala wake ni kuhuisha kile chama tena lakini katika majumuisho yake sikupata jawabu. Mheshimiwa Waziri anaweza kuwafanya watu wa Mbinga waendeleo kuiamini Serikali yake ya Awamu ya Nne, kwa sababu kule Mbinga tunasema Mbinga ni mbinguni na watu wa mbinguni mara nyingi wanapenda kuamini? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wanasema Mbinga mbinguni na unajua mbinguni huwezi kupadanganya. Kwa hiyo, nataka kusema tumeenda kule Mbinga, tuliahidi na tulipeleka wataalam wetu pale kwenda kuanza mchakato utakaowezesha mali zilizokuwa za Chama cha zamani kilichokuwa kinaitwa MBICU zihamishiwe MBIFACU ili Chama hiki kipya kiweze kuingia kwenye soko la kahawa. Tatizo ambalo liko sasa hivi ni kwamba kuna watu walienda Mahakamani dhidi ya mali zile za MBICU, sasa mambo ya Mahakamani huwa yanasumbua kidogo. Lakini mimi matumaini yangu ni kwamba hili jambo tutalimaliza mwaka huu wa fedha. Inawezekana tukachelewa kununua kahawa ya wakulima wa Mbinga kwa msimu huu lakini tukichelewa kwa msimu huu ambao unaanza mwezi ujao tunaweza tukaingia kwenye msimu unaokuja lakini tumeahidi kulimaliza, tutalimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya iliyotokea, nilipotuma hawa wataalam kwenda kule kutazama mambo ya ufilisi wakakaa na mfilisi wakamkagua siku tatu, mfilisi yule naye tena akapata ajali akafariki. Sasa tukapata tatizo lingine. Kwa hiyo,

bado tunayo taarifa tuliyoipokea kutoka kule, tunaifanyia kazi kabla hatujafikia hatua ambayo tutafanya maamuzi ambayo inaweza kufanya MBIFACU sasa iwe ndiyo mrithi halali wa MBICU.

**MHE. OMARI S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naungana na Mheshimiwa Waziri, kwamba tunahitaji kuwa na mkutano mkubwa wa kujadili tatizo hili la kilimo na kuioanisha hasa na MKUKUTA kwa sababu malengo ya MKUKUTA tunayajua. Sasa ninaomba tu ufafanuzi juu ya jambo dogo. Mimi nilipata nafasi ya kusema na nimezungumza mengi lakini nataka ufafanuzi juu ya bei ya mazao ya *SGR*. Wizara imetangaza bei ya mazao hasa mahindi na mtama kwenye gazeti na nilisema leo kwamba ni kilo 100 au gunia moja sawasawa na shilingi 30,000. Sasa nataka kujua Wizara inatumia vigezo gani kupanga hizi bei za *SGR* nchi nzima inakuwa *uniform*? Tunataka kujua hili ili wananchi wetu waelewe kwamba Serikali yao inaangalia baadhi ya mambo kwa sababu gharama za uzalishaji zinapanda na kila mwaka zinapanda na wanapata matatizo. Sasa nataka kujua ni vigezo gani ambavyo Serikali imetumia katika kupanga bei hizo. Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mwenyekiti, mara nyingi vigezo ambavyo vinaweza vikatumika ni kwa kutazama bei ya soko. Kama bei ya soko iko chini ya hiyo shilingi 300, kama nilivyosema kule Rukwa sasa hivi wananunua gunia moja kwa shilingi 22,000 au sawasawa na shilingi 220 kwa kilo, kwa hiyo ukiwa Rukwa bei ya soko ndiyo hiyo, sasa sisi tungependa kuwa juu kidogo zaidi kuliko bei ya soko. Ndiyo maana tumesema tunalipa shilingi 300 lakini tumesema kuna malori ya *SGR* yatakuwa yanaenda kununua vijijini ili kuwapunguzia wakulima hawa gharama za kuleta kwenye vituo vya *SGR*. Huko tukienda ndiyo tunanunua kwa bei ya shilingi 250 kwa sababu wanakuwa wamepunguza *cost* ya kuleta hasa wale wanaoishi mbali zaidi. Kwa hiyo, hivyo ndiyo vigezo. Lakini kama Mheshimiwa Kwaangw’ anataka vigezo zaidi, tuko tayari kumkaribisha kwenda kuzungumza naye naye tupate mawazo yake, yeye anafikiri tungetumia vigezo gani.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kupata ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri. Katika michango yangu yote miwili ya kuzungumza hapa Bungeni na kimaandishi, nimehoji maamuzi makubwa mawili ya Serikali kuhusu makusanyo ya ushuru za Bodi za Mazao. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri ni msikivu. Moja nimejibiwa kwamba watalichukua lile la kuwaruhusu na kwamba watakwenda kulifanyia kazi. Lakini niligusia vile vile tatizo la ushuru wa korosho, ile asilimia tatu na nusu ambayo inakwenda Hazina. Niliishauri Serikali waachie iende kwa wakulima, ndiyo Kilimo Kwanza hicho, kule ndiko waliko na kuwapa moyo lakini sikusikia lolote lile. Je, Waziri anasemaje juu ya suala hilo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Janguo hakisikia hilo kwa sababu liko nje ya uwezo wetu kwa sasa kulitolea majibu ya hapana au ndiyo. Kwa sababu liko katika Sheria na huwezi kubadili Sheria peke yako. Kwa hiyo, kwa sababu ile Sheria inasema tutatoza asilimia 10 na nasema kati ya hizo asilimia 6.5 zitakwenda kwenye Halmashauri na asilimia 3.5 zitakwenda Hazina, sasa ukitaka kubadili hilo inabidi tufanye mashauriano na wenzetu

wa Hazina katika utaratibu wa kawaida wa kubadili Sheria. Ndiyo maana tuliamua kunyamaza sisi kwa sababu hatukuwa tunaona kama tunalo jibu sasa hivi la kuweza kutosheleza.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa mchango wangu na kueleza jinsi nilivyofurahi kuona kwa mara ya kwanza Wizara ya Kilimo inazingatia masuala ya matumizi bora ya ardhi pamoja na hifadhi ya mazingira. (*Makofi*)

Lakini nikasema vile vile kwamba kwa vile sisi kule Ludewa tunatarajia kuwa na miradi mikubwa ya uchimbaji madini ya chuma na ujenzi wa viwanda vikubwa vya chuma ghafi na vyuma vya pua na uzalishaji wa umeme kule Mchuchuma, kutakuwa na matatizo sana ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji, makazi na maeneo ya viwanda. Tunahitaji mpango bora wa matumizi ya ardhi ili tuondokane na yaliyotokea Kaskazini. Sasa niliona kwenye Wizara hii, kuna mpango huo katika Wilaya kadhaa kutakuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na tathmini ya athari ya mazingira ya mpango huu wa Kilimo Kwanza, nikawa nimeuliza Wizara hii hamkuona kwamba Wilaya ya Ludewa pamoja na malalamiko ya siku nyingi mngeweza na sisi mkatuingiza kwenye mpango huo kwa ajili ya faida ya nchi tu, kwa sababu Wilaya hii inazalisha chakula sana na kuna mapori makubwa yatakayofunguliwa kwa ajili ya kilimo na ufugaji. Je, Wizara hii hamwezi kweli tukusaidia Ludewa? Naomba ufafanuzi au maelezo. Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mwenyekiti, ni kweli nilisikia ombi la Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, lakini ninachoweza kusema ni kwamba nitamwomba Mheshimiwa Profesa Mwalyosi tuzungumze juu ya jambo hili kwa sababu tatizo ambalo lipo katika Wizara ni upungufu wa rasilimali watu pamoja na rasilimali fedha katika kufanya kazi hiyo. Kitengo hiki cha Hifadhi ya Ardhi, kina watu wachache tu na ndiyo tunajaribu sasa kukijenga. Lakini pamoja na hayo, kutokana na umuhimu wa maelezo ya Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, kwa sababu yeye mwenyewe ni mtu wa mazingira, ni mkereketwa wa mazingira, namwomba tuje tuzungumze ili anisaidie vile vile kuelewa halafu tutaona jinsi tunavyoweza kusaidia tatizo analolizungumza hapa.

**NAIBU SPIKA:** Tumeshaingia kutumia saa zile za Kanuni ya 104 (1).

**MHE. WILLIAM B. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitasema kwa ufupi sana. Mimi nadhani nilikuwa miongoni mwa Wabunge wa kwanza kabisa kuhoji faida ya mbolea ya Minjingu. Niliuliza swali na mwaka jana nilisema kwamba wananchi wa Mufindi wameathirika sana na mbolea ya Minjingu na mwaka huu, dakika chache zilizopita nimesema kwamba wananchi wa Kata ya Mtambula na nimetaja Kata kama nane hivi wameathirika sana na mbolea ya Minjingu na hivi sasa wana njaa. Sasa swali je, Serikali au Wizara hii iko tayari badala ya kutuletea mbolea ya Minjingu iwe inatuletea mbolea ya *DAP*?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu na majibu ya Serikali ni kwamba tumeshasema

kwamba maeneo ambayo mbolea ya Minjingu haikukubali vizuri, kwanza tunafanya utafiti, tukisharidhika kwamba kwa kweli haikufanya vizuri kutokana na mbolea yenyewe kwamba inahitaji sehemu ambayo *PH* yake iko chini, basi tutapeleka mbolea ya ruzuku ya *DAP*. Lakini kama mazao hayakupatikana vizuri kutokana na wakulima wale kutotumia vizuri mbolea ile kwa kutokufuata masharti ya utumiaji wa mbolea ile, basi tutaendelea kutoa elimu juu ya mbolea ya Minjingu, kusudi iweze kutumika katika eneo lile. Kwa hiyo, asiwe na wasi wasi, kama kuna Kata ambazo kwa kweli haikukubali kwa sababu *PH* iko juu ama kuna *phosphorus* nyingi ama *calcium* nyingi basi sisi tutapeleka *DAP* ili iweze kuwasaidia.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua fikra za Wizara kuhusu jambo hili ninalotaka kulisema kwamba inavyoonekana mwaka huu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kuna njaa. Je, isingekuwa vizuri *SGR* wakawezeshwa kupata fedha hata za kununua mahindi ya ziada wayauze kibiashara ili kusaidia wananchi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo hoja anayoitoa Mheshimiwa Mzindakaya inakubalika na kwa sababu *SGR* itawezeshwa kununua na kuuza kwenye masoko kwa njia mbili. Moja, ni ku-*recycle* fedha zake lakini nyingine ni kuzuia kupanda hovyoy kwa bei za vyakula katika maeneo yaliyo na matatizo. Kwa hiyo, tutazingatia ushauri huo na tutafanya hivyo. (*Makofi*)

**MHE. LUHANGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati nachangaia nilishauri kwamba tatizo la wananchi wetu kuuza mazao nje ya nchi ni kutafuta bei nzuri na kwa kuwa wanazuiwa kuuza chakula nchi za nje kwa sababu ya kujikinga na njaa hapa nchini, lakini nikaleta ushauri mwigine wa ziada kwamba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuwanunulia wananchi mazao yao ya ziada kwa bei ambayo iko sawasawa na ile iliyoko nje na baada ya hapo sasa kama kuna ziada nyingine, Serikali imeshakamilisha kwamba inahitaji kununua chakula kwa ajili ya akiba ya chakula cha Taifa tani kadhaa, lakini wananchi wakaona bado wana *surplus*, *surplus* ile waruhusiwe kuuza nje. Sasa ushauri huo nao Mheshimiwa Waziri unampa taabu gani?

**NWENYEKITI:** Ahsante. Waziri kwa kifupi tu kwa sababu tuna dakika 10 tu na nina watu wangapi sijui.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nimelieleza wakati nilipokuwa najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwa sababu unaposema ziada, unasema ziada kwa nani? Ziada kwa Tanzania au ziada kwa mkulima mmoja wa Meatu? Sisi tunazungumza juu ya ziada kwa nchi kwamba ukiifanya nchi ikakosa chakula kwa sababu umemruhusu mtu mmoja tu akapata ziada yake akauza wote tutakuwa katika tatizo. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili tunazungumza juu ya bei wapi na nani huyo anapeleka nje, maana lazima vile vile tukubali. Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe wanakuita mtoto wa mkulima na mimi ni wa mkulima kabisa, tena mkulima wa jembo la mkono. Mimi baba yangu tangu namwona analima, sijapata kuona akiuza mazao nje.

**MWENYEKITI:** Rudi kwenye kipaza sauti.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Hamna, wapi? Wanaouza nje ni wale wanaonunua kwa mkulima, walanguzi, ndiyo wanaojua njia ya kwenda nje. *Let us face it, tunamzungumzia* nani hapa? Tunamzungumzia mkulima wa jembe la mkono kweli au tunamzungumzia mlanguzi anayenunua kwa bei chini ili akauze aghali?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilipokuwa nachangia nilitaka kujua hatua ambazo Mheshimiwa Waziri amechukua kwa ile mbolea ambayo Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali alitoa taarifa kwa mbolea ya thamani ya shilingi milioni 30,802,100. Waziri anasema kwa sababu ya kasoro zile ndiyo sababu tumetoka kwenye utaratibu ule tukaenda kwenye utaratibu wa vocha lakini hoja yangu hapa ilikuwa kwa sababu mbolea hii imepotea mikononi mwa wakala ambao sio waaminifu, Serikali kupitia Wizara hii wamechukua hatua gani kuwabaini mawakala hao ili pesa hizo ziweze kurudi na baadaye zitumike?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana naomba sana tuwe *brief* kwa sababu ya muda wengine hawatafikiwa sasa.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** *Brief* ni kwamba anapotoa taarifa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kwa kawaida huwa tunafuatilia kwanza ili kujua hasa hasa kilichotokea ni nini halafu tunampa majibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo *process* imeendelea na kwa sasa siwezi nikajibu kwamba ni hatua zipi zimechukuliwa zaidi ya hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa ninyi ninapowaita muwe *brief*.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Serikali ilihamasisha kiwanda cha Minjingu kiweze kuzalisha mbolea ya kutosha ili iweze kununuliwa yote na Serikali na vile vile tuliarifiwa kwamba Serikali itatoa fedha kwa *TFC* ili iweze kununua mbolea ile yote. Naomba Mheshimiwa Waziri atujulishe Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba mbolea ile yote iliyorundikana kule Minjingu inanunuliwa ili kiwanda kile kiweze kuzalisha mbolea ya msimu ujao?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Ni kweli kuna mbolea imelundikana Minjingu, lakini tukubali kwamba mbolea kwa kawaida ni bidhaa ambayo inatumika kwa wakati fulani. Haiwezekani kila wiki uwe unauza kwa sababu watu wanaonunua inakuwa ni kiangazi, hawawezi kuinunua. Lakini kwa sababu tunaanza sasa msimu wa kilimo, tumesema *TFC* watanunua na tumewaruhusu watu binafsi wanaosambaza mbolea nchini na wao waende Minjingu na yapo makampuni ambayo wamesema wako tayari kwenda Minjingu kwenda kununua mbolea. Kwa hiyo, nafikiri tatizo hili ni la muda baada ya muda utaona kiwanda kinaendelea na mbolea ile inauzwa. (*Makofi*)

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Nataka ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Katika mchango wangu, nilikuwa nimezungumzia juu ya Mfuko wa Pembejeo na nikaelezea kwamba Mfuko wa Pembejeo hasa kwa wakulima wa kule kwetu, wa Mkoa wa Singida na Iramba, kwa ujumla juu ya ununuzi wa matrekta. Mwaka jana ulitolewa ule Mfuko lakini Mkoa wetu hasa katika Wilaya ya Iramba hawakupata. Je, nauliza katika hizi shilingi bilioni tano za mwaka huu Wilaya ya Iramba nayo itapata?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu wa Pembejeo unatoa mikopo kutokana na maombi na *applications* za wale wanaohitaji matrekta ama *power tiller* ama pembejeo zingine zozote. Sasa kupewa, inatokana na kutimiza masharti na masharti mengi ambayo yamekuwa yanawashinda wakopaji ni kutokana kwamba wanakosa dhamana. Sasa nakubaliana pia na upande wa kusema kwamba eneo lake halikupata. Nilishawahi kufika kule Liwale, kusema kweli kule ndiyo maeneo ya kilimo hasa...

**MWENYEKITI:** Huyu hapa Mheshimiwa Killimbah siyo Mbunge wa Liwale.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kwamba ni Iramba lakini nilikuwa natoa mfano wa Liwale kufanya hii hoja ieleweke kwamba hata kule Liwale unaweza kukuta kwamba wakulima wanalima sana, llakini wameomba sana kwenye Mfuko wa Pembejeo hawajapata mikopo ile. Kwa hiyo, tutajaribu kwenye Mufko ule kuangalia kwamba hata tunavyotoa mikopo tujaribu kuhakikisha kwamba nchi nzima angalau matrekta na zana zile zinafika katika maeneo mbalimbali, maana unaweza ukashangaa matreketa 300 yamekwenda kwenye Wilaya moja tu, kwa sababu wao ndiyo wameomba au kuna msukumo fulani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kililimba asiwe na wasiwasi suala hilo tutalishughulikia na nitahakikisha kwamba kama watu wako hao wamekidhi viwango vile basi watapata nao mkopo huo.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Nami naungana na mpango wa Serikali wa kuzuia chakula kuelekea nchi za jirani kama Kenya. Kwenye ule mji wangu wa Musoma, chakula chote kinachoringia pale wanategemea kununua kwa sababu si mji wa kilimo lakini sasa kinachojitokeza ukiangalia kuanzia pale Lamadi mpaka Musoma zipo *barrier* pale ambazo wale wanaonunua kule chakula wanazuiwa pale na inawalazimu kutoa fedha ili waweze kupita na matokeo yake sasa zile gharama wanaziongeza kwenye gharama zao na hizo zinamwendea yule mlaji. Mimi ninapenda kufahamu Mheshimiwa Waziri, amejipanga vipi kuhakikisha kwamba vyakula vile vinapita mpaka pale Mjini Musoma pasipokuwa na hizo gharama ambazo wanalazimika kuzitoe ili kupunguza mfumuko wa bei?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hilo analolizungumza Mheshimiwa Manyinyi nalifahamu na wasimamizi wake ni Wakuu wa Mikoa na Wilaya, kwa sababu kuna maelekezo ambayo wamepewa ya kudhibiti chakula kile kisiende nchi za nje. Lakini pale nilipomwuliza Mkuu wa Mkoa, ameweka utaratibu kwamba Mkuu wa Wilaya ya Musoma akiwajua wafanyabiashara wanaoingiza chakula Musoma au wanaoingiza Bunda au hata

wanaoingiza Rorya basi wanaweka utaratibu wao ambao unawawezesha kuingia bila ya matatizo. Lakini wapo ambao ni wajanja tu, wanataka kwenda Kenya lakini wanasingizia kuwa wanaenda Musoma. Kuna mmoja aliwahi kunipigia simu kwamba amezuiwa asiuze chakula Bunda akijua mimi ni Mbunge wa pale na mimi nikapiga simu kwa DC nikamwambia DC amwezeshe akishushe pale kwenye soko. Alipoambiwa, akasema pale bei ni chini, je, bei juu itakuwa iko wapi? (*Kicheko*)

Kwa hiyo, nafikiri huu utaratibu uliowekwa na Mkuu wa Mkoa wa Mara na Ma-DC unaweza kuwezesha kurahisha uingizaji wa chakula pale Musoma ili kutokuwadhibu watu ambao hawana hatia. Lakini kwa sababu pale ni boda inakuwa vigumu sana kujua ni nani anaenda upande wa pili wa Kenya na nani anapeleka Musoma mpaka wanapokuwa wamehojiwa. Lakini uongozi wa Mkoa tutashirikiano ili kuona jinsi wanavyoweza kurahisisha ili wasiwaumize sana walaji wa Musoma na maeneo mengine.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa aina ya Arabica kutoka Kilimanjaro, Mbinga na Kigoma ndiyo inayotumika kukoleza kahawa nyingine duniani ili iwe na ladha nzuri pamoja na bei nzuri. Kwa pamoja inaitwa Kilimanjaro *Coffee* au kahawa ya Kilimanjaro. Nilisema pia makampuni makubwa yanayofanya biashara ya kahawa kama *Vol-Coffee* ya Uswiss, *New Man* ya Ujerumani na Chibo ya Uingereza, wanatumia jina hili la *Kilimanjaro Coffee* bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo kutoka kwa Waziri, ni sababu zipi zinazofanya Wizara ambayo ina wasomi wengi pamoja na TCB kutokuandikisha hili jina kwenye *Copy Right International* ya Marekani ili kahawa hii ijulikane duniani kwamba ni kahawa ya Tanzania? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi hapa Bungeni tumeshapitisha Sheria ya Haki Miliki na kwa sasa hivi Wizara yetu pamoja TACRI wako katika mchakato na hatua ya mwisho ya kupata usajili na ulinzi wa aina tisa za kahawa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kimaro, hilo tumeshalichukua, tulishaliona toka muda mrefu, kwa hiyo, usiwe na wasi wasi kahawa yetu itakuwa kwenye Haki Miliki kwa ajili ya kuilinda.

(*Kifungu kilitotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa tunatumia Kanuni ya 104(2), kwamba zikibakia dakika 10 kabla ya saa ile ya kuahirisha baada ya kuongeza basi tunapita kwa Fungu zima.

*Kif. 1002 – Finance and Accounts... ... Shs.1,111,642,000/=*  
*Kif. 1003 – Policy and Planning .... ...Shs.1,438,776,600/=*  
*Kif. 1004 – Agriculture*  
*Training Institute... ... Shs.6,176,259,000/=*  
*Kif. 1005 – Internal Audit Unit .... ... Shs.249,117,000/=*

*Kif. 1006 – Procurement Management*  
*Unit... ..Shs.443,278,000/=*  
*Kif. 1007 – Information, Education and*  
*Communication... ..Shs.394,217,000/=*  
*Kif. 1008 – Legal Unit.... ..Shs.247,235,000/=*  
*Kif. 1009 – Management Information*  
*System Unit... ..Shs.286,683,000/=*  
*Kif. 1010 – Environmental Management*  
*Unit... ..Shs.216,548,000/=*  
*Kif. 2001 – Crop Development .... Shs.81,004,015.100/=*  
*Kif. 2002 – Agricultural Mechanization... Shs.689,326,000/=*  
*Kif. 2003 – Agriculture Land Use Planning*  
*and Manage Shs.462,329,000.00*  
*Kif.2004-Plant Breeders Unit.. ...Shs.232,015,000/=*  
*Kif. 3001 – Research Development. ...Shs.13,927, 709,200/=*  
*Kif. 4001 – Cooperative Development..Shs.5,811,790,100/=*  
*Kif. 5001 – National Food Security ... Shs.20,485,837,000/=*  
*Kif. 5002 – Strategic Grain Reserve... ..Shs.00*

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

## **MPANGO WA MAENDELEO**

### **FUNGU 43 - WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**

*Kif. 1001 – Administration and General ... Shs.79,919,000/=*  
*Kif. 1003 – Policy and Planning... ..Shs.3,652,450,000/=*  
*Kif. 1004 – Agricultural Training*  
*Institute... ..Shs.1,166,709,000/=*  
*Kif. 1007 – Information, Education*  
*and Communication... ..Shs.50,000,000/=*  
*Kif. 1009 – Managementg Information*  
*Systems Unit... ..Shs.170,240,000/=*  
*Kif. 1010 – Environmental Management*  
*Unit... ..Shs.471,400,000/=*  
*Kif. 2001 – Crop Development... ..Shs.72,470,233,570/=*  
*Kif. 2002 – Agricultral Mechanization... ..Shs.700,000,000/=*  
*Kif. 2003 – Agricultural Land Use Planning*  
*and Manage... ..Shs.00*  
*Kif. 3001 – Research Development... ..Shs.13,133,301,630/=*  
*Kif. 4001 – Cooperative Development... Shs.100,000,000/=*  
*Kif. 5001 – National Food Security... ..Shs.700,000,000/=*



*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na  
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu, limekaa kama Kamati na kupitia bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Fungu 43 kwa mwaka 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuipitisha bila mabadiliko. Naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako liidhinishe Fungu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na  
Ushirika kwa Mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunapenda kuitakia kheri Wizara hii pamoja na Kauli Mbiu ya Kilimo Kwanza na sisi tunazingatia kwamba amesema kwa wakati muafaka, tutakuwa angalau na semina kuelewa kwa undani kauli hii ya Kilimo Kwanza maana yake nini kwa upande wa Bunge na ingekuwa vizuri zaidi tukawa kabla hatujaenda huko nyumbani, maana tunapokwenda nyumbani ni wakati wa kilimo, tungejua kabla ingekuwa vizuri zaidi kuliko Bunge lijalo litakalokuwa Novemba itakuwa kidogo gumu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri jaribu kuona kama unaweza ukafanya kabla ili kusudi tunapokwenda nyumbani na sisi tuwe tumeweza kuelewa Kilimo Kwanza maana yake nini. *(Makofi)*

Ila lingine ni kwamba utaratibu wa Vocha unasaidia sana akina mama wajane, waathirika, wazee na wengine. Sasa hii ya kusema kwamba mtakuwa mnataka walipe kwanza, nadhani muiangalie vizuri, itakuwa inavunja heshima ya vocha.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nina tangazo moja tu. Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, anaomba niwatangazie Wajumbe wote wa Chama Cha Mapinduzi kwamba Alhamisi tarehe 23 kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi, sio wote, Kamati ya Uongozi, kitakachofanyika kesho saa saba mchana mara tu baada ya kusitisha Kikao cha Bunge, awamu ya kwanza. Kwa hiyo, ni Kamati ya Uongozi sio Wabunge wote, kitafanyika katika Ukumbi Na. 118, ni Ukumbi ule wa Spika, kwa hiyo, Kamati ya Uongozi ya Chama Cha Mapinduzi kesho saa saba mchana.

Waheshimiwa Wabunge, mimi sina matangazo mengine. Naomba niwashukuru sana kwa kazi mliyofanya siku mbili ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, mmejadili vizuri na Waziri amejitahidi kujibu vizuri maswali yenu. Kwa hiyo, tunawatakieni kheri na nyie mkapumzike vizuri kesho asubuhi tukutane saa tatu. Kwa hiyo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.14 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi  
Tarehe 23 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*